**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA 30 JUNI, 2020

JUNI, 2020

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **AfDB** | African Development Bank |
| **AGITF** | Agricultural Inputs Trust Fund |
| **AGYI** | African Germany Youth Initiative |
| **AJISO** | Action For Social Justice |
| **AMCOS** | Agricultural Marketing Cooperative Society |
| **AMEDA** | Africa and Middle East Depository Association |
| **ASCAs** | Accumulating Savings and CreditAssociations |
| **ASDP** | Agricultural Sector Development Programme |
| **ATCL** | Air Tanzania Company Limited |
| **BOT** | Bank of Tanzania |
| **BRELA** | Business Registrations And Licencing Authority |
| **CAF** | Contractors Assistance Fund |
| **CAG** | Controler Auditor General |
| **CBT** | Cashewnut Board Of Tanzania |
| **CFGs** | Community Financial Groups |
| **COCOBA** | Community Conservation Banks |
| **COSTECH** | Commission for Science and Technology |
| **COSTECH** | Tanzania Commission For Science And Technology |
| **CSDR** | Central Securities Depository and Registry Services |
| **CSR** | Corporate Social Responsibility |
| **DCB** | Dar es Salaam Commercial Bank |
| **DIT** | Dar es Salaam Institute of Technology |
| **DITF** | Dar es Salaam International Trade Fair |
| **DOT** | Digital |
| **DSE** | Dar es Salaam Stock Exchange |
| **DTBi** | Dar Teknohama Business Incubator |
| **EACOP** | East Africa Crude Oil Pipeline |
| **EAMCEF** | Eastern Arc Mountains Conservation Endowment Fund |
| **EPZA** | Export Processing Zone Authority |
| **EWURA** | Energy and Water Utilities Regulatory Authority |
| **FSDT** | Financial Sector Deepening Trust |
| **GCF** | Green Climate Fund |
| **GCLA** | Government Chemistry Laboratory Authority |
| **GDP** | Gross Domestic Product |
| **GePG** | Government electronic Payment Gateway |
| **GMRA** | Global Master Repurchase Agreement |
| **GMS** | Government Mailing System |
| **GS1** | Global Standard One Tanzania Barcode |
| **HESLB** | Higher Education Students' Loans Board |
| **HIDF** | Human Innovation and Development Fund |
| **IFMIS** | Intergrated Financial Management Information System |
| **ILO** | International Labour Organization |
| **ILO** | International Labour Organisation |
| **IR VICOBA** | Inter Religious VICOBA |
| **JKT** | Jeshi La Kujenga Taifa |
| **JNHPP** | Julius Nyerere Hydropower Project |
| **JNIA** | Julius Nyerere International Airport |
| **JOSACA** | Jozan Saving and Credit Association |
| **KJP** | Kigoma Un Joint Programme |
| **KKCF** | Kilimo Kwanza Fund |

| | |
|---|---|
| **LCF** | Land Compansition Fund |
| **MEF** | Mwananchi Empowerment Fund |
| **MGOV** | Mfumo wa Huduma za Serikali kupitia Simu za Mikononi |
| **MIVARF** | Programu ya Miundo Mbinu ya Masoko na Huduma za Kifedha Vijijini |
| **MKURABITA** | Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania |
| **MSCL** | Mfumo huu unaotumiwa na Kampuni ya Huduma za Meli |
| **NACTE** | National Council For Technical Education |
| **NBC** | National Bank of Commerce |
| **NEDC** | National Entrepreneurship Development Committee |
| **NEDF** | National Entrepreneurship Development Fund |
| **NEEC** | National Economic Empowerment Council |
| **NFA** | National Fund Antiquities |
| **NHIF** | National Health Insurance Fund |
| **NICOL** | National Investment Company Limited |
| **NM AIST** | Nelson Mandela African Institute Of Science And Technology |
| **NMB** | National Microfinance Bank |
| **NSSF** | National Social Security Fund |
| **OSBC** | One Stop Business Centre |
| **OSHA** | Occupational Safety And Health Authority |
| **OWM** | Ofisi ya Waziri Mkuu |
| **PASS** | Private Agriculture Sector Support |
| **PASS** | Trust Private Agricultural Sector Support Trust |
| **PEP** | Probono Entrepreneurship Programme |
| **PPRA** | Public Procurement Regulatory Authority |
| **PSC** | Programme Steering Committee |
| **REF** | Rural Energy Fund |
| **RFB** | Road Fund Board |
| **SACCOS** | Savings and Credit Cooperative Societies |
| **SAGCOT** | Southern Agriculture Growth Coridor of Tanzania |
| **SAGCOT-CTF** | Southern Agricultural Growth Corridor Of Tanzania - Catalytic Trust Fund |
| **SANVN** | Sido, Azania Bank, Neec, Veta & Nssf |
| **SCTF** | SAGCOT Catalytic Trust Fund |
| **SDF** | Skills Develeopment Fund |
| **SEECO** | Sustainable Economic And Environment Conservation Organization |
| **SGR** | Standard Gauge Railways |
| **SIDO** | Small Industries Development Organisation |
| **SIDO** | Small Industries Development Organization |
| **SILC** | Savings for Internal and Lending Community |
| **SMEs** | Small and Medium Enterprises |
| **SUA** | Sokoine University of Agriculture |
| **TAA** | Tanzania Airport Authority |
| **TADB** | Tanzania Africultural Development Bank |
| **TADB** | Tanzania Agricultural Develeopment Bank |
| **TaFF** | Tanzania Forest Fund |
| **TAGEDO** | Tanzania Gender Development Organization |
| **TAMISEMI** | Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **TAMTF** | Teach A Man To Fish |
| **TANePS** | Tanzania National eProcurement System |
| **TANESCO** | Tanzania Electricity Supply Company |
| **TANROADS** | Tanzania National Roads Agency |
| **TANTRADE** | Tanzania Trade Development Authority |

| | |
|---|---|
| **TAREA** | Tanzania Renewable Energy Association |
| **TASAF** | Tanzania Social Action Fund |
| **TBS** | Tanzania Burear Of Standads |
| **TCC** | Tanzania Cigarette Company |
| **TCCIA** | Tanzania Chamber of Commerce, Industry and Agriculture |
| **TCDC** | Tanzania Cooperative Development Comission |
| **TCDC** | Tanzania Cooperative Development Commission |
| **TDL** | Tourism Development Levy |
| **TECC** | Tanzania Entrepreneurship Competitive Center |
| **TECC** | Tanzania Entrepreneurship And Competitiveness Centre |
| **TECU** | Tanroads Engineering Consulting Unit |
| **TEDAP** | Tanzania Energy Development and Expansion |
| **TEF** | Tanzania Education Fund |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TFDA** | Tanzania Food And Drugs Authority |
| **TIB** | Tanzania Investment Bank |
| **TIMAP** | Tanzania Informal Microfinance Association of Practioners |
| **TIRDO** | Tanzania Investment and Research Development Organisation |
| **TIRP** | Tanzania Intermodal and Rail Development Project (TIRP) |
| **TPB** | Tanzania Postal Bank |
| **TPDC** | Tanzania Petroleum Development Cooperation |
| **TPSF** | Tanzania Private Sector Foundation |
| **TRC** | Tanzania Railway Cooperation |
| **TWCC** | Tanzania Women Chamber of Commerce |
| **TWPF** | Tanzania Wildlife Protection Fund |
| **TYC** | Tanzania Youth Coalition |
| **TYDS** | Tanzania Youth Digital Summit |
| **UNCTAD** | United Nations Conference on Trade and Development |
| **UNDP** | United Nations Development Program |
| **USSD** | Unstructured Supplementary Service Data |
| **UTT** | Unit Trust Fund |
| **VETA** | Vocational Education and Training Authority |
| **VETA** | Vocational Education And Training Authority |
| **VICOBA** | Village Community Banks |
| **VICOBA-FETA** | VICOBA Federation Tanzania |
| **VITOVU** | Vituo vya Maendeleo ya Jamii vya Kuondoa Umaskini |
| **VSO** | Voluntary Service Overseas |
| **VVU** | Virusi vya UKIMWI |
| **WDF** | Women Development Fund |
| **WFE** | World Federation of Exchanges |
| **Y4SED** | Youth For Social Economic Developent |
| **YBI** | Youth Business International |
| **YDF** | Youth Development Fund |

## YALIYOMO

**vifupisho ... 2**
**1.0. Baraza La Taifa La Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ... 9**
1.1. Utangulizi ... 9
1.2. Dira ... 10
1.3. Dhamira ... 10
1.4. Amali Za Baraza ... 10
1.5. Majukumu Ya Baraza ... 10
1.6. Wajumbe Wa Baraza ... 12
1.7. Uongozi Wa Sekretariati Ya Baraza ... 15
1.8. Muundo Na Wafanyakazi Wa Sekretariati ... 17
1.9. Ukaguzi Wa Hesabu Za Baraza ... 19
1.10. Ofisi Za Baraza ... 19
**2.0. Hali Ya Ukuaji Wa Uchumi ... 19**
2.1. Utangulizi ... 19
2.2. Pato La Taifa ... 20
2.3. Mfumuko Wa Bei ... 22
2.4. Hali Ya Maisha Ya Wananchi ... 23
2.5. Sekta Ya Fedha ... 24
**3.0. Sera, Sheria, Kanuni Na Miongozo ... 25**
3.1. Utangulizi ... 25
3.2. Kanuni ... 27
3.3. Miongozo ... 29
**4.0. Sekta Ya Ardhi, Nyumba Na Maendeleo Ya Makazi ... 30**
4.1. Utangulizi ... 30
4.2. Hali Halisi Ya Utekelezaji ... 30
4.3. Mradi Wa Kupanga, Kupima Na Kumilikisha Ardhi ... 35
4.4. Mradi Wa Kuwezesha Umilikishaji Wa Ardhi ... 35
4.5. Mradi Wa Kuwezesha Ushindani Wa Sekta Binafsi (Sekta Ya Ardhi) ... 37
4.6. Mradi Wa Uzalishaji Umeme Wa Julius Nyerere (Jnhpp) ... 37
4.7. Mradi Wa Ujenzi Wa Reli Ya Kisasa ... 39
4.8. Mradi Wa Ujenzi Wa Bomba La Mafuta ... 39
**5.0. Ushirika ... 40**
5.1. Utangulizi ... 40
5.2. Idadi Na Aina Ya Vyama Vya Ushirika ... 40
5.3. Hali Ya Vyama Vya Ushirika ... 40
5.4. Udhibiti Na Usimamizi Wa Vyama Vya Ushirika Nchini ... 42
5.5. Mafanikio ... 43
5.6. Viwanda Vilivyoanzishwa Na Vyama Vya Ushirika ... 44
5.7. Kuimarisha Masoko Katika Vyama ... 44

5.8. Changamoto ........ 45
**6.0. Vikundi Vya Kifedha Vya Kijamii ........ 47**
6.1. Utangulizi ........ 47
6.2. Ir-Vicoba ........ 47
6.3. Timap ........ 48
6.4. Vicoba-Feta ........ 49
6.5. Utekelezaji Wa Sera, Sheria Na Kanuni Za Sekta Ya Huduma Ndogo Za Fedha ........ 50
**7.0. Mpango Wa Viwanda Vidogo Na Vya Kati (Sanvn Viwanda Scheme) ........ 54**
7.1. Utangulizi ........ 54
7.2. Masharti Na Vigezo Vya Utoaji Mikopo ........ 55
7.3. Muundo Wa Mkopo ........ 55
7.4. Utaratibu Wa Kuomba Mkopo ........ 55
7.5. Viambatisho Vya Maombi Ya Mkopo ........ 56
7.6. Majukumu Ya Taasisi Kwenye Mradi Huu ........ 56
7.7. Utekelezaji Wa Programu ........ 57
7.8. Hitimisho ........ 57
**8.0. Mifuko Ya Uwezeshaji Na Programu Za Mitaji ........ 59**
8.1. Utangulizi ........ 59
8.2. Uratibu Wa Mifuko Ya Uwezeshaji ........ 59
8.3. Utendaji Wa Mifuko Ya Uwezeshaji ........ 61
8.4. Mifuko Inayotoa Ruzuku ........ 61
8.5. Mifuko Inayotoa Dhamana ........ 69
8.6. Programu Za Uwezeshaji ........ 81
8.7. Changamoto Za Mifuko ........ 84
**9.0. Maendeleo Ya Ujasiriamali Tanzania ........ 85**
9.1. Utangulizi ........ 85
9.2. Kamati Ya Kitaifa Ya Maendeleo Ya Ujasiriamali (National Entrepreneurship Development Committee) ........ 85
9.3. Uboreshaji Wa Mazingira Ya Biashara ........ 86
9.4. Kuimarisha Elimu Ya Ujasiriamali Na Kuendeleza Ujuzi ........ 90
9.5. Kuwezesha Matumizi Ya Teknojia Na Ubunifu ........ 94
9.6. Kuboresha Upatikanaji Wa Mitaji ........ 94
9.7. Kuhamasisha Utamaduni Wa Ujasirimali Na Mitandao Ya Biashara ........ 95
**10.0. Ubunifu Tanzania ........ 98**
10.1. Utangulizi ........ 98
10.2. Mazingira Ya Kuwezesha Ubunifu Tanzania ........ 98
10.3. Uendelezaji Ubunifu Tanzania ........ 98
10.4. Changamoto Za Ubunifu Tanzania ........ 115
**11.0. Ushiriki Wa Watanzania Miradi Ya Kimkakati Na Uwekezaji (Local Content) ........ 116**
11.1. Utangulizi ........ 116

11.2. Hali Ya Ajira ........ 116
11.3. Zabuni/Manunuzi ........ 122
11.4. Usajili Makandarasi Na Thamani Ya Miradi ........ 125
11.5. Huduma Za Ushauri Wa Kitaalam (Uhandisi) ........ 126
11.6. Idadi Ya Zabuni Na Thamani Ya Miradi Ya Barabara ........ 127
11.7. Mafunzo, Ujuzi Na Teknolojia ........ 129
11.8. Programu Za Huduma Kwa Jamii ........ 135
**12.0. Uwezeshaji Kwa Vijana ........ 140**
12.1. Utangulizi ........ 140
12.2. Programu Ya Mafunzo Kwa Vijana Wa Jkt ........ 140
12.3. Programu Ya Probono ........ 141
12.4. African-German Youth Initiative ( Agyi ) ........ 143
12.5. Tanzania Innovation Explore Gala ........ 144
12.6. Kijana Jiandalie Ajira (Via) ........ 146
12.7. Tanzania Youth Digital Summit (Tyds) ........ 147
12.8. Programu Ya Serikali Ya Kukuza Ujuzi ........ 148
12.9. Programu Ya Mafunzo Ya Ujasiriamali Na Usimamizi Wa Biashara ........ 149
12.10. Kongamano La Maadhimisho Ya Kitaifa Ya Wiki Ya Vijana ........ 150
**13.0. Uwezeshaji Kiuchumi Wa Wanawake Na Wenye Ulemavu ........ 151**
13.1. Utangulizi ........ 151
13.2. Utekelezaji Wa Programu Mbalimbali Za Uwezeshaji Kwa Wanawake Na Wenye Ulemavu151
13.3. Ushiriki Wa Wanawake Na Wenye Ulemavu Katika Manunuzi Ya Umma ........ 156
**14.0. Uwezeshaji Katika Mikoa Na Serikali Za Mitaa ........ 158**
14.1. Vituo Vya Uwezeshaji Mikoani ........ 158
14.2. Vituo Vya Urasimishaji Na Uendelezaji Wa Biashara (One Stop Business Development Centres) ........ 159
14.3. Vituo Vya Uwezeshaji Vilivyoanzishwa Na Halmashauri Za Wilaya ........ 162
14.4. Taarifa Ya Kituo Cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Kahama ........ 162
14.5. Vituo Vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Kwenye Mikoa Mingine ........ 165
14.6. Vitambulisho Vya Ujasiriamali ........ 173
14.7. Mikopo Ya 10% Ya Halmashauri ........ 175
14.8. Uanzishwaji Wa Masoko Na Vituo Vya Ununuzi Wa Madini ........ 176
14.9. Hadithi Za Mafanikio ........ 180
**15.0. Uwezeshaji Wa Vodacom Kwa Watanzania ........ 186**
15.1. Matokeo Katika Jamii ........ 187
15.2. Matokeo Ya Shughuli Za Kikanda ........ 188
15.3. Miradi Ya Kijamii ........ 189
15.4. Uwezeshaji Wa Jamii Iliyounganishwa ........ 190
15.5. Kuwasilisha Tunu Za Jamii ........ 191

15.6. Matokeo Ya Tafiti ........................................................................................ 192
15.7. Upimaji Wa Matokeo ........................................................................................ 193
15.8. Miradi Ya Afya Ya Uzazi........................................................................................ 194
15.9. Mradi Wa Kuwawezesha Wasichana ........................................................................ 195
15.10. Miradi Na Michango Katika Sdgs.......................................................................... 196

# 1.0. BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

## 1.1. UTANGULIZI

Serikali ya Awamu ya tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imekuwa ikitilia mkazo suala la wananchi kujikwamua na kuondokana na umaskini. Mikakati mbalimbali ya kuwakwamua wananchi kutoka kwenye umaskini iliyobuniwa kabla ya Serikali ya awamu ya tano imeboreshwa na kuimarishwa na mikakati mipya yenye ufanisi zaidi imebuniwa na kufanyiwa kazi. Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali inayolenga kumwezesha mwananchi ashiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kupunguza umaskini imepitiwa na kuboreshwa na mingine kubuniwa.

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge namba 16 ya mwaka 2004. Jukumu la msingi la Baraza ni kusimamia kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Kwa mujibu wa sheria hiyo Baraza linatakiwa kuandaa miongozo ya kitaifa ya sekta mtambuka kwa ajili ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Mojawapo ya miongozo iliyoandaliwa kwa ajili ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni Mkakati wa Taifa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambao ndio mwongozo mkuu kitaifa wa kusimamia, kufuatilia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji. Mkakati huo unahusisha sekta zote za uwezeshaji wananchi kiuchumi, ambapo majukumu ya kila mdau yameainishwa. Aidha, uliandaliwa Mwongozo wa Utekelezaji wa Mkakati huo ambao ulizinduliwa tarehe 9 Februari 2016. Baraza pia lina jukumu la kuandaa taarifa ya utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji na kuiwasilisha kwa wadau kila mwaka.

Baraza limeandaa mpango mkakati wake wa tatu kwa kipindi cha miaka mitano (*NEEC strategic plan* 2018/19–2022/23). Mpango mkakati wa Baraza unaainisha Dira, Dhima na Malengo Makuu Matano (5) na malengo mengine yanayoiongoza Ofisi katika utekelezaji wa majukumu yake kwa kipindi cha miaka hiyo mitano. Malengo hayo ni;

a. Baraza kutafuta rasilimali (fedha, watumishi wenye sifa, vitendea kazi na technolojia ya kisasa)
b. Baraza kuwajengea uwezo kuhusu dhana ya uwezeshaji wadau wake wakuu.
c. Baraza kutekeleza jukumu lake la kusimamia na kuratibu shughuli zote za uwezeshaji wananachi kichumi ambazo zinafanywa na wadau mbalimbali
d. Baraza kutumia njia mbalimbali za kujitangaza kwa wadau na wananachi ili litambulike;
e. Huduma zinazotolewa na Baraza ziwafikie wananachi wengi zaidi
f. Kuhakikisha masuala ya mtambuka yanajumuishwa katika mpango na shughuli za Baraza la Uwezeshaji Wananchi kiuchumi.

### 1.2. DIRA

Kuona watanzania wengi wanashiriki na kumiliki sehemu kubwa ya uchumi wa nchi yao.

### 1.3. DHAMIRA

Dhamira ya Baraza ni kuongoza, kuwezesha na kuratibu shughuli zote za uwezeshaji wananchi kiuchumi nchini Tanzania.

### 1.4. AMALI ZA BARAZA

Misingi ya Maadili katika kutoa huduma zenye ubora, Baraza linaongozwa na kuamini msingi ifuatayo:-

- *Ubunifu*: Sisi ni asasi ambayo wakati wote inahamasisha utamaduni wa kupokea na kuendeleza mawazo mapya kutoka ndani na nje ya asasi.
- *Uwazi:* Tunafanya shughuli zetu kwa uwazi na shirikishi kwa wadau wetu;
- *Uadilifu:* Sisi ni Taasisi adilifu inayotoa huduma kiuhakikifu na bila upendeleo
- *Uwajibikaji:* Tutahakikisha tunatumia uwezo wetu kutekeleza majukumu yetu kwa umahiri mkubwa na pale tutakapokosea tupo tayari kulaumiwa kwa hilo;
- *Umoja:* Tunaamini kufanya kazi kwa pamoja ndiyo njia pekee ya kutufikisha kwenye malengo yetu kwa haraka.
- *Matokeo:* Sisi ni Taasisi yenye weledi inayotoa huduma bora kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali ya Serikali;
- *Kuwalenga watu*: Tunalenga zaidi matarajio ya wadau wetu kwa kujenga utamaduni mzuri wa kuhudumia wateja na kuwa na watumishi wataalamu na wenye motisha ya kazi.

### 1.5. MAJUKUMU YA BARAZA

Majukumu ya Baraza yametokana na maudhui yaliyoainishwa katika Sera ya Uwezeshaji na Sheria ya Uwezeshaji ya mwaka 2004. Majukumu makuu ya Baraza ni:

a) Kuwapatia watanzania fursa za kushiriki kikamilifu katika shughuli za Kiuchumi;
b) Kuhamasisha na kuhimiza uwekaji wa akiba, uwekezaji na ushirikishwaji makini wa wananchi kwenye shughuli za kiuchumi;
c) Kuendeleza na kuwezesha shughuli za kibiashara zinazoanzishwa na kuendeshwa na watanzania;
d) Kusimamia, Kuongoza na kutafuta vyanzo vya fedha na michango kwa ajili ya Mfuko wa Uwezeshaji;
e) Kuandaa Mpango Mkakati wa Sekta na Kisekta na kuhamasisha matumizi ya rasilimali kwa shughuli za Uwezeshaji wa Wananchi;
f) Kuandaa Mkakati wa kitaifa wa Uraghibishi wa sekta mbalimbali wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi;

g) Kushauri kwenye shughuli zote za uanzishaji wa vikundi, ushirika, ushirikiano na uashirikiano wa biashara wa muda mfupi;
h) Kuishauri Serikali, Taasisi za umma na binafsi katika masuala mbalimbali yenye lengo la kusaidia kukuza uchumi wa Watanzania;
i) Kuhamasisha utafiti wa shughuli za kiuchumi na kuhimiza ushirikiano na mashirika ya Kitafiti;
j) Kuandaa na kusimamia mfumo wa kufuatilia maendeleo ya shughuli za uwezeshaji Wananchi kiuchumi na kutathmini matokeo;
k) Kukuza na kusaidia shughuli za kiuchumi zinazoanzishwa na kuendeshwa na watanzania;
l) Kuwezesha na kuratibu mafunzo ya mikopo na ujasiriamali kwa vikundi mbalimbali vya wananchi kutegemeana na mahitaji yao na changamoto zao;
m) Kushirikiana na Mashirika mbalimbali kwa nia ya kuhamasisha uwezeshaji na upatikanaji wa huduma zinazohusiana na fursa za kiuchumi; na
n) Kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali kwa lengo la kutoa mapendekezo ambayo yatalenga kuboresha mazingira ya uwezeshaji wananchi kiuchumi.
o) Kutoa mikopo kwa wajasiriamali kwa dhamana au bila dhamana kadri Baraza litakavyoona inafaa

## 1.6. WAJUMBE WA BARAZA

Kwa mujibu wa Sheria ya Uwezeshaji Baraza linaundwa na wajumbe tisa (9) pamoja na Mwenyekiti. Mwenyekiti wa Baraza huteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wajumbe huteuliwa na Waziri mwenye dhamana ya Uwezeshaji. Baraza lilipo sasa ni la tano (5) tangu kuanzishwa kwa taasisi hii. Wakati Mwenyekiti wa Baraza aliteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 9 Septemba, 2018 wajumbe wengine wa Baraza waliteuliwa tarehe 11 Juni, 2020. Baraza limeundwa na wajumbe wenye uzoefu wa fani mbalimbali kama vile viongozi wastaafu wa Serikali, wanataaluma, watafiti, wafanyabiashara na viongozi wa taasisi zisizokuwa za serikali za maendeleo ya wananachi. Yafuatayo ni majina na wasifu wa wajumbe wa Baraza:

**Jedwali Na. 1: Wajumbe wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**



**Dkt. Festus B. Limbu,** ***Mwenyekiti wa Baraza***

Ni Mhadhiri Mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika masuala ya Uchumi. Vilevile ni Mtafiti mwandamizi na Mshauri mwelekezi wa masuala ya uchumi chini ya Taasisi ya Utafiti (Economic and Social Research Foundation - ESRF). Mbunge Mstaafu wa jimbo la uchaguzi la Magu mkoani Mwanza (2000-2015). Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo na Naibu waziri wa fedha katika serikali ya awamu ya tatu. Aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Pamba Tanzania (Tanzania Cotton Board) na kuwa mjumbe katika bodi mbalimbali hapa nchini, Afrika Mashariki na Dunia kwa ujumla. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alimteua Dkt. Festus B. Limbu, kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Septemba 2018.



**Profesa Lucian A. Msambichaka,** ***Mjumbe***

Ni Profesa Mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam katika masuala ya Uchumi wa kilimo. Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW) na ni Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Biashara DCB. Alikuwa Mwenyekiti Mwanzilishi wa Bodi ya Bima ya Afya (NHIF), Mwenyekiti Mwanzilishi wa Bodi ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Usihirika na Biashara (MUCCoBS), Moshi na Mkurugenzi Mwanzilishi wa Kituo cha Ushauri cha Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam. Pia aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo cha Uwekezaji (TIC) na Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA). Alikuwa Mshauri Mkuu na Mwezeshaji Kiongozi wa "Majadiliano ya Ushirikiano kwa Manufaa ya Wote (Global Smart Partnership Dialogue)" na Mshauri Mkuu na Mwezeshaji Kiongozi wa "Majadiliano ya Kitaifa Kuhusu Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Tanzania".



**Profesa Timothy E. Simalenga, *Mjumbe***

Ni Naibu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha St. John kilichopo Dodoma Tanzania tangu mwaka 2019. Pia ni Mwenyekiti Mtendaji wa Taasisi ya kusaidia Wananchi kujikwamua Kiuchumi (Social Economic Support Organization) tangu mwaka 2017. Aliwahi kuwa Mtendaji Mkuu wa Kituo cha uratibu wa tafiti za maendeleo ya Kilimo katika ukanda wa Kusini mwa Afrika kuanzia mwaka 2012 mpaka 2016. Profesa Simalenga ni mtafiti mbobezi aliyeshika nafasi mbalimbali katika taasisi za utafiti ndani na nje ya nchi kuanzia mwaka 1983 mpaka mwaka 2012. Amekuwa mwalimu katika vyuo vikuu mbalimbali vya ndani ya na nje ya nchi kuanzia mwaka 1983 mpaka hivi sasa.



**Bw. Ladislaus J. Mwamanga, *Mjumbe***

Ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Rais wa kusaidia kaya maskini (Social Action Fund - TASAF). Kabla ya kujiunga TASAF alifanyakazi Shirika la Petroli Tanzania (Tanzania Petroleum Development Corporation - TPDC), Benki ya Taifa ya Biashara (National Bank of Commerce - NBC); Oil Marketing Company na Total Tanzania Limited (1994 – 1999).



**Dkt. Frederick S. Ringo, *Mjumbe***

Ni Wakili wa Mahakama Kuu ya Tanzania na ni Mhadhiri Mwandamizi wa Shule ya Sheria katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika masuala ya sheria ya biashara na fedha. Aliwahi kuwa Afisa Sheria Mkuu (PSRC), Mkuu wa kitengo cha Huduma za Kisheria (Africa Export-Import Bank -Cairo) na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani wa Biashara (Fair Competition Commission). Ni mwanachama wa Taasisi ya Wasuruhishi wa Migogoro (UK na Tanzania).



**Bibi Anna T. Maembe, *Mjumbe***

Ni Katibu Mkuu mstaafu kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, akiwa hapo alifanya mambo mengi ya kimkakati kwa ajili ya wanawake na watoto. Cheo hiki alidumu nacho kati ya mwaka 2011 mpaka 2015. Amekuwa mtumishi wa umma kwa kipindi cha miaka 34. Ameshiriki kuongoza masuala mengi ya Serikali ikiwamo kuongoza Bodi mablimbali za Taasisi za Umma. Pia ametoa machapisho mbalimbali katika masuala ya utunzaji wa mazingira na kutoa ushauri kwa Taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi. Yeye ni mbobezi katika masuala ya mazingira.

**Brig Jenerali (Mstaafu) Aloyce D. Mwanjile, *Mjumbe***



Ni Mstaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Akiwa mtumishi wa Jeshi alishika nafasi mbalimbali za uongozi ndani na nje ya nchi. Wakati anastaafu mwaka 2017 alikuwa Mkuu wa Ukaguzi Jeshini (Chief Inspector General). Pia aliwahi kuwa Kamishna Msaidizi wa *Logistics* katika wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuanzia mwaka 2013 mpaka 2014. Alikuwa Mkuu wa Vikosi mbalimbali vya Jeshi kuanzia mwaka 2006 mpaka 2013. Alikuwa mwalimu katika Chuo cha Kijeshi Arusha na Pangawe kuanzia mwaka 1994 mpaka 2002. Aliwahi kuwa mjumbe wa Bodi ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Kampuni ya Jitegemee.



**Dkt. Astronaut Bagile, *Mjumbe***

Ni Mkurugenzi Mtendaji na mwanzilishi wa shirika lisilo la kiserikali la Women In Social Entrereneurship (WISE). Amefanya kazi katika mashirika yasiyo ya kiserikali ya kitaifa na kimataifa kwa miaka 25 akichangia kuinua hali za uchumi za wananchi husan makundi yaliyo na hali duni zaidi kama wakulima, wanawake, vijana na watoto. Ni mjumbe wa bodi wa shirika la kimataifa linalojihusisha na utafiti wa masuala ya kijinsia na wanawake Afrika (AAWORD) lililo na makao yake Senegal. Pia ni Mjumbe wa bodi wa shirika lisilo la kiserikali lijulikanalo kama SCODIA.



**CPA. Nicodemus D. Mkama, *Mjumbe***

Ni Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji Tanzania (CMSA) tangu mwaka 2018, Ana uzoefu katika shughuli za masoko ya mitaji zaidi ya miaka 23. Kabla ya hapo alifanya kazi Benki Kuu ya Tanzania; Benki ya Eurafrican; na Taasisi ya Agakhan Foundation, International Organisation. CPA. Mkama ni mtaalamu mbobezi katika fani ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu anayetambuliwa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi Tanzania (NBAA). Ni mtaalam mwelekezi (Consultant) katika uandaaji na ukaguzi wa hesabu katika viwango vya kitaifa na kimataifa.

## 1.7. UONGOZI WA SEKRETARIATI YA BARAZA


Kwa mujibu wa kifungu cha 14 cha Sheria ya Uwezeshaji ya mwaka 2004, Menejimenti ya Baraza inaongozwa na Katibu Mtendaji ambaye huteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza huajiri Wakurugenzi na Mameneja. Kwa sasa timu ya Menejimenti ina watumishi wafuatao:-

**Jedwali Na. 2: Uongozi wa Sekretariati ya Baraza**



***Bibi Beng'i M. Issa, Katibu Mtendaji***

Aliteuliwa kushika nafasi hiyo na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 4 Desemba, 2014. Pia ni Katibu wa Baraza. Kabla ya uteuzi huo alifanya kazi Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (Tanzania Commission For AIDS - TACAIDS) kama Mkurugenzi wa Fedha, Utawala na Utafutaji Rasilimali kwa miaka 12. Pia alikuwa Mdhibiti wa fedha wa CARE International Tanzania kwa miaka 3. Aliwahi kuwa mhadhiri wa masuala ya fedha na uhasibu katika kilichokuwa Chuo cha Maendeleo ya Uongozi - Mzumbe kwa kipindi cha miaka 9 (1992- 2000). Alikuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Wanawake(TWB 2016-2018). Ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Ushindani ya Ujasiriamali Tanzania (TECC) na Mwenyekiti wa Bodi ya Tanzania Legal Services Facility, vile vile ni Makamu Mwenyekiti wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Mafuta na Gesi (PURA). Ni mjumbe wa Bodi ya Soko la Hisa la Dar es Salaam, Mjumbe wa bodi ya Social Economic Empowerment of Women in Tanzania (SOWETA). Aliwahi kuwa mjumbe wa Bodi ya Benki ya DCB (2015-2016).



***Bw. Suleiman M. Malela, Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi***

Aliteuliwa kushika nafasi hiyo mwaka 2018. Kabla ya uteuzi huo alikuwa akikaimu nafasi ya Mkurugenzi wa Fedha na Utawala tangu mwezi Octoba, 2016. Hapo awali alikuwa Mkuu wa kitengo cha Ukaguzi ndani kutoka mwezi Octoba, 2008 alipoajiriwa na Baraza. Kabla ya kujiunga na Baraza, Bw. Malela alifanya kazi Shirika la Bima la Taifa Tanzania (National Insurance Corporation - NIC) katika nafasi mbalimbali chini ya kurugenzi ya udhibiti wa mali za shirika kuanzia mwaka 1993 mpaka 2008.



***Bi. Esther .B Mmbaga, Kaimu Mkurugenzi wa Uwezeshaji na Ushiriki wa Watanzania kwenye uwekezaji***

Aliteuliwa kushika nafasi hiyo mwaka 2018. Kabla ya uteuzi huo alikuwa akikaimu nafasi ya Mkurugenzi wa Ushiriki wa Watanzania kwenye Uwekezaji kuanzia mwaka 2015. Hapo awali alikuwa ni Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Sheria kutoka mwaka 2007 alipoajiriwa na Baraza. Kabla ya kujiunga na Baraza, Bi Esther alifanya kazi katika idara ya mahakama kama Hakimu Mkazi toka mwezi Mei, 2003 mpaka mwezi Aprili, 2007 alipojiunga na Baraza.



***Bw. Isaac Zachariah Dirangw, Meneja wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano***

Bwana Dirangw ameajiriwa tangu Mei 2007 na tangu wakati huo amekuwa Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA na Takwimu ambapo anawajibika kusimamia shughuli za kila siku za masuala ya TEHAMA na Takwimu. Kabla ya kujiunga na Baraza, alifanyakazi kama Mtakwimu Mkuu Mwandamizi na Mshauri Mkuu wa masuala ya TEHAMA katika Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC).Dirangw ni mtaalamu wa utafiti na uchambuzi wa takwimu zitokanazo na tafiti mbalimbali kwa zaidi ya miaka 20 sasa, pia ni mtaalamu wa kusimamia na kutayarisha mifumo mbalimbali za TEHAMA kama tovuti, kanzidata, n.k. Anauzoefu katika kutayarisha na kusimamia Bajeti (MTEF) tangu mwaka 2000 kwa kushiriki katika utayarishaji wa Bajeti za Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto na pia amekuwa akishiriki katika kutayarisha bajeti ya Baraza tangu mwaka 2007. Dirangw ana uzoefu katika masuala ya Menejimenti na

Uongozi kwa zaidi ya miaka 12, ni mkuu wa kitengo kwa muda wa miaka 13 na amekuwa mjumbe wa Meneijimenti ya Baraza tangu 2007 hadi sasa.

***Bi. Simphroza V. Mvanda, Mkaguzi wa Ndani***




Ni Mkaguzi wa Ndani katika baraza la Uwezeshaji kuanzia Mwezi Mei 2020, kabla ya kuhamia Baraza nilikua Mkaguzi wa Ndani , Risk champion na mjumbe wa CAMFED katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilala kuanzia July 2013 mpaka April 2020,Nimefanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe kama Mkaguzi wa Ndani kuanzia January 2011 mpaka June 2013, nikitokea katika Halmashauri ya Wilaya ya Makete nilikofanya kazi kama Mkaguzi wa Ndani kuanzia April 2010 mpaka December 2011.

### 1.8. MUUNDO NA WAFANYAKAZI WA SEKRETARIATI

Uratibu wa utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji na ufuatiliaji wake unafanywa na Sekretarieti ya Baraza ambayo inaongozwa na Katibu Mtendaji. Kwa mujibu wa Muundo mpya ulioidhinishwa na Serikali mwaka 2018, Katibu Mtendaji anasaidiwa na Wakurugenzi wawili na Wakuu wa Vitengo wanne kama inavyooneshwa kwenye mchoro hapa chini:


**Mchoro Na. 1: Muundo wa wafanyakazi wa Sekretariati**




Katika muundo huo mpya ulioidhinishwa na Serikali, Sekretarieti ya Baraza iliidhinishiwa kuwa na watumishi 57. Kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni,


2020 Sekretarieti ina watumishi 35, kati yao wanaume ni 25 na wanawake ni 10. Watumishi 32 ni wa ajira ya kudumu na malipo ya uzeeni, mtumishi 1 ni wa ajira ya mkataba, na watumishi 2 ni wa ajira ya muda maalum. Baraza pia linatekeleza mpango wa Serikali wa kutoa fursa kwa wahitimu wa vyuo vikuu kufanya mafunzo kwa vitendo (Interns). Kwa mwaka unaoishia 30 Juni, 2020 Baraza lilipokea vijana wa mpango huo wapatao 12. Mchoro ufuatao unaonesha idadi ya wafanyakazi waliopo kijinsia:

**Mchoro Na. 2: Wafanyakazi waliopo kijinsia**




Sekretariati ya Baraza ina muundo wa utekelezaji unaoainisha mtiririko wa uwajibikaji na wenye gharama nafuu ukilinganisha na muundo uliopita. Muundo mpya una Kurugenzi mbili zinazoongozwa na Wakurugenzi na Vitengo vinne vinavyoongozwa na Wakuu wa Vitengo. Watumishi wote wa Baraza wana sifa zinazokidhi mahitaji ya Baraza. Mafunzo ya mara kwa mara kwa ajili ya kuwajengea uwezo huwa yanatolewa kwa mujibu wa mpango wa mafunzo na hali ya kifedha ya Baraza. Watumishi wanashirikishwa katika maamuzi kupitia tawi la TUGHE lililopo hapa ofisini na Baraza la Wafanyakazi ambalo hukutana mara mbili kwa mwaka. Kupitia vyombo hivyo watumishi wanashirikishwa kikamilifu katika maamuzi. Idadi ya watumishi kwenye kila Kurugenzi na Kitengo kwa jinsia zao ni kama inavyooneshwa kwenye mchoro hapa chini:

**Mchoro Na. 3: Mgawanyo wa watumishi kwenye Idara Na Vitengo na jinsia zao**




### 1.9. UKAGUZI WA HESABU ZA BARAZA

Ripoti za fedha za kila mwaka zimekuwa zikikaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Baraza limekuwa likipata hati safi (*Unqualified Audit Opinion*) ya hesabu kwa kipindi chote cha utendaji kazi wake. Ukaguzi wa hesabu za mwaka 2018/19 umekamilika na kupata hati safi kama ilivyo kwa miaka iliyopita.

### 1.10. OFISI ZA BARAZA

Ofisi za Baraza kwa sasa zipo Mtaa wa Kivukoni wilaya ya Ilala Mkoani, Dar es Salaam. Baraza pia limeshirikiana na Halmashauri ya mji wa Kahama, mkoani Shinyanga kufungua kituo cha Uwezeshaji. Kituo hicho ni cha mfano kwa sasa kina taasisi 14 wezeshi ambazo zinatoa huduma. Jitihada za kuanzishwa vituo vya uwezeshaji kwenye mikoa iliyobaki zinaendelea.

## 2.0. HALI YA UKUAJI WA UCHUMI

### 2.1. UTANGULIZI


Serikali ya Tanzania imeendelea kutekeleza na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Jitihada mbalimbali zimetekelezwa ili kuboresha maisha ya wananchi na

uchumi wa nchi kwa ujumla. Lengo la Serikali ni kuwawezesha watanzania kumiliki sehemu kubwa ya uchumi wanchi ifikapo mwaka 2025.

### 2.2. PATO LA TAIFA

Uchumi wa Afrika ulitegemewa kukua kwa wastani wa 3.9% mwaka 2020 na 4.1% mwaka 2021. Ukuaji huo unachangiwa na nchi 6 kati ya 10 zenye uchumi unaokua zaidi katika kipindi hiki. Tanzania ni miongoni mwa nchi 6 za Afrika zinazoongoza katika ukuaji wa uchumi katika kipindi hiki. Nchi hizo pamoja na viwango vya ukuaji wa uchumi katika mabano ni Rwanda (9.4%), Ethiopia (7.4%), Ivory Coast (7.4%), Ghana (7.1%), Tanzania (6.8%) na Benin (6.7%). Mojawapo ya vigezo vya kupima ukuaji wa uchumi wa nchi husika ni Pato la Taifa. Pato halisi la Taifa la Tanzania lilikukua kwa 7.0% mwaka 2019 kama ilivyokuwa mwaka 2018. Kiwango cha ukuaji wa uchumi wa Tanzania katika kipindi hiki kilikuwa juu ya kiwango cha ukuaji wa uchumi kwa nchi ya Kenya (5.4%) na Uganda (4.9%), nchi pekee iliyoipita Tanzania ni Rwanda (9.4%). Sekta zilizokuwa na mchango mkubwa katika Pato la Taifa katika kipindi hiki ni pamoja na Kilimo (26.6%), Uchimbaji wa Madini na Mawe (17.7%), Ujenzi (14.1%), Sanaa na Burudani (11.2%) na Usafirishaji na Uhifadhi wa Mizigo (8.7%). Aidha, nakisi ya bajeti ya Serikali katika mwaka 2020 inatarajiwa kufikia 2.8%, mapato ya ndani 14.5% na mapato ya kodi 12.5% ya Pato la Taifa. Matarajio haya ni kutokana na matokeo ya awali kufuatia athari za mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu (unaosababishwa na Virusi vya CORONA) kwenye sekta mbalimbali. Ofisi ya Taifa ya Takwimu inachukua hatua madhubuti kuhakikisha kwamba, takwimu za mwenendo wa uchumi za jumla zinapatikana kwa wakati ili kuiwezesha Serikali na wadau wengine kufanya maamuzi sahihi (Wizara ya Fedha- Hotuba ya Bajeti, 2020). Kwa ujumla, Tanzania, nchi nyingine za Afrika pamoja na mataifa mengine duniani yameathirika na mlipuko wa Virusi vya CORONA na hivyo kupunguza kiwango cha kufikiwa kwa malengo ya ukuaji wa uchumi uliotegemewa. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2019 Tanzania ilikuwa kati ya 1/3 ya nchi za Afrika zilizokuwa na uchumi shirikishi zaidi na hivyo kuchangia katika kuboresha maisha ya wananchi wake. Pia, mikakati na juhudi mbalimbali za Serikali ya Tanzania hasa katika kuboresha miundo mbinu ya kiuchumi katika kipindi cha hadi kufikia mwezi Desemba 2019 zimechangia katika kuiwezesha Tanzania kuingia katika uchumi wa kati tarehe 1 Julai, 2020 ambapo ni miaka 5 kabla ya matokeo yaliyotarajiwa kwenye Maono ya Taifa ya mwaka 2025 (Benki ya Dunia, 2020).

**Mchoro Na. 4: Mwenendo wa Ukuaji wa Pato la Taifa Mataifa ya Afrika 2019-2020**





*Chanzo: Taarifa ya Hali ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa, 2020*

**Jedwali Na. 3: Nchi 10 za Afrika Zenye Uchumi Unaokua Zaidi 2019-2020**

| Nchi | Idadi ya watu | Pato la Taifa (GDP)-Bilioni za Marekani | Wastani wa kipato kwa mtu (per capita income) Dola za Marekani | Nafasi |
|---|---|---|---|---|
| Nigeria | 10,000,000 | 450 | 2,200 | 1 |
| Afrika Kusini | 58,600,000 | 360 | 6,100 | 2 |
| Misri | 100,000,000 | 300 | 3,000 | 3 |
| Algeria | 43,100,000 | 170 | 4,000 | 4 |
| Moroko | 36,500,000 | 120 | 3,300 | 5 |
| Kenya | 52,600,000 | 99 | 1,900 | 6 |
| Angola | 31,800,000 | 92 | 2,900 | 7 |
| Ethiopia | 112,000,000 | 91 | 800 | 8 |
| Ghana | 28,800,000 | 67 | 2,300 | 9 |
| Tanzania | 58,000,000 | 62 | 1,100 | 10 |

*Chanzo: Benki ya Maendeleo ya Afrika 2020.*

**Mchoro Na. 5 Pato la Taifa na Wastani wa Kipato kwa Mtu**




*Chanzo: Chanzo: Benki ya Maendeleo ya Afrika 2020.*

## MWENENDO WA UCHUMI KWA TANGU TANZANIA KUPATA UHURU

Tanzania imepata mafanikio makubwa kiuchumi kutokana na utekelezaji wa mipango ya maendeleo. Uchumi umekuwa ukikuakwa kasi, kwa wastani wa asilimia 6.9 kwa miaka minne iliyopita, ikiwa ni ukuaji mkubwa zaidi ikilinganishwa na miaka iliyopita na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi chache barani Afrika zinazokua kwa kasi zaidi.

**Jedwali Na. 4: Muhtasari wa Viashiria Mbalimbali vya Uchumi**

| Kipindi cha miaka | Pato la Taifa kwa Mwaka Husika (TZS) | Ukuaji wa Pato la Taifa (Asilimia) | Wastani wa Kipato cha Mtu kwa USD (GDP per capita) | Wastani wa Kipato cha Mtu kwa TZS (GDP per capita | Wastani wa Kipato cha Mtu kwa USD (GNI per capita) | Wastani wa mfumuko wa Bei (% |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1961 - 1985 | 32.7 Bilioni | 3.1 | 190.3 | 1 | | 18.6 |
| 1985 - 1995 | 1.2 Trilioni | 3.0 | 205.8 | 46 | 178.3 | 29.7 |
| 1995 - 2005 | 9.5 Trilioni | 5.7 | 311.2 | 277 | 365.0 | 8.8 |
| 2005 - 2015 | 52.9 Trilioni | 6.3 | 622.0 | 979 | 747.0 | 9.2 |
| 2015 - 2020 | 124.0 Trilioni | 6.9 | 1,063.3 | 2 | 1,010.0 | 4.3 |


*Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Benki Kuu ya Tanzania*

### 2.3. MFUMUKO WA BEI

Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kisera na kiutawala ili kuhakikisha kwamba mfumuko wa bei unabaki katika wigo wa tarakimu moja pamoja na kuboresha

mazingira mengine yenye kuleta unafuu kwa watanzania. Mwezi Machi, 2020 mfumuko wa bei ulikuwa 3.4% na ulichangiwa na kupungua kwa bei za vyakula kwenye maeneo mengi hapa nchini. Mfumuko wa bei katika kipindi cha miezi 12 iliyopita katika nchi jirani ya Kenya ulikuwa kwa wastani wa 5.82 na wastani wa 5.48 kwa mwezi Februari, 2020 ambapo uliongezeka kwa 1.17 kutoka wastani wa 4.65 mwezi Februari, 2019. Aidha, nchi ya Uganda ilishuhudia mfumuko wa bei katika miezi 12 ya mwaka 2019 ukifikia wastani wa 2.87% na 3.2 % mwezi Aprili, 2020. Kwa upande mwingine mfumuko wa bei nchini ulikuwa 3.2% ikilinganishwa na 3.5% katika kipindi kama hicho mwaka 2019 (*Benki Kuu ya Tanzania, 2020, 2019*). Kupungua kwa mfumuko wa bei kulichangiwa na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula na kushuka kwa bei ya mafuta katika soko la dunia kulikochangia kushuka kwa gharama za usafirishaji chakula pamoja na bidhaa nyingine muhimu katika kipindi hicho.

**Mchoro Na. 6: Pato la Taifa na wastani wa mfumuko wa Bei**





*Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu na Benki Kuu ya Tanzania*

## 2.4. HALI YA MAISHA YA WANANCHI

Jitihada za Serikali ya Tanzania katika kuinua maisha ya watanzania zimeendelea kuboresha upatikanaji wa huduma muhimu miongoni mwa watanzania pamoja na kuinua nguvu kazi na hivyo kuchangia katika kupunguza umaskini nchini. Jitihada hizi ziliwezesha kupungua kwa umaskini uliokithiri miongoni mwa watanzania kutoka 34.4 % mwaka 2007 hadi kufikia 26.4% mwaka 2018 na umaskini uliuokithiri kutoka 12% hadi kufikia 8% katika kipindi hicho kwa ujumla. Hata hivyo umaskini ulipungua kutoka 33.4 % mpaka 31.3% kwenye maeneo ya vijijini. Pia, kiwango cha umaskini kilikuwa kikubwa zaidi maeneo ya kanda ya Magharibi na ziwa na kiwango cha chini katika kanda ya Mashariki (Utafiti wa Hali ya Umaskini Tanzania Bara, Benki ya Dunia 2018). Kupungua huku kwa umaskini kumechangiwa na kupatikana kwa huduma za jamii kama vile maji, elimu, miundombinu ya masoko, afya na raslimali ambazo zimechangia zaidi kwenye kuboresha maisha ya watanzania. Pia, watanzania wengi wamejihusisha na

ujasiriamali na biashara mbalimbali ambazo zimewaongezea kipato na hivyo kuwawezesha kumudu mahitaji ya msingi ya familia.

**Mchoro Na. 7: Viwango vya umaskini Tanzania (%) mwaka 2007-2018**





*Chanzo: Taarifa ya Utafiti wa Kaya 2007,2011/12 na 2017/18 (NBS)*.

## 2.5. SEKTA YA FEDHA

Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali zenye lengo la kuboresha huduma za fedha nchini na kurahisisha upatikanaji wa mitaji ili kuwawezesha watanzania kushiriki vema katika shughuli za kiuchumi. Juhudi hizo ni pamoja na kutunga sera, sheria na kanuni mbalimbali pamoja na kufuatilia utekelezaji wake. Hadi kufikia mwezi Machi 2020, Serikali imekamilisha uandaaji wa Kanuni za Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018 ambapo zilianza kutumika rasmi mwezi Novemba 2019. Pia utekelezaji wa Mpango Maalum wa Elimu kwa Umma kuhusu sekta ya fedha umeanza kwa lengo la kujenga uelewa kwa wananchi kuhusu Sheria na Kanuni za sekta hiyo. Benki Kuu ya Tanzania kwa kushirikiana na wadau mbalimbali likiwemo Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi wameshiriki katika utoaji wa elimu hii. Aidha, Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha pamoja na Kanuni za Kumlinda Mtumiaji wa Huduma za Fedha zimeandaliwa, ili pamoja na kuongeza uelewa miongoni mwa wananchi, utekelezaji huu itasaidia katika kutambua mchango wa sekta ya fedha katika ukuaji wa uchumi na uboreshaji wa maisha ya watanzania kwa ujumla. Pia, ili kuweka mazingira rafiki kwa wakopaji nchini, Serikali kupitia Benki Kuu imetoa mikopo ya muda mfupi kwa benki za biashara; imenunua fedha za kigeni katika soko la ndani; imezipunguzia benki 17 za biashara kiwango cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu kutoka 8% hadi 7%; imeongeza wigo wa benki kutumia amana walizoweka Benki Kuu kutoka 10% hadi 20% mwezi Julai 2019; imeridhia mfumo wa kisheria wa makubaliano ya utoaji wa mikopo ya muda mfupi baina ya benki (*Global Master Repurchase Agreement - GMRA*) ili kuongeza ufanisi na ukwasi

katika masoko ya fedha (Wizara ya Fedha, 2020). Hatua hizi zilizochukuliwa na Serikali zimesaidia kuongeza kiwango cha ukwasi katika uchumi na kusababisha wastani wa amana za benki za biashara katika Benki Kuu (*clearing balances*) kufikia shilingi bilioni 628.8 kati ya Julai 2019 na Machi 2020 ikilinganishwa na wastani wa shilingi bilioni 462.7 kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Vile vile, wastani wa ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 ulifikia 9.0% ikilinganishwa na 6.5% kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Pia, mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka shilingi trilioni 18.6 Aprili mwaka 2019 mpaka trilioni 19.7 Aprili 2020 (Wizara ya Fedha, 2020). Aidha, kulingana na uchambuzi uliofanywa na Price water Coopers (2020) kiwango cha riba kwa wakopaji binafsi katika benki kimepungua kutoka wastani wa 17.16% hadi kufikia 16.85% kati ya mwezi Julai 2019 na Aprili, 2020. Uchambuzi huo pia umeonesha kuwa mikopo mingi (45%) iliyotolewa na taasisi za fedha katika kipindi kilichoishia Desemba 2019 ilikuwa ya biashara na ya watu binafsi na ilielekezwa zaidi katika sekta za kilimo (9.5% ya mikopo yote) ikilinganishwa na 5.6% katika kipindi hicho mwaka 2018.

**Mchoro Na. 8: Mikopo iliyotolewa katika baadhi ya sekta za uchumi**




*Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania, Jarida la Uchumi Robo inayoishia Desemba 2019 na 2017.*

## 3.0. SERA, SHERIA, KANUNI NA MIONGOZO

### 3.1. UTANGULIZI

Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni jitihada za makusudi zinazochukuliwa na nchi ili kuhakikisha wananchi wake wanashiriki kikamilifu katika uchumi wa nchi. Mmojawapo ya nyenzo ya kuwawezesha wananchi kiuchumi ni kupitia Sera na Sheria mbalimbali zinazotungwa na Serikali. Sera na Sheria zina nafasi kubwa ya kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi kushiriki kikamilifu katika sekta mbalimbali za uchumi.

Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2019/2020 Sheria na Kanuni mbalimbali zilitungwa na Sheria nyingine zilifanyiwa marekebisho. Aidha, Sheria zilizotungwa au kufanyiwa marekebisho na ambazo zinalenga kuwawezesha watanzania ni kama ifuatavyo:-

i. Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira, 2019
ii. Sheria ya Madini, Sura ya 123 imefanyiwa marekebisho na Sheria ya marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na 7, 2019
iii. Sheria ya Kodi la Ongezeko la Thamani , Sura ya 148, imefanyiwa marekebisho na Sheria ya marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na 6, 2019
iv. Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa, imefanyiwa marekebisho na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na 5, 2019
v. Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, imefanyiwa marekebisho na Sheria ya Marekebishoya Sheria Mbalimbali Na 5, 2019

#### 3.1.1. Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira, 2019

Sheria hii imeanzishwa chini ya Kifungu cha 55, Mfuko wa Taifa wa Maji. Mfuko huu utakuwa na jukumu la kutafuta vyanzo vya fedha na kuwezesha miradi ya uwekezaji kwa ajili ya kutoa huduma ya maji. Aidha, Mfuko huu utaweza kutoa mikopo nafuu kwa taasisi za maji na vikundi vya kijamii vinavyotoa huduma za maji kulingana na Sheria hii.

#### 3.1.2. Sheria ya Madini, 2010 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na 7, 2019

Sheria hii imeongeza Kifungu cha 86G ambacho kinaitaka kampuni yenye leseni kubwa ya Kutengeneza vito vya thamani *( large Lapidary Licence*) ambayo ni ya nje ihamishe ujuzi wa kutengeneza vito kwa watanzania. Lengo la kifungu hiki ni kuhakikisha watanzania wanaongezewa ujuzi katika eneo la kutengeneza vito ili kuwainua kiuchumi.

#### 3.1.3. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (Value Added Tax), Sura ya 148,

Sheria imefanyiwa marekebisho na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na 6, 2019 kwa kufanya mabadiliko ya kifungu cha 6 kwa kubadilisha kipengele kidogo cha 2. Mabadiliko hayo yamempa mamlaka Waziri kutoa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani kwa kutangaza kwenye Gazeti la Serikali kwenye vitu vifuatavyo:-

(a) Uagizaji wa malighafi zinazotumika kwa ajili tu ya uzalishaji wa vyandarua vya muda mrefu na wazalishaji wa ndani (Local Manufacturers) wenye mkataba wa utendaji (Performance Contract) na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(b) Taasisi ya Serikali inapoagiza bidhaa au huduma ambazo zitatumika kwa madhumuni tu ya kutekeleza mradi uliofadhiliwa na Serikali au kupitia mkopo wa *Consessional au* ufadhili kupitia mkataba baina ya Serkali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali nyingine, Mfadhili au Mkopeshaji; au mkataba wa ufadhili uliyoidhinishwa na Waziri kulingana na Sheria ya Serikali ya Mikopo, Ufadhili na Dhamana iliyoingiwa baina ya Serikali za Mitaa na Mfadhili; na

(c) Uagizaji au utoaji wa bidhaa au huduma kwa ajili ya kutoa nafuu kwenye majanga ya asili au majanga mengine.

#### 3.1.4. Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa, imefanyiwa marekebisho na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na 5, 2019

Kipengele cha 19 cha Sheria hii kimefanya marekebisho ya kipengele cha 4 cha Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa kwa kuongeza chini ya aya ya (i) majukumu ya Baraza kuwa ni pamoja na kuwezesha wasanii au kikundi cha Sanaa ambao ni raia wa Tanzania kupata mafunzo au ziara ya mafunzo ndani au nje ya Tanzania ili kuongeza ujuzi kwenye shughuli za sanaa chini ya aya (n). Aidha chini ya aya (o) Baraza limepewa jukumu la kutafuta na kusimamia vyanzo mbalimbali vya fedha kwa utaratibu utakaoidhinishwa na Waziri ili kuliwezesha Baraza kufanya shughuli zake na kuwawezesha wasanii kufanya shughuli zao za Sanaa.

#### 3.1.5. Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, imefanyiwa marekebisho na Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali Na 5, 2019

Kipengele cha 56 kimebadilisha kipengele cha 39 cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori kwa kubadilisha kipengele kidogo cha (3) (b) ambacho kinaeleza kwamba asilimia ya vitalu vya uwindaji kwa wakati wowote vitakavyotengwa kwa ajili ya maombi kutoka kwa kampuni za kitanzania itakuwa si chini ya asilimia 30 ya jumla ya vitalu vya uwindaji. Kipengele hicho kimeongeza pia kwamba hakuna Kanuni itakayozuia kampuni ya kitanzania kufanya maombi kwa ajili ya vitalu vya uwindaji vilivyotengwa kwa ajili ya maombi na kampuni zinazomilikiwa na wageni.
Aidha kipengele cha 3A kimeongezwa chini ya kipengele cha 3 ambacho kinatafsiri Kampuni inayomilikiwa na Watanzania kuwa ni kampuni iliyosajiliwa kulingana na Sheria za Tanzania na ambayo sehemu kubwa ya hisa zake zinamilikiwa na watanzania.

## 3.2. KANUNI

Wananchi wengi wa kipato cha chini wamekuwa wakitumia huduma za Taasisi ndogo za fedha ili kupata mitaji kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kiuchumi. Hata hivyo wananchi hao wamekuwa wakipata changamoto mbalimbali kutokana na huduma za Taasisi hizo ikiwemo riba kubwa za mikopo inayotolewa, wizi, na utaratibu usio mzuri wa kukusanya madeni ambao umesababisha wananchi kupoteza mali zao. Ili kukabiliana na changamoto hizi Serikali ilitunga Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha mwaka 2018 pamoja na Kanuni mahususi za biashara ya huduma ndogo za fedha za 2019 kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa Sheria husika. Kanuni zifuatazo zimetungwa ili kuweka masharti na utaratibu wa usimamizi na udhibiti wahuduma ndogo za fedha kwa madaraja tofauti yaliyoainishwa kwenye Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha:-

1. Kanuni ya Huduma Ndogo za Fedha (Watoa Huduma Ndogo za Fedha Wasiopokea Amana)

2. Kanuni ya Huduma Ndogo za Fedha (Vyama vya Ushirika na Akiba na Mikopo) 2019
3. Kanuni ya Huduma Ndogo za Fedha (Vikundi vya Huduma Ndogo za Fedha za Kijamii) 2019

### 3.2.1. Kanuni ya Huduma Ndogo za Fedha (Watoa Huduma Ndogo za Fedha Wasiopokea Amana)

Kanuni hizi ni kwa ajili ya Taasisi za Huduma Ndogo za Fedha zilizo katika daraja la 2 ambazo hazipokei amana. Kanuni hizi zinaeleza kwamba mtu yoyote anayetaka kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha kwenye daraja la 2 atatakiwa kuwasilisha maombi ya leseni Benki Kuu ya Tanzania. Kanuni hii imeweka vipengele ambavyo vinalenga kuhakikisha watanzania wanashiriki na kuongezewa ujuzi kwenye sekta hii ya huduma ndogo ya fedha. Kanuni hizo ni kama zifuatazo:-

a) Kanuni ya 6(4) imeainisha kwamba kama maombi ya leseni ya huduma ndogo ya fedha yatawasilishwa na taasisi inayotoa huduma inayomilikiwa na watu wa nje basi maombi hayo yatatakiwa yaambatanishwe pamoja na mambo mengine Mpango wa Mafunzo (*Training Plan*) unaoainisha muda maalum wa kuhamisha ujuzi wa huduma ndogo za fedha kwa wafanyakazi wa kitanzania. Aidha, pia atatakiwa kuambatanisha Mpango wa Urithishaji (*Succession Plan*) na mipango na mikakati inayoainisha muda na utaratibu ambao wafanyakazi wa kitanzania watachukua nafasi za uongozi wa juu kwenye taasisi hiyo.
b) Kanuni ya 18 imeainisha kwamba Taasisi ya Huduma Ndogo ya Fedha chini ya Daraja la 2 inatakiwa kuteua angalau wajumbe 2 wa kitanzania kwenye Bodi ya Wakurugenzi.
c) Kanuni ya 20(1) inaainisha kwamba Taasisi inayotoa huduma ndogo za fedha haitaruhusiwa kuajiri mtu ambaye si mtanzania au kumuongezea muda wa mkataba mfanyakazi ambaye si mtanzania mpaka iombe na kupata kibali kutoka Benki Kuu. Aidha, Kanuni ya 20(2) imeainisha kwamba idadi ya wafanyakazi ambao sio watanzania watakaoruhusiwa kuajiriwa kwenye Taasisi hizi katika muda wowote hawatazidi watano. Kanuni ya 20 (3) imeainisha mazingira ambayo wafanyakazi wa nje wanaweza kuzidi watano ikiwemo kukosekana kwa watanzania wenye ujuzi unaohitajika katika nafasi husika, ugumu wa kazi na majukumu husika, kupata idhini kutoka kwenye Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), mazingira ya dharura ambayo yatahitaji mtu wa ziada na muda ambao mtu wa ziada atatakiwa kukaa kwenye Taasisi ili kuhamisha ujuzi kwa watanzania.

### 3.2.2. Kanuni ya Huduma Ndogo za Fedha (Vyama vya Ushirika na Akiba na Mikopo (SACCOS)) 2019

Kanuni hizi ni kwa ajili ya watoa huduma ndogo za fedha waliopo kwenye daraja la tatu (3). Kanuni ya 4 imeanisha kwamba SACCOS yoyote haitaruhusiwa kufanya biashara ya huduma ndogo ya fedha bila kuwa na leseni iliyotolewa na Benki kuu au Mamlaka

iliyokasimishwa. Aidha, Benki Kuu imekasimisha jukumu la usimamizi wa watoa huduma ndogo za fedha katika daraja hili la tatu kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC). Kanuni hizi pamoja na masuala mengine imeainisha taratibu za kupata leseni, mitaji ya SACCOS ambayo kulingana na Kanuni ya 18(1) SACCOS za Daraja A zinatakiwa kuwa na mtaji wa Shillingi milioni 10 na SACCOS za Daraja B zinatakiwa kuwa na mtaji wa shilling milioni 200. Aidha Kanuni hizi pia zimeainisha utaratibu wa utoaji wa mikopo ambayo inatakiwa kuwa na uwazi, masuala ya Akaunti na Ukaguzi, usimamazi na ulinzi wa maslahi ya walaji (wanachama).

#### 3.2.3. Kanuni ya Huduma Ndogo za Fedha (Vikundi vya Huduma Ndogo za Fedha za Kijamii) 2019

Kanuni hizi ni kwa ajili ya watoa huduma ndogo za fedha waliopo kwenye daraja la nne(4) kulingana na Kanuni ya 2. Kanuni imeainisha utaratibu wa kuunda kikundi cha kijamii cha Huduma Ndogo za Fedha ambapo kulingana na Kanuni ya 4(2) Vikundi hivi vinaundwa na watu kuanzia kumi hadi hamsini. Kanuni ya 8(1) inavitaka Vikundi vya Kijamii vya Huduma Ndogo za Fedha kusajiliwa na Benki au Mamlaka iliyokasimishwa. Aidha, Benki Kuu imekasimu jukumu la usajili wa vikundi hivi kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kanuni hizi pia zimeainisha utaratibu wa uendeshaji wa vikundi hivi na masuala ya ufuatiliaji na mifumo ya ndani ya udhibiti.

### 3.3. MIONGOZO

#### 3.3.1. Mwongozo wa Ushiriki wa Watanzania katika Sekta Ndogo ya Mafuta,2019

EWURA kwa kushirikiana na Wadau wa Sekta ya Mafuta na Gesi asilia hapa nchini iliandaa Mwongozo ***(Petroleum (Local Content)Guidelines*****, 2019)** kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa Kanuni za Ushiriki wa Watanzania katika Sekta Ndogo ya Mafuta na hivyo kuongeza ushiriki wa watanzania kiuchumi kupitia fursa zinazojitokeza kwenye sekta ya mafuta na gesi asilia hapa nchini.

# 4.0. SEKTA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

## 4.1. UTANGULIZI

Ardhi ni rasilimali muhimu kwa jamii na matumizi yake ni mtambuka hivyo maendeleo katika sekta mbalimbali nchini yanategemea ardhi. Serikali inaendelea kuhakikisha ardhi inatumika kwa ajili ya kuongeza uwekezaji katika uzalishaji mali, kilimo, viwanda, ufugaji, uchimbaji madini, ujenzi wa miundombinu ya kimkakati ambayo itaongeza ajira, mapato na mauzo ya nje. Serikali inatambua na kuhakiki uwekezaji katika ardhi ili kutambua mchango wake katika uchumi wa nchi.

Sekta ya Ardhi imeendelea kuimarika na kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa kila mwananchi na Taifa kwa ujumla hasa kwa kuwa mhimili na kichocheo cha uwekezaji na uzalishaji katika sekta za kilimo, viwanda, ujenzi, mifugo, uvuvi, maliasili, nishati, madini na miundombinu, hivyo kuongeza ajira na kukuza pato la Taifa. Hali ya uendelezaji wa makazi nchini imeendelea kuimarika kwa kutekeleza programu na mikakati ya upangaji na urasimishaji makazi nchini. Serikali kupitia imeendelea kushirikiana na mamlaka za upangaji, sekta binafsi na washirika wa maendeleo katika kutekeleza kazi hizo. Vilevile, miongozo mbalimbali ya upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi imeendelea kuandaliwa na kusimamiwa.

Kuimarisha huduma za upimaji wa ardhi nchini kwa kusimika miundombinu ya mtandao mpya wenye alama za upimaji **831** nchi nzima zinazorahisisha upimaji wa ardhi ndani ya kilometa **40** imekuwa ni kipaumbele. Pamoja na juhudi hizi, usalama wa milki kwa wananchi kwa kurahisisha mifumo ya utoaji hati, utambuzi wa vipande vya ardhi mijini na vijijini na upatikanaji wa taarifa za wamiliki uliimarishwa. Vilevile, maboresho ya sera, sheria na kanuni mbalimbali zinazohusiana na sekta ya ardhi kwa lengo la kuimarisha utendaji kazi na utoaji huduma kwa wananchi yamefanyika.

## 4.2. HALI HALISI YA UTEKELEZAJI

### 4.2.1. Uandaaji na Usajili wa Hati

Upimaji, uandaaji na usajili wa Vyeti vya Ardhi ya Vijiji **2,905** ulifanyika na hivyo kuzipatia Halmashauri za Vijiji mamlaka ya usimamizi wa ardhi ya kijiji kwa mujibu wa sheria. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/20, hadi kufikia mwezi Aprili, 2020, jumla ya Vyeti vya Ardhi ya Kijiji **540** viliandaliwa. Hii inafanya kuwa na jumla ya vijiji **11,743** vilivyopimwa na kupewa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji kati ya vijiji **12,319** vilivyopo nchini. Vilevile, uandaaji na utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila **375,259** katika Halmashauri mbalimbali nchini ulifanyika. Hadi kufikia Aprili 2020, jumla ya Hati za Hakimiliki ya Kimila **92,585** zimetolewa. Kwa kipindi hicho jumla ya hati **1,516** zimetumika kama rehani ya mikopo yenye thamani ya shilingi **bilioni 61.3** kwenye taasisi za fedha.

Kwa kipindi cha miaka mitano, zilitolewa Hatimiliki **195,170,** na hati za umiliki wa sehemu ya jengo zipatazo **3,522** katika Halmashauri mbalimbali nchini. Aidha, hadi kufikia Aprili, 2020, jumla ya hatimiliki **37,870**, na hati za umiliki wa Sehemu ya Jengo zipatazo **310** zimetolewa. Vilevile zimesajiliwa rehani za ardhi **3,070** ambazo zimesaidia wananchi kupata mikopo na hivyo kuwanufaisha kiuchumi.

**Jedwali Na. 5: Usajili wa Vyeti vya Ardhi ya Kijiji (CVL) na Hati za Hakimiliki ya Kimila (CCRO) Zilizotolewa na Wizara na Wadau Wengine (2015/16 hadi 30 Aprili 2020)**

| MKOA | 2015/2016 | | 2016/2017 | | 2017/2018 | | 2018/2019 | | 2019/20 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | CVL | CCRO | CVL | CCRO | CVL | CCRO | CVL | CRO | CVL | CCRO |
| Arusha | 29 | 213 | 3 | 2782 | 8 | 783 | 9 | 202 | 79 | 1854 |
| Dar es salaam | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Dodoma | 5 | 102 | 11 | 198 | 12 | 1518 | 27 | 3217 | 4 | 1678 |
| Geita | 1 | 103 | 12 | 59 | 0 | 264 | 3 | 5 | 6 | 96 |
| Iringa | 178 | 1354 | 0 | 2578 | 23 | 26046 | 0 | 21249 | 7 | 2760 |
| Kagera | 32 | 2719 | 0 | 1360 | 0 | 863 | 1 | 467 | 2 | 1892 |
| Katavi | 0 | 0 | 15 | 6021 | 7 | 214 | 25 | 1900 | 8 | 1486 |
| Kigoma | 0 | 0 | 26 | 2911 | 22 | 1310 | 9 | 2199 | 0 | 3936 |
| Kilimanjaro | 9 | 167 | 2 | 276 | 49 | 275 | 0 | 103 | 60 | 1372 |
| Lindi | 0 | 22 | 2 | 1038 | 0 | 613 | 0 | 634 | 99 | 415 |
| Manyara | 4 | 98 | 5 | 534 | 5 | 1156 | 8 | 979 | 25 | 1055 |
| Mara | 103 | 71 | 31 | 0 | 5 | 251 | 6 | 52 | 94 | 866 |
| Mbeya | 153 | 399 | 1 | 94 | 0 | 269 | 2 | 289 | 0 | 10,837 |
| Morogoro | 2 | 22 | 45 | 13128 | 103 | 33,329 | 64 | 129,150 | 31 | 56,558 |
| Mtwara | 0 | 1044 | 5 | 401 | 9 | 661 | 3 | 360 | 48 | 194 |
| Mwanza | 10 | 96 | 108 | 0 | 2 | 301 | 58 | 215 | 3 | 122 |
| Njombe | 186 | 172 | 0 | 2 | 0 | 64 | 0 | 619 | 0 | 311 |
| Pwani | 28 | 943 | 7 | 912 | 3 | 385 | 0 | 1537 | 4 | 213 |
| Rukwa | 54 | 44 | 0 | 0 | 0 | 55 | 0 | 92 | 0 | 429 |
| Ruvuma | 23 | 96 | 0 | 4 | 0 | 473 | 60 | 392 | 0 | 1020 |
| Shinyanga | 11 | 0 | 19 | 136 | 30 | 357 | 0 | 215 | 0 | 15 |
| Simiyu | 0 | 213 | 197 | 184 | 3 | 302 | 0 | 335 | 4 | 2227 |
| Singida | 0 | 2059 | 0 | 2040 | 15 | 343 | 2 | 569 | 4 | 39 |
| Songwe | 38 | 176 | 0 | 35 | 27 | 142 | 0 | 913 | 56 | 2457 |
| Tabora | 0 | 0 | 11 | 68 | 19 | 245 | 29 | 475 | 0 | 583 |
| Tanga | 284 | 778 | 5 | 245 | 27 | 80 | 35 | 310 | 6 | 170 |
| | **1,150** | **10,891** | **505** | **35,006** | **369** | **70,299** | **341** | **166,478** | **540** | **92,585** |
| **JUMLA KWA MIAKA MITANO (2015/16 - 2019/20)** | | | | | | **CVL** | **2,905** | | | |
| | | | | | | **CCRO** | **375,259** | | | |

#### 4.2.2. Usimamizi wa Masharti ya Umiliki

Sheria za Ardhi zinamtaka kila mmiliki kuiendeleza ardhi aliyomilikishwa kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika nyaraka za umiliki. Kwa kipindi cha miaka mitano, mashamba **1,985** yalikaguliwa ili kujiridhisha uendelezaji wake. Aidha, mashamba **45** yenye jumla ya ekari **121,032.2** yalibatilishwa umiliki wake baada ya kukiuka masharti ya umiliki. Kati ya ekari hizo zilizobatilishwa ekari **12,448.5** zilitengwa kwa ajili ya uwekezaji na sehemu kuandaliwa mipango ya matumizi mengine na kugawiwa kwa wananchi kupitia mamlaka za upangaji.

#### 4.2.3. Uthamini wa Mali

Uthamini wa mali zinazohamishika na zisizohamishika, na uidhinishaji wa taarifa za uthamini ni miongoni mwa majukumu yanayotekelezwa. Uthamini hufanyika ili kuwezesha ulipaji wa fidia, utozaji wa ushuru wa Serikali unaotokana na mauzo au uhamisho wa umiliki wa mali, utozaji wa malipo ya awali (*premium*) wakati wa kutoa milki, mizania, kuweka mali rehani kwa ajili ya kupata mikopo, mirathi, kinga ya bima na utozaji kodi ya pango la ardhi.

Kwa kipindi cha miaka mitano, taarifa za uthamini wa kawaida wa mali **52,645** na uthamini wa fidia wa mali **84,223** uliidhinishwa. Katika kipindi hicho, Wizara pia imeshiriki kufanya uthamini wa mali katika maeneo ya miradi mikubwa ya kitaifa na ya kimkakati. Katika miradi hiyo jumla ya wafidiwa **9,881** na fidia ya mali kiasi cha shilingi bilioni **113.9** ziliandaliwa na kuidhinishwa.

#### 4.2.4. Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi nchini

Serikali imeendelea kushughulikia migogoro ya ardhi ambayo imekuwa kero kubwa nchini kadri inavyojitokeza kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Migogoro hiyo ipo katika sura mbili ambazo ni migogoro ya mipaka ya kiutawala na migogoro inayotokana na mwingiliano wa matumizi ya ardhi. Sheria za ardhi zimeweka utaratibu wa namna ya kushughulikia migogoro ya ardhi na pale inaposhindikana migogoro hiyo hupelekwa katika ngazi ya mahakama kutatuliwa.

Kwa kipindi cha miaka mitano, Serikali iliweka mikakati mbalimbali ya kushughulikia utatuzi wa migogoro. Mikakati hiyo ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu utatuzi wa migogoro, kuanzisha madawati ya malalamiko katika ofisi za ardhi za halmashauri nchini, na programu ya '**Funguka kwa Waziri'.** Kupitia mikakati hiyo jumla ya migogoro **15,808** ilitatuliwa kwa njia ya kiutawala katika halmashauri mbalimbali nchini. Pia, jumla ya migogoro **131,603** ya matumizi ya ardhi ilitatuliwa kupitia Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

**a. Kamati ya Mawaziri wa Kisekta kutafuta ufumbuzi wa kudumu**

Kutokana na kukithiri kwa migogoro ya ardhi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli aliunda Kamati ya Mawaziri wa Kisekta ili kutafuta ufumbuzi wa kudumu. Kufuatia mapendekezo ya Kamati, Baraza la Mawaziri mnamo mwezi Septemba, 2019, liliridhia kuwa vijiji **920** kati ya vijiji **975** vilivyokuwemo ndani ya hifadhi, mapori ya akiba na ranchi kuhalalishwa rasmi kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji na kijamii. Aidha, Serikali inaendelea kufanya tathmini ya vijiji **55** vilivyobaki ili kutoa maamuzi. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta na wadau mbalimbali inaendelea kuhakiki mipaka, kupanga na kupima ili kuzipa Serikali za vijiji mamlaka ya kusimamia ardhi za vijiji hivyo.


**b. Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi**

Kamati ya Taifa ya Ugawaji Ardhi ina jukumu la kuidhinisha maombi ya umilikishaji ardhi kwa ajili ya uwekezaji, uendelezaji fukwe, pamoja na maeneo ya kimkakati yenye maslahi ya umma. Katika kipindi cha miaka mitano, Kamati ilipokea na kuidhinisha jumla ya maombi **527** ya umilikishaji ardhi. Maombi **331** yalikuwa ya uwekezaji na **196** ya viwanja vya fukwe, ofisi za Balozi na Mashirika ya Kimataifa.

#### 4.2.5. Upimaji wa Viwanja na Mashamba

Serikali imeendelea kuratibu na kusimamia upimaji wa viwanja na mashamba unaofanywa na Mamlaka za Upangaji na sekta binafsi. Upimaji huu umewezesha wananchi na taasisi mbalimbali kupata hatimiliki za ardhi na kutatua migogoro ya ardhi. Katika kipindi cha miaka mitano, ramani za upimaji zenye viwanja **988,526** na mashamba **5,940** kutoka Halmashauri mbalimbali nchini kama mchoro unavyoonesha hapo chini zilidhinishwa.

**Mchoro Na. 9: Upimaji wa viwanja na mashamba**



Sambamba na hili, katika kufanikisha utekelezaji wa dhana ya viwanda nchini Tanzania, jumla ya ekari **284,349.07** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda katika miji mbalimbali nchini iliyoandaliwa mipango kabambe. Aidha, Serikali itaendelea kufuatilia utekelezaji wa mipango kabambe kwa mujibu wa sera, sheria, kanuni na miongozo iliyopo.

#### 4.2.6. Urasimishaji Makazi

Urasimishaji makazi nchini unahusisha kutambua, kupanga, kupima na kumilikisha maeneo yaliyoendelezwa bila kupangwa. Lengo la urasimishaji ni kuhakikisha usalama wa milki na kuwezesha upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya huduma za kijamii na miundombinu kwa njia shirikishi. Vilevile, katika kipindi cha miaka mitano, michoro ya Mipangomiji ya urasimishaji yenye viwanja **703,836** ambapo viwanja **419,240** vilikuwa vya makampuni binafsi iliidhinishwa**.**

#### 4.2.7. Mikopo ya ujenzi wa nyumba

Upatikanaji wa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba imeboreshwa kama ifuatavyo:-

i. Mikopo midogo midogo ya ujenzi wa nyumba kutoka taasisi za fedha kiasi cha shilingi **bilioni 29.87** kilitolewa kwa wananchi **1,914**


ii. Benki za biashara zinazotoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zimeongezeka kutoka tatu (**3**) hadi **34** ambapo, mikopo ya nyumba yenye thamani ya shilingi **bilioni 438.58** ilitolewa kwa wananchi **5,460**

iii. Kiwango cha riba ya mikopo ya ujenzi wa nyumba katika taasisi za fedha kimeshuka kutoka kati ya asilimia **21-23** hadi kufikia kati ya asilimia **13-18**;

iv. Muda wa kurejesha mikopo midogo midogo umeongezwa kutoka miaka mitano (**5**) hadi **10**.

Hadi kufikia mwezi Aprili, 2020, taarifa za waendelezaji na wasimamiaji milki **139** ambao wamejenga jumla ya nyumba **26,421** zimeingizwa katika kanzidata ya nyumba. Aidha, Vyama vya Ushirika wa Nyumba vinne (4) vimeongezeka katika kanzidata na kufikia vyama vilivyo hai **38** ambavyo vimejenga jumla ya nyumba **1,056** katika Mikoa ya Dar es Salaam (**818**), Dodoma (**77**), Iringa (**16**), Kagera (**56**), Musoma (**22**), Morogoro (**36**), Mwanza (**15**) na Shinyanga (**16**) kama mchoro hapo chini unavyoonyesha.

**Mchoro Na. 10: Idadi ya Nyumba zilizojengwa na vyama vya ushirika wa nyumba**





### 4.3. MRADI WA KUPANGA, KUPIMA NA KUMILIKISHA ARDHI

Katika kipindi cha miaka mitano, Programu hii yenye lengo la kuhakikisha uwezeshaji wa milki salama kwa wananchi imetekelezwa. Kiasi cha shilingi bilioni **10.8** zilitolewa na Serikali kutekeleza mradi ambapo shilingi bilioni **8.36** zilitolewa ili kuwezesha upangaji, upimaji, umilikishaji, ununuzi wa vifaa na ulipaji wa fidia katika Halmashauri **27** nchini. Jumla ya viwanja **37,351** vilipimwa na hatua za umilikishaji wake zinaendelea. Aidha, jumla ya shilingi bilioni **2.44** zilitumika kuandaa mpango kabambe wa Jiji la Dodoma, kuandaa mipangokina ya vitovu vya vijiji katika vijiji vitano (5) katika Wilaya ya Morogoro na kutoa hati za Hakimiliki za Kimila **5,845.** Vilevile vipande vya ardhi **134,239** vilitambuliwa na leseni za makazi **868** zilitolewa katika jiji la Dar es Salaam.

### 4.4. MRADI WA KUWEZESHA UMILIKISHAJI WA ARDHI

Programu ya Kuwezesha Umilikishaji Ardhi *(Land Tenure Support Programme)* imetekelezwa katika Halmashauri za Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi kuanzia Januari, 2016 kwa kushirikiana na mashirika ya maendeleo ya Serikali za Uingereza (DFID), Sweden (SIDA), na Denmark (DANIDA). Programu imewezesha uandaaji wa Mipango mitatu (**3**) ya Matumizi ya Ardhi ya Wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi. Mipango hiyo imebainisha mgawanyo wa rasilimali mbalimbali katika kila Wilaya. Jumla ya mipaka ya vijiji **129** imepimwa katika Wilaya za Kilombero (**65**), Ulanga (**42**) na Malinyi (**22**). Pia, jumla ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Vijiji **119** imetayarishwa katika Wilaya za Kilombero (**50**), Ulanga (**42**) na Malinyi (**27**). Wataalam **32** wa Halmashauri hizo wamejengewa uwezo kuhusu uandaaji na usimamizi wa mipango hiyo.

Kama mchoro unavyoonyesha hapa chini Programu imewezesha utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila **182,126** kwa wananchi katika wilaya za Kilombero (**76,750**), Ulanga (**62,055**) na Malinyi (**43,321**). Hati hizo zimewawezesha wananchi kuzitumia kama dhamana kwa ajili ya kupata mikopo yenye thamani ya takriban shilingi bilioni **1.64** kutoka benki za CRDB, NMB na TADB. Sehemu kubwa ya wanufaika wa mikopo hiyo wameitumia mikopo yao kuwekeza katika shughuli za kilimo na biashara.




**Mchoro Na. 11: Hati za Hakimiliki za kimila**

Programu hii pia imewezesha ujenzi wa ofisi za ardhi za Halmashauri za wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi. Vilevile, jumla ya vijiji **75** vimewezeshwa kukarabati masjala za ardhi za vijiji kwa ajili ya kutunza nakala za hati zilizoandaliwa. Wajumbe **641** wa Mabaraza ya Kata **66** na wajumbe **1,102** wa Mabaraza ya Ardhi ya Vijiji katika vijiji **129** wamejengewa uwezo kuhusu utatuzi wa migogoro ya ardhi. Aidha, Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Na. 2 ya 2002 na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya 1999 zilitafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuwawezesha wananchi kuelewa zaidi sheria na kanuni za sekta ya ardhi, ambapo nakala **15,000** zilichapishwa na kugawiwa kwa wananchi.

### 4.5. MRADI WA KUWEZESHA USHINDANI WA SEKTA BINAFSI (SEKTA YA ARDHI)


Mradi huu ulianza kutekelezwa chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu kwa madhumuni ya kuboresha mazingira ya biashara nchini. Kwa upande wa sekta ya ardhi, mradi ulilenga mambo ya msingi yafuatayo:-

i. Kuimarisha utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kwa kusanifu na kutengeneza mfumo unganishi wa kielektroniki wa taarifa za ardhi,
ii. Ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi,
iii. Ununuzi wa vifaa vya kisasa vya upimaji na uwekaji wa alama za msingi za upimaji.

Kwa kipindi cha miaka mitano, mradi umewezesha kuundwa na kusimikwa kwa mfumo wa taarifa ILMIS katika Mkoa wa Dar es Salaam. Jumla ya kumbukumbu za majalada yenye taarifa **728,370** za usajili wa hati; upimaji na umilikishaji wa ardhi yamebadilishwa kutoka mfumo wa analojia na kuwa wa kidijitali. Viwanja **239,317** viliingizwa kwenye mfumo wa ILMIS na hatimiliki za ardhi **3,868** ziliandaliwa na kutolewa kwa njia ya kielektroniki. Jumla ya miamala **254,944** ilifanyika kupitia huu mfumo. Uanzishwaji wa mfumo wa ILMIS umehusisha pia ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu za Ardhi kilichopo jijini Dar es Salaam ambacho kinatumika kuhifadhi kumbukumbu zote za ardhi kwa njia ya kielektroniki kwa nchi nzima. Vilevile, mradi huu umewezesha ununuzi wa vifaa vya kisasa vya upimaji vilivyosambazwa katika Ofisi za Ardhi za Mikoa na uwekaji wa mtandao wa alama za msingi ardhini.

### 4.6. MRADI WA UZALISHAJI UMEME WA JULIUS NYERERE (JNHPP)

Katika uendelezaji wa eneo la mradi wa uzalishaji umeme wa Julius Nyerere, Serikali inaendelea kuandaa mpango wa uendelezaji wa ukanda wa mradi (Corridor Development Plan) utakaowezesha mamlaka za upangaji kuandaa mipangokina katika miji midogo na mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji katika ukanda huu. Hadi kufikia 30 Aprili, 2020 jumla ya mipangokina **19** yenye viwanja **4,309** iliandaliwa katika mji mdogo wa Kisaki na upimaji unaendelea. Aidha, mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji cha Mloka wenye matumizi ya Makazi, uwekezaji, hifadhi za wanyamapori, utalii, kilimo, misitu na vyanzo vya maji uliandaliwa.




**Mchoro Na. 12:**

Katika mpango huo jumla ya viwanja **1,342** vimepangwa kwa ajili ya makazi (**1,110**), biashara (**217**), hoteli za kitalii (**15**) na matumizi mengine. Shughuli nyingine ni uwekaji alama za Upimaji ardhi nne (**4**) kwa ajili ya ujenzi wa bwawa na upimaji wa hekta **1,402** za eneo la kujenga mitambo ya umeme kwenye maporomoko ya Mto Rufiji na hekta **4,711** kwa ajili ya ujenzi wa karakana na makazi ya mradi wa umeme.

### 4.7. MRADI WA UJENZI WA RELI YA KISASA

Kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Taasisi mbalimbali imeandaliwa rasimu ya awali ya mpango wa uendelezaji wa ukanda wa mradi (Corridor Development Plan). Mpango huu utawezesha mamlaka za upangaji kuandaa mipangokina katika maeneo ya miji na mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya vijiji. Maeneo yote yaliyopendekezwa kuwa vituo vya treni na kwa matumizi mengine yanayohusiana na reli, yametambuliwa na taratibu za kisheria za kuyatangaza kuwa maeneo ya kimipangomiji zinaendelea.

### 4.8. MRADI WA UJENZI WA BOMBA LA MAFUTA

Kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta na Taasisi mbalimbali imeandaliwa rasimu ya awali ya mpango wa uendelezaji ukanda wa mradi wa Bomba la Mafuta. Mpango huu utawezesha mamlaka za upangaji kuandaa mipangokina katika maeneo ya miji na mipango ya matumizi ya ardhi katika maeneo ya vijiji. Mamlaka za Upangaji za Wilaya za Misenyi, Bukombe, Kondoa, Handeni na Muheza zimeandaa Mipangokina katika maeneo yatakayojengwa kambi na mitambo ya mafuta. Mipangokina iliandaliwa kama ifuatavyo: Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi viwanja **306** vimepangwa na kupimwa katika eneo la Bulifani; Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe viwanja **341** katika eneo la Bukombe mjini; Halmashauri ya Kondoa viwanja **794** katika eneo la Serya; Halmashauri ya Muheza viwanja **185** katika eneo la Komoza na viwanja **144** katika eneo la Kwedigongo pamoja na eneo lenye ukubwa wa ekari **44.93** katika eneo la Tanganyika, Halmashauri ya Wilaya ya Muheza.

Sanjari na hayo, uchambuzi wa maandalizi ya mipango ya matumizi ya ardhi kwa vijiji 236 vinavyopitiwa na Bomba la Mafuta (EACOP) umefanyika.

# 5.0. USHIRIKA


## 5.1. UTANGULIZI

Vyama vya Ushirika ni moja ya nyenzo muhimu ya kuwakwamua wananchi kiuchumi. Vyama vya Ushirika huanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika namba 6 ya mwaka 2013 na husimamiwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania *(Tanzania Cooperatives Development Commission-TCDC)* ambayo inajukumu la kuhamasisha maendeleo uya ushirika, udhibiti na usimamizi wa shughuli za vyama vya ushirika.

## 5.2. IDADI NA AINA YA VYAMA VYA USHIRIKA

Hadi kufikia Desemba mwaka 2019, kwa mujibu wa daftari la kudumu la vyama vya ushirika (rejista), kulikuwa na jumla ya vyama vya ushirika 11,626. Kati ya hivyo, AMCOS 3,835; Ufugaji wa nyuki 56; Walaji 98; Uvuvi 121; Miradi ya ubia 40; Nyumba 31; viwanda 91; Umwagiliaji 82; Ufugaji 238; Madini 98; Akiba na Mikopo 6,178; Huduma 121; Usafirishaji 17; vyama vikuu (Union) 56; Benki 1 na vyama vya aina nyingine 563. Kwa ujumla vyama hivyo vilikuwa na wanachama 5,880,736.

**Mchoro 13: Idadi ya Vyama vya ushirika katika asilimia kwa sekta, hadi kufikia Desemba 2019**




## 5.3. HALI YA VYAMA VYA USHIRIKA

Hali ya vyama vya ushirika ikilinganishwa na takriban mwaka mmoja uliopita inaonesha ongezeko la vyama 295 (asilimia 2.6). Mlinganisho wa takwimu za vyama vya ushirika

kwa kipindi cha Februari mwaka 2019 hadi Desemba 2019 umeoneshwa kwenye Jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 6: Mlinganisho wa vyama vya ushirika kwa kipindi cha Februari mwaka 2019 hadi Desemba 2019**

| Na. | AINA YA USHIRIKA | FEBRUARI 2019 | DESEMBA 2019 | ONGEZEKO/ PUNGUFU | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | AMCOS | 3,719 | 3,835 | 116 | 3.1 |
| 2 | SACCOS | 6,137 | 6,178 | 41 | 0.7 |
| 3 | HUDUMA | 144 | 121 | -23 | -16.0 |
| 4 | MADINI | 94 | 98 | 4 | 4.3 |
| 5 | MIFUGO | 181 | 238 | 57 | 31.5 |
| 6 | MULTPURPOSE | 24 | 0 | -24 | -100.0 |
| 7 | NYUKI | 20 | 56 | 36 | 180.0 |
| 8 | NYUMBA | 19 | 31 | 12 | 63.2 |
| 9 | UMWAGILIAJI | 25 | 82 | 57 | 228.0 |
| 10 | VYAMA VIKUU (UNION) | 46 | 56 | 10 | 21.7 |
| 11 | USAFIRISHAJI | 16 | 17 | 1 | 6.3 |
| 12 | UVUVI | 687 | 121 | -566 | -82.4 |
| 13 | VIWANDA | 30 | 91 | 61 | 203.3 |
| 14 | WALAJI | 36 | 98 | 62 | 172.2 |
| 15 | BENKI | 0 | 1 | 1 | #DIV/0! |
| 16 | MIRADI YA PAMOJA | 34 | 40 | 6 | 17.6 |
| 17 | VYAMA VINGINE | 119 | 563 | 444 | 373.1 |
| | **JUMLA** | **11,331** | **11,626** | **295** | **2.6** |

**Hali ya wanachama wa vyama vya ushirika, hisa akiba na mikopo**

Kufikia Desemba 2019 Wanachama wa vyama vyote vya ushirika waliongezeka na kufikia 5,880,736 ikilinganishwa na idadi ya wanachama 3,998,193 Februari mwaka 2019. Aidha, kwa kipindi hicho hisa kwenye SACCOS ziliongezeka kwa asilimia 12.5, akiba kwenye SACCOS iliongezeka kwa asilimia 23 na mikopo iliyotolewa kwenye SACCOS iliongezeka kwa asilimia 15.49. Ufafanuzi zaidi umetolewa kwenye Jedwali hapa chini.


***Jedwali Na. 7: Hali ya wanachama, hisa akiba na mikopo***

| Na | WANACHAMA, AKIBA NA MIKOPO | FEBRUARI 2019 | DESEMBA 2019 | ONGEZEKO/PUNGUFU | % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Wanachama (vyama vyote) | 3,998,193 | 5,880,736 | 1,882,543 | 47.1 |
| 2 | Hisa-SACCOS | 78,751,193,414 | 88,603,751,985 | 9,852,558,571 | 12.5 |
| 3 | Akiba-SACCOS | 538,413,737,576 | 663,777,390,907 | 125,363,653,331 | 23.28 |
| 4 | Mikopo tolewa-SACCOS | 1,299,661,801,996 | 1,500,943,078,69 | 201,281,276,703 | 15.49 |

## 5.4. UDHIBITI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA NCHINI


Hadi kufikia Februari 2020 jumla ya vyama vya ushirika 2,964 (sawa na asilimia 44 ya lengo lililowekwa la kukagua vyama 6,613) vilikuwa vimekaguliwa. Pia, kupitia Shirika la ukaguzi na Usimamizi wa Vyama Vya Ushirika nchini (Cooperative Audit and Supervision Corporation-COASCO) jumla ya vyama vya ushirika 3,160 (sawa na asilimia 48 ya lengo lililowekwa la kukagua vyama 6,613) vilifanyiwa ukaguzi wa nje.

**Mchoro Na. 14: Ukaguzi wa vyama vya ushirika kwa asilimia kufikia Februari 2019**



Kati ya vyama vya ushirika 3,160 vilivyofanyiwa ukaguzi wa nje, vyama 69 (sawa na asilimia 2.18) vilipata hati inayoridhisha. Vyama 1,545 (sawa na asilimia 48.89) vilipata hati yenye shaka. Vyama 330 (sawa na asilimia 10.44) vilipata hati isiyoridhisha na vyama 1,216 (sawa na asilimia 38.48) vilipata hati mbaya.

**Mchoro Na. 15: Hati ya ukaguzi wa Vyama vya ushirika katika asilimia**




Katika jitihada za kudhibiti wizi na ubadhirifu katika Ushirika nchini, Serikali ya Awamu ya Tano imefanikiwa kurejesha mali zilizokuwa za Vyama Vikuu Vya Ushirika ikiwemo NCU (1984) Ltd cha Mwanza, SHIRECU (1984) Ltd cha Shinyanga, KNCU cha Mkoani Kilimanjaro na shirika lake tanzu la TCCco zilizouzwa kinyume na utaratibu. Jumla ya mali nane (8) za NCU (1984) Limited na mali mbili (2) za SHIRECU (1984) Limited ambazo ni nyumba za makazi, maghala, viwanda na viwanja viliuzwa kinyume cha sheria na taratibu za manunuzi bila kuzingatia thamani halisi ya mali husika.

Aidha, baada ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kukabidhiwa ripoti ya ukaguzi wa Vyama vya Ushirika ya mwaka 2018/2019 ambayo ilibaini ubadhilifu wa zaidi ya shilingi Bilioni 124.5, uchunguzi ulifanyika na shilingi bilioni 8.8 za Wanaushirika ziliokolewa.

## 5.5. MAFANIKIO

Ushirika umefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika kuwahudumia wananchi. Hali hiyo imejidhihirisha katika zao la korosho, tumbaku, kahawa, pamba ,n.k. Aidha, idadi ya vyama vya ushirika iliongezeka kutoka vyama 11,331 Februari mwaka 2019 hadi kufikia vyama 11,626 Desemba, 2019. Pia, thamani ya mikopo iliyotolewa na vyama vya akiba

na mikopo (SACCOS) iliongezeka kutoka shilingi trilioni 1.3 Februari, 2019 hadi kufikia shilingi trilioni 1.5 Desemba 2019. Aidha, thamani ya hisa iliongezeka kutoka shilingi bilioni 78.8 Februari, 2019 hadi kufikia shilingi bilioni 88.6, Desemba 2019. Akiba kwenya SACCOS iliongezeka kutoka shilingi bilioni 538.4, Februari, 2019 hadi kufikia shilingi bilioni 663.8 Desemba 2019. Mafanikio hayo na mengine mengi ni matokeo ya jitihada za Serikali za kuimarisha ukaguzi na udhibiti wa vyama vya ushirika nchini kwa lengo la kuakisi dhana ya uwazi, uwajibikaji na utawala bora katika kuendeleza ushirika nchini.

## 5.6. VIWANDA VILIVYOANZISHWA NA VYAMA VYA USHIRIKA

Vyama vya ushirika vimeanzisha viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Jumla ya viwanda 78 vidogo na vya kati vimeanzishwa na kufufuliwa ili kutumika kuchakata mazao ya mpunga, pamba, mahindi, alizeti na utengenezaji wa bidhaa kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 8: Idadi ya viwanda vilivyoanzishwa na vyama vya ushirika**

| Na. | MKOA | IDADI YA VIWANDA |
|---|---|---|
| 1. | Mwanza | 7 |
| 2. | Mbeya | 35 |
| 3. | Arusha | 8 |
| 4. | Kagera | 4 |
| 5. | Manyara | 4 |
| 6. | Tanga | 7 |
| 7. | Dar es salaam | 10 |
| 8. | Kahama – Shinyanga | 1 |
| 9. | Geita | 2 |
| | **JUMLA** | **78** |

## 5.7. KUIMARISHA MASOKO KATIKA VYAMA

Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeimarisha masoko na uwekezaji kwenye mifumo ya kimasoko kama vile stakabadhi za ghala, soko la bidhaa (Commodity Exchange) na kilimo cha mkataba. Masoko ya mazao yafuatayo yaliimarika kupitia mifumo hiyo:

**Jedwali Na. 9: Mazao katikia mikoa na bei zake**

| **Na.** | **ZAO** | **MIKOA** | **KIASI** | **Tshs** |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ufuta | Ruvuma, Lindi, Manyara, Dodoma | Tani 146,833,022 | 33,125,379,110 |
| 2. | Kakao | Mbeya | Kilo 21,885,595 | 111,747,851,644 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3. | Maziwa | Mbeya, Songwe, Tanga | Lita 15,186,093 | 11,605,725,807 |
| 4. | Pamba | Mwanza, Katavi, Shinyanga, Mara, Simiyu, Singida, Manyara, Kagera Dodoma | Tani 378,956 | 343,682,175,916,800 |
| 5. | Chai | Mbeya, Njombe, Iringa, Tanga, Kagera, Kilimanjaro | Tani 9,119,436 | 480,449,760,470 |
| 6. | Tumbaku | Katavi, Mbeya, Tabora, Kigoma, Shinyanga, Geita, Kagera, Iringa, Ruvuma | Kilo 140,000,000 | 489,440,000,000 |
| 7. | Korosho | Lindi, Mtwara, Ruvuma, Tanga, Pwani | Tani 224,247,551 | 575,416,173,690 |
| 8. | Kahawa | Mbeya, Kigoma, Kagera | Tani 41,246,581 | 55,695,997,900 |
| 9. | Zabibu | Dodoma | Kilo 1,500,000 | 1,800,000,000 |
| 10. | Choroko | Shinyanga, Tabora, Mwanza, Singida | Kilo 256,306 | 333,197,800 |
| | | | | |

## 5.8. CHANGAMOTO

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na maendeleo ya Ushirika nchini bado zipo changamoto zinazokwamisha maendeleo kwenye ushirika kwenda kwa kasi zaidi. Baadhi ya changamoto ni pamoja na:

i. Baadhi ya viongozi wa vyama vya ushirika kutenda kinyume na matarajio ya wanachama wao, kinyume na sheria ya ushirika, kanuni na miongozo yake;
ii. Baadhi ya vyama vya ushirika kutofanya kazi, kutotekeleza majukumu yake ya msingi na vingine kuwa vyama hewa;
iii. Malalamiko kutoka katika baadhi ya mikoa kuwa wananchi wananyanyasika sana na mfumo wa Vyama vya Ushirika na Stakabadhi Ghalani;

Serikali imejipanga kutatua changamoto hizo kwa kufanya yafuatayo:

i. Kuendelea kujenga uwezo wa vyama vya ushirika kwa kupitia upya sheria ya ushirika, namna bora ya kusimamia na kuboresha sifa za kuwapata viongozi wake;
ii. Kuendelea kuwachukulia hatua wale wote watakaokiuka au watakaoenda tofauti na sheria, kanuni na miongozo ya ushirika;
iii. Kuendelea kuvifuta vyama vya ushirika ambavyo havifuati Sheria, kanuni na miongozo ya ushirika;

iv. Kuhimiza Wakulima/Wanachama wanaotumia Vyama vya Ushirika nchini kufungua Akaunti Benki ili Mkulima kujihakikishia malipo yake. Hii itakuwa mojawapo ya suluhu kwa udanganyifu unaofanywa na baadhi ya viongozi wa Vyama vya Ushirika wasio waaminifu wakati wa malipo.

v. Ili kuboresha/kuimarisha mfumo wa stakabadhi ghalani mambo yafuatayo lazima yazingatiwe:-

   a) Kuwepo kwa chama cha msingi kilichosajiliwa katika kijiji husika;

   b) Kuwepo na ghala lililosajiliwa na Bodi ya Maghala;

   c) Kuwepo kwa mfumo wa kufanya minada kwa njia ya ushirika;

   d) Kuwepo kwa wanunuzi wa kununua kwa minada.

# 6.0. VIKUNDI VYA KIFEDHA VYA KIJAMII

## 6.1. UTANGULIZI

Vikundi vya kifedha vya kijamii ambavyo huanzishwa na wananchi hasa wa kipato cha chini mijini na vijijini kwa ajili ya kupata mitaji ya kuendesha shughuli za kiuchumi vimeendelea kushamiri nchini. Hapa nchini vikundi hivyo vinaitwa kwa majina mbalimbali kama vile VICOBA, VSLA, ROSCAs, VITOVU, SILC, ASCAs, Benki Imani, Benki Jamii, JOSACA, COCOBA, n.k. Vikundi hivyo huanzishwa kwa usaidizi wa taasisi wezeshi (promoters). Kwa kiasi kikubwa taasisi hizo ziko chini ya miavuli mitatu ya kitaifa ambayo ni *VICOBA Federation of Tanzania* (VICOBA-FETA), *Tanzania Informal Microfinance Association of Practictioners* (TIMAP) na *Inter Religious VICOBA* (IR-VICOBA).

**Jedwali Na. 10: Taasisi miavuli, idadi ya wanachama na mitaji yao**

| Na. | MWAVULI | Vikundi | Wanachama | Mtaji (TZS) | Mikopo (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | IR VICOBA | 4,128 | 110,499 | 61,100,000,000 | 35,550,000,000 |
| 2. | TIMAP | 26,670 | 627,952 | 65,290,000,000 | 62,490,000,000 |
| 3. | VICOBA FETA | 20,809 | 541,034 | | |
| JUMLA | | | | | |

*Chanzo: NEEC*

Maendeleo ya taasisi hizo chini ya miavuli hiyo ni kama ifuatavyo.

## 6.2. IR-VICOBA

**Jedwali Na. 11: Idadi ya vikundi na wanachama wa IR-VICOBA**

| Na | Taasisi | Idadi ya vikundi | Wanachama | Na | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | me | ke | |
| 1 | Evangelical Lutheran Church, Northern Diocese | 1,033 | 9,531 | 20,233 | 29,764 |
| 2 | Ilula Orphanage Program | 52 | 304 | 849 | 1,153 |
| 3 | Anglican Church of Tanzania, Morogoro Diocese | 63 | 1,071 | 1,425 | 2,496 |
| 4 | Tanganyika Christian Refugee Services | 304 | 3,214 | 4,194 | 7,408 |
| 5 | Tanzania Episcopal Conference | 634 | 3,979 | 11,513 | 15,492 |
| 6 | DIRVA Kigoma | 68 | 264 | 1,776 | 2,040 |
| 7 | Four Corners Cultural Project | 227 | 1,546 | 2,953 | 4,651 |
| 8 | DIRVA Singida | 103 | 609 | 3,571 | 4,180 |
| 9 | DIRVA Tanga | 90 | 436 | 2,045 | 2,481 |
| 10 | Christian Council of Tanzania | 636 | 4,975 | 10,073 | 15,048 |
| 11 | ELCT-Mbulu Diocese | 112 | 1,501 | 1,773 | 3,254 |

| Na | Taasisi | Idadi ya vikundi | Wanachama | Na | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | me | ke | |
| 12 | DIRVA Lushoto | 300 | 3,500 | 5,500 | 9,000 |
| 13 | ELCT-Eastern Coastal Diocese | 321 | 1,259 | 7,304 | 8,563 |
| 14 | BAKWATA | 176 | 1,408 | 3,278 | 4,686 |
| 15 | Norwegian Church Aid | 9 | 113 | 170 | 283 |
| | **JUMLA** | **4,128** | **33,710** | **76,657** | **110,499** |

Hadi kufikia Machi 2020 taasisi mwavuli ya IR-VICOBA ilikuwa na jumla ya taasisi wezeshi 15 katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Iringa, Morogoro, Shinyanga, Kagera, Kigoma, Songwe, Mtwara, Njombe, Dar es Salaam, Dodoma, Singida, Tanga, Mbeya, Geita, Pwani, na Lindi. Kwa ujumla taasisi hizo zilikuwa na vikundi 4,128, vyenye jumla ya wanavikundi 110,499 (Wanawake 76,657 na wanaume 33,710). Vikundi hivyo vilikuwa na jumla ya mtaji wa shilingi bilioni 61.1. Jumla ya mikopo iliyotolewa kwa vikundi vyote chini ya IR-VICOBA ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 35.55 na kiasi kilichokuwa kimerejeshwa ni shilingi bilioni 8.56

### 6.3. TIMAP

Hadi kufikia Machi 2020 taasisi mwavuli ya TIMAP ilikuwa na jumla ya taasisi wezeshi 11 katika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Kagera, Geita, Mtwara, Lindi, Arusha, Kilimanjaro, Mara, Mwanza na Mbeya. Kwa ujumla taasisi hizo zilikuwa na vikundi 26,670, vyenye jumla ya wanavikundi 627,952 (Wanawake 406,204 na wanaume 221,748). Vikundi hivyo vilikuwa na jumla ya mtaji wa shilingi bilioni 65.29. Jumla ya mikopo iliyotolewa kwa vikundi vyote chini ya TIMAP ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 62.49.

**Jedwali Na. 12: Idadi ya vikundi na wanachama wa TIMAP**

| Na. | Taasisi | Idadi ya vikundi | Wanachama | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Me | Ke | Jumla |
| 1. | Umoja wa VICOBA KILWA | **273** | **2,431** | **5,201** | **7,026** |
| 2. | FAIDERS - Savings and Credit Associations (SACAS) | 107 | 1370 | 986 | 2356 |
| 3. | Jumuiya ya Miradi ya Maendeleo Kisarawe na Ilala(JUMIMAKI) | 539 | 4,288 | 6,918 | 11,206 |
| 4. | Jumuiya ya Kukuza Uchumi Ilala (JUKUILA) | 1,653 | 10,724 | 33,839 | 44,563 |
| 5. | AGA-KHAN FOUNDATION | 9,219 | 60,133 | 119,103 | 179,236 |
| 6. | EARDP-Community Initiatives | 27 | 201 | 649 | 850 |

| Na. | Taasisi | Idadi ya vikundi | Wanachama | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Me | Ke | Jumla |
| 7. | PACT-Tanzania | 6,174 | 23,388 | 99,472 | 122,860 |
| 8. | RUDIA | 529 | 4,730 | 9,909 | 14,639 |
| 9. | Catholic Relief Service (CRS) | 6,877 | 47,730 | 103,039 | 150,729 |
| 10. | Ruvu Credit and Development Organization (RUCDO) | 545 | 2410 | 10,248 | 12,658 |
| 11. | Jozani Credit and Development Organization (JOCDO) | 727 | 4,210 | 16,840 | 21,050 |
| | **GRAND TOTAL** | **26,670** | **221,748** | **406,204** | **627,952** |

## 6.4. VICOBA-FETA

Hadi kufikia Machi 2020 taasisi mwavuli ya VICOBA-FETA ilikuwa na jumla ya taasisi wezeshi 24. Kwa ujumla taasisi hizo zilikuwa na vikundi 20,809, vyenye jumla ya wanavikundi 541,034 (Wanawake 378,724 na wanaume 162,310). Taasisi hiyo ilikuwa imefikia mikoa 25 ambayo ni: Arusha, Dar-es,salaam, Dodoma, Geita, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Njombe, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Singida,Tabora naTanga.

**Jedwali Na. 13: Idadi ya vikundi na wanachama wa VICOBA-FETA**

| Na. | Taasisi | Idadi ya vikundi |
|---|---|---|
| 1 | SEDIT | 3,849 |
| 2 | UYACODE | |
| 3 | AHADIWAY | 1,047 |
| 4 | SELL | 4,614 |
| 5 | PESCODE | 909 |
| 6 | KIVINET | 609 |
| 7 | NAPAD | |
| 8 | KIBASILA | |
| 9 | LTF | 272 |
| 10 | MDF | |
| 11 | CARITAS | |
| 12 | VISUDENET | 567 |
| 13 | FERUSCO | 473 |
| 14 | MVITA | 1744 |

| | | |
|---|---|---|
| **15** | PHILETAJO | 2340 |
| **16** | YEMCO | 71 |
| **17** | WMEO | 10 |
| **18** | UJASIRIAMALI | |
| **19** | ENDELEZA JAMII | |
| **20** | ASE | |
| **21** | ERICK | |
| **22** | VSDA | |
| **23** | WINAMWANGA | |
| **24** | DELTA | |
| | **GRAND TOTAL** | **16,575** |

## 6.5. UTEKELEZAJI WA SERA, SHERIA NA KANUNI ZA SEKTA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA

Serikali ilitunga Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2017 na Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 kwa lengo la kuboresha usimamizi na uendelezaji wa sekta ya Huduma Ndogo za Fedha nchini. Sera na Sheria hiyo inavitambua vikundi vya kifedha vya kijamii kama mojawapo ya watoa huduma ndogo za fedha. Kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 Benki Kuu ya Tanzania imepewa mamlaka ya kusimamia watoa huduma ndogo za fedha katika madaraja manne yafuatayo:-

i. Daraja la Kwanza: Benki na Taasisi zinazopokea amana
ii. Daraja la Pili: Taasisi za Huduma Ndogo za Fedha zisizopokea amana na wakopeshaji binafsi
iii. Daraja la Tatu: Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo(SACCOS)
iv. Daraja la Nne: Vikundi vya kifedha vya kijamii (*Communuty Microfinance Groups*)

Kwa mujibu wa Sheria hiyo Benki kuu ya Tanzania imekasimisha jukumu la kusimamia Vikundi vya Kifedha vya Kijamii. kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa (Local Government Authorities-LGAs).

### 6.5.1. Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha

Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha za mwaka 2019 kwa ajili ya kutekeleza Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 ziliandaliwa na Sheria imeanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 1 Novemba mwaka 2019. Mojawapo ya kanuni hizo ni za kusimamia vikundi vya kifedha vya kijamii. Katika kusimamia Daraja hilo Kanuni hizo zinaelekeza ifuatavyo:

**Jedwali Na. 14: Kanuni za huduma ndogo za fedha za mwaka 2019**

| Na | Eneo | Maelekezo |
|---|---|---|
| **1** | Kiwango cha chini cha mtaji | Vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha havina sharti la kiwango cha mtaji wa kuanzia. |
| **2** | Utaratibu wa kusajiliwa | Kusajiliwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na masharti ya kusajiliwa ni pamoja na:<br>i. Kujaza Fomu ya maombi ya usajili<br>ii. Idadi ya wanachama 10 hadi 50<br>iii. Katiba iliyosainiwa na wanachama wote<br>iv. Muhtasari wa mkutano wa uazishwaji na<br>v. Barua ya utambulisho ya kata/kijiji/Mtaa |
| **3** | Masharti ya uendeshaji wa biashara ya huduma ndogo za fedha | i. Kuwa na anuani au mahali pa kufanyia mikutano<br>ii. Kutunza kumbukumbu za masuala ya fedha<br>iii. Hakuna sharti la kukaguliwa na mkaguzi wa nje<br>iv. Sharti la kuzingatia sheria zingine za nchi ikiwemo Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu<br>v. Ubadilishanaji wa taarifa za wakopaji kupitia mfumo wa taarifa za wakopaji (Credit Reference System<br>vi. Misingi ya kumlinda mtumiaji wa huduma ndogo za fedha ikiwa ni pamoja na uwazi katika utoaji wa taarifa zote za bidhaa na huduma zinazotolewa ikiwemo viwango vya riba za mikopo na gharama nyingine |
| **4** | Shughuli zinazoruhusiwa kufanywa na watoa huduma | i. Kupokea akiba<br>ii. Kutoa mikopo kwa wanachama,<br>iii. Kukusanya michango kwa ajili ya shughuli za kijamii na shughuli zingine kama zilivyoainishwa katika Kanuni |
| **5** | Shughuli zisizoruhusiwa kufanywa na watoa huduma | i. Kupokea amana kutoka kwa wateja wasio wanachama;<br>ii. Kufungua tawi au kuwa wakala wa benki na shughuli zingine kama zilivyokatazwa katika Kanuni; |

### 6.5.2. Programu ya kutoa elimu kuhusu Sera na Sheria ya Huduma Ndogo Za Fedha

Kufuatia kupitishwa kwa Sera ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2017, Sheria na Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha, Serikali iliandaa Programu ya kutoa elimu kwa umma kuhusu Sera na Sheria hiyo. Kuandaliwa kwa Programu hiyo kunatokana na ukweli kwamba watanzania wengi hawana uelewa wa kuwepo kwa Sera, Sheria na

Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha. Pia kumekuwepo na upotoshaji wa umma kuhusu madhumuni ya kuwa na Sera na Sheria hiyo.

Madhumuni ya Programu hiyo ni:

i. Kufahamisha umma kuhusu umuhimu wa Sera na kusudi la kuwepo kwa Sheria na Kanuni zake na pia kujenga uelewa kwa umma kuhusu sekta ndogo ya huduma ndogo za fedha;
ii. Kuhakikisha kuwa wadau muhimu wanapata uelewa kuhusu sheria na mfumo mzima wa kisheria katika utoaji wa huduma ndogo za fedha na kuwezesha uzingatiaji wa sheria hiyo;
iii. Kuwezesha wadau na umma kujua wajibu, majukumu na fursa zilizopo katika sekta ndogo ya fedha;
iv. Kuhamasisha na kukuza sekta ndogo ya fedha kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zake.

Walengwa wa Programu hiyo ni:

i. Watekelezaji: Ofisi ya Rais TAMISEMI, Wizara ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania, Wizara ya Kilimo, Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
ii. Watumiaji wa Huduma Ndogo za Fedha: Mtu mmoja mmoja, asasi, taasisi;
iii. Vyama na mashirikisho kama vile TAMFI, VICOBA-FETA, TIMAP, IR-VICOBA, SCCULT, COBAT na TFC;
iv. Watoa huduma ndogo za fedha:Vikundi vya kifedha vya kijamii, wakopeshaji binafsi, taasisi, vyama vya akiba na mikopo;
v. Wahamasishaji wa huduma ndogo za fedha: wawezeshaji (promoters);na
vi. Vyombo vya habari

Utaratibu/njia ya kutoa  elimu ni kama ifuatavyo:

i. Warsha na semina;
ii. Kuchapisha na kusambaza Sera, Sheria, *popular versions* za Sera, Sheria na Kanuni za huduma ndogo za fedha; Katuni,Mabango na vipeprushi;
iii. Vyombo vya habari: magazeti, redio, luninga, mitandao ya kijamii, tovuti, n.k.

Mafunzo yalipangwa kutolewa kikanda kama ifuatavyo:

- Kanda ya Mashariki: Dar es Salaam, Pwani na Morogoro;
- Kanda ya Kaskazini: Arusha, Manyara, Tanga na Kilimanjaro;
- Kanda ya Ziwa 1: Mwanza, Mara na Kagera;
- Kanda ya Ziwa2: Shinyanga, Simiyu na Geita;
- Kanda ya Magharibi: Kigoma, Katavi na Tabora
- Kanda ya Nyanda za juu Kusini: Mbeya, Rukwa, Songwe na Njombe; na
- Kanda ya Kusini; Mtwara, Lindi na Ruvuma

Utekelezaji wa Programu ya kutoa elimu kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za huduma ndogo za fedha ulipangwa kufanyika katika kipindi cha kuanzia Desemba 2019 hadi April 2020. Hata hivyo kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona 19 elimu kwa njia ya warsha na semina haikuweza kufanyika. Hata hivyo katika kipindi hicho elimu ilitolewa kwa kutumia vyombo vya habari (magazeti, redio, luninga na mitandao ya kijamii).

# 7.0. MPANGO WA VIWANDA VIDOGO NA VYA KATI (SANVN VIWANDA SCHEME)

## 7.1. UTANGULIZI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatekeleza Sera ya maendeleo ya viwanda. Maendeleo ya viwanda ni muhimu sana kwa kuharakisha maendeleo ya wananchi, kwani utekelezaji ukifanyika kwa mfumo wa kuangalia pande zote, yaani uendelezaji wa kilimo, mifugo na uvuvi. vilevile kwa upande mwingine uendelezaji wa viwanda vidogo na vya kati vya uchakataji wa mazao hayo ilim kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Tangu mwaka 2017, Serikali, kupitia Taasisi zake tano, yaani SIDO, AZANIA BENKI, NSSF, VETA na NEEC ilibuni mpango wa kuendeleza viwanda kwa kushirikisha Taasisis hizi tano ambazo kila moja ina majukumu ya msingi katika kutekeleza maendeleo ya viwanda. Mpango huu unajulikana kwa jina la SANVN ambayo kirefu chake ni taasisi zinazoshiriki SIDO, AZANIA, NSSF, VETA, na NEEC. Mpango huu wa pamoja ni wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kweye eneo la uendelezaji wa Viwanda vidogo na vya kati (SANVN Viwanda Scheme) ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa mitaji na ujuzi katika Viwanda vidogo na vya kati hususani katika eneo la kuongeza mnyororo wa thamani wa kuchakata mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Programu ya SANVN Viwanda Scheme imeanzishwa ili kuweza kuunga mkono jitihada za Serikali yenye ajenda ya kuleta Maendeleo katika sekta ya Viwanda Vidogo na vya Kati kwa ajili ya Maendeleo ya Kiuchumi.

Makubaliano ya Programu hii yalisainiwa mwezi Februari 2020 kati ya SIDO, VETA, AZANIA, NEEC na NSSF. Taasisi hizi ndio zinashirikiana katika Utekelezaji wa programu hiyo kama inavyoonekana kwenye picha hapo chini.



Fedha zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa programu ni Shilingi Bilioni tano ambazo zimetolewa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) na kupelekwa Benki ya Azania kwa ajili ya kukopeshwa walengwa wa mpango huo. Mpango ulizinduliwa Rasmi tarehe 10 Julai 2020 jijini Dodoma ambapo mawaziri watatu walishuhudia uzinduzi huo (Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Waziri wa Viwanda na Biashara na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia).

Walengwa wa Mpango walioanishwa ni Watu Binafsi na Vikundi. Mpango unatoa mikopo ya thamani ya kuanzia Shilingi milioni 8 hadi 50 kwa miradi midogo na kuanzia milioni 50 hadi Shilingi Milioni 500 kwa miradi mikubwa. Aidha Riba ya mikopo ni asilimia 13 kwa mwaka katika njia ambayo deni linapungua kila deni linapolipwa (*Reducing Balance)*.

Katika Mpango huu waombaji wote wanapaswa kuwasilisha maombi yao katika Taasisi ya VETA au SIDO kisha maombi hayo kuwasilishwa na taasisi hizo katika benki ya Azania kwa ajili ya hatua za utoaji mikopo kwa wale watakaoonekana wamekidhi vigezo. Moja ya majukumu ya SIDO na VETA ni kutoa mafunzo, kupitia mpango wa biashara, kutembelea eneo la mradi na kutoa mapendekezo kwa Benki ya Azania.

### 7.2. MASHARTI NA VIGEZO VYA UTOAJI MIKOPO

i. Mwombaji wa mkopo lazima awe raia wa Tanzania
ii. Mradi unaoombewa mkopo lazima uwe na uwezo wa kukopesheka na kuwa na uzoefu katika uendeshaji wa angalau mwaka mmoja
iii. Mradi unaoombewa mkopo lazima ujikite katika kuongeza mnyororo wa thamani kwenye eneo la uzalishaji ama uchakataji wa bidhaa za Kilimo
iv. Muombaji wa mkopo lazima awe mhitimu wa mafunzo yatolewayo na SIDO/VETA
v. Kwa mkopo wa mashine: Muombaji lazima achangie asilimia 20 ya gharama ya kifaa. Fedha hii itakaa kwa mkopeshaji ambae ni Benki ya Azania na itarudishwa kwa mteja baada ya mkopo kukamilika
vi. Kwa waombaji wa vikundi; kikundi lazima kiwe na watu 5 hadi 10 waliopata mafunzo ya ujuzi na kutambuliwa na Mamlaka husika
vii. Muombaji lazima awe mwanachama wa au akubali kuwa mwanachama wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF)

### 7.3. MUUNDO WA MKOPO

i. Muda wa mkopo ni mwaka 1 hadi 7 kulingana na aina ya mradi na mkopo
ii. Riba ya mkopo ni asilimia 13 kwa mwaka (Reducing Balance Method)
iii. Bima ya mkopo ni asilimia 2 ambayo italipwa mara moja.

### 7.4. UTARATIBU WA KUOMBA MKOPO

Wadau wanashauriwa kutembelea Ofisi za SIDO/VETA zilizo karibu nao kwa ajili ya kuwasilisha maombi yao ama kupata ufafanuzi wa kina juu ya programu hii.

## 7.5. VIAMBATISHO VYA MAOMBI YA MKOPO

**Jedwali Na. 15: Viambatisho vya maombi ya mkopo – SANVN Viwanda Scheme**

| WAOMBAJI BINAFSI/VIKUNDI | MAKAMPUNI |
|---|---|
| i. Barua ya maombi ya mkopo;<br>ii. Barua ya utambulisho kutoka Serikali ya Kijiji ama mtaa;<br>iii. Picha mbili za pasipoti zilizopigwa hivi karibuni;<br>iv. Nakala ya Kitambulisho cha Taifa<br>v. Andiko la Mradi;<br>vi. Sitatimenti ya benki ya miezi 12;<br>vii. Cheti cha usajili wa biashara [Certificate of registration & extract from registrar] – Kama biashara imeshajiliwa;<br>viii. Nakala ya Hati ya Dhamana ya mkopo kama leseni za makazi;<br>ix. Ripoti ya uthamini wa mali (*Kuanzia mkopo wa Milioni 20*)<br>x. Mahesabu ya miaka 3 iliyopita yaliyokaguliwa (*Mkopo wa Sh Mil 50 na kuendelea*)<br>xi. Barua ya Utambulisho/Udhamini kutoka kwa taasisi mwamvuli (*Kwa mikopo ya Vikundi*)<br>**xii.** Ankra yenye kuonesha bei ya mashine (*Kwa Mikopo ya Vifaa/mashine*) | i. Barua ya Maombi<br>ii. Mahesabu ya miaka 3 iliyopita yaliyokaguliwa<br>iii. Makadirio yote ya mradi kwa kipindi cha mkopo<br>iv. Wasihi wa uongozi wa kampuni<br>v. Mwongozo wa kampuni<br>vi. Vitambulisho vya wamiliki<br>vii. Maelezo mafupi kutoka kwa Wakurugenzi ama wasimamizi wakuu<br>viii. Marejesho ya kampuni ya mwaka ulioisha<br>ix. Cheti cha usajili wa kampuni<br>x. Leseni ya biashara na cheti cha kulipa kodi<br>xi. Barua ya utambulisho kutoka Serikali ya Kijiji ama Mtaa<br>xii. Picha mbili za pasipoti za Wakurugenzi<br>xiii. Makubaliano ya kikao cha bodi ya kampuni kuomba mkopo<br>xiv. Mchanganuo wa biashara<br>xv. Dhamana za mkopo<br>xvi. Uthaminishaji wa dhamana inayowekwa<br>xvii. Statimenti ya benki ya miezi 12 |

## 7.6. MAJUKUMU YA TAASISI KWENYE MRADI HUU

### 7.6.1. VETA NA SIDO

Taasisi hizi mbili zitakuwa na majukumu yafuatayo;

i. kusimamia miradi iliyopata mikopo kupitia kwake na
ii. kutoa mafunzo na ushauri wa kitaalam kwa Wajasiriamali ili kuwasaidia kuboresha miradi yao na kuendesha uzalishaji kwa tija na ufanisi zaidi
iii. Pia kutoa ujuzi unaostahili kwa wananchi kulingana na viwanda husika na kwamba itasimamia vyema zoezi la kutambua Wajasiriamali hao

### 7.6.2. AZANIA

Benki ya Azania itahusika na kutoa mikopo kwa Wajasiriamali mara baada ya kupokea maombi kutoka VETA Na SIDO na kuyafanyia tathmini maombi hayo kwa kushirikiana na taasisi hizo. Pia itafanya ufuatiliaji kwenye urejeshaji wa mikopo hiyo, kuhakikisha wanufaika wote wanajisajili na NSSF, kulipa asilimia saba (7%) riba kwa NSSF kwa mwaka.

#### 7.6.3. NEEC
Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi lina majukumu ya kuratibu utendaji mzima wa Programu hii kwa kufanya tathmini juu ya miradi iliyopewa fedha na programu hii. Kufanya vikao na taasisi shiriki na kujadili juu ya maendeleo ya mradi.

#### 7.6.4. NSSF
Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) utakua na jukumu la kutoa Elimu ya programu hii kwa wanachama wa NSSF na Jamii kwa ujumla. Pia watawasajili wanufaika wote wa programu.

### 7.7. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU
Mwongozo wa Programu umetayarishwa na kuzinduliwa rasmi siku ya uzinduzi. Vilevile mwongozo huu umesambazwa kwenye vituo vya SIDO na VETA nchi nzima.

Hadi sasa kuna Wajasiriamali tisa (9) ambao wametambuliwa, ambapo kati yao Wajasiriamali watatu (3) wameingia kwenye mfumo wa kuomba mkopo ambao ni;

i. **NATE INVESTMENT**
Hiki ni kiwanda kinachojishughulisha na uzalishaji wa ‘’tissue’’. Mjasiriamali huyu yupo katika hatua za mwisho za kupatiwa mkopo wa kiasi cha Shilingi Milioni Mia Nne Themanini na Sita (TZS.486, 000,000.00).

ii. **SUMA JKT**
Hili ni Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT).Kikao kiliitishwa na Katibu Mkuu wa Chama ili kuwapa fursa SUMA JKT waweze kuwasilisha miradi yao ambayo ni; uzalishaji wa ‘’toothpicks’’, ‘tissues’’ na ‘’cotton buds’’.Waliomba jumla ya Shilingi Milioni Mia Nne Tisini na Nane (TZS. 498,000,000.00).Mteja atatembelewa na wataalamu kutoka Benki mara baada ya kupata ridhaa ya Menejimenti.

iii. **RHANA LIME COMPANY LTD**
Hawa wameomba kiasi cha Shilingi Milioni Mia Moja na Hamsini (TZS. 150,000,000.00) kwa ajili ya biashara ya unga wa gypsum. Wameomba kiasi hiki kwa ajili ya ununuzi wa mashine.

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni mratibu wa kusimamia utekelezaji wa Programu nzima.

### 7.8. HITIMISHO
Kupitia utekelezaji wa programu hii maendeleo chanya yanatarajiwa na vilevile ukuaji wa Viwanda vidogo na vya kati hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi kupitia;

i. Ajira mbalimbali zitaweza kutengenezwa kupitia utekelezaji wa programu hii

ii. Uhitaji wa malighafi utaongezeka kwa ajili ya uzalishaji wa viwandani
iii. Pato la Taifa litaongezeka kutokana na mauzo ya bidhaa mbalimbali za viwandani.
iv. Programu hii itasaidia kuboresha hali za Maisha ya Wananchi kwa kuweza kupata mahitaji yao muhimu ya kila siku kupitia ajira watakazozipata.
v. Usimamizi makini wa viwanda hivyo utasaidia ongezeko la ukusanyaji wa kodi hivyo kusababisha maendeleo katika sekta mbalimbali ikiwemo Afya na Elimu.

# 8.0. MIFUKO YA UWEZESHAJI NA PROGRAMU ZA MITAJI

## 8.1. UTANGULIZI

Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ilianzishwa kwa lengo la kupanua wigo wa utoaji huduma za kifedha pamoja na huduma nyingine za uwezeshaji ili kuwafanya wananchi washiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wa nchi yao.

Madhumuni mahsusi ya mifuko hii ni pamoja na kutatua changamoto zinazozuia wananchi kutoa mchango katika kukuza uchumi wao na taifa kwa ujumla. Miongoni mwa changamoto hizo ni kuwepo kwa vikwazo vinavyosababisha benki kusita kutoa mikopo kama vile gharama kubwa za kuhudumia utoaji wa mikopo, ukosefu wa utambulisho rasmi, kutokuwa na taarifa muhimu za waombaji mikopo na ukosefu wa dhamana, udhaifu unaowafanya wananchi wasikopesheke, ukosefu wa ujuzi wa kuandaa na kusimamia miradi inayokopesheka, ukosefu wa mitaji ya kuchangia uanzishaji wa miradi nk.

Walengwa wakuu wa mifuko ni wananchi wote nchini Tanzania wanaofanya shughuli za kiuchumi katika nyanja za Kilimo, Mifugo, Maliasili na Utalii, Afya, Viwanda na Biashara, Ujenzi na Maendeleo ya Ardhi, Mawasiliano na Uchukuzi, Nishati, Maji na Elimu.

Baraza la Uwezeshaji linaratibu Mifuko ya Uwezeshaji 51 iliyogawanyika katika makundi makuu manne ambayo ni: Mifuko inayotoa mikopo moja kwa moja kwa walengwa (18), Mifuko inayotoa dhamana za mikopo kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za fedha (10), Mifuko inayotoa ruzuku (20) na Programu za Uwezeshaji (3). Kati ya mifuko 51 mifuko 40 iko hai na inatoa huduma, mifuko 6 inafuatilia marejesho ya mikopo na mifuko 5 imelala (dormant).

## 8.2. URATIBU WA MIFUKO YA UWEZESHAJI

Uratibu wa mifuko unaofanywa na Baraza unatokana na utekelezaji wa majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa nguzo ya tatu (Upatikanaji wa Mitaji) ya Sera ya Taifa ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi 2004 pamoja na matakwa ya Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Kifedha ya mwaka 2017 (NMP, 2017) pamoja na Sheria yake ya Mwaka 2018 (MPA, 2018)

Baraza la Taifa la Uwezeshaji limefanya shughuli zifuatazo katika uratibu wa Mifuko na Programu za Uwezeshaji

### 8.2.1. Kutunza Daftari la Orodha ya Mifuko ya Uwezeshaji

Mifuko minne imeongezwa katika rejesta na kufikisha idadi ya mifuko 51, Aidha kati ya Mifuko 51, Mifuko 40 iko hai na inatoa huduma, Mifuko 6 inafuatilia marejesho, Mifuko 5 imelala (Dormant). Mifuko iliyoongezeka ni :-

i. Mfuko wa uhamasishaji wa matumizi ya ethanol kama nishati mbadala ya kupikia;
ii. Mfuko wa uzalishaji maji kwa kutumia pampu zinazoendeshwa kwa nishati ya jua katika kuongeza kasi ya upatikanaji wa maji vijijini;
iii. Mfuko wa Tafa wa Umwagiliaji; na

iv. Mfuko wa Mabadiliko ya Tabia Nchi (Green Climate Fund – GCF).

#### 8.2.2. Kuitangaza Mifuko ya Uwezeshaji

Baraza limendelea kuelimisha wadau mbalimbali kuhusu uwepo wa mifuko hii. Njia mbalimbali zimetumika katika kutoa elimu hiyo kama vile Makongamano, Vyombo vya habari, Maonesho, Vipeperushi, Tovuti na Mitandao ya Kijamii. Miongoni mwa njia zilizotumika ni:

i. Kuratibu Maonesho ya Mifuko ya Uwezeshaji ambapo mpaka sasa yamefanyika katika mikoa ifuatayo:

- **Maonesho ya Kwanza** : Mkoa wa Dodoma (18 - 22 Aprili, 2017)
- **Maonesho ya Pili** : Mkoa wa Mbeya (19 - 23 Oktoba, 2018)
- **Maonesho ya Tatu**: Mkoa wa Simiyu (14 - 20 Oktoba, 2019)

ii. Kushirikiana na Serikali za Mikoa na Mifuko ya Uwezeshaji kuandaa Makongamano ya Uwezeshaji Wananchi kiuchumi katika Wilaya 12. Wilaya hizo na tarehe za mafunzo katika mabano ni Mkoa wa DSM yaliyohusisha Wilaya zake tano (6 - 7 Machi, 2019), Halmashauri ya Mji wa Mafinga (27-28 Julai, 2019), Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe (20-21 Mei, 2019), Halmashauri ya Wilaya ya Busega (26 Mei, 2019), Halmshauri ya Wilaya ya Kibiti na Rufiji (23 Julai, 2019), Halmashauri ya Mji wa Kilolo (04-05 Sept, 2019), Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma (11 Sept. 2019), Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni (05 - 06 Novemba, 2019), Wilaya ya Nyamaga (11 Jan, 2020), Wilaya ya Bukoba Mjini (15 Febr, 2020), Wilaya ya Shinyanga Mjini (26 Febr, 2020) Mafunzo hayo yaliwafikia wananchi 6,978 ambapo kati ya hao (Wanawake 4,047 ambao sawa na asilimia 58 na Wanaume 2,931 sawa na asilimia 42.

iii. Kushiriki katika maonesho mbalimbali ya kitaifa pamoja na kliniki za biashara zinazoratibiwa na Mamlaka ya Taifa ya Uendelezaji Biashara (Tan- Trade)

#### 8.2.3. Kuitisha vikao/mikutano na Taasisi za Mifuko/Programu

Baraza liliratibu vikao viwili vilivyokutanisha wakuu wa Taasisi za mifuko na wasaidizi wao kwa kipindi tajwa, vikao hivyo vilifanyika tarehe 06 Machi, 2019 na tarehe 28 Novemba, 2019. Madhumuni makuu ya vikao hivyo yalikuwa ni kujadili maonesho ya Mifuko ya uwezeshaji, kupitia taarifa za nusu mwaka za mifuko na kubadilishana uzoefu juu ya utendaji wa mifuko.

#### 8.2.4. Kupokea taarifa za Mifuko, kuzipitia na kuandaa taarifa ya pamoja

Baraza limefanikiwa kuandaa taarifa za Mifuko kwa vipindi vya nusu mwaka yaani Jan- Juni 2019 na Julai - Desemba 2019.

#### 8.2.5. Kuwaunganisha wananchi na Mifuko ya Serikali ya Uwezeshaji

Jumla ya wajasiriamali 736 wameunganishwa na Mifuko ya Uwezeshaji pamoja na taasisi mbalimbali za Serikali na za Binafsi kwa ajili ya kupata huduma zitolewazo kama mikopo, mafunzo ya Ujasiriamali, Ushauri wa kibiashara nk. Hata hivyo asilimia kubwa ya wananchi waliounganishwa na mifuko ya Uwezeshaji kwa ajili ya kupata mikopo hawakufanikiwa kwa kutokuwa na vigezo stahiki.

#### 8.2.6. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya huduma na matokeo ya Uwezeshaji.

Baraza kwa kushirikiana na UN Women lilifanya tathmini ya Mifuko ya Uwezeshaji Mwaka 2016. Kwa sasa andiko la mradi juu ya kutekeleza shughuli hii limekwisha andaliwa na kuwasilishwa kwa wadau. Tathmini ijayo ya mifuko inategemewa kufanyika mwaka 2021.

### 8.3. UTENDAJI WA MIFUKO YA UWEZESHAJI

Baraza linaratibu Mifuko ya Uwezeshaji 51 ambapo kati ya mifuko hiyo 40 iko hai na inafanya shughuli zake, mifuko 6 inakusanya marejesho/madeni na mifuko 5 imelala. Mchanganuo wa mifuko hiyo kimakundi pamoja na utendaji wake unaonekana katika Jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 16: Mchanganuo wa mifuko ya Uwezeshaji kimakundi**

| KUNDI LA MFUKO | MIFUKO INAYOTOA HUDUMA | MIFUKO INAYOKUSANYA MADENI | MIFUKO ILIYOLALA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| Mifuko inayotoa Mikopo Moja kwa Moja | 14 | 4 | 0 | 18 |
| Mifuko inayotoa Dhamana | 8 | 2 | 0 | 10 |
| Mifuko inayotoa Ruzuku | 15 | 0 | 5 | 20 |
| Programu za Uwezeshaji | 3 | 0 | 0 | 3 |
| **JUMLA YA MIFUKO** | **40** | **6** | **5** | **51** |

### 8.4. MIFUKO INAYOTOA RUZUKU

#### 8.4.1. MFUKO WA KUHIFADHI WANYAMAPORI TANZANIA (TWPF)

Mfuko huu ulianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 21 ya mwaka 1978 baada ya marekebisho ya kifungu cha 69 cha Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na.12 ya mwaka 1974. Hivyo unatambuliwa na Sheria ya Kuhifadhi Wanyamapori Na.5 ya mwaka 2009 kifungu cha (91)1.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Umelipa fidia ya Sh.984,758,000 kwa wananchi 5,056 baada ya kuathiriwa na wanyamapori waliosababisha uharibifu wa ekari 4,064 za mazao mbalimbali, Wananchi ishirini na wanne (24) waliojeruhiwa na wanane (8) waliouawa.
ii. Umezipatia taasisi za mafunzo na utafiti jumla ya Sh.2,805,312,692.46 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.

### 8.4.2. MFUKO WA MISITU TANZANIA (TaFF)

Mfuko umeanzishwa chini ya Sheria ya Misitu Sura Na.323 kwa lengo la kukabiliana na changamoto za usimamizi wa rasilimali za misitu hususan katika kuimarisha utekelezaji wa sera na sheria ya misitu.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Umetoa ruzuku kwa miradi 119 yenye thamani ya Shilingi 1,533,794,810 inayotekelezwa katika mikoa 23 Tanzania bara na Wilaya 52;
ii. Umetoa mizinga ya nyuki bora 5,288 pamoja na vifaa vingine kama mavazi ya kujikinga na mashambulizi ya nyuki seti 160, mashine za kukamulia asali (100), bomba za kufukiza moshi kwa nyuki (73), ndoo za kuhifadhia asali (694) na vifungashio vya ujazo mbalimbali 9,970 kwa vikundi 144; na
iii. Umegharamia ujenzi wa vituo saba vya kukusanyia asali kutoka kwa wafugaji wa nyuki katika mikoa ya Geita, Shinyanga, Tabora, Dodoma, Mara na Mbeya.

### 8.4.3. MFUKO WA TOZO YA MAENDELEO YA UTALII (TDL)

Mfuko umeanzishwa kwa Sheria ya Utalii Na.29 ya mwaka 2008, Kifungu kidogo cha 59(2) ili kuendeleza mazao ya utalii na kudhibiti ubora wa huduma za biashara za Utalii, Kukuza na kutangaza vivutio vya utalii, Kujenga uwezo katika sekta ya Utalii na Kufanya tafiti katika sekta ya Utalii, na shughuli nyingine yoyote kwa ajili ya maendeleo na kuboresha sekta ya utalii.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Kushiriki katika kongamano nchini China lenye lengo la kuhamasisha soko la utalii la Uchina kwa kutumia ndege za ATCL;
ii. Kuwezesha kutoa mafunzo ya ukarimu na utalii kwa wanafunzi wa Chuo cha Taifa cha Utalii kwa kuzingatia viwango vya NACTE;
iii. Kufanya mapitio ya mitaala yote inayotumika kufundishia ili kukidhi mahitaji ya soko; na
iv. Kufanya utafiti wa watalii wanaoondoka nchini pamoja na kukusanya na kuainisha takwimu za watalii walioingia nchini mwaka 2019.

### 8.4.4. MFUKO WA TAIFA WA MAMBO YA KALE (NFA)

Mfuko ulianzishwa kwa Sheria ya Mambo ya Kale Na.22 ya mwaka 1979, kifungu kidogo cha 19B ili kuwezesha shughuli za utafiti, uhifadhi na uendelezaji wa malikale.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Umekusanya taarifa za maeneo mapya ya malikale ikiwemo Lemaguru, Arusha; Kiwasihi Kigera, Mara; Mogitu-Manyara; Ndala, Tabora; na Nang'oma, Lindi ambayo yatatumika kuhuisha rejesta ya Taifa ya maeneo ya malikale;

ii. Umeratibu utafiti kwenye nyanja za akiolojia (5), paleontolojia (3) na paleonthropolojia (2) katika mikoa ya Arusha, Manyara, Mbeya, Tanga, Mara, Lindi na Tabora; na

iii. Umewezesha Shirika la Makumbusho ya Taifa kufanya utafiti, kuhifadhi, kukusanya, kuonesha na kuelimisha umma kuhusu urithi wa utamaduni wa Taifa.

#### 8.4.5. MFUKO WA UHIFADHI WA MILIMA YA TAO LA MASHARIKI (EAMCEF)

Mfuko ulianzishwa mwezi Juni, 2001 chini ya Sheria ya Ujumuisho wa Wadhamini (Trustees' Incorporation Act) kama ilivyorejewa mwaka 2002 (Cap.318 R.E.2002). Mfuko umetoa ruzuku (project grants) kwa miradi 57 yenye jumla ya Shilingi. 368,400,000 Kwa ajili ya kusaidia jitihada za uhifadhi endelevu wa maliasili zilizomo kwenye Milima ya Tao la Mashariki nchini Tanzania.

#### 8.4.6. MFUKO WA ELIMU TANZANIA (TEF)

Mfuko umeanzishwa kwa Sheria Namba 8 ya mwaka 2001, ili kusaidia juhudi za Serikali katika kuwezesha maendeleo ya Elimu katika ngazi zote kwa Tanzania Bara na Elimu ya Juu kwa Tanzania na Zanzibar.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Umefadhili miradi mitatu yenye thamani ya Shilingi 3,131,245,255.30 katika mikoa 19. Mikoa hiyo ni Arusha, Dar es salaam, Iringa, Kagera, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Mwanza, Njombe, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Simiyu, Songwe, Tabora na Tanga; na

ii. Umetoa ruzuku kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia mambo ya usafiri wa anga katika chuo cha Taifa cha Usafirishaji.

#### 8.4.7. MFUKO WA KUENDELEZA UJUZI (SDF)

Mfuko huu ni sehemu ya Programu ya Kuendeleza Elimu ya Ujuzi na Mafunzo ya Stadi za Kazi zenye kuleta tija katika ajira (Education and Skills for Productive Jobs-ESPJ) na Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza na Kuendeleza Ujuzi nchini (National Skills Development Strategy-NSDS). SDF inatoa ufadhili wa mafunzo ya kuendeleza ujuzi katika sekta sita za kipaumbele zinazoratibiwa na Programu ya ESPJ. Sekta hizo za kipaumbele ni: Kilimo-Uchumi, Utalii na

Huduma za ukarimu, Uchukuzi, Ujenzi, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), na Nishati.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Umefadhili miradi 95 yenye thamani ya shilingi bn 12.6 katika mikoa 24 ya Tanzania; na
ii. Umetoa mafunzo kwa Wanufaika 5,042 katika Kozi nyingine katika Taasisi zinazotekeleza SDF aidha kiasi cha shilingi 3,124,689,328.26 kimetumika kutoa mafunzo.

### 8.4.8. MFUKO WA BODI YA BARABARA (RFB)

Bodi ya Mfuko wa Barabara ilianzishwa kwa Sheria ya Barabara na Tozo ya Mafuta, Sura ya 220.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Umewezesha wananchi 18,460 kati ya hao wanawake ni 2,915 ambao ni sawa na asilimia 16;
ii. Umeongeza makusanyo toka Shilingi bilioni 40 kwa mwaka 2000 hadi Shilingi bilioni 784.8 kwa mwaka 2019; na
iii. Umeongeza ufanisi katika usimamizi wa matunzo ya barabara kupitia wakala barabara kama TANROADS, TARURA, MoWTC na TAMISEMI.

### 8.4.9. MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

Mfuko huu ni chombo cha Serikali chenye jukumu la kusaidia jamii na wananchi ambao wameathirika zaidi na umaskini na walioishi katika mazingira hatarishi ili waweze kujikwamua na hatimaye kutoka katika hali hiyo. Serikali ilianzisha TASAF mwaka 2000 na kwa sasa ipo katika Awamu ya Tatu (TASAF III). Utekelezaji wa TASAF unafanyika Tanzania Bara na Zanzibar.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Umehawilisha ruzuku ya Shilingi bilioni 35.6 kwa kaya maskini zilizopo kwenye Mpango ambazo zina watu 4,920,344 kwa Tanzania Bara na Zanzibar katika Vijiji/Mitaa/Shehia 9,867. Kaya hizo zimeweza kupata ruzuku hiyo kwa masharti ya lishe, afya na elimu;

ii. Umeunda vikundi 22,303 vya Kuweka Akiba na Kukuza Uchumi wa Kaya vyenye jumla ya walengwa 311,114 katika Mamlaka ya Maeneo ya Utekelezaji 44. Vikundi hivyo vimeweka akiba ya Jumla ya Shilingi bilioni 2.5 na kukopeshana Shilingi bilioni 1.6;

iii. Umetoa mafunzo ya kuwajengea uelewa kuhusu Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Waheshimiwa madiwani 57, Waheshimiwa Masheha 154, Wajumbe wa Kamati za Mradi 220, Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa 30, Wawezeshaji wa Halmashauri 200, Walengwa wa Vikundi vya Kuweka Akiba na Kuwekeza 892 na Wajumbe wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia Viongozi Wakuu wa kitaifa Zanzibar 22;

iv. Umeunda mfumo wa malipo kwa Walengwa kwa njia za kielektroniki (kupitia mitandao ya simu na Benki) na majaribio yamefanyika katika Mamlaka ya Maeneo ya utekelezaji ambayo ni 16. Walengwa 55,087 walinufaika na Shilingi bilioni 2.14 zimelipwa kwa kutumia njia hiyo; na

v. Kupitia mpango wa kutoa ajira za muda, miradi 1,521 kutoka katika Vijiji, Mitaa na Shehia zipatazo 1,212 imefikiwa, ambapo kaya za walengwa 161,416 zilipata ajira za muda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 42 na Wilaya zote za Zanzibar. Miradi hiyo ina thamani ya Shilingi bilioni 6.4. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa malambo ya maji, uanzishaji wa vitalu vya miche ya miti, uchimbaji wa visima vifupi, uboreshaji wa barabara, uhifadhi wa vyanzo vya maji na hifadhi ya mazingira.

### 8.4.10. MFUKO WA FIDIA YA ARDHI TANZANIA (LCF)

Mfuko ulianzishwa kwa Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 chini ya Kifungu Na. 173 ili kuratibu masuala yote ya ulipaji wa fidia ya ardhi. Mlengwa wa Mfuko ni mmiliki wa ardhi ambaye anaondolewa kwenye eneo lake lililotwaliwa kwa manufaa ya umma na kupangiwa matumizi mengine tofauti na yale yaliyopo kwa sasa.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Kuratibu katika mchakato wa malipo ya fidia katika Mji wa Kiserikali Mtumba;
ii. Kuandaa rasimu ya Mpango Mkakati wa miaka 3 wa Mfuko wa Fidia ya Ardhi 2018/2019 hadi 2020/2021; na
iii. Kuandaa Mwongozo wa ulipaji fidia na vyanzo imara vya mapato ili kuuwezesha mfuko kujiendesha wenyewe.

### 8.4.11. MFUKO WA MAWASILIANO KWA WOTE (UCSAF)

Mfuko ulianzishwa na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sheria ya Bunge nambari 11 ya Mwaka 2006 kwa lengo la kupeleka na kufanikisha huduma ya mawasiliano kwa wananchi waishio katika maeneo machache ya mijini na maeneo mengi yaliyo mbali, vijijini, yasiyo na mvuto wa kibiashara kwa watoa huduma ya mawasiliano.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Umetoa mafunzo kwa Walimu 1,029 tarehe 21-25 Oktoba 2019 katika vituo vitatu vya Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu cha Sayansi cha Mbeya (MUST) na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT);

ii. Umetoa vifaa vya TEHAMA vikijumuisha kompyuta 5 na printa moja kwa shule 320;

iii. Umejenga vituo 10 vya TEHAMA kwa upande wa Tanzania. Ujenzi wa vituo hivyo umekamilika ikiwemo ufungwaji wa vifaa vya TEHAMA, Viyoyozi pamoja na Samani zingine;

iv. Umetumia ruzuku ya Shilingi bilioni 13,136,262,412/= Kujenga miundombinu ya mawasiliano katika kata 52 zenye vijiji 316;

v. Umetumia Shilingi bilioni 57.92 kukarabati vyumba vitakavyotumika kutolea huduma kupitia Tiba Mtandao katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili pamoja na Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili (MOI);

vi. Umeratibu ujenzi wa mradi wa minara mitatu kwa kushirikiana na TTCL pamoja na wadau wengine kama Vodacom, Airtel na MIC Tz katika mji mpya wa Serikali wa Mtumba pamoja na vijiji vya jirani. Gharama za mradi huu ni takribani shilingi bilioni 1.05. Mpaka sasa mnara mmoja uliojengwa Mtumba umekamilika na huduma zinapatikana; na

vii. Umetumia Shilingi 3,337,684,882/= kutoa huduma za mawasiliano katika kata 10 zilizopo katika maeneo ya mipakani katika kulinda na kuimarisha ulinzi na usalama wa Taifa.

### 8.4.12. MFUKO WA NISHATI VIJIJINI (REF)

Mfuko wa Nishati Vijijini unasimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini. Sheria pia imebainisha uwepo wa Wakala wa Amana (Trust Agent) pamoja na majukumu yake. Wakala wa Amana huratibu upelekaji wa fedha kwa watekelezaji pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi husika mara baada ya mikataba kusainiwa kati ya mtekelezaji na Bodi ya Nishati Vijijini.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Katika kipindi cha Januari 2016 hadi Machi 2020 jumla ya vijiji 6,707 vimepatiwa umeme na hivyo kufanya vijiji vilivyopatiwa umeme nchini kote kufikia 8,725 ambayo ni sawa na asilimia 71.1;

ii. Umeunganisha huduma za umeme kwa Taasisi 4,036; na

iii. Umetoa ruzuku kwa kampuni binafsi 14 ili kuvipatia umeme vijiji 119 kutokana na vyanzo vya nishati jadidifu. Jumla ya ruzuku iliyokwishatolewa ni Dola za Marekani milioni 7.34 na kupelekea jumla ya vijiji 102 kati ya 119 kupatiwa umeme.

### 8.4.13. SAGCOT-CTF

Mfuko ulianzishwa kwa ushirikiano wa Serikali na Sekta binafsi (wakulima, wabia wa maendeleo, na majukwaa mbalimbali ya Kilimo) kwa lengo la kuchochea uwekezaji wa sekta binafsi katika kilimo kama soko kuu la mazao ya wakulima wadogo na kuwekeza katika kutatua changamoto za kilimo biashara. Aidha Mfuko huu umefadhili ujenzi wa ghala lenye uwezo wa kuhifadhi Tani 7,500 za mpunga katika kijiji cha Mwakanga, Kata ya Ubaruku, Wilaya ya Mbalari. Ujenzi wa ghala hili umelenga kuwawezesha wakulima waliopo kwenye Skimu ya Umwagiliaji ya Mwendamtitu kuhifadhi mpunga wao baada ya mavuno na hivyo kuweza kuendana na mahitaji ya soko kwa ujazo pamoja na kupata bei nzuri.

### 8.4.14. MFUKO WA TAIFA WA MAJI (NWIF)

Mfuko kwa mwaka 2019/2020 ulitengewa Shilingi 169,949,000,000 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maji na usafi wa mazingira katika maeneo mbalimbali nchini. Kiasi kilichopatikana ni Shilingi 124,863,295,133.58 sawa na asilimia 73 ya fedha zilizotengwa ambazo zimetumika kutekeleza miradi mbalimbali ya utoaji huduma ya maji kwenye maeneo ya vijijini na mijini pamoja na usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za maji nchini. Mfuko wa Taifa wa Maji umepanga kuanza kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa Mamlaka hizo kwa ajili ya uwekezaji kwenye miradi ya utoaji huduma ya maji.

### 8.4.15. MFUKO WA MAENDELEO YA SANAA NA UTAMADUNI

Mfuko huu unaosimamiwa na Wizara ya Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo umejikita katika kuwasaidia wasanii kujiendeleza kiuchumi kupitia masuala mbalimbali nje ya sanaa ambapo msanii yeyote mwenye wazo lolote kama vile wazo la siasa, biashara au la sanaa yenyewe ataweza kuwasilisha wazo hilo Wizarani ili liwezeshwe kupata msaada wa fedha. Mfuko unategemea kuanza kazi rasmi katika mwaka wa Fedha 2020/2021

### 8.4.16. MFUKO WA UBUNIFU VIJIJINI (RIF)

Chimbuko la Mfuko linatokana na utekelezaji wa mradi wa MIVARF, unaosimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu. Katika kutekeleza malengo ya mradi huo, moja ya malengo hayo yalikua ni ushirikishwaji na uwezeshwaji kifedha (finacial inclusion) kwa wananchi vijijini hasa wanaojihusisha katika kilimo kwa kuchagiza ubunifu vijijini. IlI kufanikisha azimio hilo , Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ilichagua benki ya maendeleo ya Kilimo Tanzania kuwa msimamizi wa mfuko wa RIF ambao fedha zake zinatoka Mfuko wakimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (The International Fund for Agricultural Development - IFAD). Madhumuni ya Mfuko ni kuongeza wigo wa maendeleo kwa kufadhili juhudi na mipango

inayochagiza ubunifu katika kutatua changamoto mbalimbali zinazomkabili mkulima vijijini. Mtaji wa mfuko ni USD 1,000,000. Mfuko huu bado haujaanza kazi.

### 8.4.17. MFUKO WA MADINI KWA WACHIMBAJI WADOGO NCHINI

Mwaka 2013, Wizara ya Nishati na Madini ilisaini mkataba na TIB kwa ajili ya kusimamia mfuko wa kuendeleza wachimbaji wadogo nchini ambao ulilenga kuwapa ruzuku na mikopo kwa ajili ya shughuli zifuatazo:

i. Uchimbaji
ii. Uchenjuaji
iii. Uongezaji wa thamani
iv. Shughuli nyingine zinazohusiana na uchimbaji mdogo wa madini

Awamu ya pili Wizara ya Nishati na Madini ilipokea kiasi cha dola za kimarekani milioni tatu (3) kwa ajili ya kuwawezesha wachimbaji wadogo nchini wapatao 111

**Utendaji wa Mfuko**

i. Mtaji anzia wa mfuko kwa awamu ya kwanza ulikuwa ni Dola za Kimarekani laki tano (500,000.0) kati ya hizo kiasi cha Tshs 367.8 million (kama Dola za Marekani 160,000.0) zilikopeshwa na kiasi kilichobaki kutolewa kama ruzuku.

ii. Mtaji anzia kwa awamu ya pili ulikuwa ni Dola za Kimarekani Milioni tatu (3,000,000.0) ambazo zote zilitolewa kama ruzuku. Mtaji uliopo kwa sasa ni shilingi za Tanzania 119,893,446.00

iii. Mfuko umefanikiwa kuwafikia wachimbaji wadogo nchini wapatao 124.

iv. Mfuko huu kwa sasa hautou huduma

### 8.4.18. MFUKO WA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA

Mfuko huu unaosimamiwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) umejikita katika kutoa huduma za ukaguzi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika ili viwe na tija na endelevu. Chanzo cha pesa za Mfuko ni ada zinazopatikana baada ya kuuza mazao ya kilimo Kutoka kwa wanachama kwenda kwa wateja.

#### 8.4.19. MFUKO WA KUDHIBITI UKIMWI

Mfuko huu unaosimamiwa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) umejikita katika kupunguza maambukizi mapya ya VVU, Vifo vinavyohusiana na UKIMWI na unyanyapaa na ubaguzi nchini.

#### 8.4.20. MFUKO WA TAIFA WA UHIFADHI WA MAZINGIRA

Mfuko huu unaosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais umejikita katika kufadhili miradi yenye kuchochea hifadhi za mazingira.

### 8.5. MIFUKO INAYOTOA DHAMANA

#### 8.5.1. MFUKO WA DHAMANA ZA MIKOPO KWA WAKULIMA WADOGOWADOGO (SCGS)

Mfuko unasimamiwa na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB). Unatoa dhamana za mikopo ya kilimo kwa wakul ima wadogo wadogo kutoka Tasisi mbalimbali za kifedha Tanzania bara na Visiwani.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Umetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 20,567,885,277.48;
ii. Wanufaika wa mikopo ni wanawake 931 waliopatiwa mikopo yenye thamani ya Shilingi 2,816,714,372.93 na wanaume 4,885 waliopata Shilingi 17,751,170,904.55;
iii. Umetengeneza ajira 3200 zimeweza kutengenezwa; na
iv. Una mtaji wa Shilingi bilioni 46.

#### 8.5.2. MFUKO WA KUDHAMINI MIKOPO KWA AJILI YA MAUZO YA BIDHAA ZA TANZANIA NJE YA NCHI (ECGS)

Mfuko ulianzishwa mwaka 2002/03 ili kuhamasisha uzalishaji kwa ajili ya mauzo nje ya nchi kwa malengo ya kuchangia kukuza pato la Serikali. Mfuko hudhamini mikopo itolewayo na mabenki kwa sekta binafsi zinazojihusisha na uzalishaji pamoja na uuzaji wa bidhaa nje ya nchi aidha wakopaji wenye miradi mikubwa yenye mahitaji ya kifedha ya kuanzia TZS 500 million na kuendelea ndio walengwa wakuu wa mfuko huu.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Ulianza na mtaji wa Shilingi bilioni 26.8 ambapo mtaji wa sasa ni shilingi bilioni 139.6;
ii. Umetumia dhamana ya Shilingi bilioni 1,358.16 kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi trilioni 1.786;
iii. Kiwango cha marejesho ya mikopo ni asilimia 97.36 ; na

iv. Kiwango cha madeni chechefu cha mfuko ni Shilingi bilioni 15.32.

### 8.5.3. MFUKO WA KUDHAMINI MIKOPO KWA WAJASIRIAMALI WADOGO NA WA KATI (SME-CGS)

Mfuko ulianzishwa mwaka 2004/05 kwa malengo ya kukuza na kuendeleza miradi midogo na ya kati (SMEs) ili kujenga mazingira ya kuwezesha wajasiriamali wenye miradi midogo na ya kati kupata mitaji kwa njia ya mikopo .

**Utendaji wa Mfuko**

i. Ulianza na mtaji wa Shilingi bilioni 5.5 ambapo mtaji wa sasa ni shilingi bilioni 21.6;
ii. Kiwango cha marejesho ni asilimia 91.51;
iii. Umetumia dhamana ya Shilingi bilioni 5.14 kutoa mikopo yenye thamani ya shs bilioni 10; na
iv. Kiwago cha madeni chechefu ni Shilingi bilioni 0.25.

### 8.5.4. MFUKO WA KUENDELEZA UMEME JADIDIFU TANZANIA (TEDAP)

Mfuko huu ulianzishwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa taasisi za kifedha ili kuwezesha upatikanaji wa umeme wa maji katika maeneo mbalimbali ya Tanzania. Malengo ya yake ni kuwezesha upatikanaji wa umeme uliozalishwa kutokana na maji katika maeneo mbalimbali ya Tanzania ambayo hayajafikiwa na umeme wa Gridi ya Taifa. Mfuko huu unatoa mikopo kwa taasisi za kifedha kwa ajili ya kusaidia upatikanaji wa umeme wa maji unaozalishwa na taasisi binafsi.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Ulianza na mtaji wa Dola milioni 23 ambapo mtaji uliopokwa sasa ni Shilingi bilioni 3.06;

ii. Mfuko umefanikisha uzalishaji wa gridi za umeme kama ifuatavyo

   a) Andoya Hydro Power -1.0 MW (Ruvuma, Mbinga)
   b) Mwenga Hydro Power - 4.0 MW (Iringa, Mafinga)
   c) Ngombeni Power project - 2.4 MW(Pwani, Mafia)
   d) Darakuta Hydro Power - 0.24 MW (Manyara, Babati)

iii. Kiwango cha madeni chechefu ni bilioni 0.25

### 8.5.5. MFUKO WA DHAMANA KWA WAJASIRIAMALI WADOGO NA WAKATI (SIDO SME-CGS)

Mfuko huu ulizinduliwa rasmi tarehe 8 Aprili 2015 kwa mkataba wa makubaliano kati ya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo ( SIDO) na Benki ya CRDB PLC kwa lengo la kuwawezesha Wajasiriamali Wadogo na Wakati waweze kupata mikopo kuendeleza miradi yao kwenye Sekta ya uzalishaji wa mazao ya Kilimo (Agro Processing).

**Utendaji wa Mfuko**

i. Umetoa udhamini wa mikopo 47 yenye thamani ya Shilingi 1,523,000,000/= kwenye mikoa ya Dar es salaam, Morogoro, Arusha, Kigoma, Mwanza, Singida, Mbeya, Njombe, Ruvuma, Kilimanjaro, Iringa, Manyara na Dodoma;
ii. Dhamana iliyowekwa ya Shilingi bilioni moja (1bn) haijapungua kwa kuwa hakuna makato ya wateja wasiolipa ambayo yamekwishafanyika; na
iii. Kuongezeka kwa mikoa tisa (9) ya utekelezaji wa mfuko imeongezeka kutoka mikoa saba (7) ya awali na kuleta hamasa kwa Wajasiriamali walengwa.

### 8.5.6. ASASI YA KUSAIDIA SEKTA BINAFSI YA KILIMO (PASS TRUST)

PASS ni chombo kilichoanzishwa Mwaka 2000 na kuanza utekelezaji kama mradi chini ya wizara ya Kilimo/Fedha ili kuchochea uwekezaji na kukuza kilimo cha biashara na sekta zinazohusika. Baada ya ufanisi wake kuonekana, ilisajiliwa mwaka 2007 kama asasi isiyokuwa ya Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Ushirikishaji Wadhamini ya mwaka 2002.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Umedhamini miradi 4,404 yenye thamani ya Shilingi bilioni 71.5 na kunufaisha wananchi 62,749 kati ya hao wanawake ni 18,719 na wanaume ni 41,030;

ii. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2000, PASS imewezesha uwekezaji katika sekta ya kilimo kiasi cha Shilingi bilioni 916.4 na wanufaika ni 1,196,891. Zaidi ya watanzania 2,531,909 wameajiriwa mpaka sasa kupitia jumla ya miradi 36,007;

iii. Umetengeneza Ajira zipatazo 89,079;

iv. Umeanzisha kituo atamizi cha Kongwa mkoani Dodoma chini ya usimamizi wa TALIRI ambacho kinachukua vijana 10 na mabanda 5 yanayochukua mbuzi 200. Lengo ni kufikia mabanda 10 yanayochukua mifugo 2,000; na

v. Umeandaa ekari 10 kwajili ya kilimo cha nje katika eneo la chuo kikuu cha Sokoine Morogoro ambapo hatua ya maandalizi ni nzuri. Eneo hilo litachukua vijana 50 kwenye

kilimo cha mboga mboga na matunda, na mazao mengine yenye soko na tija kwa eneo husika kuanzia mwezi Juni 2020.

### 8.5.7. MFUKO WA KUSAIDIA MAKANDARASI (CAF)

Bodi ya Usajili wa Makandarasi ilianzisha mfuko wa kusaidia Makandarasi (Contractors Assistance Fund – CAF) mwaka 2002 kwa lengo la kusaidia Makandarasi wazalendo wa madaraja madogo kupata dhamana za zabuni na malipo ya awali. Bodi inashirikiana na Benki kutoa dhamana hizi.

Mfuko umeendelea kuwa na mtaji wa Shilingi bilioni 3.75 kwa mwaka 2019/20. Aidha idadi ya wanachama wa Mfuko ilipungua kutoka 1,186 mwaka wa fedha 2018/19 hadi kufikia 1,134 mwaka 2019/2020. Kushuka kwa idadi ya wanachama kumetokana na zoezi la kufuta makandarasi waliokosa sifa ya kuendelea na ukandarasi kwa mujibu wa sheria iliyofanyiwa marekebisho mwishoni mwa mwaka 2019.

### 8.5.8. MFUKO WA MIKOPO MIDOGO YA NYUMBA (HMF)

Mfuko wa Kuwezesha utoaji wa mikopo midogomidogo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kwa watu wa kipato kidogo (Housing Microfinance Fund (HMFF)) unaendeshwa kama sehemu ya Mradi wa Mikopo ya Nyumba (*Housing Finance Project).* Mradi huu unaendeshwa na kusimamiwa na Benki Kuu kwa mujibu wa Mkataba kati ya Serikali na Benki Kuu (*Subsidiary Loan Agreement*).

**Utendaji wa Mfuko**

i. Mikopo yenye thamani ya Shilingi 17,870,000,000/= (sawa na dola za Marekani 8,089,950.79) imekwishatolewa kwa benki na taasisi za fedha kwa ajili ya kuwakopesha wananchi walengwa.
ii. Jumla ya wananchi walengwa wanaokadiriwa kufikia 700 wamefaidika na mikopo hii.
iii. Mfuko umefanikiwa kutoa elimu kwa benki, taasisi za fedha na wananchi juu ya uwepo wa Mfuko huu.

### 8.5.9. MFUKO WA KUPAMBANA NA UMASKINI NA KUONGEZA AJIRA (JK FUND)

Lengo la Mfuko huu lilikuwa ni kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa kutumia taratibu za kibenki kuwawezesha wananchi kiuchumi, wakiwemo wajasiriamali wadogo na wa kati (micro, small and middle entrepreneurs), wajasiriamali wa vijijini na mijini ili kuanzisha na kuendeleza miradi inayolenga kuongeza kipato, tija na fursa za ajira.

Hadi kufikia Juni 2014, Mpango huu (kwa awamu zopte mbili) ulikuwa umetoa mikopo yenye thamani ya **shilingi bilioni 50.06** na kuwanufaisha Wajasiriamali **76,546** ambapo urejeshaji wa mikopo ulikuwa asilimia **84**.

**Changamoto za Mpango**

i. Wakopaji walio wengi hawakuwa na elimu ya kutosha ya ujasiriamali ambayo ingewasaidia katika kupanga matumizi bora ya mikopo waliyopewa;
ii. Dhana potofu iliyoenezwa kuwa fedha za Mpango huo zilikuwa zawadi ya Rais kwa wananchi kwa kumpigia kura na kumwezesha kuwa Rais na hivyo sio mikopo ambayo inapashwa kurejeshwa;
iii. Baadhi ya maafisa wa benki kutokuwa waaminifu na kula njama za kuiba fedha za mpango huo;
iv. Kutokuwepo kwa dhamana zilizowekwa na wakopaji (dhamana ilikuwa imebebwa na Serikali) kulifanya mabenki yashindwe kukamata mali za wadaiwa
v. Wakopaji kubadili malengo ya awali waliyoombea mikopo na hivyo kujikuta wakipoteza fedha walizokopa;
vi. Baadhi ya SACCOS kuweka kiwango kikubwa cha riba kwa mikopo iliyotolewa kwa wanachama wake kuliko kiwango kilichowekwa chini ya Mpango huo hivyo kuwaumiza wananchi;

### 8.5.10. MFUKO WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI WA MWANANCHI (MEF)

Kifungu 16 (1) cha Sheria ya Uwezeshaji Wananchi kiuchumi namba 16 ya mwaka 2004 kinaelekeza kuanzishwa kwa Mfuko wa Taifa wa Uwezeshaji wa Mwananchi (MEF). MEF ni moja ya mifuko ya uwezeshaji iliyotajwa katika Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 ambayo inatumiwa na Serikali kusaidia utekelezaji wa jitihada mbalimbali za uwezeshaji wananchi kiuchumi. MEF hasa inasaidia katika kuondoa vikwazo vinavyosababisha ukosefu wa mitaji na mikopo kwa wananchi wajasiriamali.Mfuko unafanya kazi ya kutoa dhamana za mikopo kwa kushirikiana na Taasisi za fedha ambap mpaka sasa umefanya kazi kwa kushirikiana na CRDB Micrifinance, TPB Bank, UTT MFI na TIB Development Bank

**Utendaji wa Mfuko**

i. Hadi kufikia Desemba 2018 mikopo iliyokuwa imedhaminiwa na Mfuko wa MEF ni kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 17: Mikopo iliyodhaminiwa na MEF kufikia Desemba 2018**

| Na. | Taasisi ya Fedha | Mikopo iliyotolewa |
|---|---|---|
| **1** | TPB | 2,682,334,333.00 |
| **2** | CRDB | 10,658,549,080.00 |

| | | |
|---|---|---|
| **3** | UTT MFS | 50,000,000.00 |
| **4** | TIB | 18,700,000.00 |
| **5** | **JUMLA** | **13,409,583,413.00** |

ii. Mikopo hii imewanufaisha wajasiriamali 31,948 kati yao wanawake 20,832 na wanaume 11,116 na hali ya marejesho ya mikopo ni 93%

iii. Mfuko huu hautoi huduma kwa sasa.

### 8.5.11. MFUKO WA TAIFA WA KUENDELEZA WAJASIRIAMALI WANANCHI (NEDF)

Mfuko ulianzishwa mwaka 1994 kwa Azimio la Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Madhumuni ya mfuko huu ni kutoa mikopo kwa wenye viwanda vidogo na wafanyabiashara wadogo Tanzania Bara kwa lengo la kuondoa umaskini kwa kuanzisha na kuendeleza miradi yao katika sekta ya uzalishaji inayohusika na viwanda vidogo, kilimo na kusindika vyakula (matunda na mboga), ufugaji, uvuvi na madini, sekta ya biashara inayohusika na uuzaji wa vyakula na vinywaji, maduka ya bidhaa mchanganyiko na Sekta nyinginezo kama vile afya (maduka ya dawa baridi), huduma za uchapishaji, ujenzi, utalii na uchukuzi.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Mfuko ulianza na mtaji wa Shilingi bilioni 5.05 na sasa una mtaji wa Shilingi bilioni 8.2

ii. Umetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 2.8 ambapo Wanaume 687 waliopata mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.5 na wanawake 723 walipata mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 1.3 katika mikoa yote Tanzania bara.

iii. Umetoa jumla ya ajira 4,471, miongoni mwa ajira hizo Wanaume ni 2,034 na wanawake 2,437.

iv. Umetoa mafunzo kwa wanawake 723 na wanaume 687.

v. Kiwango cha marejesho ya mikopo ni asilimia 91.6.

### 8.5.12. SELF MICROFINANCE (SELF MF)

Mfuko ulisajiliwa rasmi tarehe 04/09/2014 kwa Sheria ya Kampuni ya mwaka 2002 chini ya Udhamini wa Serikali '*Company Limited by Guarantee'*na kupata Hati ya Usajili namba 112091 kwa jina la *SELF Microfinance Fund (SELF MF)*. Lengo kuu la Mfuko ni kukuza na kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wananchi wenye kipato cha chini, hususan waishio vijijini, hivyo kuwapa fursa ya kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali kujiongezea kipato na hatimaye kuondokana na umaskini.

Mfuko unatekeleza lengo hilo kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu pamoja na mafunzo ya tija kwa Asasi na wajasiriamali wadogowadogo hususan wa vijijini. Mfuko unawafikia wajasiriamali kwa kupitia asasi ndogo na za kati za fedha. Aidha Mfuko wa SELF unatoa huduma nchi nzima kupitia ofisi nne za kanda na kituo kimoja cha huduma.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Mfuko ulianza na mtaji wa awali wa Shilingi 42,189,302,000.00 uliotolewa na Serikali kama mkopo wenye masharti nafuu toka Benki ya Maendeleo ya Afrika ambapo mtaji wa sasa ni Shilingi 68.9 bilioni;

ii. Umetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 29.838 ambapo Shilingi bilioni 4.3 zilielekezwa katika kilimo na Shilingi bilioni 25.5 zilielekezwa katika viwanda Vidogo;

iii. Umetoa mafunzo kwa watendaji 72 kutoka katika Asasi 36; na

iv. Kiwango cha urejeshaji mikopo ni asilimia 94.

### 8.5.13. MFUKO WA DIRISHA LA KILIMO KWANZA (KKCF)

Mfuko ulianzishwa mwaka 2009 chini ya Usimamizi wa Benki ya TIB. Mfuko unatoa mikopo kwa wakulima wadogo na wa kati, Taasisi ndogo za fedha na vyama vya ushirika (SACCOS). Mikopo kwa Bidhaa zinazonunuliwa na mikopo ni vifaa na pembejeo za kilimo kama trekta na mitambo ya umwagiliaji na magari ya kubebea mazao, mitambo ya upandaji na uvunaji wa mazao n.k.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Hadi mwezi Desemba,2019 Mtaji wa Mfuko umeweza kukua na kufikia Shilingi bilioni 65.4 kutoka Shilingi bilioni 42;
ii. Marejesho ya Shilingi bilioni 1.49 yaliweza kukusanywa kutoka kwa wakulima;
iii. Wakopaji wanne waliweza kumaliza mikopo yao; na
iv. Kiasi cha Shilingi bilioni 2.0 kilikopeshwa kwa wateja mbalimbali.

### 8.5.14. MFUKO WA USAMBAZAJI MAJI KWA MFUMO WA UMEME JUA

Mfuko huu ulianzishwa ili kusaidia jumuiya za watumia maji kutoka kwenye mfumo wa kutumia diseli kama chanzo cha nishati kwa mashine za kusukuma maji na kwenda kwenye umeme jua kwa ajili ya kusukuma maji ili kuongeza ufanisi wa upatikanaji maji safi na salama. Pamoja na kupunguza gharama kubwa za uendeshaji wa mradi na kuweka mifumo ya malipo kabla ya matumizi kwa ajili ya kukuza na kudhibiti mapato yaliyokuwa yanayopotea kutokana na mfumo wa uliopo sasa, mfuko umelenga kuhudumia zaidi ya kaya elfu 55,998 kwa mkoa wa

Dodoma na kaya elfu 44,323 kwa mkoa wa Singida kwa kipindi cha miaka 4 ya utekelezaji wa miradi kama ifuatavyo:

i. Dodoma - Jumuiya za watumia maji 39;

ii. Singida- Jumuiya za watumia maji 43; na

iii. Mtwara, Shinyanga, Tabora, Kagera, Mara, na Lindi - Jumuiya za watumia maji 83.

### 8.5.15. MFUKO WA MAENDELEO YA VIJANA (YDF)

Mfuko ulianzishwa na Serikali mwaka 1993 chini ya Sheria ya Fedha (The Exchequer and Audit Ordinance, cap 439), namba 21 ya mwaka 1961 kifungu cha 17 (1). Lengo la kuanzishwa kwa Mfuko huu ni kuwawezesha vijana wote nchini (Tanzania Bara) kupata mitaji kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu ili kuanzisha au kuendeleza miradi yao ya uzalishaji mali. Kupitia utaratibu huu, vijana huwezeshwa kujitegemea, kupunguza umasikini wa kipato na kujiajiri wenyewe. Aidha, mikopo itolewayo kupitia mfuko huu huwasaidia vijana kujenga tabia ya kukopa kwa busara na kurejesha kwa wakati. Mfuko huu umefaikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 5,434,641,000 kwa miradi (Vikundi) 899 vyenye wanachama 26,970. Mfuko huu unasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu.

### 8.5.16. MFUKO WA TAIFA WA WATU WENYE ULEMAVU (NFPD)

Mfuko huu umeanzishwa chini cha sheria na.9 ya watu wenye ulemavu ya mwaka 2010. Mfuko una kanuni ambazo zinategemewa kusainiwa hivi karibuni na unaendelea kufanya yafuatayo;

i. Serikali imepanga kuingiza Shilingi milioni 100 kwenye mfuko kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha kwa bajeti ijayo ya 2020/21 imepanga kuingiza Shilingi milioni200; na
ii. Mfuko unaendelea kutafuta wadau kwa ajili kuongeza nguvu ya kutatua changamoto ya Bajeti

### 8.5.17. MFUKO WA MZUNGUKO WA MKOA (RRF)

Mfuko huu ulianzishwa mwaka 1997 kwa maelekezo ya Bodi ya SIDO baada ya kufungwa kwa Mfuko wa Karadha (Hire Purchase) ambapo kila Mkoa uliendeleza fedha za RRF kwa fedha zilizokua zinakusanywa kutoka kwa wateja wa mfuko wa Karadha.

Madhumuni ya mfuko huu ni kutoa mikopo kwa wenye viwanda vidogo na vya kati na wafanyabiashara wadogo na wakati Tanzania Bara kwa lengo la kuanzisha na kuendeleza miradi yao katika sekta ya uzalishaji inayohusika na viwanda Vidogo, Kilimo na kusindika vyakula, ufugaji, uvuvi na madini, sekta ya biashara inayohusika na uuzaji wa vyakula na vinywaji, maduka ya bidhaa mchanganyiko.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Mtaji anzia wa Mfuko ni Shilingi bilioni 0.6 na mtaji wa sasa ni Shilingi bilioni 1.1;

ii. Mfuko umetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni 0.43;
iii. Marejesho ya mikopo ni asilimia 89.3;
iv. Kiwango cha madeni chechefu cha mfuko ni asilimia 32

### 8.5.18. MFUKO WA MIKOPO YA NYUMBA KWA WATUMISHI WA SERIKALI (RHLF)

Serikali ilianzisha Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa watumishi wake (Revolving Housing Loan Fund) Kwa Waraka wa Utumishi wa Umma Na. 8 wa mwaka 1992 ili kuwawezesha kupata mikopo yenye masharti kama ilivyokuwa mwanzo kwa ajili ya kujenga, kukarabati au kununua nyumba. Mfuko uliendelea kutoza riba ya mkopo ya asilimia 3 kwa mwaka ambayo haibadiliki (*flat rate*) ndani ya muda wote wa mkopo.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Mfuko ulianza na mtaji wa Shilingi Milioni **300** hadi kufikia Desemba, 2019 mtaji ulikuwa umefikia Shilingi Bilioni **8.93;**
ii. Makusanyo ya marejesho ya mikopo kutoka Julai hadi Desemba 2019 ni Sh. 210,788,326.28;
iii. Wastani wa urejeshwaji wa mikopo ni kiasi cha Shilingi 43,000,000.00 kwa mwezi; na
iv. Maombi ya mikopo yaliyopokelewa kwa kipindi hicho ni 121 yenye thamani ya Shilingi 2,013,400,000.00. Maombi haya yanaendelea kushughulikiwa kwa kukamilisha taratibu za kutoa mikopo.

### 8.5.19. MFUKO WA MAENDELEO YA WANAWAKE (WDF)

Mfuko ulianzishwa kutokana na Azimio la Bunge lililopitishwa Agosti, 1993 na kwa mujibu wa kifungu 17 (1) cha Sheria ya Exchequer and Audit Ordinance (Cap 439) ya mwaka 1961 ambapo ulianza kufanya kazi mwaka 1993/94 ili kuwezesha wanawake kiuchumi kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake wasio na vigezo au sifa za kukopesheka katika taasisi za fedha. Mfuko huu unasimamiwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Mfuko umeweza kukuza mtaji toka Shilingi 515,628,846.00 hadi kufikia Shilingi 1,276,844,995.79;
ii. Kiasi cha Shilingi 33,197,748 cha marejesho ya mikopo kilikusanywa kwa kipindi cha kuanzia Julai-Desemba, 2019; na
iii. Mafunzo ya Ujasiriamali na uendeshaji wa biashara yametolewa kwa wanawake 542.

### 8.5.20. MFUKO WA PEMBEJEO WA TAIFA (AGITF)

Mfuko ulianzishwa mwaka wa 1994 kwa Sheria ya Bunge Na. 9 ya mwaka wa 1994. Kuanzishwa kwake kulitokana na sababu mbalimbali zilizoathiri upatikanaji wa pembejeo za kilimo, mifugo na Uvuvi, hususani kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo wadogo.

**Utendaji wa Mfuko**

i. Kuanzia mwezi Julai 2019 hadi Desemba 2019 mfuko umeweza kutoa jumla ya mikopo 93 yenye thamani ya Shilingi 837,059,000 kwa wanawake 43 na wanaume 50;
ii. Tangu mfuko ulipoanzishwa hadi Desemba, 2019 umetoa mikopo 3606 yenye thamani ya Shilingi 83,608,610,770; na
iii. Wastani wa ajira 10,230 zilizalishwa kwa kipindi cha mwaka 2015-2020.

### 8.5.21. BODI YA MIKOPO YA WANAFUNZI WA ELIMU YA JUU (HESLB)

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ilianzishwa na Sheria ya HESLB (SURA 178) mwaka 2004 na kuanza rasmi utekelezaji wa majukumu yake mwezi Julai, 2005.

Katika mwaka wa masomo 2019/2020, Serikali imetoa mikopo ya elimu ya juu yenye jumla ya thamani ya TZS 450 bilioni kwa wanufaika 132,119 wanaosoma katika taasisi mbalimbali za elimu ya juu hapa nchini. Fedha hizi zinagharamia vipengele sita ambavyo ni chakula na malazi; ada; vitabu na viandikwa; utafiti; mafunzo kwa vitendo; na mahitaji maalum kwa baadhi ya vitivo.

### 8.5.22. MFUKO WA MABADILIKO YA TABIANCHI (GCF)

Mfuko huu unaosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais unalenga kutatua changamoto ya upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu kwa miradi inayolenga kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hapa nchini. Ofisi inaendelea kuhamasisha Taasisi za Umma na Sekta Binafsi hapa nchini kuomba ithibati (accreditation) ya kusimamia fedha za miradi ya mabadiliko ya tabianchi zinazotolewa na Mfuko huu, Aidha kupitia uhamasishaji huo Benki ya CRDB imepata ithibati mwezi Novemba, 2019, hivyo kuwa na uwezo kusimamia fedha za miradi kwa ufadhili wa Mfuko huo. Hatua hii itasaidia kuongeza ushiriki wa Sekta Binafsi katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi hapa nchini.

### 8.5.23. MFUKO WA UFILISI WA BENKI YA NYUMBA (THB)

Mnamo Agosti 1995 Serikali iliweka benki ya nyumba (Tanzania Housing Bank -THB) chini ya ufilisi na Mr. Simon Matafu aliteuliwa kuwa msimamizi wa THB. Mwaka 1997, TIB Development Bank iliteuliwa kusimamia ufulisi huo kwa niaba ya mfilisi wa awali. Mnamo

Agosti 2005 serikali ilisitisha rasmi usimamizi wa Mr Simon Matafu. Malengo muhimu yalikuwa kusimamia ukusanyaji wa mikopo ya wateja wa THB na kutoa Hati mara baada ya kuthibitisha mkopo umelipwa pamoja na kusimamia uendeshaji wa kesi zilizokuwa zinaendelea za wateja wa THB kuhakikisha zinakamilika.Mfuko huu hautoi huduma mpya kwa sasa zaidi ya kufuatilia madeni kutoka kwa wadaiwa.

### 8.5.24. MFUKO WA JAPAN WA UAGIZAJI BIDHAA KUTOKA NJE (CIS)

Mnamo Septemba 2002, Benki ya Maendeleo TIB iliteuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kusimamia ukusanyaji wa madeni ya mikopo iliyokuwa imetolewa na Serikali kupitia Wizara ya Fedha chini ya Mfuko wa Serikali ya Japani kwa ajili ya uagizaji bidhaa kutoka nje ya nchi [Japanese Commodity Import Support – (CIS)]. Jukumu kubwa la benki ni kufuatilia urejeshaji wa madeni yaliyokuwa yametolewa na kuhakikisha fedha inayokusanywa inawasilishwa Wizara ya Fedha kuanzia mwaka 2002. Kiasi cha mikopo iliyopokelewa na TIB kwa ajili ya kukusanya mwaka 2002 ilikuwa jumla ya shilingi bilioni 16.8 sawa na fedha ya kijapani bilioni 1.53 (JPY 1.53 bilioni). Mfuko huu hautoi huduma mpya kwa sasa zaidi ya kufuatilia madeni kutoka kwa wadaiwa.

### 8.5.25. MFUKO WA KUSAIDIA KILIMO CHA MAUA NA MBOGAMBOGA

Mwaka 2003 hadi 2009, Serikali ilibainisha makampuni yanayojihusisha na kilimo cha maua na mbogamboga kwa ajili ya kuuza ndani na nje nchi ili kuwezesha wakulima kuongeza uzalishaji na uuzaji wa mbogamboga na maua ndani na nje ya nchi ili kuliongezea taifa fedha za kigeni na kuinua uchumi kwa ujumla. Makampuni hayo ni Kiliflora Limited, Tanzania Flowers Limited (TFL), Arusha Blooms Limited (ABL), Tengeru Flowers Limited (TEFLO), Tanzania Flowers Limited na Hortanzia Limited.

Malengo muhimu yalikuwa yafuatayo:

i. Kuongeza uzalishaji ili kufikia kiwango cha kuwezesha upatikanaji wa ndege za mizigo za kusafirisha mazao hayo nje ya nchi kupitia uwanja wa ndege wa kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) badala ya kupitia nchi jirani.

ii. Kuwezesha nchi kupata fedha za kigeni (foreign exchange).

iii. Kukuza sekta ya kilimo cha maua na mbogamboga kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi baada ya mazao mengine kama vile katani, pamba, kahawa, kushuka sana uzalishaji kufuatia kushuka kwa bei katika soko la dunia.

iv. Kutoa ajira za kutosha kwa kuwa kilimo hiki kinahitaji nguvu kazi kubwa (Labour Intensive).

v. Uboreshaji wa maendeleo ya jamii katika maeneo yanayojishughulisha na kilimo kama vile elimu, afya n.k

Jumla ya mikopo iliyokuwa imetolewa na Serikali ilifikia shilingi bilioni 50.5. Kufuatia maamuzi hayo, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Benki Kuu, iliiteua TIB ili kushirikiana na wadau wengine kusimamia mikopo iliyotolewa. TIB imeendelea kusimamia zoezi hili na kutoa taarifa pamoja na mapendekezo mbalimbali Wizara ya Fedha kupitia Benki Kuu. Pamoja na changamoto mbalimbali madeni yameendelea kulipwa na kuwasilishwa Wizara ya Fedha kupitia Benki Kuu kama inavyotakiwa.

### 8.5.26. MFUKO WA KIWANDA CHA NYAMA (SAAFI)

Mnamo April 2008, Serikali kupitia benki kuu (BOT) iliiteua benki ya TIB kusimamia uendeshaji wa kiwanda ambapo serikali ilitoa jumla ya kiasi cha shilingi billioni 14.59 kama mtaji wa ujenzi wa kiwanda, uagizaji wa mitambo, magari pamoja na kununua ngombe.

Hata hivyo uendeshaji wa kiwanda hiki umekuwa na changamoto nyingi kwa kipindi chote kiasi cha kufanya uzalishaji wake usiwe wa kuridhisha na hivyo kusababisha kusimama kabisa kwa utendaji wake. Kati ya changamoto hizo ni pamoja na:-

i. Uongozi duni wa kampuni kushindwa kusimamia uendeshaji wa kiwanda kwa ufanisi (kwa mfano, mwenyekiti wa bodi kuingilia mipango na watendaji),
ii. Vilevile matumizi yasiyo sahihi ya mali za kiwanda (magari) na fedha za mauzo na za uendeshaji wa kiwanda.
iii. Magonjwa ya mifugo yaliyosababisha vifo kwa ng’ombe zaidi ya 400 kwa wakati mmoja.

Hadi kufikia mwezi Oktoba 2017 deni la SAAFI lilifikia shilingi 27,778,194,484, sababu za kupanda kwa deni hili ni kutokana na mkopo huu kutolipwa na pia ongezeko la riba na adhabu za kuchelewa kulipa, kutokana na hali hii Serikali mnamo Julai 2017 iliunda kamati tendaji inayojumuisha timu kutoka TIB,Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kutoka ofisi ya Msajili wa Hazina chini ya uenyekiti wa Msajili wa Hazina (Treasurar Registrar) ili kufanya upembuzi yakinifu wa mradi ili kuufufua na kuhakikisha unaendeshwa kiufanisi. Kamati hii imetoa mapendekezo kwa serikali ikiwa ni pamoja na uwezekano wa kupata mbia mwingine atakaesimamia uongozi na kuingiza fedha za uendeshaji wa mradi.

### 8.5.27. MFUKO WA TAIFA WA UMWAGILIAJI

Mfuko huu unaosimamiwa na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji umenzishwa kwa lengo la kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kukuza kilimo cha umwagiliaji nchini. Mfuko huu unategemea kuanza kutoa huduma katika mwaka wa fedha 2020/2021

## 8.6. PROGRAMU ZA UWEZESHAJI

### 8.6.1. UTT AMIS

UTT ilianzishwa chini ya Sheria ya Udhamini Sura Na. 318 ya Sheria za Tanzania. Malengo yake yameainishwa katika waraka ulioanzisha chombo hiki yaani Deed of Trust, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha utamaduni wa kuweka akiba miongoni mwa Watanzania. Kuanzisha na kuendesha Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja. Kwa ujumla, malengo ya UTT yanahusisha uwezeshaji (empowerment). Uwezeshaji ni dhana pana ambayo inaweza kutekelezwa kwenye sekta mbalimbali za kitaifa kwa mipango ya aina nyingi. UTT ni taasisi iliyoko kwenye sekta ya masoko ya mitaji na hivyo kufanya kazi zake chini ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana.

**Jedwali Na. 18: Programu mbalimbali za uwezeshaji zilizopo UTT AMIS**

| NA | MFUKO | UTENDAJI WA MFUKO |
|---|---|---|
| 1 | Mfuko wa Ukwasi | i. Mfuko umefikia ukubwa wa Shilingi bilioni 84.6 kutoka Shilingi bilioni 0.7 mwaka 2013.<br>ii. Thamani ya kipande imeongezeka kwa Shilingi 135 na kufikia Shilingi 235 kwa kipande ikilinganishwa na kiasi cha Shilingi 100 mwaka 2013. |
| 2 | Mfuko wa Watoto | i. Mfuko umefikia ukubwa wa Shilingi bilioni 3.3 ukilinganisha na Shilingi bilioni 0.7 kwa mwaka 2013<br>ii. Thamani ya kipande imeongezeka kutoka kiasi cha shilingi 262 kwa kipande na kufikia shilingi 362 |
| 3 | Mfuko wa Wekeza Maisha | i. Thamani ya kipande imeongezeka kutoka shilingi 337 kwa kipande na kufikia kiasi cha shilingi 437<br>ii. Ukubwa wa mfuko umeongezeka kutoka Shilingi bilioni 0.6 na kufikia Shilingi bilioni 1.2. |
| 4 | Mfuko wa Umoja | i. Mfuko umenakili ongezeko kutoka shilingi bilioni 113 na kufikia Shilingi bilioni 221.<br>ii. Thamani ya kipande kwa kipindi chote imeongezeka hadi kufikia Shilingi 616 kutoka 100 mwaka 2005 ongezeko ambalo ni zaidi ya mara sita ya mtaji wa awali. |
| 5 | Mfuko wa Jikimu | i. Ukubwa wa mfuko wa kujikimu umeongezeka kutoka Shilingi bilioni 0.7 hadi kufikia Shilingi bilioni 17.8.<br>ii. Thamani ya kipande imeongezeka na kufikia kiasi cha Shilingi132, mwezi Machi 2020 ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 32 kutoka mwaka 2008 kipande kilipouzwa kwa mara ya kwanza kwa Shilingi 100.<br>iii. Mfuko umelipa wawekezaji gawio (income distribution) lenye zaidi ya thamani ya Shilingi Bilioni 10.2, |

| | | |
|---|---|---|
| 6 | Mfuko wa Hati Fungani | i. Ulianzishwa mwezi Septemba 2019 na kufanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 16 wakati dirisha la mauzo ya awali lilipofungwa mwezi oktoba 2019<br>ii. Kiwango cha ongezeko la ukubwa wa mfuko ni Shilingi bilioni 18.7 na kiwango cha faida tangu kuanzishwa hadi Machi 2020 ni asilimia 13.<br>iii. Mfuko wa hati fungani umelipa gawio lenye jumla ya thamani ya Shilingi bilioni 0.3 ikiwa ni sawa na malipo ya Shilingi 3 kwa kila kipande. |

### 8.6.2. MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI ZA WANYONGE TANZANIA (MKURABITA)

MKURABITA ilianzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Novemba, 2004 kwa Tamko la Rais wa Serikali ya Awamu ya Tatu, Mh. Benjamin William Mkapa. Aidha, Serikali kwa kumtumia Mshauri Elekezi kutoka Taasisi ya "Institute for Liberty and Democracy (ILD)" ya Peru Iliyoongozwa na mchumi maarufu Hernando de Soto na washauri wa Kitanzania ilipanga kutekeleza Mpango huu kwa awamu nne (4). Mfuko huu umetekeleza yafuatayo:-

i. Wakulima 180 na viongozi 22 wa Vyama vya wakulima wamejengewa uwezo wa kutumia Hati za Haki Miliki za Kimila kupata Mitaji katika Benki na Taasisi zingine za Fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa katika Vijiji vya Mvumi na Magubike. Aidha, mafunzo yaliyotolewa yamewezesha Wakulima 48 kufungua akaunti katika benki;

ii. Huduma za Urasimishaji wa Biashara zimesogezwa kwa wananchi kwa kuanzisha Vituo vya Huduma kwa Pamoja katika Manispaa ya Tabora na Mji wa Babati ambapo huduma muhimu za utoaji leseni za biashara, utoaji wa Namba ya Utambulisho wa Mlipa kodi (TIN) kupitia TRA, usajili wa jina la biashara kupitia BRELA, huduma za benki na mifuko ya hifadhi ya jamii zinapatikana sehemu moja. Aidha, wafanyabiashara 1,529 wamepata mafunzo ya urasimishaji na uendeshaji wa biashara. Katika kipindi husika Vituo vimesajili biashara 396 na wafanyabiashara 420 wamefungua akaunti katika benki kwa ajili ya kuweka akiba na kukopa fedha ili kujiongezea mitaji. Uwekaji wa huduma za Urasimishaji wa Biashara kwa wananchi kwa kuanzisha vituo katika Halmashauri ya Manispaa ya Nyamagana pamoja na Miji ya Kahama na Songea umeanza;

iii. Zoezi la Urasimishaji wa Ardhi Mijini kwa dhana ya Mfuko Endelevu wa Wilaya limeanza kwa kufanya utambuzi wa milki 200 kati ya 1,000 zilizopangwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa;

iv. Hati za Haki Milki za Kimila 159 katika kijiji cha Inzomvu kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa zimetolewa;

v. Wamiliki 526 wenye Hati za Hakimiliki za kimila wametumia hati kama dhamana na kupata mikopo kwenye mabenki yenye thamani ya Shilingi bilioni 4.99. Aidha, vyama vitano (5) vya wakulima vimedhamini wakulima kupata mikopo ya thamani ya Shilingi milioni 625.9;

vi. Wamiliki 93 waliorasimisha viwanja vyao mjini wametumia hati miliki kupata mikopo ya thamani ya Shilingi bilioni 3;

vii. Mipango ya Matumizi ya Ardhi 102 imeandaliwa na kupunguza migogoro katika vijiji 102 inayohusu wakulima na wafugaji, kijiji na kijiji pamoja na kijiji na hifadhi;

viii. Wananchi 88 katika Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi wamefungua makampuni matano (5) ya biashara yatakayojishughulisha na uanzishaji na uendeshaji wa viwanda vya kusindika karanga, kuchakata pamba, kuchakata ngozi na kusindika alizeti;

ix. Wananchi 48 katika Halmashauri ya Wilaya ya Urambo wamefungua kampuni moja ya biashara itakayojishughulisha na uchakataji na uuzaji wa asali; na

x. Kuwezesha wafanyabiashara 2,300 kurasimisha biashara zao na kupata mikopo ya thamani ya Shilingi bilioni **1.1** kwa ajili ya kuongeza mitaji biashara.

### 8.6.3. MFUKO WA KUENDELEZA SEKTA YA FEDHA TANZANIA (FSDT)

Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Fedha ni taasisi ya Kitanzania, inayojikita (pamoja na wadau mbali mbali) katika kutafuta njia za kuhakikisha upatikanaji na utumiaji wa huduma za kifedha unaongezeka na kuwa endelevu ili Watanzania wengi wapate fursa ya kuzitumia huduma bora za kifedha kwa ajili ya kujiletea maendeleo yao, kuongeza tija katika uzalishaji na ujasiliamali, hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi kwa ujumla. FSDT ilianzishwa mwaka 2004 na kuanza kazi rasmi mwaka 2005. FSDT imesajiliwa chini ya Sheria ya Muunganisho wa Wadhamini Sura 318.

Malengo ya FSDT ni kama ifuatavyo:

i. Kuona mazingira ya sera, sheria na taratibu za uendeshaji wa masoko ya fedha na huduma zake unaimarika ili kuharakisha upatikanaji na utumiaji wa huduma za kifedha nchini;
ii. Kuona miundo mbinu ya usambazaji wa huduma za kifedha inakua, inaimarika na kuwa karibu na watu au biashara ili zitumike kuleta manufaa mapana;
iii. Kupanua upatikanaji na kuboresha bidhaa na huduma za kifedha mahususi kwa wajasiliamali na biashara zao; na
iv. Kupanua upatikanaji na kuboresha bidhaa na huduma zinazowalenga watu wa kipato cha chini na kaya maskini hasa waishio vijijini.

**Matokeo ya Utendaji wa Mfuko**

i. Kumekuwa na matokeo chanya katika upatikanaji na utumiaji wa huduma za kifedha nchini kwa ujumla. Tanzania imepiga hatua kubwa katika kipindi cha miaka minne (2013-2017). Kwa mfano idadi ya watanzania wanaotumia huduma za kifedha imekua kutoka asilimia 58% hadi 65% kati ya mwaka 2013 na 2017 kulingana na taafira ya FinScope Tanzania 2017

ii. Imefanikisha katika kutengeneza Mkakati wa Huduma Jumuishi za Kifedha uliozinduliwa mwezi Desemba 2017, wa Sera mpya ya Huduma Ndogo za Kifedha (National Microfinance Policy 2017) iliyozinduliwa mwezi Octoba 2017 na Sheria yake

iii. Kwa kushirikiana na Serikali imefanikisha kutungwa kwa sheria ya mifumo ya malipo nchini pamoja na kanuni zake (NPS Act, Licensing rules and regulations) na kutengeneza Mpango wa Elimu ya Fedha kwa wananchi (Financial Education Framework);

iv. FSDT imesaidia kuimarika kwa ujuzi na kuongezeka kwa ufahamu na utaalamu wa uendeshaji wa masoko ya fedha nchini Tanzania kupitia mafunzo, tafiti, au kugharamia utaalamu;

v. Ushirikiano kati ya taasisi za serikali na sekta binafsi katika sekta ya fedha umeimarika zaidi hasa kupitia Baraza la Taifa la Huduma Jumuishi za Kifedha Shirikishi (yaani National Financial Inclusion Council). Ushirikiano huu umewezesha kupatikana kwa Mkakati wa Pili wa Huduma Jumuishi za kifedha nchini (yaani National Financial Inclusion Framework 2018-2022); na

vi. Tanzania imekuwa miongoni wa nchi zilizoshika nafasi ya juu katika maboresho ya mazingira ya sekta ya Fedha na kukua kwa kasi kwa huduma za kifedha kwa njia za kidijitali na kupelekea nchi zingine kujifunza kutoka Tanzania. FSDT imekuwa moja ya taasisi zinazoeneza mafanakio hayo.

### 8.7. CHANGAMOTO ZA MIFUKO

Kila Mfuko umeeleza changamoto zake na kuanisha mkakati wa kukabiliana nazo, aidha changamoto za kiujumla za Mifuko ni kama ifuatavyo:

i. Upungufu wa Mitaji na Fedha za Kuendeshea shughuli za Mifuko kama utoaji wa mafunzo na ufuatiliaji;
ii. Kutokuwa na Mfuko unaotoa huduma kwa Wajasiriamali wanaoanza shughuli za Ujasiriamali; na
iii. Baadhi ya Sekta za Uchumi kutofikiwa na huduma za Mifuko kama Madini, Utalii, Uvuvi nk.

# 9.0. MAENDELEO YA UJASIRIAMALI TANZANIA

## 9.1. UTANGULIZI

Uendelezaji wa Ujasiriamali katika nyanja zote ni miongoni mwa nguzo muhimu sana katika kufikia azma ya Uwezeshaji wananachi kiuchumi. Uendelezaji wa Ujasiriamali kimkakati ni muhimu sana ili kuwawezesha watanzania kiuchumi. Kupitia uendelezaji wa ujasiriamali watanzania wanajengewa hali ya kujiamini, kuthubutu, kujisimamia, kujitambua na kupambana bila kukata tamaa.

Uendelezaji wa Ujasiriamali wenye manufaa unahitaji kutambua mikakati muhimu, kutekeleza, kufuatilia utekelezaji wake na kutathimini. Hiyo ni pamoja na *uboreshaji wa mazingira ya biashara; kuimarisha ujuzi na maarifa;kuboresha upatikanaji wa mitaji; kuwezesha matumizi ya teknojia; kuongeza uhamasishaji, kujenga na kutumia mitandao ya biashara na upatikanaji wa taarifa*. Aidha, mifumo ya uratibu, ufuatiliaji, tathimini na upatikanaji wa taarifa kuanzia ngazi ya Halmashauri, Mkoa na Kitaifa kupitia Kamati ya Kitaifa ya Uendelezaji Ujasiriamali (*National Entrepreneurship Development Committee)* ni ya umuhimu ili kufikia adhma na malengo ya Sera na Mikakati inayolenga kuendeleza Ujasiriamali hapa Tanzania. Nguzo za ujasiriamali zimeainishwa katika Mkakati Jumuishi wa Kitaifa wa Ujasiriamali *(Inclusive National Entrepreneurship Strategy –INES)* ambapo utekelezaji wake unafanywa na wadau mbalimbali ikiwemo Serikali, sekta binafsi, wadau wa maendeleo, asasi za kiraia jamii kwa ujumla. Katika kipindi cha mwaka 2019/20 maendeleo ya Ujasiriamali kupitia utekelezaji wa Mkakati wa Ujasiriamali yalikuwa kama ifuavyo:-

## 9.2. KAMATI YA KITAIFA YA MAENDELEO YA UJASIRIAMALI (NATIONAL ENTREPRENEURSHIP DEVELOPMENT COMMITTEE)

Kamati ya Kitaifa ya Maendeleo ya Ujasiriamali ni chombo kilichoundwa kimkakati mahususi kwa ajili ya kuratibu na kuendeleza Ujasiriamali Tanzania. Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi linaratibu kamati hii ambayo inahusisha wadau muhimu wa uendelezaji Ujasiriamali Tanzania kutoka kwenye Serikali, sekta binafsi na jamii kwa ujumla.

Katika kipindi cha mwaka 2019/20 utekelezaji wa Mkakati Jumuishi wa Kitaifa wa Ujasiriamali ulifanyika kupitia:

**9.2.1.** Uwepo wa vikao vya kitaifa vya kimkakati vya ujasiriamali vilikaa na kubaini changamoto zinazozuia kuendelea kwa ujasiriamali Tanzania na kupendekeza njia zinazofaa kwa ajili ya kuzitekeleza. Mapendekezo yaliyotolewa ni pamoja na kuanzisha vituo vya malezi ya biashara kwa wajasiriamali. Hivyo Vyuo vikuu, taasisi za elimu ya juu na za utafiti na teknolijia zinawajibika kuanzisha Atamizi. Katika utekelezaji SIDO imefanikiwa kusaidia kuendeleza jumla ya teknolojia na mawazo 25 kupitia Atamizi za mikoa ya Dar Es salaam, Tanga, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Mara na Mbeya. Teknolojia hizi zilihusu utengenezaji wa sabuni, uyeyushaji wa vyuma ili kupata vipuri mbalimbali, usindikaji wa vyakula, uchakataji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi na utengenezaji wa zana za kilimo.

Aidha, ilishauriwa kuanzishwa kwa mwavuli wa Atamizi Tanzania ambayo itaratibiwa na COSTECH, Human Development Innovation Fund na NEEC. Vilevile ilishauriwa kuhakikisha kuwa mazingira ya uendelezaji ujasiriamali nchini yanakuwa jumuishi bila kumuacha mtanzania yeyote kwa kuanzisha *Venture Capital Fund* ambayo itakuwa chanzo cha mtaji kwa wajasiriamali.

## 9.3. UBORESHAJI WA MAZINGIRA YA BIASHARA

**9.3.1.** Mazingira ya biashara ni chachu katika kuendeleza ujasiriamali nchini. Mazingira ya biashara yanajumuisha uwepo wa mifumo ya kisheria kwa ajili ya kuendeleza, ujasiriamali jamii (social entrepreneurship), viwanda vidogo vidogo vya kati na vikubwa. Uwepo wa miundombinu (umeme, uchukuzi, barabara, maji, mahali pa kufanyia kazi bila usumbufu na mawasiliano) ambayo inawezesha na kurahisisha ufanyaji wa biashara ikiwemo ujasiriamali ni sehemu ya mazingira ya biashara ambayo yanatakiwa kuboreshwa kwa lengo la kuchochea uchumi nchini. Serikali imeendelea kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa mazingira yanakuwa rafiki kwa wajasiriamali kufanya shughuli zao kwa tija kama ifuatavyo:-

**9.3.1.1.** Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara Nchini (Blueprint for Regulatory Reform to improve Business Environment). Mpango huo umewezesha maboresho ya tozo 173 ambapo kati ya tozo hizo, tozo 163 zimefutwa na tozo kero 10 zimepunguzwa kiwango. Kati ya tozo zilizofutwa, 114 ni za Sekta ya Kilimo na Mifugo, 5 za OSHA, 44 za TBS, GCLA, Utalii, Maji, Uvuvi na iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa-TFDA. Aidha, tozo zilizopunguzwa ni za Mamlaka za Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA). Mpango huo umewezesha kuhamisha jukumu la usimamizi wa masuala ya chakula kutoka iliyokuwa TFDA kwenda TBS, ili kuondoa mwingiliano wa majukumu. Maboresho hayo yamesaidia kuondoa urasimu na kupunguza gharama za kufanya biashara ha hivyo kuvutia wajasiriamali wengi kurasimisha biashara zao. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kutokana na kufutwa kwa tozo ni pamoja na ongezeko la usajili wa usalama mahali pa kazi (workplace) 16,457 zilizosajiliwa kwa mwaka 2019 ikilinganishwa na mahala pa kazi 11,963 zilizosajiliwa kwa mwaka 2018. Aidha, Serikali inaendelea na maandalizi ya kutunga Sheria ya Uwezeshaji Biashara ya mwaka 2020 (Business Facilitation Act, 2020), ili kuipa nguvu ya kisheria misingi ya maboresho iliyobainishwa katika Blueprint.

**9.3.1.2.** Serikali imefanikiwa kutenga maeneo maalum kwa ajili ya wajasiriamali kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Suala hilo limewezesha ujenzi wa majengo ya viwanda (Industrial Shades) 12 katika Mitaa ya Viwanda ya SIDO iliyopo mikoa ya Dodoma (3), Manyara (3), Kagera (1), Mtwara (1) na Geita (4). Jumla ya viwanda 29 vimeweza kusimikwa katika

majengo hayo ambapo ajira 648 zimezalishwa. Aidha, Serikali imefanikisha kusogeza karibu huduma za kusaidia na kuhamasisha wananchi kushiriki katika ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa kujenga ofisi nne za SIDO katika mikoa mipya ya Simiyu, Katavi na Geita

**9.3.1.3.** Ujenzi wa Maghala ya mazao ni miongoni mwa mindombinu wezeshi ambayo ina hamasisha wajasiriamali wanaojihusisha na kilimo kufanya shughuli zao kwa urahisi na tija. Katika mwaka 2019/2020, Ghala za mazao ya Korosho, Ufuta, Dengu, Kakao, Mbaazi na Choroko zilijengwa katika Wilaya za Ruangwa, Tunduru, Kondoa na Babati. Kutokana na hatua hizo, Serikali imefanikisha kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna (post harvest loss), kuongeza uhai wa muda wa matumizi wa bidhaa za kilimo (shelf life) na kuweka mfumo rafiki wa utunzaji wa mazao;

**9.3.1.4.** Serikali imeboresha Mfumo wa Usajili wa Majina ya Biashara, Makampuni, Alama za Biashara na Huduma, Hataza, Leseni za Viwanda na Leseni za Biashara kwa njia ya mtandao (Online Registration System-ORS) kupitia tovuti ya BRELA (www.brela.go.tz), na Dirisha la Taifa la Biashara (National Business Portal - NBP). Maboresho haya yatasaidia wajasiriamali kurasmisha shughuli zao na kupata tija zaidi. Hadi kufikia Machi, 2020, BRELA imesajili Makampuni 7,549, Majina ya Biashara 12,627, Alama za Biashara na Huduma 1,970, Hataza 55, Leseni za Viwanda 200 na Leseni za Biashara 9,927;

**9.3.1.5.** Katika kuhakikisha kuwa wajasiriamali wanapata vifungashio (Karatasi, chupa, chuma na plastiki) venye ubora na kwa uhakika, SIDO wameyatambua na kuyasajili makampuni tisa ya vifungashio ili kurahisisha upatikanaji wake. Kupitia makampuni haya SIDO inasambaza vifungashio nchi nzima kupitia mtandao wake wa ofisi za mikoa. Huduma hii inawawezesha watanzania wajasiriamali kupata soko la uhakika na kwa bei nzuri. Urahisi wa uzalishaji wa vifungashio. Makampuni hayo ni kama yanavyoonyeshwa katika jedwali.

**Jedwali Na. 19: Jedwali la Makampuni ya Vifungashio**

| Jina la Kampuni | Maelezo ya Kampuni | Aina ya Vifungashio | Mawasiliano |
|---|---|---|---|
| **BONPAK** | Bonpak Glass and Plastic Containers ni ya mwaka 1989 | Machupa ya glasi kontena na chupa kubwa | 7 Angus Crescent, Longmeadow Business Park East - Edenvale, Tel: (011) 608 4990, Fax: (011) 608 4994, ray@bonpak.co.za, website: |

| Jina la Kampuni | Maelezo ya Kampuni | Aina ya Vifungashio | Mawasiliano |
|---|---|---|---|
| | | | bonpak.co.za |
| **BORA IMANI COMPANY** | Iko Ofisi za SIDO Mkoani Mbeya | Chupa | S.L.P 652, Mbeya . Namba ya Simu 0755 641508 |
| **CELLO INDUSTRIES (T) LTD** | Cello Tanzania | Bidhaa za plastiki | Cello Industries (T) Ltd Mbozi Road, Chang'ombe Industrial Estate, SLP 19689, Dar es Salaam, Simu: +255 22 2862625, barua pepe info@cellotz.com |
| **DUKA LA VIFUNGASHIO** | Iko Morogoro mjini | Sabuni, Asali, Juisi, Matunda, Viungo | Simu 0717 099997/0783 173777, SLP 166, Msamvu Stand - Morogoro. |
| **MIFUKO SHOP** | Iko Morogogoro mjini | Plastiki za Juisi na kontena za kuchukulia chakulia chakula | Phone: 0716 911327, Box 166,Nunge Street - Morogoro. |
| **NAMPAK (T) LTD** | Nampak Tanzania, imeanzishwa mwaka 1947. | Makopo, mifumiko ya betri, vyombo vikubwa, viafaa vya chuma | SLP 618, Dar es Salaam, Tanzania Simu +255 22 286 4251/2/3; +255 763 333551 Fax: +255 22 286 3853 Simu 255 22 286 3853 |
| **OMAR PACKAGING INDUSTRIES LTD** | Iko Dar E salaam<br><br>Nyerere Road Inatazamana na SIDO Vingunguti | Vifungashio vya aina mbalimbali | Simu +255 652 665151, +255 688 680211, +255 714 216620, info@bakhresa.com, opil.markerting2@bakhresa.com |
| **PRINCEWARE** | Iko Dar Es salaam | Vifungashio vya plastiki | SLP 5838-DSM, Simu +255 22 2843094, Email: tzsales@princewareafrica.net, Website: www.princeware.net |
| **SIDO MOROGORO** | | Sabuni, Asali, Mvinyo, Juisi, Unga wa Lishe na vibandiko vya alama za bidhaa | Phone: 0752 430923/0717 778235, Box 1022, Kihonda |

**9.3.1.6.** Mazingira ya biashara yanachangia kwa kiasi kikubwa katika kuongezeka au kupungua kwa idadi ya wajasiriamali na bidhaa zao nchini. Urahisi wa kupata Nembo za ubora wa bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali unatakiwa uwekewe mazingira rafiki ili kuwezesha wajasiriamali wengi kusajili Nembo za bidhaa na Shirikia la Viwango Tanzania.

Kwa kutambua mchango wa wajasiriamali katika kuzalisha bidhaa kwa ajili ya walaji hapa nchini, TBS wameandaa viwango vinavyogusa wazalishaji mbalimbali wakiwemo wajasiriamali wadogo hasa viwango vya kilimo na chakula. Kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 TBS imeandaa jumla ya viwango 228 sawa na asilimia 84.4 ya lengo la kuandaa jumla ya viwango 270 kwa kipindi hicho. Idadi hii ni ongezeko la asilimia 16.9 ikilinganishwa na viwango 195 vilivyoandaliwa mwaka jana.

Katika kuboresha mazingira kwa ajili ya wajasiriamali kufanya biashara TBS wameweka vipaumbele katika utoaji wa leseni za ubora mbalimbali ikiwemo bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wadogo. Jumla ya leseni 366 za ubora zilitolewa kati ya Julai 2019 hadi Machi, 2020 ambapo ni sawa na asilimia 135.6 ya lengo la kutoa leseni 270. Aidha, TBS kwa kutumia fedha zake za ndani iligharamia jumla ya leseni 126 zilizotolewa kwa wajasiriamali wadogo. Idadi hii ya leseni za ubora zilizotolewa kwa kipindi hicho ni ongezeko la asilimia 91.6 ikilinganishwa na viwango 191 vilivyoandaliwa katika mwaka wa fedha 2018/19 ambapo kati ya hizo jumla ya leseni 29n zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo.

Kutokana na uwepo wa soko huria na utawandazi katika biashara, TBS inaendelea kuwalinda wajasiriamali wadogo kwa kuwawekea mazingira wezeshi ya ushindani wa kimataifa kwa kufanya ukaguzi wa bidhaa kabla hazijaingizwa hapa nchini. Katika ukaguzi huu vigezo vya ubora vinavyo tambulika nchini huzingatiwa na bidhaa ambazo hazijakidhi viwango huzuiliwa. Kuzuiliwa kwa bidhaa hizo ni fursa kwa wazalishaji wa ndani kuuza bidhaa zao nchini. Vilevile kaguzi hizi zinawezesha wajasiriamali kupata bidhaa na teknolojia zenye ubora kwa ajil ya shughuli zao. Kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya vyeti 25,821 vya ubora vimetolewa sawa na asilimia 90.6 ikilinganishwa na lengo la kutoa jumla ya vyeti ubora 28,500 kwa shehena za bidhaa zitokazo nje ya nchi. Idadi hii ya vyeti vya ubora ni ongezeko la asilimia 0.8 ikilinganishwa na vyeti vya ubora 25605 vilivyotolewa katika mwaka wa fedha 2018/19

Kwa kipindi cha kuanzia Julai 2019 hadi machi 2020 jumla ya vyeti vya ukaguzi wa magari 28,820 vilitolewa ambazo ni sawa na asilimia 93.7 ya lengo la kutoa jumla ya vyeti 30,750. Idadi ya vyeti vya magari ni pungufu ya asilimia 5.8 ikilinganishwa na ukaguzi wa vyeti vya magari 30,580 vilivyotolewa katika mwaka wa fedha 2018/19. Upungufu huu unasababishwa na mabadiliko ya mienendo ya kibiashara duniani. Ukaguzi wa magari yaliyotumika yanayoingia hapa nchini ni muhimu sana ili kudhibiti magari yasiyo na ubora ambayo yatasababisha kuathiri shughuli za biashara ikiwemo usafirishaji na usambazaji wa bidhaa za wajasiriamali hivyo kuingiza hasara kwa wahusika.

**9.3.1.7.** Katika kuboresha mazingira ya ujasiriamali katika kilimo, Serikali imeshirikiana na Tanzania Horticultural Association (TAHA) kuwezesha upatikanaji wa usafiri wa moja kwa moja wa mazao ya bustani kutoka Tanzania kwa kutumia ndege ya Shirika la Ndege la Ethiopia kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro badala ya kupitia uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyata nchini Kenya. Ndege hiyo inachukua mizigo wastani wa tani 55 kwa wiki. Hatua hiyo imesaidia kuwa na usafiri wa uhakika, kupunguza gharama za usafirishaji, kupunguza upotevu wa mazao kwa kupunguza muda wa usafirishaji na kuongeza fedha za kigeni kwa wajasiriamali.

**9.3.1.8.** Ili kuwawezesha wajasiriamali wa mazao ya kilimo kupata mbolea yenye ubora na kwa wakati, Serikali imeimarisha upatikanaji wa mbolea nchini kwa kuanzisha mfumo wa ununuzi wa pamoja (Bulk Procurement System - BPS). Mpango huu umeongeza upatikanaji wa mbolea kutoka tani 302,482 mwaka 2015/2016 hadi 633,197 mwaka 2019/2020. Mfumo huo umewezesha wajasiriamali wa kilimo kupata mbolea kwa wakati na bei nafuu. Aidha, idadi ya viwanda vinavyotengeneza mbolea na visaidizi vya mbolea (fertilizer suppliment) vimeongezeka kutoka viwanda vinne (4) mwaka 2015 hadi viwanda 13 mwaka 2019. Kati ya viwanda hivyo, viwanda viwili (2) ni vya visaidizi na 11 ni vya mbolea. Uwepo wa mifumo huu wa upatikanajiwa mbolea unaweka mazingira rafiki katika upatikanaji wa mbolea na hivyo matumizi yake.

**9.3.1.9.** Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na wadau wa huduma za Bima ikiwemo Mamlaka ya Kudhibiti Shughuli za Bima nchini (TIRA), Shirika la Bima la Taifa (NIC), kampuni binafsi tano (5) za bima zimeanzisha Bima ya Mazao kwa lengo la kumsadia mkulima kujikinga na athari za majanga ya asili na mabadiliko ya tabianchi pamoja na kupata dhamana ya mkopo. Hadi sasa, wakulima wajasiriamali 1,279,884 wa mazao ya biashara wamesajiliwa na kutengeneza kanzidata kwa lengo la kuwatambua na kusaidia katika utoaji wa huduma za kilimo ikiwemo huduma ya bima ya mazao.

## 9.4. KUIMARISHA ELIMU YA UJASIRIAMALI NA KUENDELEZA UJUZI

Mkakati wa Ujasiriamali wa Kitaifa umeelekeza, kuandaa mada mahususi kwa ajili ya ufundishaji kwa makundi mbalimbali; kuandaa programu za kujenga uwezo na kuanzisha mtandao wa waalimu wa Ujasiriamali ili kubadilishana uzoefu, mbinu na vifaa vya kufundishia; na kuhakikisha kuwa Ujasiriamali unafundishwa shule zote za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu.

Katika kuimarisha elimu ya ujasiriamali na kuendeleza ujuzi, Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limeratibu Mpango wa uanzishaji wa Mafunzo ya Ujasiriamali kwa Wanafunzi wa Shule 12 za Sekondari katika Mikoa ya Dar Es salaam, Kilimanjaro na Arusha. Shule hizi ni zile zinazoshirikiana na *PROBONO School Partnerships for One* World yenye makao makuu nchini Ujerumani. Taasisi wadau katika kutekeleza Mpango huu ni AJISO (*Action for Justice In Society*) ya Mjini Moshi na Teach *A Man To Fish (TAMTF) ya Uganda.* Mpango huu unalenga wanafunzi wa shule za sekondari ambazo ziko katika Halmashauri za Mwanga DC, Siha DC, Moshi Rural DC Arusha CC, Meru DC, Monduli DCg, Ubungo MC, Kinondoni MC na Ilala MC). Mpango huu ulizinduliwa na Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananachi Kiuchumi tarehe 2 Machi, 2020 Uhuru Hostel, Mjini Moshi ni wa miaka mitatu kuanzia 2020 hadi 2022.

**Jedwali Na. 20: Shule zinazotekeleza Mpango wa Ujasiriamali**

| S/n | Secondary School | Council | Region |
|---|---|---|---|
| 1. | Dr. Asha Rose Migiro Girls | Mwanga District Council | Kilimanjaro |
| 2. | Mwanga | Mwanga District Council | |
| 3. | Kilobeni | Mwanga District Council | |
| 4. | Kisomachi | Moshi Rural District Council | |
| 5. | Magnificany | Siha District Council | |
| 6. | St. Mary’s Duluti | Meru District Council | Arusha |
| 7. | Olesirway | Arusha City Council | |
| 8. | Edmundrice | Arusha City Council | |
| 9. | Irikisongo | Monduli District Council | |
| 10. | Kiluvya Secondary School | Ubungo Municipal Council | Dar es Salaam |
| 11. | Mbonea Secondary School | Ilala Municipal Council | |
| 12. | Fanaka Secondary School | Kinondoni Municipal Council | |

***Chanzo:*** *Probono Entrepreneurship Program, Machi, 2020*

**9.4.1.** Mkakati unaelekeza kuwa elimu ya ujasiriamali itolewe kwa ufanisi kwa makundi ambayo hayapo katika mfumo rasmi wa elimu. Kwa mwaka wa fedha wa 2019/20 ofisi za SIDO za Mikoa, Tanzania nzima, ziliendesha jumla ya kozi 419 ambapo wajasiriamali 12,589 walinufaika. Mafunzo yalikuwa katika usindikaji wa vyakula, ngozi, chaki, vyakula vya mifugo na kuongeza thamani ya bidhaa za kilimo (value addition). Aidha, SIDO ilitoa ushauri katika nyanja za ufundi, uchumi, uongozi, masoko, ubora wa bidhaa na teknolijia kwa wajasiriamali 13,058 kwa mwaka 2019/20.

**9.4.2.** Shirika la Viwango Tanzania, limetoa elimu kwa wajasiriamali kwa njia mbalimbali ikiwemo mikutano ya hadhara, vyombo vya habari, makongamano na maonyesho. Dhima ya hadhira hizi ambazo TBS wametumia fedha za ndani walizotenga pamoja na michango ya wadau ni kuwahamasisha wajasiriamali

umuhimu na jinsi ya kupata nembo ya ubora katika kuendeleza bidhaa wanazozalisha. Hatua hizi zimewawezesha wajasiriamali kuzalisha bidhaa zenye ubora na zenye kuweza kushindana katika soko la ndani na la nje. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya mafunzo na semina 100 zilifanyika. Katika hadhira hizo jumla ya wajasiriamali 9,592 walipata fursa ya kuhudhuria.


**9.4.3.** Shirika la SUGECO chini ya Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), limetoa mafunzo kwa vijana 1,000 kuhusu kilimo biashara, uzalishaji na ujasiriamali katika vituo atamizi vya mikoa ya Morogoro na Pwani. Kati ya vijana hao, vijana 100 wamekwenda Israel na 87 wamekwenda Marekani kwa ajili ya kuongeza ujuzi zaidi. Baadhi ya vijana hao wameanzisha mashamba ya mazao ya bustani ikiwa ni pamoja na parachichi, vitunguu, nyanya na wengine wameanzisha maduka ya pembejeo.

**9.4.4.** Kuwatambua wawezeshaji wa maendeleo ya biashara (Mapping of Business Development Service Providers-BDSP) mahali walipo, shughuli wanazozifanya na changamoto wanazokutana nazo

Katika mwaka 2019 Baraza lilifanya utambuzi wa maendeleo ya biashara Tanzania (BDSP) ili kufahamu mahali walipo, shughuli za kiuwezeshaji wanazozifanya na changamoto wanazokutana nazo. Taarifa hizi ni muhimu na zinahitajika sana ili kuzitambua Taasisi na wadau mbalimbali wanaotoa huduma za maendeleo ya biashara; changamoto zao ili zitatuliwe na kuharakisha utoaji wa huduma za maendeleo ya biashara kwa maendeleo ya Taifa. Watoa huduma wamegawanyika katika makundi ya huduma za kifedha na mitaji, mafunzo ya uzalishaji bora na wenye tija, biashara na ujasiriamali, masoko, miundombinu ya kiuchumi, viwanda, utaalamu hivyo kuwatambua na kutatua changamoto zao kutachangia katika kuhakikisha kuwa watanzania wanashiriki na hivyo kuchangia katika uboreshaji wa hali ya uchumi

Zoezi la utambuzi wa waendelezaji biashara Tanzania limeonyesha kuwa, 42% ya Wawezeshaji ni Asasi za Kiraia (CSO's); 29% ni sekta binafsi; Wadau wa Maendeleo ni 18% na 11% ni Mashirika na Wakala wa Serikali. Ni muhimu kuwatambua wawezeshaji wananchi hawa hapa Tanzania kwa kuwa wana mchango mkubwa katika kutoa huduma za elimu ya biashara na ujasiriamali; matumizi ya teknolojia rafiki na ubunifu; upatikanaji wa masoko; utoaji wa ushauri na huduma za kifedha na upatikanaji wa mitaji; wanatoa mafunzo ya uzalishaji bora na wenye tija katika shughuli za kiuchumi kwa kila eneo; upatikanaji wa masoko; kuunda vikundi vya kiuchumi na vya kifedha; kuwezesha miundombinu ya kiuchumi, kuanzisha viwanda na utaalamu.

**Mchoro Na. 16: Makundi ya wawezeshaji maendeleo ya biashara**




*Chanzo: Utafiti wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi uliofanywa na ESRF*

**9.4.5.** Wizara ya kilimo imeendelea na juhudi za kutambua mchango wa sekta binafsi katika Sekta ya Kilimo ambapo imekamilisha mfumo wa kuwasajili wadau wote wa sekta ya kilimo ikiwemo Sekta Binafsi (Stakeholders mapping). Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2020, jumla ya wadau wa sekta binafsi 564 wamesajiliwa ambapo Wazalishaji na wasambazaji wa pembejeo ni 198, Wazalishaji wa bidhaa za kilimo 103 na wasindikaji 363. Aidha, jumla ya miradi 105 inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo yenye thamani ya Shilingi Trilion 3.3 imesajiliwa kwenye mfumo. Mfumo huo utaiwezesha Serikali kutambua juhudi na uwekezaji wa wadau wote na kuimarisha ushirikiano kati yao na Serikali katika kuendeleza sekta ya kilimo kupitia program ya ASDP II

**9.4.6.** Kuhamasisha utoaji wa elimu ya ujasiriamali kwa njia ya mtandao ili kuwafikia vijana na makundi maalumu kwa wingi na gharama nafuu (Massive Open Online Course – MOOC approach). Katika kutekeleza Mipango inayolenga kuongeza idadi ya watanzania wajasiriamali wanaohitaji kupata alama za ubora kwa ajili ya bidhaa wanazozalisha, Shirika la Viwango Tanzania (Tanzania Bureau of Standards –TBS) kwa kushirikiana na Trade Mark East Africa na wadau wengine ikiwemo Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi wamekamilisha maandalizi ya utoaji wa Mafunzo ya wajasiriamali kwa njia ya mtandao E-Leaning for Entrepreurs. Mafunzo kwa njia ya mtandao yatatolewa kwa wajasiriamali watakao kuwa wanazalisha bidhaa zitokanaazo na mazao ya Muhogo, Embe, Nyanya, Korosho, Pamba, Asali, Nguo, Nondo na Samaki.

**9.4.7.** Ufundishaji wa falsafa ya KAIZEN umefanywa kwa makundi ya wajasiriamali ili kuongeza tija na ubora wa bidhaa. Kwa mwaka 2019/2020, idadi ya wakufunzi iliongezeka kutoka 91 hadi 130 watakaosaidia kueneza falsafa hiyo. Lengo ni kuwezesha wajasiriamali wawe na ukuaji endelevu na wenye tija.

## 9.5. KUWEZESHA MATUMIZI YA TEKNOJIA NA UBUNIFU

Uendelezaji wa Ujasiriamali unahitaji matumizi ya teknolojia na ubunifu. Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limeratibu utekelezaji wa mkakati katika kuhakikisha kuwa teknolojia na ubunifu inakuwa chachu ya maendeleo ya ujasiriamali nchini. Taasisi mbalimbali zimehusika kuhakikisha upatikanaji wa teknolojia na ubunifu hapa nchini

**9.5.1.** SIDO imefanikiwa kutambua, kuzalisha na kusambaza jumla ya teknolojia 197. Teknolojia hizi zimewezesha kuanzishwa na kuimarishwa kwa shughuli za viwanda vidogo na vya kati pamoja na miradi, Viwanda hivyo vimejikita katika maeneo ya ubanguaji wa Korosho, usindikaji wa Muhogo, ukamuaji wa mafuta ya mawese, usindikaji wa vyakula, upunguzaji wa matumizi ya misitu na mazao yake, utengenezaji wa vifaa vya ujenzi, ukamuaji wa mafuta n.k.

**9.5.2.** Jumla ya mashine/vifaa 268 vilitengenezwa na kuuzwa kwa wajasiriamali wadogo na wakati wa mijini na vijijini. Mashine hizo pamoja na vifaa vilitengenezwa na vituo/karakana za SIDO katika mikoa ya Arusha, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi na Shinyanga.

**9.5.3.** Katika kuimarisha na kuboresha miundombinu ya vituo vya ubunifu kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali kuanzisha na kuendeleza viwanda, Serikali kupitia SIDO imetoa shilingi bilioni 2 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya viwanda ambapo shilingi bilioni 1 kwa ajili ya mikoa ya Mtwara, Ruvuma na Kigoma na shilingi bilioni 1 kwa ajili ya ununuzi wa mashine/mitambo ya vituo vya uendelezaji teknolojia vya Lindi, Shinyanga na Kigoma

**9.5.4.** Ili kuendeleza wajasiriamali nchini, Mkakati umeelekeza kuwezesha wajasiriamali kupata masoko ya bidhaa wanazozalisha, kuhamasisha ubunifu na kuendeleza vipaji vyao kupitia uwepo wa maonyesho ya bidhaa za wajasiriamali. Maonyesho yanajenga ari ya kujiamini, kujifunza kutoka kwa wazalishaji wengine hivyo kuboresha zaidi utendaji na kuleta tija. Katika kutekeleza hilo SIDO ilishirikiana na wadau mbalimbali kuandaa maonyesho 37 ya bidhaa ambapo jumla ya wajasiriamali 465 walishiriki. Aidha, katika maonyesho hayo wajasiriamali 31 walipata fursa ya kufanya biashara na makampuni makubwa.

## 9.6. KUBORESHA UPATIKANAJI WA MITAJI

Wajasiriamali wanahitaji Mitaji ili kuboresha kazi zao na kuleta tija. Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananachi Kiuchumi ya mwaka 2004 inaelekeza kuwa Mitaji kwa wajasiriamali na

jamii kwa ujumla inaweza kupatikana kwa njia tatu kubwa ambazo ni kuweka akiba, kupata ruzuku na kupitia mikopo. Wajibu wa Serikali ni kuweka mazingira yatakayowezesha wajasiriamali kupata mitaji ili kuendeleza shughuli zao. Uboreshaji wa Sera. Sheria, mifumo na taasisi katika kuhakikisha kuwa wajasiriamali wanapata mikopo na kuitumia ni jambo muhimu sana ambalo serikali imeipa kipaumbele. Baraza linaratibu upatikanaji wa mikopo kwa wajasiriamali kwa kuiratibu mifuko ya Uwezeshaji wananachi kiuchumi inayosimamiwa na taasisi mbalimbali za umma na binafsi ili kupanua wigo na kuleta tija. Hivi sasa kuna jumla ya Mifuko 51 ambayo inasaidia Wajasiriamali Tanzania. Aidha, katika kuboresha upatikanaji wa Mitaji kwa Wajasiriamali Serikali imetekeleza yafuatayo:-

**9.6.1.** NEEC imeshirikiana na SIDO, VETA, NSSF na Azania Bank kwa kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wakati wanaojishughulisha na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo. Mikopo hiyo inaanzia shilingi milioni 8 hadi milioni 500 ambayo inalenga kuwezesha upatikanaji wa mashine na teknolojia za kurahisisha uzalishaji viwandani.

**9.6.2.** Wizara ya Kilimo kupitia Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi Ghalani (WRRB) kwa kushirikiana na Mfuko wa Kuimarisha Sekta ya Fedha (FSDT), Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), Soko la Bidhaa Tanzania (TMX),Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), taasisi za fedha za CRDB na NMB, Shirika la Bima la Taifa (NIC) na Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF) ziliunda Jukwaa Jumuishi kwa lengo la kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu mifumo rasmi ya kifedha kwa mkulima na biashara za kijasiriamali vijijini. Lengo ni kuhakikisha kwamba wakulima wanapata huduma za kifedha ili kuwawezesha kuendeleza shughuli zao. Uhamasishaji huo ulifanyika katika Mkoa wa Kagera Wilaya za Karagwe, Bukoba (M), Bukoba (V), Misenyi, Kyerwa, Muleba, Ngara na Biharamulo kwa kuhamasisha na kutoa elimu katika AMCOS na wakulima waliopo katika Wilaya hizo. Zoezi hilo liliambatana na ufunguzi wa akaunti ambapo zaidi ya wakulima 3,200 walipata elimu ya huduma za kifedha na baadhi yao kuweza kufungua akaunti na kuunganishwa na huduma nyingine za kifedha kupitia simu kama vile Simu Account ya CRDB na NMB mobile.

## 9.7. KUHAMASISHA UTAMADUNI WA UJASIRIMALI NA MITANDAO YA BIASHARA

Katika kuhamasisha utamaduni wa ujasiriamali na mitandao ya biashara suala la uhakika wa masoko ni muhimu sana. Katika kuhakikisha kuwa wajasiriamali wanapata masoko ya ndani na nje yafuatayo yametekelezwa

**9.7.1.** Kuchambua kampuni za ndani zinazofanya biashara ya uuzaji na uingizaji wa mazao na bidhaa zake kwa lengo la kuwaunganisha wajasiriamali ambao

wanazalisha, wanasindika na wanao fanyabiashara. Jumla ya kampuni 19 zinajishughulisha na zao la mahindi, kampuni 9 kwa zao la vitunguu, Kampuni 23 kwa zao la Pamba, na wasindikaji wapatao 33 wametambuliwa kwa ajili ya kuwahamasisha kutumia rasilimali za ndani. Aidha, mwaka 2019 minada mitatu ya Kahawa imeanzishwa katika mikoa ya Kagera, Ruvuma na Songwe lengo likiwa ni kuwasogezea na kuwaunganisha na soko wazalishaji katika mikoa husika. Hadi kufikia tarehe 3 Aprili, 2020 tani 58,547 za Kahawa zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 111.3 ziliuzwa. Kati ya hizo, tani 24,282 ziliuzwa kupitia minada ya ndani na tani 34,265 ziliuzwa moja kwa moja kwenye soko la nje.

**9.7.2.** TanTrade iliwezesha Wajasiriamali 38 kushiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Nairobi yaliyofanyika tarehe 30 Septemba hadi 6 Oktoba, 2019 kwa ajili ya kukuza soko la Bidhaa na Huduma za Tanzania nchini Kenya ikiwa ni sehemu ya jitihada ya kutumia vyema fursa za soko katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vile vile, kampuni 7 kutoka Sekta ndogo za nguo, Sanaa za Mikono na ngozi ziliwezeshwa kushiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Eswatin yaliyofanyika tarehe 30 Agosti hadi 9 Septemba, 2019. Maonesho hayo yalitoa fursa ya kutangaza bidhaa za Tanzania katika soko la Ukanda wa Kusini wa Afrika.

**9.7.3.** Makubaliano na Kampuni 3 kufanya biashara ya mbogamboga na matunda zenye thamani ya jumla Shilingi 8,376,235,793.36 kwa mwaka yalifanyika. Kampuni husika ni TanzaNice ambayo ilipata oda ya kuuza tani 700 za parachichi zenye thamani ya Euro 3,250,000 kwenye nchi za Ufaransa, Ujerumani, Uingereza na Uholanzi; Frank Horticultural & Timber Company Ltd ilipata oda ya kuuza parachichi, maharage machanga (green beans), njegere changa (snow peas) na njegere mbichi (Garden peas) zenye thamani ya Dola za Marekani 1,980,000 kwenda Denmark, Dubai, Kuwait na Ubelgiji; na Kampuni ya Hortanzia ilipata oda ya kuuza kitunguu jani (chives) yenye thamani ya Euro 2,000 kwenda Ujerumani. Aidha, TanTrade kwa kushirikiana na Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) kusimamia mauzo ya tani 215,484.90 za korosho kwa njia ya minada kwa msimu wa Mwaka 2019/2020; Kuunganisha wadau wa muhogo na kampuni yenye uwezo wa kununua wastani wa tani 100 za muhogo mbichi kwa wiki kutoka kwa wakulima wadogo; na kushiriki katika mnada wa mauzo ya miti katika mashamba ya miti ya Serikali yaliyopo Mtibwa katika Mkoa wa Morogoro, na Longuza, Muheza katika Mkoa wa Tanga ambapo mauzo ya jumla ya Shilingi Bilioni 4.77 yalifanyika

**9.7.4.** TANTRADE wanahamasisha mitandao ya biashara kupitia B2B inayofanyika katika kila maonesho ya Kimataifa ya Biashara. Katika maonesho ya 43 kampuni

kadhaa zilifanikiwa kuendelea kufanya biashara. Kampuni hizo ni pamoja na Dow elef Agri yenye bidhaa za Pilipili zenye thamani ya Shilingi Milioni 400, Dar Carton yenye bidhaa ya Mihogo zenye thamani ya Shilingi Milioni 90, Follow Honey yenye bidhaa ya Nta yenye thamani ya Shilingi Milioni 900 na Shilingi Milioni 390 za bidhaa ya asali. Kampuni hizo zina fursa ya kuuza kwa miezi 10 toka kumalizika kwa Maonesho ya 43 ya DITF

**9.7.5.** Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imeanzisha Mfumo wa Usajili wa Wakulima (Farmers Registration System- FRS) na kutengeneza kanzidata ya wakulima ambayo itasaidia kuwatambua na kuwapatia vitambulisho, kuainisha mahitaji yao ikiwemo pembejeo za kilimo, huduma za kifedha na masoko na hatimae kuweka mipango ya kuwahudumia. Hadi Aprili, 2020 jumla ya wakulima 1,275,220 katika mazao nane makuu ya kibiashara ambayo ni korosho, pamba, kahawa, chai, mkonge, pareto, tumbaku na sukari wamesajiliwa kupitia mfumo huo sawa na asilimia 88.1 ya wakulima wote wa mazao hayo nchini.

## 10.0. UBUNIFU TANZANIA

### 10.1. UTANGULIZI

Ubunifu ni kitendo cha kufikiria kwa kina na kutumia akili ya ziada kugundua mbinu au bidhaa mpya ambayo inalenga kutatua changamoto inayoikabili jamii husika. Ubunifu hutafsiriwa kama matumizi ya mbinu bora katika kutatua changamoto inayoikabili jamii, au kuboresha utendaji kazi au kuzalisha bidhaa ambazo tayari zipo lakini changamoto zake hazijapatiwa ufumbuzi bado. Dhana hiyo hukamilika pale ambapo kuna uzalishaji wa bidhaa zenye ubora, taratibu na huduma zinazokidhi matakwa ya wateja, teknolojia rafiki au mbinu za kibiashara zinazoweza kuleta tija katika soko.

Ubunifu unapatikana katika sekta zote ambazo zinamuhusisha binadamu na shughuli za maendeleo. Kutokana na mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia, vijana wengi wamekuwa wakijitokeza na kutumia uwezo na ubunifu wa teknolojia kutafuta suluhisho la changamoto zilizopo katika jamii inayowazunguka, lengo ikiwa kujipatia kipato na kujiajiri na kuajiri wengine. Ubunifu unakua kwa kasi sana Tanzania kufuatia Serikali kuweka mazingira ya kuwezesha Ubunifu.

### 10.2. MAZINGIRA YA KUWEZESHA UBUNIFU TANZANIA

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka mazingira ya kuwezesha ubunifu katika sekta zote kwa kuweka Mwongozo wa Ugunduzi na Ubunifu Tanzania. Mwongozo huu uliandaliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa kushirikiana na wadau wa Ubunifu. Aidha, kupitia COSTECH kuna Kamati ambayo inahusika na kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu. Vilevile Seikali imehamasisha Taasisi za Utafiti, Vyuo vya Elimu ya Juu vya Serikali na binafsi kuanzisha vituo vya kuwalea wabunifu (Atamizi) katika sekta mbalimbali. Baadhi ya taasisi zilizotekeleza ni pamoja na COSTECH ambayo ina Dar Technohama Business Innovation (DtBi); SIDO, Chuo Kikuu cha Dar Es salaam (UDSM); Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA); Mbeya University of Science and Technology; Voluntary Service Overseas (VSO); University of Dodoma (UDOM) na zinginezo. Hadi sasa kuna jumla ya Atamizi 40 hapa Tanzania.

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wanachi Kiuchumi linafuatilia suala la uendelezaji wa Ubunifu Tanzania kama nyenzo ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi.

### 10.3. UENDELEZAJI UBUNIFU TANZANIA

#### 10.3.1. Uhamasishaji kupitia Makongamano, Maonyesho na Vyombo vya Habari

Pamoja na suala la uendelezaji Ubunifu kukua kwa kasi hapa Tanzania, bado kuna changamoto zinazokwamisha jitihada hizo zisilete matunda yanayokusudiwa. Ili kutatua changamoto hizo

Serikali imeshirikiana na wadau mbalimbali kuandaa makongamano, maonyesho na kutumia vyombo vya habari ili kutatua changamoto hizo:-

i. Human Development Innovation Fund (HDIF) waliandaa Kongamano ili kujadili upatikanaji wa Mitaji kwa wabunifu. Kongamano hilo liliwaleta pamoja wadau wa maendeleo, wakezaji katika ubunifu (Angel Investors), Taasisi za kifedha na mabenki. Madhumuni ya Kongamano hilo yalikuwa ni kupata uelewa wa pamoja kuhusu ugharamiaji wa ubunifu Tanzania; kuwaunganisha pamoja wadau wa ubunifu na vyanzo vya mitaji; na kuangalia mapungufu na fursa zilizopo katika tasnia ya ubunifu. Nia ni kufikia muafaka wa pamoja wa kuanzisha mfuko wa kugharamia ubunifu Tanzania. Kongamano hili limelenga kuzitafutia kwa ufumbuzi wa pamoja changamoto za ubunifu ili kuendeleza tasnia hii muhimu kwa Uwezeshaji wananchi kiuchumi.

ii. Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) na COSTECH kwa kushirikiana na HDIF waliandaa Kongamano kwa ajili ya watumishi wa Wizara, Taasisi na Wakala ili kusisitiza umuhimu wa Ubunifu katika sekta zote za kiuchumi na kijamii ikiwemo wafanyakazi wa Serikali. Lengo ni kuwaelimisha watumishi wa Serikali kuwa Ubunifu ni nguzo muhimu katika kuleta tija wakati wa utekelezaji wa shughuli za Serikali;

iii. HDIF waliandaa Kongamano la Wahariri wa habari na Waandishi waandamizi ili wapate uelewa kuhusu uendelezaji ubunifu nchini. Kongamano hilo ambalo lilijikita katika kutafakari umuhimu wa vyombo vya habari katika uendelezaji Ubunifu nchini lilishirikisha vyombo vya habari ambavyo ni ITV, Clouds, The Citizen, The Guardian na Michuzi blog. Tasnia ya Habari ina mchango mkubwa sana katika kupeleka mbele ajenda ya Ubunifu wenye kuleta tija;

iv. Katika kuhakikisha kuwa uandishi wa masuala ya Ubunifu ni endelevu COSTECH imeshirikiana na HDIF na Baraza la Habari Tanzania kuanzisha Tuzo ya Waandishi wa habari wa Ubunifu. Tuzo hii ambayo inajulikana kama *Innovations for Human Development Reporting ilipangwa kutolewa kwenye 11th Edition of Annual Excellence in Journalism Awards Tanzania (EJAT) 2019*.

v. Uwepo wa Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini (MAKISATU) ni chachu katika kuendeleza Ubunifu Tanzania. Maonyesho haya ambayo huwaleta pamoja wabunifu, wajasiriamali, wafanya maamuzi, wanasiasa, sekta binafsi na jamii kwa ujumla hufanyika kila mwaka.

### 10.3.2. Maendeleo ya Atamizi (Incubator) na Vituo vya Ubunifu (Innovation Hubs) Tanzania

Mfumo wa uendelezaji Ubunifu hapa Tanzania umezidi kuimarika na kuleta tija kutokana na uwepo wa Atamazi, Vituo vya ubunifu na teknolojia na uwepo wa mazingira rafiki katika kuendeleza tasnia hiyo. Serikali imewezesha uwepo wa Atamizi kwa ajili ya kulea mawazo

mapya ya teknolojia au biashara (start up) kwa lengo la kuzifanya ziweze kukua, kusimama, kujitegemea na kukomaa kwa lengo la kushindana na kupata faida endelevu.

Kutokana na umuhimu wa Atamizi, Vituo vya ubunifu na teknolojia na uwepo wa mazingira rafiki katika kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA, Kilimo, Afya, Mifugo, Elimu, Uziduaji, Fedha Huduma, Sayansi na Teknolojia. Serikali inashirikiana na wadau wa maendeleo, sekta binafsi na jamii kwa ujumla ili kunufaika na ubunifu. Maendeleo ya Atamizi na Vituo vya ubunifu na teknolojia hapa Tanzania ni kama ifutavyo:

##### 10.3.2.1. Dar Teknohama Bussiness Incubator

Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) inashirikiana na InfoDev kuanzisha Dar Teknohama Business Incubator (DTBi) ambayo inapatikana kwenye majengo ya Tume hiyo. Kwa sasa DTBi inashirikiana na Ubalozi wa Denmark pamoja na Magilatech Company Limited na Institute for Management and Entrepreneurship Development (IMED). DTBi imedhamiria kuwa kitovu cha Ubunifu katika kutumia teknolojia hapa nchini ambayo inatoa huduma za kusaidia uendelezaji wa Atamizi. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2011 DTBi imeweza kuwalea na kuwakuza wabunifu 29 wa fani ya TEHAMA ambao waliweza kuingia sokoni. Kwa sasa DTBi ina wabunifu 30 ambapo wamebuni teknolojia katika fani ya Tehama

##### 10.3.2.2. SUGECO's Incubator Program

Atamizi ya SUGECO iko chini ya Chuo Kikuu cha Kilimo Morogoro (SUA). Atamizi hii inawapa wabunifu waliohitimu masuala ya kilimo nafasi ya kujaribu na kuendeleza Ubunifu wao ili kuweza kufanya biashara endelevu hapa Tanzania na hata nchi za nje. Kwa sasa SUGECO ina wajasiriamali 6 ambao wanaboresha bidhaa zao kabla ya kuzipeleka sokoni. Bidhaa hizo ni pamoja na:-

i. Ukaushaji wa bidhaa za matunda (ndizi, nanasi, embe na Strawberries);
ii. Uvuvi na uzalishaji wa mboga;
iii. Uzalishaji wa Juice;
iv. Usindikaji wa machungwa
v. Unga wa viazi vitamu kwa ajili ya uji, mkate na biskuti;
vi. Uzalishaji wa viungo (tangawizi, mchaichai, mdalasini, chai ya soya, masala na pilau masala
vii. Uzalishaji wa viungo "*superfood*'' kama vile mlonge na bizari.

Aidha, Atamizi ya SUGECO inashirikiana na Agribusines Incubation Centre (AIC) katika kuendeleza Atamizi za Vitalu Nyumba (Green Houses) vya mboga mboga na unenepeshaji wa Mbuzi wa nyama.

##### 10.3.2.3. Agribusiness Incubator Centre-AIC (Kituo cha Ubunifu cha Kilimobiashara)

Kituo hiki ni idara ndani ya Taasisi ya Private Agricultre Sector Support (PASS) inayolenga kutoa huduma za maendeleleo ya biashara kwa wajasiriamali wa kilimo biashara wenye mrengo wa kukua kibiashara. Aidha, AIC inatoa kipaumbele kwa kilimo biashara zinazowahusisha au kumilikiwa na vijana na wanawake. Lengo la AIC ni kusaidia ukuaji wa kilimo biashara kwa kuongeza ufanisi na tija ili kukuza ushindani katika masoko ya ndani, kikanda na kimataifa. Hili litafikiwa kwa kuwapatia wajasiriamali waanzilishi maarifa ya Kilimo biashara, kuwaunganisha na mitandao ya biashara, teknolojia, masoko na upatikanaji wa mitaji/fedha zinazohitajika kukuza biashara zao.

AIC inaendesha vituo viwili ambavyo vipo Morogoro na Kongwa kwa kushirikiana na taasisi za kitaifa na kimataifa za elimu, utafiti na kilimobiashara ili kufanikisha shughuli hii ya kutamia vijana. Taasisi hizo ni pamoja na Sokoine University of Agriculture (SUA), Tanzania Livestock Research Institute (TALIRI), Small and Medium Industry Development Agency Zanzibar (SMIDA), Tanzania Agriculture Development Bank (TADB), International Crops Research Institute for the Semi-Arid Tropics (ICRISAT), na mengineyo.

Mwaka 2018 Kituo Atamizi cha Kilimobiashara, Morogoro, kimeatamia vijana 20 kwenye kilimobiashara cha mbogamboga kwa kutumia shambanyumba (Greenhouse). Aidha, Kituo cha Kongwa, kimeanza kuatamia vijana 10 kwenye unenepeshaji wa Mbuzi.

#### 10.3.2.4. Kiota Hub

Kiota Hub ni kituo ambacho kimeanzishwa mwaka 2016 katika Chuo Kikuu cha Iringa (Iringa University). Kiota Hub inalelewa katika Kituo cha Ujasiriamali na Ubunifu (Centre for Entrepreneurship and Innovation) cha Chuo hicho. Kituo hiki kinaruhusu na kupokea wajasiriamali wanafunzi na wananchi wanaotoka kwenye jamii inayozunguka Chuo hicho. Malengo ya Kiota Hub ambacho kilishawahi pata ufadhiIi wa Mradi wa Mawasiliano kati ya Tanzania na Finland unaoitwa TANZICT ni kuhamasisha Ubunifu miongoni mwa jumuiya ya wanachuo na jamii kwa ujumla. Aidha, Kiota Hub inalenga kutoa mafunzo yanayohamasisha ari ya ujasiriamali miongoni mwa walengwa pamoja na utoaji wa taarifa na changamoto zinazohitaji ufumbuzi wa kibunifu.

Matokeo ya Kiota Hub ni kupatikana kwa ajira kwa watu zaidi ya 30; biashara na Kampuni zaidi ya 10 zimeanzishwa na kuweza kuwafikia watu zaidi ya 400 moja kwa moja na zaidi ya 2000 wamepata taarifa kuhusu Kiota Hub.

#### 10.3.2.5. Kinu Co-Creation Hub

Kinu Co Creation Hub ni Kituo kinachotoa nafasi kwa wajasiriamali kukutana na kufanya kazi za ujasiriamali ili kuziendeleza shughuli za kibunifu. Kituo hiki kinapatikana katika Jiji la Dar Es salaam. Kinu Co Creation kimeanza kusaidia wajasiriamali ambao wenye mawazo ya biashara na wale wanaoanza biashara ili kuziendeleza kwa tija zaidi (startups and nurturing ideas). Hivyo kwa sasa Kinu Hub wanaendelea kutafuta njia ipi inayofaa kuwalea wajasiriamali kwa manufaa.

Katika kutekeleza hilo Kinu wameaandaa Programu mbalimbali za kusaidia wabunifu na wagunduzi katika jiji la Dar Es salaam hasa zile zinazolenga kwenye teknolojia.

#### 10.3.2.6. Mara Space

Mara Space ni Kituo kinachotoa nafasi ya kufanyia kazi kwa wajasiriamali ili kuendeleza shughuli zao katika Jiji la Dar Es salaam. Mara Space imeanza kusaidia wajasiriamali ambao wanaanza biashara ili kuziendeleza kwa tija zaidi **(**startups and nurturing ideas). Hivyo wanaendelea kutafuta njia ipi inayofaa kuwalea wajasiriamali kwa manufaa. Wameandaa Programu mbalimbali za kusaidia wabunifu na wagunduzi katika jiji la Dar Es salaam hasa zile zinazolenga kwenye teknolojia.

#### 10.3.2.7. Mbeya Living Lab

Kituo cha Mbeya Living Lab, kilianzishwa mwaka 2012 kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Finland chini ya mradi wa TanzICT. Kituo hiki kilianzishwa kwa lengo la kutoa Elimu ya ujasiriamali kwa wakazi wa Jiji la Mbeya hasa Vijana na wanawake. Mbeya Living Lab imewaleta pamoja Vijana ili kujifunza, kubuni, kushirikiana katika kuendeleza ujasiriamali na bidhaa wanazozalisha.

#### 10.3.2.8. Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknoloji (Mbeya University of Science and Technology)

Masuala ya kuendeleza Ubunifu katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya yanasimamiwa na Kituo cha Ubunifu na Uhaulishaji wa Teknlojia (Centre for Innovation and Technology Transfer CITT). Kituo hiki kina wajibu wa kusimamia ubunifu, teknolojia na undelezaji wa ujasiriamali Tanzania. Kituo hiki kina idara mbili ambazo ni Ubunifu na Atamizi na Idara ya Ujasiriamali na Usimamizi wa Biashara. Majukumu ya Kituo cha Ubunifu ni pamoja na kuandaa programu zinazolenga kutekeleza masuala ya ubunifu na uhaulishaji wa teknolojia; kufuatilia na kutathimini utekelezaji wa mausala ya Ubunifu na program za uhaulishwaji wa teknolojia; kuwezesha mafunzo kwa wabunifu na wagunduzi kupitia Atamizi, semina, makongamano na mikutano ya hadhara;

#### 10.3.2.9. UDOM

Chuo Kikuu cha Dodoma (UNIVERSITY of Dodoma -UDOM) kimeanzisha Kituo cha Ubunifu ambacho kinatoa ofisi na nafasi kwa wabunifu kukutana na wadau mbalimbali ili kuendeleza kazi zao. Kituo hiki kinawezesha mawazo ya kibunifu yaendelezwe na kufikishwa sokoni. Ubunifu unaoendelezwa katika kituo hiki ni ule ambao ni rafiki wa mazingira, ambao ni endelevu na una mchango katika uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Kituo hiki kimeweza kuendesha mashindano mbalimbali ya wabunifu ambao huwasilisha mawazo yao kwa ajili ya kuchujwa na kuchaguliwa ili yaweze kuendelezwa.

### 10.3.2.10. EQWIP Hub

EQWIP ni kituo cha Ubunifu ambacho kimeanzishwa na taasisi mbili ambazo zinajulikana duniani katika kuhamasisha Maendeleo ya Ubunifu kwa Vijana. Taasisi hizo ni Canada World Youth (CWY) na Youth Challenge International (YCI). Taasisi hizi zimeamua kuanzisha EQWIP Tanzania ili kutatua changamoto za uhaba wa fursa za kuajiriwa ambayo inakwenda sambamba na uwepo wa ujuzi, maarifa na uzoefu ambao au wahakikishii Vijana ajira. EQWIP HUBs, ni jitihada zilizoanzishwa ili kuwaleta pamoja wadau wa ubunifu kimataifa ambao ni UN-Habitat, TakingITGlobal na Education Development Centre ili kufikiria na kupata ufumbuzi jinsi gani vijana wa kike na wa kiume watakavyoendelezwa vipaji na ujuzi wao pamoja na rasilimali zinazohitajika ili kuchangia katika uchumi.

EQWIP HUB inakwenda sambamba na mabadiliko ya kiuchumi na kiteknolojia kwa kuanzisha vituo 18 kwenye majiji Duniani katika nchi za Bolivia, Ghana, Indonesia, Peru, Senegal, na Tanzania. Tanzania EQWIP Hub inatoa huduma zake kupitia chuo cha Tumaini Dar Es salam (TURDACO); Taasisi ya Mipango ya Undelezaji Vijijini (IRDP) tawi la Mwanza; na Zanzibar. EQWIP HUB inatoa fursa ya kipekee kwa Vijana hasa wanawake kuwa jengea uwezo katika upatikanaji na utumiaji wa masoko ya uhakika, kupata mafunzo kwa wataalamu ambao wanafanya shughuli husika (mentorship), kujenga mtandao wa wadau, upatikanaji wa teknolojia na mitaji ili kuwaandaa kuanzisha biashara. Vijana wenye weledi na umakini kutoka Canada wanahusika katika kusaidia shughuli za kitaalamu za HUB, ili kuhamasisha kubadilishana utamaduni katika ubunifu, program za jinsia, kufundishana kwa rika (peer-to-peer mentorship)

EQWIP HUB pia, inatoa kozi fupi fupi kwa taasisi za elimu ya juu kulingana na mahitaji ya vijana kwa kuweka mazingira ya kutumia ujuzi na maarifa katika kutatua changamoto za maisha. Kozi zinazotolewa ni pamoja na Ujasiriamali, elimu ya fedha, masuala ya bajeti, kujenga na kuimarisha mtandao, biashara ya pamoja, elimu ya mtandao. EQWIP HUB inalenga kuwafikia vijana zaidi ya 100,000 Duniani kwa mwaka 2020.

### 10.3.2.11. VSO International T-LED

Mradi wa Tanzania Local Enterprise Development (T-LED) ambao uko chini ya Voluntary Services Oversee –VSO umeanzishwa kwa lengo la kusaidia, kukuza na kuziendeleza shughuli za biashara ndogo ndogo na za kati *(small- and medium-sized enterprises- SMEs)* ili ziwe na uwezo wa kuongeza nafasi za ajira miongoni mwa watanzania wakiwemo wanawake.

VSO T-LED inalenga kuzalisha ajira mpya 2,500 na kuongeza kipato cha kampuni ndogo na za kati zaidi ya 1,300 SMEs. Ili kufikiwa kwa matokeo haya T-LED imepanga kufanya yafutayo:

i. Kuwajengea uwezo wananchi juu ya fursa za masoko na vyanzo vya fedha vilivyopo ili viweze kuzitumika kwa ukamilifu;

ii. Kuwajengea uwezo wajasiriamali wanawake ili wapate maarifa na ujuzi wa kuanzisha biashara; na
iii. Kushawishi kuimarishwa kwa mifumo ya kisera, kisheria, miongozo, kiutamaduni na kijamii ili iwezeshe upatikanaji wa masoko na huduma za jinsia zenye ubora wa kuwezesha SMEs.

Hadi sasa T-LED imewezesha shughuli za biashara ndogo na za kati kufikia SMEs 1,361 ambazo zimezalisha ajira 2,156. Kupitia Mpango huu 76% ya wafanya biashara za ujasiriamali ambao ni wanawake wamejengeka kibiashara kwa kuongeza ari ya kujiamani, kushawishi ili kupata biashara na kuwa na mtandao mpana kwa ajili ya taarifa

Vituo hivi vya Ujasiariamali (Enterprise Innovation Centres) viko katika Mikoa ya Mwanza, Iringa, Lindi na Mtwara. Vituo hivi ni muhimu sana kwa ajili ya kuwaunganisha wafanyabiashara na wadau wengine ambao ni muhimu katika uendelezaji wa biashara hasa wale ambao ndio wanaanza.



*Mjasiriamali, Bora Mganda akiuza vyakula vyenye Lishe ambapo alipata ufadhili kupitia mradi wa T-LED*

### 10.3.2.12. Twende

Twende ni kituo cha Ubunifu jamii na mafunzo kilichopo Arusha ambacho kinalenga kuwezesha watu mbalimbali kubuni na kutumia teknolojia kuboresha bidhaa na maisha kwa jamii inayowazunguka. Lengo la Twende ni kutatua changamoto ya watanzania kushindwa kuvifanyia matengenezo vifaa vinavyozalishwa nje ya nchi; na vile ambavyo havizingatii mazingira yetu na raslimali zilizopo. Vilevile, Twende ina madhumuni ya kuzalisha bidhaa ambazo zitamfaa mtanzania wa kawaida hivyo kuzalisha bidhaa zinazotatua mahitaji halisi ya mtanzania

Twende inashirikiana na wanafunzi na jamii husika kutambua changamoto na kubuni njia, mbinu au bidhaa ili kupata ufumbuzi wa matatizo yanayowakabili kwa kuhakikisha kuwa Tanzania inaboresha mazingira ya upatikanaji na matumizi ya teknolojia ambayo itaboresha maisha. Twende inahitaji kutumia ubunifu na teknolojia kuimarisha uchumi ambao utawezekana kwa kuwa na jamii ya wabunifu na wagunduzi ambao wanatatua changamoto zinazoikabili jamii.

Hivyo, Twende inafundisha jamii

i. Kutatua matatizo yanayowagusa

ii. Kutumia raslimali zinazowazunguka katika kutatua matatizo
iii. Kubuni bidhaa za gharama nafuu na zinazopatikana
iv. Kubuni bidhaa zinazoweza kufanyiwa matengenezo hapa Tanzania.

**Baadhi ya ubunifu waliowezesha:**



*Frank Mollel MCA Technologies Kisambaza Mbolea (Manure Spreader imesaidiwa na Eduardo Montes & Jim Elsworth*

*Elliot Avila Imara Tech Mashine ya Kuvunia (Multi-Crop eThresher Amewezeshwa na Alfred Chengula, Adriana Garties, Athumani Misunga*



### 10.3.2.13. Kakute

KAKUTE ni Mradi unaondeleza Ubunifu Tanzania ambao unatekelezwa katika jiji la Arusha kwa udhamini wa DOEN Foundation. KAKUTE inalenga kuendeleza Ubunifu katika Nishati ambayo inahitajika vijijiji ili kujikwamua na umaskini *(Developing Grassroots Energy Innovations for Productive use and Wellbeing in Rural Tanzania)*.

Uendelezaji Ubunifu unaofanywa na KAKUTE unahusisha utoaji wa ushauri, usimamizi (mentoring), uendelezaji wa kazi za ubunifu na kuwaunganisha wabunifu na wafanya biashara wakubwa ili kuendeleza ubunifu. KAKUTE inaboresha upatikanaji wa masoko kwa kuongeza na kuhamasisha mahitaji ya bidhaa husika na kuboresha uzalishaji wenye tija. Aidha, Majukumu ya KAKUTE ni pamoja na:-

i. Kuhamasisha upatikaji na matumizi ya teknolojia rafiki kwa kuwezesha vituo vya utafiti na elimu ya juu ili zifanye tafiti zinazotatua changamoto zinazoikabili jamii;
ii. Kuhamasisha ushirikiano kati ya vituo vya utafiti vya Tanzania na vya kimataifa na kuviunganisha na sekta binafsi yenye mahitaji ya matokeo ya tafiti husika;
iii. Kuimarisha Taasisi za Ubunifu wa Teknolojia kwa ajili ya utekelezaji wa Sera kwa kushauri kuhusu ujengaji wa uwezo;

iv. Kuimarisha Atamizi na Programu za Usimamizi wa wajasiriamali wanaoanza ili kuedeleza ubunifu kwa tija; na
v. Kukusanya na kusambaza taarifa mahsusi za masoko na kutambua fursa za ushirikianao kati ya taasisi za ndani na za kimataifa kwa ajili ya kuendeleza biashara za wajasiriamali.

#### 10.3.2.14. Nelson Mandela African Institute of Science and Technology (NM-AIST)

Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Afrika, inaendeleza Ubunifu hapa Tanzania kupitia Kituo cha Africa Centre for Research, Agricultural Advancement, Teaching Excellence And Sustainability (CREATES). Kituo hiki kimeanzishwa January, 2017 kwa ushirikianao na Benki ya Dunia *(World Bank's African Centers of Excellence).* CREATES imejipanga kuwa Kituo cha Ubunifu cha Kikanda kwa ajili ya kubuni uendelezaji wa Chakula na Lishe katika Kanda ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini kwa kufundisha vijana katika ngazi ya Uzamili, Uzamivu na Utafiti. Vilevile Kituo hiki kimejipanga kuhakikisha kuwa kinatoa Kozi za muda mfupi, Semina, Makongamano na maonyesho kwa ajili ya kuendeleza Ubunifu na Ujasiriamali hapa nchini. CREATES ambayo ina Atamzi ya Data Driven Innovation (DDI) iko chini ya Shule ya Life Science and Bio-Engineering (LiSBE). DDI ni miongoni mwa Atamizi nne katika Kanda ya Afrika ya Mashariki ambayo imedhaminiwa na Baraza la Vyuo Vikuuu la Afrika ya Mashariki (Inter Universities Council for East Africa -IUCEA) na ufadhili kutoka Benki ya Dunia. DDI imeitisha na kuwaalika wabunifu wenye mawazo, bunifu, bidhaa na huduma zinazohitaji kuendelezwa ili waweze kushiriki ili kuendeleza biashara zao. Jumla ya maombi 10 yalipokelewa kwa ajili ya hatua zinazofuata ili waweze kuendeleza ubunifu wao na kati yao sita wakatangazwa kuchaguliwa baada ya mchakato kukamilika ambao ni Never Zekeya, Angela Mkindi, Geofrey Raymond, Christina Charles, Shakila Mshana and Michael Hudson. Waliochaguliwa watafadhiliwa na DDI na kunufaika na :-

I. Usimamizi wa Biashara na Ushauri (Mentorship and guidance)
II. Miundombinu ya Atamzi (Incubation infrastructures)
III. Kuwezeshwa kwenye utafutaji wa masoko yenye tija ikiwemo usajili, Alama za Ubora na ujuzi wa kibiashara.

#### 10.3.2.15. Obuntu

Obuntu ni kituo cha kuendeleza ubunifu kwa lengo la kuwawezesha Vijana ambacho kipo Dar es salaam. Obuntu kinatoa nafasi kwa ajili ya kazi, ujuzi, maarifa na kusaidia jamii. Kituo kina wasimamizi waliobobea katika uendelezaji ujasiriamali na kuwaunganisha na wawekezaji wakubwa ambao wanahitaji kuwekeza katika kuendeleza ubunifu. Pia huhusisha mashirika ya umma na binafsi ambayo yana nia ya kuendeleza vijana katika kazi zao za ubunifu.

Katika kuendeleza uendelezaji wa ujuzi wa kazi kwa vitendo *(Practical Skills Development)* Obuntu imebuni mbinu ya kipekee ya kufundishia ambayo inaitwa *Class Enterprise Model*.

Washiriki wanafikiria kuhusu ujasiriamali na kufanya shughuli ya kijamii kutokana na mafunzo kupitia Jijenge na Maisha Yangu *(entrepreneurship and life skills training)*. Mafunzo humalizika kwa mshindi wa wazo la biashara kupata kiasi cha fedha kutoka kwa mwekezaji aliyealikwa.

#### 10.3.2.16. Vision for Youth

*Vision for Youth* inawalenga Vijana ili waweze kubuni na kuzalisha bidhaa zenye tija kwa ajili ya biashara. *Vision for Youth* huwaendeleza vijana kwa kujitolea na ilianzishwa tarehe 29 julai 2000 kama non governmental organization. *Vision for Youth* inawalenga Vijana ili kuwahamasisha na kuwawezesha kushiriki katika njia za uchumi.

Kituo hiki kipo Dar es Salaam na kilianzishwa ili kutatua changamoto za jamii na kundi la vijana ambalo halishiriki kikamilifu katika shughuli za uchumi. Kituo hiki kinalenga kuwajengea uwezo vijana katika elimu ya uraia, kuendeleza biashara ili vijana waweze kujitambua na kushiriki katika shughuli za kiuchumi.

#### 10.3.2.17. CAMARTEC

*Centre for Agricultural Mechanization and Rural Technologies* (CAMARTEC) ni Taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara ambayo imeundwa pamoja na mambo mengine ni kwa ajili ya kuendeleza kazi za ubunifu Tanzania. CAMARTEC inafanya tafiti za teknolojia katika kilimo kwa kuzingatia mazingira.

Majukumu ya CAMARTEC katika kuendeleza wabunifu ni pamoja na; kufanya tafiti ili kubuni teknolojia rafiki katika uhandisi wa kilimo vijijini; Kubuni na kuziendeleza bidhaa zilizothbitishwa na kutathmini kama zinafaa kwa watumiaji; kuhaulisha teknolojia za nje ili ziweze kufaa na kutumika katika mazingira ya Tanzania; kuzifanyia majaribio zana zinazobuniwa kwa ajili ya kilimo kama zinafaa; na kuendesha kozi fupi kwa ajili ya kuongeza maarifa na ujuzi katika kuendeleza kilimo.

#### 10.3.2.18. Nafasi Arts Space

Nafasi Art Space ni kituo cha kuendeleza Ubunifu katika Sanaa ambacho kilianzishwa mwaka 2008 na kipo Dar es Salaam. Kituo hiki kinaendeleza Ubunifu wa sanaa katika fani zote ikiwemo uchoraji, maigizo na uchongaji. Hivyo, katika kituo hiki wabunifu wanabuni, wanajifunza, wanaonesha kazi za sanaa na kufanya majaribio. Kwa hiyo ni kituo ambacho kinatoa nafasi kwa wapenda sanaa na wasanii kwa ujumla kuja kujifunza na kubuni kazi mbalimbali za kisanii.

*Nafasi Art Space* inauwezo wa kutoa mafunzo kwa wasanii 50 kwa kipindi kimoja kwa kutumia studio 37, na nafasi mbalimbali za maonyesho. Mafunzo hutolewa kupitia programu mbalimbali, semina, makongamano, maonesho na majadiliano kwa njia ya filamu. Kwa ujumla *Nafasi Arts*

*Space* inapokea wageni zaidi ya 1000 kwa mwezi. Aidha, Nafasi Art Space ina Studio za watoto kwa ajili ya kujifunza, nafasi kwa ajili ya maonyesho, michezo ya sanaa ya nje na ndani.

#### 10.3.2.19. Ndoto Hub

Ndoto Hub ni kituo cha kuendeleza Ubunifu ambacho kipo Dar Es salaam mahsusi kwa ajili ya kuendeleza wajasiriamali na wabunifu wanawake. Kituo hiki kinalenga kuwajengea uwezo wabunifu wanawake ili wawe wajasiriamali wenye uweledi mkubwa, wenye kujiamini na kuwa na uwezo wa kuzitafuta fursa za kiuchumi na kuzitumia kikamilifu.

#### 10.3.2.20. Apps and Girls

*Apps and Girls* ni kituo cha Ubunifu kinacholenga kuwawezesha wasichana na wanawake ili waweze kutatua changamoto zinazowakabili kwa kutumia teknolojia. Kituo hiki kinatoa ujuzi na maarifa kwa wanawake ili waweze kufanya kazi zao za uajsiriamali kwa ufanisi kwa kutumia teknolojia ya TEHAMA.

Kupita *Apps and Girls* wasichana walio katika mpango huu wanapewa wasimamizi waliobobea (*mentors*) na kuingizwa katika programu ya Atamizi ili kuendeleza kazi zao za TEHAMA. Kupitia Mpango wa Uendelezaji wa Ujuzi, wasichana waliohitimu elimu ya juu na kukosa ajira wanajengewa uwezo katika TEHAMA ili wawe wabobezi na kuwa mahiri ili kufikia viwango vinavyoohitajika. Aidha, Kituo kinaendesha Kozi za juu za TEHAMA na Atamizi kwa njia ya mtandao kwa ajili wasichana ambao hawakupata nafasi ili waweze kushindana kwenye TEHAMA hivyo kupata ajira na kuwawezesha kuanzisha biashara zao. *Apps and Girls* wanaendesha Makongamano, Maonyesho, Mijadala, Makambi na program mbalimbali ili kuwajengea wasichana ari ya kupenda kujifunza na kutumia teknolojia katika shughuli za kila siku

#### 10.3.2.21. Buni Hub

*Buni Hub* ni kituo kinacholenga kuendeleza teknolojia na ubunifu kwa watanzania na kilianzishwa mwaka 2011, ikiwa sehemu ya mradi wa TANZICT ambao ulitekelezwa kwa ushirikianao kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Finland. Buni inalenga kubuni, kuendeleza na kusimamia vijana ili waendeleza ubunifu katika teknolojia. *Buni hub* ni kituo cha kwanza kuanzishwa ili kuwaendeleza wabunifu Tanzania.

*Buni Hub* imesaidia Vijana 350 ambao wote ni watanzania ambapo 60% ni wanafunzi wa elimu ya juu kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania. Kutokana na kukua Buni Hub kwa sasa imepokea na kusajili wabunifu zaidi ya 5000 ambao wanataka kutumia nafasi ya kituo ili kuendeleza ubunifu wao.

Mpango wa muda mrefu wa Buni hub ni kuwezesha hatua za awali za ubunifu kwa kutumia mtandao (online and offline innovation space toolkit) ambao zina maelezo ya jinsi ya kutumia

mtandao huo katika kuendeleza ubunifu. Mpango huu umefanikiwa katika Vyuo vikuu zaidi ya 10 Tanzania ambavyo ni UDOM (Dodoma University Innovation Space), Chuo Kikuu cha Iringa (Tumaini University), SUZA (State University of Zanzibar), Zanzibar Teknohama Business Incubator, Mkwawa University, Mzumbe University, NM-AIST (Nelson Mandela Institute of Science and Technology), Marian University College and Mbeya University of Science and Technology.

#### 10.3.2.22. UDIEC

Kituo cha UDIEC kinaendeshwa na Idara ya Ubunifu na Ujasiriamali ya Chuo Kikuu cha Dar Es salaam ambapo lengo lake ni kuwa kituo kinachoongoza katika masuala ya ubunifu na Ujasiriamali Afrika. UDIEC ina wezesha ujasiriamali na ubunifu unaolenga kutatua changamoto za jamii kwa kutoa mafunzo yenye ubora, ushauri wa kitaalamu na kuatamia wanafunzi, wafanyakazi wa chuo na wajasiriamali wadogo na wakati pamoja na wadau wengine wenye ubunifu ili kuwaendeleza.

Huduma zinazotolewa na UDIEC kwa wabunifu, wajasiriamali na viwanda ni pamoja:-

i. Kuandaa Mpango wa biashara (Business plan development);
ii. Kuchambua faida za kiuchumi za teknolojia na upatikanaji wa masoko;
iii. Kutangaza biashara na Masoko;
iv. Usimamizi wa Biashara Ushauri wa kifedha;
v. Kujenga Mitandao ya wadau wa biashara; na
vi. Kufundisha wabunifu na wajasiriamali katika maeneo yao.

#### 10.3.2.23. Jenga

Jenga Hub ni kituo kinachotumia teknolojia kutoa elimu ambayo inafudisha jinsi ya kutunza kumbukumbu na mawazo muhimu na hivyo kufanya mafunzo yanayovutia kwa walengwa. Kupitia Jenga Hub Vijana wanafundishwa kuwa na ari ya kujifunza na kubuni kwa kutumia kumbukumbu walizojifunza kutumia teknolojia ya neno la siri (*coding*). Hadi sasa Jenga Hub imefundisha Vijana zaidi ya 8000 kuweka kumbukumbu kwa kutumia neno la siri (*coding*) na waalimu zaidi ya 1500 wamefundishwa mitaala kuhusu neno la siri (*coding*)kutoka kwenye shule 20 ambazo zimeanzisha club za coding

Jenga Hub inawajengea uwezo waalimu kwa kuwapatia ujuzi, maarifa na vifaa ili kuongeza maarifa ya elimu ya mtandao kwa wanafunzi darasi na hata katika mazingira mengine. Vilevile imeanzisha clubs kwenye shule 20 ambazo zinawajengea wanafunzi uwezo wa kutumia teknolojia na kuwa wabunifu

#### 10.3.2.24. Seedspace

Seedspace inapatikana katika eneo maarufu kama *Silicon Dar* ambayo inalengo la kuwawezesha Vijana kutumia maarifa na ujuzi kwa kuwapatia nafasi ya kufanyia kazi, fursa za mafunzo sahihi na kukutana na jumuiya ya wajasiriamali waliofanikiwa pamoja na wawekezaji

#### 10.3.2.25. Safespace Co

Safespace Co Hub inapatikana Dar Essalaam na inalenga kuwaendeleza wajasiriamali wanawake ili waweze kubuni biashara zenye tija. Kupitia Safespace wanawake wanapata nafasi ya kupata mafunzo, kuboresha kazi zao za ubunifu na taarifa hivyo kuwajengea ari ya kuwa jasiri, kujiamini, kujisimamia na kutokukata tamaa.

#### 10.3.2.26. TAREBI /IMED

TAREBI Hub ni Kituo ambacho kipo Dar Es salaam chini ya *Institute of Management and Entrepreneurship Development* ambacho kinaendeleza ubunifu katika Nishati Mbadala (umeme jua, majiko bainifu na mkaa endelevu). Vijana wanaolelewa katika kituo hiki wanapata mafunzo ya ujasiriamali katika nishati mbadala ili waweze kuanzisha makampuni mbalimbali. Kupitia TAREBI kuna Makampuni zaidi ya 8 yameanzishwa ambayo yametoa ajira ya nishati ya jua yako Makampuni 4 na 4 wamegawanyika katika Pellets na Briquette. Awamu ya pili ya TAREBI ambayo ilizinduliwa tarehe 17 Januari 2020 imechukua Vijana 20 ambao wanatoka katika Mikoa ya Dar Es salaam, Iringa na Dodoma. TAREBI ya pili inawalea vijana na kutoa mafunzo katika Nishati ya Jua pekee.

#### 10.3.2.27. AMCET Hub

AMCET hub ipo Chuo cha Al-maktoum ambayo inalenga kuwalea vijana na kuwasimamia ili waweze kuendeleza mawazo na bidhaa zao. AMCET inawasaidia wanafunzi na jamii inayozunguka kwa ajili ya kuwapatia ari ya ubunifu katika teknolojia. AMCET ina maono ya kuwa taasisi inayoongoza katika kuendeleza ubunifu, ugunduzi na teknolojia kwa vijana hapa Tanzania. Huduma zinazotolewa AMCET hub ni pamoja na:-

i. Kuendeleza mawazo ya ubunifu ya vijana ili yawe biashara halisi
ii. Kukutana na wajasiriamali wengine kwa ajili ya kubadilishana uzoefu ili kukuza biashara na kuweza kuiweka sokoni
iii. Kuwajengea uwezo vijana ili kuwa na ujuzi na maarifa ya kukabiliana na kazi katika soko la ajira
iv. Kuwawezesha Vijana wabunifu kutengeneza ajira kwa vijana wengine

#### 10.3.2.28. Dlab

Data Lab (dLab) ni Asasi Isiyo ya Kiserikali ambayo imeanzishwa June 2018 ikiwa inaendeleza miradi mitatu ambayo ni Tanzania Data Lab (dLab), Data Zetu na Data for Local Impact

Innovation Challenge (DLIIC). Hivyo, Tanzania Data Lab ilianzishwa kimkakati ili kuimarisha kazi na matokeo ya miradi ya data ilityotangulia Tanzania.

Dlab inalenga kuinua ubunifu katika kutumia data kwa kuwaongezea ujuzi wafanyakazi wa Serikali, asasi za kiraia na jamii kwa ujumla na kuwawezesha kupitia data ili kupanga shughuli za maendeleo. Dlab inawahusisha wadau mbalimbali na inatekelezwa katika maeneo ya **Kilimanjaro, Mzizima na Serengeti**

#### 10.3.2.29. Hub255

Hub255 iko Dar Es salaam na inatoa nafasi ya kukutana na wabunifu na wabobezi katika maeneo mbalimbali ambayo ni ubunifu wa mitindo, wapiga picha, wahandisi ambao hutoa huduma zifuatazo:-

1. Ofisi ya kufanyia kazi ili kuongeza tija;
2. Kukutana na wazoefu na wabunifu hivyo kubadilishana uzoefu;
3. Mafunzo na malezi kutoka kwa wataalamu

#### 10.3.2.30. SheCodes For change

*SheCodes For change* ni hub ambayo inahamasisha wanawake ili waweze kuendeleza kazi zao za ubunifu na kuwa wajasiriamali wanaoongoza katika kutumia teknolojia. *She Codes* inawandaa wasichana kuwa na ari na kupenda masomo ya **Sayansi, Teknolojia, Engineering, Arts/Design na Hesabu** (STEAM) wakiwa wadogo. Wasichana wanaolengwa ni wale wenye umri wa miaka 12-19; walioko vyuoni na vyuo vikuu.

Malengo ya SheCodesForChange ni kuongeza idadi ya wanawake wanaofanya kazi katika TEHAMA hapa Tanzania.Programu zinalenga kupunguza tofauti ya idadi ya wataalamu wa TEHAMA kwa Jinsia (Digital gender skills gap) na kuwawezesha wanawake kuwa wabunifu ili kupata nafasi katika soko la ajira kwa kuajiriwa au kutengeneza ajira. SheCodesForchange imewafikia wasichana 980 katika Miradi 50 iliyotekelezwa na matukio ya kuhamasisha 15.

Kupitia Programu mbalimbali zinazoendeshwa na SheCodesForchange wasichana wanapita katika hatua za mafunzo, malezi na kuhamasishwa kusoma masomo ya teknolojia ambayo yanahamasisha ubunifu na ujasiriamali

#### 10.3.2.31. Mkwawa Community Arts Space

Kituo hiki kinapatikana Mkoani Iringa na kinalenga kuwasaidia jamii husika ili kuwa wabunifu na wajasiriamali katika masuala ya sanaa. Kituo hiki kinatoa fursa kwa vijana kuboresha ubunifu wa kazi zao za kisanii ili kujikwamua kiuchumi. *Mkwawa Community Arts Space* inatumia sanaa kama njia ya kuwawezesha Vijana.

#### 10.3.2.32. Kilihub (Anza)

*Anza Hub* ni kituo kinachotoa ofisi kwa ajili ya wabunifu na wajasiriamali kukutana na kufanya kazi za ubunifu. Kupitia Anza Hubs ambayo iko mjini Moshi, Mkoani Kilimanjaro wajasiriamali wanahamasishwa kufikiria ubunifu na kuendeleza mawazo yao. *Anza Hub* inatoa ofisi za kufanyia kazi, usimamizi, malezi, vyumba vya mikutano na uwepo wa mtandao.

**Kituo cha Atamizi Zanzibar (Zanzibar incubation Centre)**

Uanzishaji wa Kituo cha Atamizi Zanzibar ni miongoni mwa jitihada zinazofanywa na Serikali kupitia COSTECH katika kuhamasisha Ubunifu na Ujasiriamali ndani ya mipaka ya Tanzania. Kituo hiki kinatoa nafasi kwa ajili ya wabunifu waliopo Zanzibar waweze kukutana, kubadilishana mawazo miongoni mwa makundi mbalimbali, kutumia miundombinu inayohamasisha ubunifu kwa pamoja kwa lengo la kuendeleza ubunifu Tanzania.

**Rlabs**

Rlabs inapatikana mjini Iringa na imeanzishwa mahususi kwa ajili ya kutoa nafasi itakayowajumuisha wabunifu pamoja na wajasiriamali. Kupitia mpango huu Serikali kupitia COSTECH wameweza kutoa fedha za uendeshaji kwa mwaka mmoja ambazo zinatumika katika kujenga uwezo wa kituo ili kitimize madhumuni ya uanzishwaji wake.

**St. Joseph Technepreneur Incubation Centre**

Kituo hiki kipo Dar es Salam kimeanzishwa ili kuhamasisha ubunifu na ujasiriamali nchini. Serikali kupitia COSTECH wanahusika katika kukijengea uwezo ili kiweze kutimiza malengo yake.

**Anza Accelerator**

Hiki ni kituo kilichopo Jijini Arusha kwa ajili ya kusaidia Vituo mbalimbali vinavyolenga kuhamasisha Ubunifu Tanzania. COSTECH inakilea kituo hiki ili kiweze kuleta tija kwa kukijengea mitandao pamoja na uwezo utakaowawezesha kushindana katika soko na tasnia ya Ubunifu nchini.

**Bio Innovation Space**

Kituo hiki kinalenga kuhamasisha Ubunifu unaohusu viumbe hai na kinapatikana Bagamoyo. COSTECH imehamasisha uanzishaji wake.

**Mushroom Innovation Centre**

Kituo hiki cha Ubunifu kinahusika na kuendeleza Ubunifu wa Uyoga na bidhaa zake. Kituo hiki ambacho kiko Dar es Salaam kilianzishwa kwa ushirikiano na COSTECH.

**Jamii Digital Innovation Centre**

Kituo hiki ni cha Ubunifu kipo Tengeru katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii mkoani Arusha. Kituo kina lenga kuwahamasisha wanafunzi wanaomaliza, wanaoendelea na jamii ya wanataaluma kupata nafasi ya kubuni na kuendeleza ubunifu katika TEHAMA. COSTECH imesaidia katika kuanzisha, kuendelea kuwajengea uwezo wa kusimamia kituo hiki ili kitekeleze majukumu yaliyokusudiwa.

**Digital Innovation Centre Ruaha (DICR)**

Kituo hiki ni cha Ubunifu kipo katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha mkoani Iringa. Kituo cha DICR kimeanzishwa ili kuwahamasisha wanafunzi wanaomaliza chuoni hapo, wale wanaoendelea, jamii ya wanataaluma na jamii inayozunguka chuo ili kupata nafasi na vifaa vya kuwezesha kubuni na kuendeleza ubunifu katika TEHAMA. COSTECH imesaidia katika kuanzisha, kuendelea kuwajengea uwezo wa kusimamia kituo hiki ili kiendele na kutimiza malengo yake.

**Digital Innovation Centre Misungwi**

Kituo hiki ni cha Ubunifu kipo katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Misungwi kipo Mkoani Mwanza. Malengo mahususi ya kuanzisha kituo hiki ni pamoja na kuwahamasisha wanafunzi wanaomaliza, wanaoendelea na jamii ya wanataaluma kupata nafasi ya kubuni na kuendeleza ubunifu katika TEHAMA. COSTECH imesaidia uanzishwaji, kuendeleza na kuwajengea uwezo wa kusimamia kituo hiki ili kilete tija.

**Digital Innovation Centre Uyole**

Kituo hiki ni cha Ubunifu kipo katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole kipo Mkoani Mbeya. Kituo kinalenga kuwahamasisha wanafunzi wanaomaliza, wanaoendelea na jamii ya wanataaluma kupata nafasi ya kubuni na kuendeleza ubunifu katika TEHAMA. COSTECH imesaidia katika kuanzisha, kuendelea kuwajengea uwezo wa kusimamia kituo hiki ili kiweze kuleta maendeleo katika tasnia ya ubunifu.

**Digital Innovation Centre Mabughai**

Kituo hiki ni cha Ubunifu kipo katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mabughai kipo Mkoani Tanga. Kituo kinahamasisha wanafunzi wanaomaliza, wanaoendelea na jamii ya wanataaluma kwa ujumla kupata nafasi ya kubuni na kuendeleza ubunifu katika TEHAMA. COSTECH imesaidia katika kuanzisha, kuendelea kuwajengea uwezo wa kusimamia kituo hiki ili kilete matokeo yaliyotegemewa.

**Digital Innovation Centre Monduli**

Kituo hiki ni cha Ubunifu kipo katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli kipo Mkoani Arusha katika maeneo ya Monduli mjini. Kituo hiki kimeanzishwa ili kuwahamasisha

wanafunzii wanaomaliza, wanaoendelea na jamii ya wanataaluma kupata nafasi ya kubuni na kuendeleza ubunifu katika TEHAMA. Seriklai kupitia COSTECH imesaidia katika kuanzisha, kuendelea kuwajengea uwezo wa kusimamia kituo hiki ili kukuza ubunifu nchini.

**Digital Innovation Centre Rungemba**

Kituo hiki ni cha kuendeleza ubunifu kinapatina katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba kipo Mkoani Iringa. Kituo hiki kinawahamasisha wanafunzi wanaomaliza, wanaoendelea na jamii ya wanataaluma kupata nafasi ya kubuni na kuendeleza ubunifu katika TEHAMA. Seriklai kupitia COSTECH imesaidia katika kuanzisha, kuendelea kuwajengea uwezo wa kusimamia kituo hiki ili kilete matunda yaliyokusudiwa.

**Digital Innovation Centre Buhare**

Kituo hiki cha Ubunifu kipo katika Chuo cha Ustawi wa Jamii Buhare kipo Mkoani Mara katika maeneo ya Buhare. Kituo cha kuendeleza Ubunifu kinalenga kuwahamasisha wanafunzi wanaomaliza, wanaoendelea pamoja na jamii ya wanataaluma kupata nafasi ya kubuni na kuendeleza ubunifu wao na ujasiriamali katika TEHAMA. COSTECH imesaidia katika kuanzisha, kuendelea kuwajengea uwezo wa kusimamia kituo hiki ili kilete matunda yaliyokusudiwa ikiwemo kukua kwa kituo hiki.

**Digital Innovation Centre Institute of Social Work**

Kituo hiki cha Ubunifu kipo katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii ambacho iliyopo Dar E salam katika maeneo ya Kijitonyama. Kituo kinalenga kuwahamasisha wanafunzi wanaomaliza, wanaoendelea na jamii ya wanataaluma kupata nafasi ya kubuni na kuendeleza ubunifu katika TEHAMA. COSTECH imesaidia katika kuanzisha, kuendelea kuwajengea uwezo wa kusimamia kituo hiki ili kilete matunda yaliyokusudiwa.

**Arusha Institute of Accountancy Incubation Centre**

Atamizi hii ipo katika Taasisi ya Uhasibu Arusha na imeanzishwa na kulelewa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia. Kituo kinaandaa vijana wanaomaliza katika Taasisi ili wawe wabunifu katika masuala ya TEHAMA.

#### 10.3.2.33. Innovation Hub nyingine

Vituo vya Ubunifu vingine Tanzania ni pamoja na Niwezeshe Hub, University of Dar Es salaam ICT Incubator (UDCTI); Sahara; Biashara Lab TAYOA na  Elimu lab Sengerema ambayo iko Mkoani Geita.

### 10.4. CHANGAMOTO ZA UBUNIFU TANZANIA

Katika kuendeleza Ubunifu Tanzania bado kuna changamoto ambazo zinatakiwa kushughulikiwa ili kupata matokeo yanayotarajiwa. Changamoto hizo ni pamoja:-

i. Kutokuwa na taarifa za kutosha kuhusu uwepo wa Atamizi hapa nchini na hata zilizopo hazitoi taarifa za idadi ya wanaowahudumia, maeneo wanayoyafanyia kazi na changamoto wanazokabiliana nazo;
ii. Kuna hitajika kuwa na sera rafiki zitakazoelekeza juu ya uratibu wa Atamizi;
iii. Taasisi za fedha kutotoa mikopo kwa ajili ya kuwezesha ubunifu unaoanza
iv. Uwezo mdogo wa wabunifu kukamilisha kazi walizozianzisha
v. Atamizi nyingi zinaendeshwa kwa ufadhili wa wadau wa maendeleo hivyo kutokuwa na uendelevu miradi inapokwisha;
vi. Ushirikiano mdogo miongoni mwa wadau wa vituo vya ubunifu;
vii. Uhusiano mdogo kati ya tafiti, ubunifu na sekta binafsi katika kuendeleza masuala ya ubunifu

## HITIMISHO

Uanzishwaji wa Vituo vya uendelezaji ubunifu pamoja na Atamizi ni chachu katika uwezeshaji wananchi kiuchumi. Kwa kuwa Uwezeshaji wananchi ni suala mtambuka hivyo linahitaji ushirikishwaji wa wadau ili liweze kuleta tija. Lengo ni kuhakikisha kuwa vituo hivi vinakuwa endelevu hata baada ya kumalizika kwa miradi iliyohusika katika kuanzisha. Uendelevu wa atamizi ni muhimu sana kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii hivyo kuingiza kuwa miongoni mwa vipaumbele vya nchi ni suala ambalo linahitajiwa kuzingatiwa na wadau wote.

## 11.0. USHIRIKI WA WATANZANIA MIRADI YA KIMKAKATI NA UWEKEZAJI (LOCAL CONTENT)

### 11.1. UTANGULIZI

Dhana ya Ushiriki wa Watanzania *(Local Content)* katika Miradi ya Kimkakati na Uwekezaji ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi inayolenga kufanikisha shabaha ya Serikali katika kuijenga nchi ya viwanda na kuinua uchumi wa kati ili uende kwenye ngazi nyingine. Utekelezaji wa dhana ya *Local Content* ni mtambuka kwa kuwa inashirikisha wadau wa sekta mbalimbali za kiuchumi.

Uratibu wa *Local content* katika sekta mbalimbali za kiuchumi ulianza kutekelezwa mwaka 2015 kwa lengo la kuhakikisha thamani ya ziada inayotokana na miradi ya kimkakati na uwekezaji inabaki nchini na kuchangia ukuaji wa uchumi. Mazingira wezeshi yameendelea kuwekwa kwa lengo la kuhimiza ongezeko la ushiriki wa watanzania kunufaika na kumiliki sehemu kubwa ya uchumi wa nchi. Dhana hii imeendelea kufahamika kwa wadau mbalimbali sambamba na mazingatio ya vipaumbele vilivyowekwa na Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) ina jukumu la kuratibu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa dhana ya *Local Content* kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Kisekta. Wadau wa kisekta ni Wizara, Taasisi za Umma, Asasi za Kiraia, Wawekezaji, Wakandarasi, Kampuni binafsi, Wafanyabiashara, Mabenki, Wataalam Washauri Elekezi, Vyuo vya Elimu n.k.

Tanzania inatekeleza miradi ya maendeleo ya kimkakati ambayo inakisi shabaha ya mabadiliko chanya ya maendeleo ya ukuaji wa uchumi wa nchi. Baadhi ya miradi hiyo ya kimkakati ni Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP), Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), Ujenzi wa Barabara, Miradi ya maji, Ujenzi wa Uwanja wa Ndege JNIA III, Uwekezaji katika migodi (Madini), Nishati, Mafuta na Gesi Asilia n.k. Utekelezaji wa dhana ya *Local Content* umezingatia maeneo ya msingi yafuatayo:-

### 11.2. HALI YA AJIRA

Ushiriki wa watanzania kupitia ajira umeendelea kupewa kipaumbele na kuzingatiwa ipasavyo katika miradi mbalimbali ya kimkakati na uwekezaji nchini. Hii inadhihirisha wazi kuwa utekelezaji wa dhana ya ushiriki wa watanzania imeendelea kufahamika na wadau wa sekta mbalimbali za kiuchumi. Aidha, utekelezaji wa dhana ya ushiriki wa watanzania imechangia kuongeza ajira kwa watanzania na ajira chache kwa wageni tofauti na miaka ya huko nyuma. Ajira zimeongezeka kwa watanzania wenye ujuzi, ujuzi wa kati na wasio na ujuzi huku ajira za wageni zikitolewa kwa wenye ujuzi na ujuzi wa kati. Vilevile zaidi ya 92% ya ajira za wenye ujuzi wa kati na wasio na ujuzi katika miradi ya kimkakati zimetolewa kwa watanzania. Jedwali

hapa chini linaonyesha ajira za wageni na watanzania walioajiriwa katika miradi iliyoonyeshwa hapa chini:-

**Jedwali Na. 21: Hali ya Ajira za Wageni na Watanzania Katika Miradi Mbalimbali**

| Mradi | Wageni | | | Watanzania | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wenye Ujuzi | Ujuzi wa Kati | Wasio na Ujuzi | Wenye Ujuzi | Ujuzi wa Kati | Wasio na Ujuzi |
| **1. Mradi wa Kufua Umeme (JNHPP)** | 3441[1] | 38[1] | 0[1] | 137[1] | 1,023[1] | 968[1] |
| **2. Reli ya Kisasa – SGR (Lot 1 & 2)** | 1,802 | 452 | 14 | 7,168 | 909 | 2,070 |
| **3. Ukarabati wa Reli ya Zamani (TIRP)** | | - | - | 152 | 175 | 759 |
| ***4. Ubungo Interchange*** | 94 | - | - | 22 | 605 | 193 |
| ***5. New Salender Bridge*** | 23 | 19 | - | 34 | 177 | 378 |
| **6. Uwanja wa Ndege wa Kimataifa (JNIA TB III)** | 3 | - | - | 407 | 379 | 19 |
| **7. Miradi ya Ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha Lami** | | | | | | |
| **7.1 Urambo-Kaliua (km 28)** | - | - | - | 95 | 48 | 90 |
| **7.2 Nyahua-Chaya (km 85.4)** | 15 | - | - | 15 | 31 | 100 |
| **7.3 Mbinga-Mbamba Bay (Km 66)** | 4 | 21 | 5 | 5 | 130 | 79 |
| **8. Miradi ya umeme wa Nishati vijijini** | 90 | - | - | 281 | 1,462 | 4,428 |
| **9. Miradi ya Maji Mijini na Vijijini** | | | | | | |
| **9.1 Mradi wa maji kutoa Ziwa Victoria kwenda Miji ya Tabora, Igunga na Nzega** | 198 | 70 | 0 | 241 | 608 | 1,406 |
| **9.2 Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoaji wa majitaka jiji la Arusha** | 102 | 93 | - | 95 | 389 | 1,202 |
| **9.3 Mradi wa maji wa Bulongwe na Lufumbi (Masoko Gravity Main)** | - | - | - | 5 | 20 | 200 |
| **9.4 Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Majisafi (Km 55.755) kutoka Kijiji cha Mhangu hadi kijiji Ilogi - Halmashauri ya wilaya ya Msalala** | 2 | 4 | - | 1 | 10 | 64 |
| **9.5 Miradi ya Upanuzi wa Mitandao ya Maji kwa Vijiji 100 vinavyopitiwa na Bomba Kuu kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama - Shinyanga** | - | - | - | 32 | 53 | 850 |
| **9.6 Mradi wa Maji Same-Mwanga-Korogwe** | 16 | - | - | 23 | 157 | 178 |
| **10. Miradi ya TPDC** | - | - | - | 23 | 286 | 32 |
| **11. Bomba la Mafuta Ghafi (EACOP)** | - | - | - | - | - | - |


[1] *Taarifa ya nguvukazi inaonyesha jumla ya wafanyakazi 2,510 wa Mradi wa JNHPP ambao wamepata ajira kwa mkandarasi mkuu kampuni za JVACEE (1,079) na mkandarasi mdogo Sinohydro (1,431). Taarifa za wakandarasi wadogo wengine na watoa huduma waliopo katika mradi hazikujumuishwa.*

| Mradi | Wageni | | | Watanzania | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wenye Ujuzi | Ujuzi wa Kati | Wasio na Ujuzi | Wenye Ujuzi | Ujuzi wa Kati | Wasio na Ujuzi |
| **12. Maurel et Prom** | - | - | - | - | - | - |
| **13. PanAfrican Energy Tanzania Ltd** | - | - | - | - | - | - |
| **14. Songas** | - | - | - | - | - | - |
| **15. Sekta ya Bima** | 15 | 8 | - | 76 | 504 | 395 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Ushiriki wa Watanzania, 2020*

Mathalani, miradi ya nishati vijijini imeendelea kutekelezwa na Serikali na kutoa fursa za ajira kwa watanzania na wageni. Jumla ya ajira 6,261 za moja kwa moja ziliweza kuzalishwa kutokana na utekelezaji wa shughuli za nishati vijijini ambapo taarifa inaonyesha kuwa ajira za ujuzi wa juu zilikuwa 371 (watanzania 281 na wageni 90), ajira za ujuzi wa kati zilitolewa kwa watanzania pekee ambao walikuwa 1,462 sambamba na ajira za wasio na ujuzi 4,428 ambazo nazo ziliwekwa kwa watanzania pekee. Hii inaonyesha namna dhana ya ushiriki wa watanzania katika miradi ya nishati ilivyozingatiwa na kutoa fursa za watanzania kushiriki na kunufaika katika hiyo miradi. Aidha matumizi ya nishati yameongezeka nchini kwa asilimia 50 kutoka asilimia 35 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 85 mwaka 2020. Taarifa ya Wizara ya Nishati inaonyesha pia vijiji 9,000 zimepata huduma ya umeme na vijiji 3,000 bado ingawa taratibu za kupata umeme zinaendelea kufanyika.

Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (Water Sector Development Plan) ya mwaka 2015 - 2025 imeendelea kutekelezwa ambapo pamoja na mambo mengine imefanikiwa kuboresha upatikanaji wa huduma za maji nchini kufikia 70.1% kwa maeneo ya vijijini na 84% kwa maeneo ya mijini. Mafanikio yametokana na kukamilika kwa miradi mbalimbali ya maji ambapo kati ya mwaka 2015 na mwaka 2019 miradi 1,423 imetekelezwa na inatoa huduma kwa wananchi. Kati ya hiyo miradi 1,268 imetekelezwa vijijini na miradi 155 imetekelezwa mijini. Aidha, upatikanaji wa ajira umeongezeka mfano Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Miji ya Tabora, Igunga na Nzega unaonyesha umetoa jumla ya ajira 2,523 ambapo watanzania ni 2,255 na wageni ni 268. Wageni wenye ujuzi ni 198, ujuzi wa kati ni 70 na wasio na ujuzi hakuna. Watanzania wenye ujuzi ni 241, ujuzi wa kati ni 608 na wasio na ujuzi ni 595. Vilevile, mbali na ajira za kudumu za walinzi 87 katika matanki 29 ya kuhifadhia maji yenye ukubwa tofauti, pia umetoa ajira kwa wakala 724 wa kuuza maji kwenye vikosi 724 vilivyojengwa.




Aidha, miradi inayotekelezwa imeendelea kuzingatia umuhimu wa kuwashirikisha vijana kama sehemu nguvukazi inayohitajika. Kwa mujibu wa ripoti ya utafiti wa nguvu kazi – *(Integrated Labour Force Survery – ILFS)* ya mwaka 2014 inaonyesha nguvukazi ya vijana kufikia 56% ya nguvukazi iliyopo nchini. Tafsiri hii inajidhihirisha kuwa nguvukazi ya vijana wenye ujuzi, wenye ujuzi wa kati na wasio na ujuzi ni muhimu katika kufanikisha mipango ya Serikali katika kuinua viwango vya ujuzi ili watanzania waendelee kushiriki kikamilifu. Jedwali hapa chini linaonyesha ushiriki wa watanzania kwa umri kuongezeka katika miradi mbalimbali ya kimkakati na ile isiyo ya kimkakati.

**Jedwali Na. 22: Ushiriki Wa Watanzania Kwa Umri Kuongezeka Katika Miradi Mbalimbali Ya Kimkakati Na Ile Isiyo Ya Kimkakati**

| Miradi | Umri | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wenye Ujuzi | | | Wenye Ujuzi wa Kati | | | Wasio na Ujuzi | | |
| | 20-35 | 35-45 | >45 | 20-35 | 35-45 | >45 | 20-35 | 35-45 | >45 |
| **1. Mradi wa Kufua Umeme (JNHPP)** | 2,807 | 485 | 286 | 743 | 212 | 106 | 678 | 194 | 96 |
| **2. Mradi wa SGR *(Lot 1 & 2)*** | 4,507 | 3,026 | 1,438 | 862 | 336 | 163 | 1,487 | 446 | 151 |
| **3.Mradi wa Ukarabati Reli (TIRP)** | 168 | 62 | 13 | 98 | 26 | 7 | 1,863 | 864 | 33 |
| **4. Mradi wa Ubungo Interchange** | 18 | 3 | 1 | 585 | 20 | - | 178 | 15 | - |
| ***5.Mradi wa New Salender Bridge*** | 50 | 6 | 1 | 168 | 20 | 8 | 277 | 77 | 12 |
| **6. JNIA TB III** | 379 | 28 | 3 | 357 | 21 | 1 | 18 | 1 | - |
| ***7. Ujenzi wa Barabara kwa Kiwango cha Lami*** | | | | | | | | | |
| **7.1 Urambo – Kaliua** | 40 | 35 | 20 | 18 | 10 | 20 | 50 | 40 | - |
| **7.2 Nyahua-Chaya** | 10 | 20 | 0 | 10 | 20 | 1 | 22 | 58 | 20 |
| **7.3 Mbinga- Mbamba Bay** | 6 | 2 | 1 | 120 | 26 | 5 | 70 | 10 | 4 |


| Miradi | Umri | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Wenye Ujuzi | | | Wenye Ujuzi wa Kati | | | Wasio na Ujuzi | | |
| | 20-35 | 35-45 | >45 | 20-35 | 35-45 | >45 | 20-35 | 35-45 | >45 |
| ***8. Miradi ya Ujenzi wa Maji*** | | | | | | | | | |
| **8.1 Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Miji ya Tabora, Nzega hadi Igunga** | 219 | 194 | 26 | 422 | 201 | 55 | 908 | 371 | 127 |
| **8.2 Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoaji wa majitaka katika jiji la Arusha** | 104 | 58 | 35 | 306 | 121 | 54 | 841 | 280 | 82 |
| **8.3 Mradi wa Bulongwe na Lufimbi (Masoko Gravity Main)** | 1 | 3 | 1 | 13 | 5 | 2 | 103 | 68 | 29 |
| **8.4 Mradi wa Ujenzi wa Bomba la majisafi (KM 55.755) kutoka Kijiji cha Mhangu hadi Kijiji Ilogi Halmashauri ya wilaya ya Msalala** | 0 | 2 | 1 | 8 | 4 | 2 | 44 | 17 | 3 |
| **8.5 Mradi wa Upanuzi wa Mitandao ya Maji kwa Vijiji 100 vinavyopitiwa na Bomba Kuu kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama – Shinyanga** | 17 | 8 | 7 | 28 | 15 | 10 | 595 | 169 | 86 |
| **8.6 Mradi wa Maji wa Same-Mwanga-Korogwe** | 23 | 9 | 7 | 94 | 47 | 16 | 107 | 53 | 18 |
| **9. Miradi ya Nishati Vijijini** | 201 | 136 | 34 | 1,162 | 263 | 37 | 3,288 | 997 | 143 |
| **10. Equinor** | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **11. EACOP** | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **12. Maurel et Prom** | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **13. PanAfrican Energy Tanzania Ltd** | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **14. Songas** | - | - | - | - | - | - | - | - | - |

### 8.2.1. Ushiriki wa watanzania katika migodi (madini)

Ajira katika migodi zinaonyesha watanzania wameendelea kupewa kipaumbele kutokana na maboresho ya sekta ya madini. Katika kipindi cha mwaka 2018 ajira za watanzania katika migodi zilikuwa 6,623 ukilinganisha na ajira za wageni 140 ambao ni wataalam. Vilevile katika miaka ya 2019 and 2020 bado watanzania wameendelea kuongezeka na kufikia 7967 ukilinganisha na wataalam wa kigeni. Hii inaonyesha matakwa ya sheria ya madini na kanuni zake namna inavyozingatiwa katika kuongeza ushiriki wa watanzania kunufaika.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 jumla ya makampuni 100 yanayojishughulisha na uchimbaji wa mkubwa, wa kati na mdogo; utafutaji, uchenjuaji, na utoaji wa huduma waliwasilisha mipango ya ushiriki wa watanzania (Local Content Plans) kwa Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini ambapo makumpuni 57 yaliidhinishiwa mipango ya ushiriki wa watanzania.

**Mchoro Na. 17: Ajira za Migodi**




*Chanzo: Tume ya Madini (2020)*

Aidha**,** kanuni za ushiriki wa Watanzania (Kanuni ya 16 na 18) zinawataka wamiliki wa leseni za uchimbaji pamoja na wakandarasi kuitaarifu Serikali juu ya manunuzi yote yanayopangwa kufanyika ikiwa ni pamoja na mlolongo wote wa manunuzi kupata kibali cha Tume.

Kwa kipindi cha mwaka 2019/20 Tume imefanya kaguzi katika migodi mikubwa na migodi ya kati ili kujiridhisha na uzingatiaji wa utekelezaji wa Sheria na Kanuni katika eneo la ushiriki wa wazawa. Matokeo ya kaguzi hizo zilibainisha mapungufu mbalimbali yakiwemo:-

i. Ubadilishaji wa warithi wa nafasi zilizochukuliwa na wageni kinyume na Mpango wa ushirikishi wa watanzania
ii. Kutokuwa na mpango wa kuwarithisha watanzania katika baadhi ya nafasi.
iii. Wageni kukaa muda mrefu bila kuachia nafasi kwa Watanzania
iv. Wageni kufanyakazi au kutoa huduma kwa kada zinazotakiwa zifanywe na Watanzania kwa 100%.
v. Kuwepo utofauti mkubwa wa mishahara kati ya Watanzania na Wageni.
vi. Matumizi ya bidhaa na huduma za nje ya nchi.

vii. Kutokutumia huduma za Benki za Kitanzania.
viii. Kutokuwasilisha mpango wa ushiriki wa watanzania katika katika sekta ya madini kwa baadhi ya watoa huduma kwa wamiliki wa leseni za uchimbaji

Tume ya Madini ilibaini mapungufu ya kutozingatiwa utekelezaji wa Sheria ya Madini, Kanuni na Miongozo ya Ushiriki wa Watanzania katika sekta ya madini. Tume ilielekeza wamiliki wa leseni waliokaguliwa kufanyia kazi mapungufu na kuwasilisha maboresho ambayo yalifanyiwa uchambuzi na Tume ya Madini ili kuhakikisha yanakidhi matakwa ya sheria na kanuni za ushiriki wa Watanzania katika sekta ya madini.

### 11.3. ZABUNI/MANUNUZI

Masuala ya zabuni na manunuzi yameendelea kuzingatiwa katika miradi ya kimkakati na miradi mingine, ambapo imezingatia aina ya huduma na bidhaa zilizotolewa. Taarifa za watekelezaji zimeonyesha idadi ya makampuni yaliyoshiriki pamoja na idadi ya zabuni zilizotolewa kwa makampuni ya ndani na yale kutoka nje sanjari na thamani ya zabuni hizo kama jedwali hapo chini linavyofafanua zaidi.

**Jedwali Na. 23: Idadi ya makampuni yaliyoshiriki zabuni zilizotolewa kwa makampuni ya ndani na nje sanjari na thamani ya zabuni**

| Miradi | Aina ya Kazi, Bidhaa zilizonunuliwa na Huduma zilizotolewa | Idadi ya Kampuni | Idadi ya kampuni zilizouza bidhaa, kutoa huduma/ kupata kazi za ujenzi | | Thamani ya Zabuni/ Manunuzi (TZS au USD) | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Watanzania | Wageni | Ndani ya Nchi | Nje ya Nchi |
| **1. Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP)** | Kandarasi za ujenzi kwa makandarasi wa ndani, Kokoto, Mchanga, Sementi, Nondo, Huduma za chakula, Huduma za Ulinzi | 102 | 75 | 27 | - | - |
| **2. Mradi wa Reli ya Kisasa - SGR (Lot 1 & 2)** | Kumlipa mshauri ekelezi kumsimamia mkandarasi (Dar-Moro) na Moro-Makutupora, usimamizi na tathmini | 6 | 1 | 5 | 504,615,000 | 392,782,089,800 |
| **3. Mradi wa Ubungo Interchange** | *Simenti, Nondo, Lami, Vifaa Mafuta, Mawe, Huduma ya chakula, usafi n.k* | 6 | 1 | 5 | TZS 2,089,770,747 | TZS 15,581,745,251 |
| **4. New Salender Bridge** | Mchanga, Udongo,Kokoto | 3 | 3 | 0 | TZS 235,000,000 | Haikuonyeshwa |
| **5. JNIA TB III** | Huduma za matengenezo, usafi na ulinzi, Upangishaji wa maduka,ofisi za utalii, | 34 | 34 | 0 | TZS 7,089,893,970 | - |

| Miradi | Aina ya Kazi, Bidhaa zilizonunuliwa na Huduma zilizotolewa | Idadi ya Kampuni | Idadi ya kampuni zilizouza bidhaa, kutoa huduma/ kupata kazi za ujenzi | | Thamani ya Zabuni/ Manunuzi (TZS au USD) | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Watanzania | Wageni | Ndani ya Nchi | Nje ya Nchi |
| | mabenki n.k. | | | | | |
| ***6. Ujenzi wa Barabara Kiwango cha Lami*** | | | | | | |
| **6.1 Urambo - Kaliua** | Lami, Sementi, Mbao, Bati, Nondo na Tofali | 3 | 2 | 1 | TZS 15,000,000,000 | TZ 3,000,000,000 |
| **6.2 Nyahua-Chaya** | Sementi, Lami, Mchanga na Lami | 3 | 3 | 0 | - | - |
| **6.3 Mbinga-Mbamba Bay** | Dizeli, Sementi, Nondo, Lami, Mchanga, Mafuta ya Mitambo (Lubricating Oil) | 4 | 3 | 1 | TZS 4,240,021,000 | TZS 2,100,445,100 |
| **7. Miradi ya Nishati Vijijini** | Usambazaji Umeme Vijijini, Ujazilizi (densification), Nguzo, vifaa na mitambo ya umeme | 64 | 36 | 28 | TZS 1,141,457,000,000 | Haikuonyeshwa |
| ***8. Miradi ya Maji*** | | | | | | |
| **8.1 Mradi wa Maji (Ziwa Victoria kwenda Miji ya Tabora, Igunga na Nzega)** | Huduma za ulinzi katika maeneo ya kuhifadhia vifaa vya ujenzi vya wakandarasi, Ushauri elekezi wa mradi | 10 | 6 | 4 | Haikuonyeshwa | USD 268.35 |
| **8.2 Mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoaji wa majitaka katika jiji la Arusha** | Huduma ya utaalam ushauri, kazi zinazohusiana na ujenzi | 15 | 3 | 12 | USD 14,824,000 | USD 193,042,000 |
| **8.3 Mradi wa Bulongwe na Lufumbi (Masoko Gravity Main)** | Bomba, viungio bomba na vifaa vya ujenzi | 4 | 4 | 0 | TZS 150,000,000 | - |
| **8.4 Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Majisafi (Km 55.755) kutoka Kijiji cha Mhangu hadi kijiji cha Ilogi Halmashauri ya wilaya ya Msalala** | Msamaha wa kodi la ongezeko la thamani (VAT exemption) | 1 | 0 | 1 | TZS 13,860,873,200.77 | - |
| **8.5 Miradi ya Upanuzi Wa Mitandao ya Maji kwa Vijiji 100** | Huduma ya ujenzi wa Mradi wa Maji kwa vijiji | | | | TZS | - |


| Miradi | Aina ya Kazi, Bidhaa zilizonunuliwa na Huduma zilizotolewa | Idadi ya Kampuni | Idadi ya kampuni zilizouza bidhaa, kutoa huduma/ kupata kazi za ujenzi | | Thamani ya Zabuni/ Manunuzi (TZS au USD) | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Watanzania | Wageni | Ndani ya Nchi | Nje ya Nchi |
| **vinavyopitiwa na Bomba Kuu kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama/ Shinyanga** | | 6 | 6 | 0 | 11,000,034,905 | |
| **8.6 Mradi wa Maji wa Same-Mwanga-Korogwe** | Ujenzi wa usimamizi wa miradi, ufungaji wa mabomba | 8 | 4 | 4 | - | TZS 3,832,271,455 |
| **9. Equinor** | Bima, Maji na Chakula, Upangaji nyumba, Huduma za *Intaneti*, Mafuta, Huduma za Intaneti, Kufadhili masomo | 41 | 36 | 5 | USD 17,870,292.9 | USD 364,000 |
| **10. TPDC** | Utafiti wa Mafuta na Gesi Miradi ya kuunganisha Bomba kuu la Gesi na Bomba la Ubungo na kupeleka viwandani na kuunganisha nyumba 140 na taasisi 4 za Dar es Salaam, Nyumba 125 na Taasisi 4 mkoani Mtwara, Kadi za mafuta za PUMA n.k | 20 | 18 | 2 | TZS 4,992,647,088 | $ 2,508,750,862 |
| **11. PanAfrican Energy** | - | - | - | - | $ 1,353,030 | $ 477,873 |
| **12. Songas** | - | - | - | - | - | $ 738,244 |
| **13. Sekta ya Bima** | | 358 | 304 | 54 | 4,848,249,566 | 368,331,422 |

*Chanzo: Taarifa ya Ushiriki wa Watanzania, NEEC (2020)*

Thamani ya manunuzi yanayohusiana na utoaji wa huduma na bidhaa yameonekana kuwa maeneo ambayo yalitoa fursa kwa watanzania kupitia makampuni ya ndani. Michoro hapa chini inaonyesha thamani ya huduma na thamani za bidhaa zilizotumika katika migodi na hatimaye kuwezesha thamani ya ziada inayotokana na ushiriki wa watanzania kubaki nchini. Aidha katika mwaka 2019/20 huduma nyingine kama vile kazi zinazohusiana na ujenzi, ushauri wa kitaalam, huduma ya chakula, ulinzi zimeonekana kuwa na thamani kubwa ukilinganisha huduma nyingine zilizotolewa. Sambamba na hilo, pia thamani ya bidhaa kwa mwaka 2019/2020 inaonekana kuwezesha zaidi ushiriki wa wafanyabiashara wa ndani ukilinganisha na bidhaa zilizotolewa nje. Hii inatokana na maboresho yanayoendelea kufanyika katika sekta ya madini hususani uanzishwaji wa masoko ya madini nchini n.k.

Aidha, utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoaji wa majitaka katika jiji la Arusha unaonyesha ubia kati ya Kampuni ya DOCH Ltd ambayo ni kampuni ya kitanzania  na Cheil Engineering pamoja na KECC ambazo ni za kigeni. Mkataba huu una thamani ya Dola za Marekani milioni 12.104. Aidha, Muungano wa makampuni matatu ya kitanzania ya BQ Contractors Ltd, M/s Caberisa Co. Ltd na Shreeji Construction Co. Ltd ambayo ni wakanadarasi wenye mkataba wa thamani ya Dola za Marekani 668,880.83. Ushirikiano unaboresha na kuleta uzoefu kwa kampuni za kitanzania.

**Mchoro Na. 18: Thamani ya Huduma/Bidhaa za ndani na nje kwa mwaka 2019/machi,2020**





*Chanzo: Taarifa ya Ushiriki wa Watanzania, NEEC (2010)*

### 11.4. USAJILI MAKANDARASI NA THAMANI YA MIRADI

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na kipindi cha Oktoba, 2015 hadi Machi, 2020, Serikali iliendelea kutekeleza dhana ya ushiriki wa watanzania katika miradi ya kimkakati na uwekezaji mwingine ambapo imeshuhudiwa kuwa katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Juni, 2020 jumla ya makampuni ya makandarasi 767 yalisajiliwa ambapo makampuni ya kigeni yalikuwa 6 na ya kitanzania yalikuwa 761.  Aidha, katika kipindi cha Oktoba, 2020 hadi Machi, 2020, Bodi ya Usajili Makandarasi ilisajili jumla ya makandarasi 3,387 ambapo wageni walikuwa ni  54 na ya ndani yalikuwa ni 3,387 kama michoro invyoonyesha hapa chini:-

**Mchoro Na. 19:Usajili wa Makandarasi wa Ndani na Wageni**




***Chanzo:*** *CRB, 2020*

Vilevile, katika kipindi cha 2015/16 -2019/2020, jumla ya idadi ya miradi 18,015 ilisajiliwa ambapo inaonyesha makandarasi wa ndani walikuwa ni 95.9% na makandarasi wageni walikuwa ni 4.1%. Jumla ya thamani ya miradi yote ilikuwa ni Shilingi za Kitanzania 30,464,000,000 ambapo thamani ya 50.4 ilikwenda kwa makandarasi wa ndani na makandarasi wa wageni walipata 49.6. Hii inaonyesha kuwa makandarasi wa nje ambayo ni machache yalipata thamani kubwa ukilinganisha na makandarasi wa ndani hivyo kuna umuhimu wa kuhakikisha mikakati inawekwa ili kuhakikisha thamani kubwa inakwenda kwa makampuni ya ndani na kuhakikisha uhawilishaji wa teknolojia unafanyika ili makampuni ya kitanzania yaweze kuwa na ushiriki mkubwa katika miradi inayohitaji zaidi uzoefu kutoka nje. Jedwali hapa chini unaonyesha namna miradi na thamani kuanzia kipindi cha 2015/16 hadi kufikia 2019/2020.

**Jedwali Na. 24: Miradi iliyosajiliwa kwa kipindi cha 2015/16 – 2019/2020**

| Mwaka | Idadi ya Miradi | Idadi (%) | | Thamani (TZS Bn) | Thamani (%) | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ndani | Wageni | | Ndani | Wageni |
| **2015/16** | 5,025 | 94.6 | 5.4 | 6,735 | 43 | 57 |
| **2016/17** | 3,619 | 96.2 | 3.8 | 6,655 | 32.2 | 67.8 |
| **2017/18** | 3,334 | 96.0 | 4.0 | 9,469 | 20.02 | 79.08 |
| **2018/19** | 3,470 | 96.1 | 3.9 | 5,316 | 44.7 | 55.3 |
| **2019/20** | 2,567 | 96.4 | 4.0 | 2,289 | 50.4 | 49.6 |

***Chanzo:*** *Bodi ya Usajili Makandarasi - CRB, (2020)*


### 11.5. HUDUMA ZA USHAURI WA KITAALAM (UHANDISI)

Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) imeendelea kuratibu ushiriki wa wahandisi wa ndani kushiriki ipasavyo katika miradi ya kimkakati na uwekezaji. Taarifa ya ERB ya mwaka 2019/20 ya ushiriki wa watanzania inaonyesha wahandisi wameshiriki vyema katika miradi

mbalimbali ikiwa ni pamoja na Tazara Flyover, Julius Nyerere International Airport Terminal III, Kinyerezi II, Gas Fired Power Plant, Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR – Lot I & II), Upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria kwenda Tabora, Nzega na Igunga, Ubungo Interchange, Ujenzi Mpya wa Daraja la Wami, Daraja la Tanzanite, Mradi wa Kufua Umeme wa Rusumo, Upanuzi wa barabara ya Mwenge (km 4.3), Uboreshaji barabara kwa kiwango cha lami (Tabora – Koga – Mpanda) yenye urefu wa km342.9 na Mradi wa Kufua Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP).

Aidha, katika miradi 13 iliyoainishwa na ERB inaonyesha kampuni za ushauri wa kitaalam (uhandisi) kutoka nje zimeshiriki kwa 92% ukilinganisha na kampuni za ushauri wa kitaalam za ndani ambapo kupitia TECU ushiriki umekuwa ni 8% na hii inatokana na ushiriki wa TECU katika mradi wa kufua Umeme (JNHPP). Aidha, ubia wa kampuni za ndani na nje umetekelezwa katika miradi 2 ambayo ni Ubungo Interchange na Ujenzi wa Reli ya Kisasa. Taarifa za miradi ya EACOP, Kampuni ya Sukari ya Kagera, Nyumbu TATC-Kibaha na TANCOAL Energy Ltd (Coal Plant – Ngaka, Mbinga) hazikuonyeshwa.

**Mchoro Na. 20:Usajili wa Makandarasi wa Ndani na Wageni**




*Chanzo: Taarifa ya Ushiriki wa Watanzania, NEEC (2010)*

Thamani za ushauri wa kitaalam zilizotumika katika miradi 13 ziligharimu jumla ya USD bilioni 340.5, EUR 276,779,293 na TZS trilioni 7.3. Aidha Wahandisi wanafunzi na Wahandisi wataalam (140), Wahandisi wataalam wa muda mfupi (326), Wahandisi washauri (0), Wahandisi washauri wa muda mfupi(6) na uanagenzi (140).

### 11.6. IDADI YA ZABUNI NA THAMANI YA MIRADI YA BARABARA


Dhana ya Ushiriki wa Watanzania katika miradi ya ujenzi wa barabara imeendelea kutekelezwa chini ya usimamizi wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS). Taarifa ya TANROADS inaonyesha aina za manunuzi kwa kuzingatia kazi zinazohusiana na majenzi (works), bidhaa (Goods), kazi za kitaalam na ushauri (Consultancy Services) pamoja na huduma zisizo za

kitaalam na ushauri (Non Consultancy Services). Jumla ya zabuni 55 zenye thamani inayokadiriwa trilioni 2.3 zilitolewa ambapo idadi ya zabuni 29 zenye thamani ya zaidi bilioni 855 zilitolewa kwa kampuni za kitanzania na thamani ya zaidi ya TZS trilioni 1.47 zilitolewa kwa makampuni ya nje kama jedwali linavyoonyesha hapa chini. Mnyumbulisho unaonyesha kuwa 65% ya zabuni ilikuwa ikuhusiana na kaza za ujenzi ikifuatiwa na 34.6% ambazo zilitolewa kwenye kazi za ushauri wa kitaalam kama mchoro unavyoonyesha hapa chini.

**Jedwali Na. 25: Mnyumbulisho wa zabuni mbalimbali**

| | Aina ya Manunuzi | Idadi ya Zabuni | | Thamani (Tshs) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ndani | Nje | Ndani | Nje | |
| | Kazi zinazohusiana na Ujenzi | 2 | 12 | 53,546,319,859 | 1,086,104,885,347 | |
| | Bidhaa *(Goods)* | 17 | 2 | 3,942,841,125 | 1,187,020,233 | |
| | Kazi za Kitaalam na Ushauri *(Consultancy Services)* | 8 | 1 | 797,667,941,987 | 14,686,988,344 | |
| | Huduma zisizo za kitaalam na ushauri (Non Consultancy Services) | 2 | 1 | 531,586,691 | 129,456,875 | |
| | **Jumla** | | | **855,688,689,662** | **1,102,108,350,799** | |

**Mchoro Na. 21: Mnyumbulisho wa zabuni za kazi za ujenzi ikifuatiwa na ushauri wa kitaalam**




*Chanzo: Taarifa ya Local Content, NEEC (2020)*

### 11.7. MAFUNZO, UJUZI NA TEKNOLOJIA

Utekelezaji wa mpango wa Mafunzo, urithishaji wa ujuzi na uhawilishaji wa teknolojia ulifanyika katika miradi ya kimkakati, uwekezaji na ile miradi ya kawaida. Mafunzo yaliyotolewa yalilenga kujenga uwezo wa watanzania na yalikuwa ya muda mrefu na mfupi kulingana na mahitaji ya kampuni husika. Mafunzo na uhawilishaji wa teknolojia yalizingatia watanzania wenye ujuzi wa juu, ujuzi wa kati na wasio na ujuzi. Jedwali la Mafunzo na Uhawilishaji wa teknolojia hapa chini yanaonyesha namna dhana ya *Local Content* ilivyotekelezwa hapa nchini.

### 11.7.1. Mafunzo

**Jedwali Na. 26: Mafunzo yaliyotolewa kwa Watanzania katika miradi mbalimbali**

| MRADI | Wafanyakazi wa Kitanzania Waliopatiwa Mafunzo | | | Aina ya mafunzo | Muda wa mafunzo |
|---|---|---|---|---|---|
| | Ujuzi wa Juu | Ujuzi wa Kati | Wasio na Ujuzi | | |
| 1. Mradi wa Kufua Umeme (JNHPP) | 10 | 20 | - | kozi za kitaalam katika nchi zinazotengeneza vifaa vya *Electro – Mechanical* na uunganishaji vipuri na Mitambo, Ukaguzi wa mitambo, Elimu ya Bima | Miezi 2, |
| 2. Mradi wa Reli ya Kisasa –SGR (Lot 1&2) | - | - | - | - | Taarifa haikuonyesha |
| 3. TIRP | - | - | - | - | Taarifa haikuonyesha |
| 4. Mradi wa Ubungo Interchange | 7 | 1 | 0 | Elimu ya Ukimwi (HIV/AIDS), Mashule, Masoko, Watoa huduma, wafanyabiashara Kiufundi/usanifu | Masaa 9<br>Miaka 2 |
| 5. New Salender Bridge | 34 | 135 | 80 | Elimu ya Ukimwi (HIV/AIDS) | Masaa 3 |
| 6. JNIA TB III | 209 | 112 | 4 | Maadili na uaminifu, Huduma za usafiri wa anga na nchi kavu, uongozi na usimamizi, Matengenezo na ukarabati wa vifaa | Muda mfupi na mrefu |
| ***7. Ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha Lami*** | | | | | |
| 7.1 Urambo Kaliua | 26 | 0 | 0 | Ujengaji Uwezo | Miaka 2 |
| 7.2 Nyahua-Chaya | 9 | 32 | 27 | Zima moto; Mafunzo Mahali pa kazi (OSHA) | Masaa 3; siku 3 (OSHA) |
| 7.3 Mbinga-Mbamba Bay | 0 | 22 | 115 | Elimu ya Afya, Majanga ya moto na uokoaji, Huduma ya Kwanza | **Siku 3** |
| ***8. Miradi ya Maji*** | | | | | |
| 8.1 Mradi Ziwa Victoria kwenda Miji ya Tabora, Nzega hadi Igunga | 241 | 608 | 2,014 | Usimamizi wa uendeshaji miradi, mafunzo ya kiutumishi, mafunzo kwa jamii namna ya kutunza miundombinu ya mradi | - |
| 8.2. Mradi wa Ujenzi Miundombinu ya usamabazaji majisafi na uboreshaji huduma ya uondoaji wa majitaka jiji la Arusha | 152 | 422 | 1,202 | Ujenzi wa miundombinu ya usamabazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoaji wa majitaka | - |
| 8.5 Mradi wa Bulongwe na Lufumbi (Masoko Gravity Main) | 5 | 20 | 200 | Uunganishaji mabomba na ujuzi wa kutumia *water proof cement* , elimu ya kujikinga na VVU na namna salama ya | Muda mfupi |

| MRADI | Wafanyakazi wa Kitanzania Waliopatiwa Mafunzo | | | Aina ya mafunzo | Muda wa mafunzo |
|---|---|---|---|---|---|
| | Ujuzi wa Juu | Ujuzi wa Kati | Wasio na Ujuzi | | |
| | | | | kuishi na VVU | |
| 8.6 Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Majisafi (km 55.755) kutoka Kijiji cha Mhangu hadi kijiji Ilogi - Halmashauri ya wilaya ya Msalala | 6 | 46 | 35 | Uhakiki ubora wa mabomba yaliyolazwa *(hydrostatic pressure testing skills)* | - |
| 8.7 Miradi ya Upanuzi wa Mitandao ya Maji kwa vijiji 100 vinavyopitiwa na Bomba Kuu kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama, Shinyanga | 30 | 69 | 910 | Ujenzi na usimamizi miradi ya maji, uhakiki ubora wa mabomba | Muda mfupi na mrefu |
| 8.9 Mradi wa Maji wa Same-Mwanga-Korogwe | 39 | 157 | 178 | Usimamizi wa mikataba, ufungaji wa mabomba | Muda mfupi na Mrefu |
| 9. Miradi ya Nishati vijijini | 275 | 1162 | 638 | Umeme wa upepo, jua na maporoko madogo ya maji, tungamotaka, Mkaa (*Briquette)*, Majiko Bora, *Gender*, Nishati bora, na Mpango biashara | - |
| 10. Equinor | 14 | 0 | 0 | Usimamizi wa Miradi ya Kimataifa (Norway), Uongozi, Utawala wa Biashara, Usimamizi na Uchambuzi, Usimamizi wa Ulinzi, Usimamizi wa Rasilimali, | Muda mfupi na muda mrefu |
| 11. PanAfrican Energy | 5 | 16 | - | - | - |
| 12. Sekta ya Bima | - | 1030 | - | Kodi, utawala bora, madai na mafao ya bima, mawasiliano, utawala, utoaji wa taarifa, bima za maji, uwekezaji, bima za wanawake na benki, bima ya maisha, bima ya matibabu, bima ya masoko, bima ya kilimo, uhandisi wa bima n.k. | |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Utekelezaji wa Ushiriki wa Watanzania, NEEC (2020)*

Aidha, mafunzo yaliyotolewa kwa watanzania yalizingatia nguvukazi ya umri ambapo vijana wameendelea kunufaika na fursa za mafunzo ukilinganisha makundi mengine ya umri. Taarifa za miradi ya JNHPP, SGR, Songas na miradi mikubwa ya migodi ya madini hazijaonyesha taarifa za mafunzo kwa kuzingatia makundi kama yanavyoonekana katika jedwali hapa chini.

**Jedwali Na. 27: Mafunzo yaliyotolewa kwa Watanzania kwa kuzingatia umri katika miradi mbalimbali**

| Mradi | Wenye Ujuzi | | | Wenye Ujuzi wa Kati | | | Wasio na Ujuzi | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 20-35 | 35-45 | > 45 | 20-35 | 35-45 | >45 | 20-35 | 35-45 | > 45 |
| **Mradi wa Kufua Umeme (JNHPP)** | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Mradi wa Reli ya Kisasa – SGR (Lot 1&2)** | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Mradi wa TIRP** | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Mradi wa *Ubungo Interchange*** | 18 | 3 | 1 | 585 | 20 | - | 178 | 15 | - |
| **Mradi wa *New Salender Bridge*** | 32 | 1 | 1 | 127 | 10 | 6 | 80 | 0 | 0 |
| **Julius Nyrere International Airport III** | 87 | 61 | 14 | 77 | 26 | 10 | 32 | 15 | 3 |
| ***Ujenzi wa Barabara – Kiwango cha Lami*** | | | | | | | | | |
| **Urambo – Kaliua** | 4 | 15 | 7 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Nyahua-Chaya** | 6 | 0 | 0 | 16 | 9 | 3 | 2 | 0 | 0 |
| **Mbinga-Mbamba Bay** | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 | 2 | 32 | 4 | 0 |
| ***Ujenzi wa Miradi ya Maji*** | | | | | | | | | |
| **Ziwa Victoria-Tabora-Nzega na Igunga** | 143 | 68 | 30 | 477 | 88 | 43 | 1309 | 549 | 156 |
| **Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoaji majitaka jiji la Arusha** | 111 | 70 | 16 | 324 | 103 | 55 | 906 | 261 | 35 |
| **Mradi wa Bulongwe na Lufumbi (Masoko Gravity Main)** | 2 | 2 | 1 | 12 | 6 | 2 | 102 | 67 | 31 |
| **Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Majisafi (km 55.755) kutoka Kijiji cha Mhangu hadi kijiji Ilogi - Halmashauri ya wilaya ya Msalala** | 3 | 2 | 1 | 27 | 14 | 5 | 19 | 11 | 5 |
| **Miradi ya Upanuzi wa Mitandao ya Maji kwa vijiji 100 vinavyopitiwa na Bomba Kuu kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama, Shinyanga** | 16 | 11 | 4 | 32 | 21 | 16 | 546 | 227 | 137 |
| **8.6 Mradi wa Maji wa** | 23 | 10 | 6 | 94 | 39 | 24 | 178 | 45 | 26 |

| Mradi | Wenye Ujuzi | | | Wenye Ujuzi wa Kati | | | Wasio na Ujuzi | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 20-35 | 35-45 | > 45 | 20-35 | 35-45 | >45 | 20-35 | 35-45 | > 45 |
| **Same-Mwanga-Korogwe** | | | | | | | | | |
| **Equinor** | 10 | 4 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **PanAfrican Energy** | - | 2 | 1 | 10 | 7 | 2 | - | - | - |
| **Songas** | - | - | - | - | - | - | - | - | - |
| **Maurel et Prom** | 2 | 3 | - | - | - | - | - | - | - |
| **Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi (EACOP)** | - | - | - | - | - | - | - | - | - |

### 11.7.2. Ujuzi na Uhaulishaji wa Teknolojia

Ujuzi na uhaulishaji wa teknolojia umeendelea kufanyika katika miradi ya kimkakati na uwekezaji inayotekelezwa hapa nchini. Uhaulishaji wa teknolojia unazingatiwa katika miradi mbalimbali hata ile ambayo sio ya kimkakati. Taarifa ya ushiriki wa watanzania iliyowasilishwa na EWURA mathalani inaonyesha kampuni ya PanAfrican Energy mwezi Februari, 2020 ilimteua Mtanzania kuwa Naibu Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo ambaye hapo awali alikuwa ni Meneja wa Biashara ndani ya kampuni. Tangu PanAfrican Energy kuanza shughuli zake hapa nchini, nafasi hiyo haikuwepo na imeundwa ili kukidhi matakwa ya Kanuni za Ushiriki wa Watanzania katika sekta ya Mafuta ambapo asilimia kumi na tano (15%) katika ngazi ya menejimenti inapaswa kushikiliwa na wazawa. Vilevile, mwezi Februari 2020 kampuni ya Songas ilimteua Mtanzania, kuwa Mtendaji Mkuu wa Kampuni hiyo kama sehemu ya urithishaji wa ujuzi. Awali nafasi hiyo ilikuwa inashikiliwa na mgeni (expartriate). Haya ni mafanikio na matakwa ya miongozo ya utekelezaji wa dhana ya *local content* hapa nchini.

Sambamba na hayo, miradi mingine nayo imeendelea kuzingatia utekelezaji wa mpango wa ujuzi na uhaulishaji wa teknolojia kwa lengo la kuwezesha watanzania kushiriki na kunufaika kama jedwali hapa chini lilivyofafanua kwa kina zaidi.

**Jedwali Na. 28: Ujuzi na Uhaulishaji wa Teknolojia**

| Mradi | Aina ya Teknolojia | Muda wa uhaulishaji | Idadi ya Watanzania wanufaika | Gharama ya Uhawilishaji |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mradi wa Kufua Umeme (JNHPP) | Ujenzi wa Bwawa la kufua Umeme, uendeshaji na usimamizi wa Mitambo | Miezi 42 | 30 | - |
| 2. Mradi wa Reli ya Kisasa – SGR (Lot 1 & 2) | Ujenzi wa Reli ya Kisasa (majengo, majenzi, umeme, Uwekaji taaluma za reli, utumiaji mitambo, madaraja ya chini na juu, n.k) | - | - | - |
| 3. Mradi wa TIRP | Uboreshaji wa Reli ya zamani | - | - | - |
| 4. Mradi wa *Ubungo* | Ujenzi wa Barabara za juu | Miaka 2 | 8 | TZS 54,000,0000 |

| Mradi | Aina ya Teknolojia | Muda wa uhaulishaji | Idadi ya Watanzania wanufaika | Gharama ya Uhawilishaji |
|---|---|---|---|---|
| *Interchange* | | | | |
| 5. Mradi wa *New Salender Bridge* | Kujenga daraja juu ya bahari | Miezi 6 | 5 | TZS 1,625,000 |
| 6. Mradi wa JNIA TB III | Uendeshaji wa shughuli za Uwanja wa Ndege, Uongozaji abiria na mizigo | Muda mfupi na mrefu | 166 | TZS 221,200,000 |
| ***7. Miradi ya Ujenzi wa Barabara Kiwango cha Lami*** | | | | |
| 7.1 Urambo – Kaliua | Ujenzi barabara ya lami | Miaka 2 | 26 | 100,000,000 |
| 7.2 Nyahua-Chaya | Ujenzi barabara ya lami | Siku 3 | 68 | 60,000,000 |
| 7.3.Mbinga-Mbamba Bay | Ujenzi wa barabara ya lami | Siku 3 | 137 | - |
| 8. Miradi ya Nishati vijijini | Umeme wa upepo, jua na maporoko madogo ya maji, tungamotaka, Mkaa (*Briquette*), *Majiko Bora*, *Gender*, *Energy Efficient, na Mpango biashara* | Muda mfupi na mrefu | 2075 | Haikuonyeshwa |
| ***9. Miradi ya Maji*** | | | | |
| 8.1 Ziwa Victoria, miji ya Tabora, Nzega hadi Igunga | Ujenzi wa miradi ya maji | Muda mfupi na mrefu | 2,255 | Haikuonyeshwa |
| 8.2 Ujenzi miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoaji wa majitaka jiji la Arusha | Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji wa majisafi na uboreshaji wa huduma ya uondoaji wa majitaka jiji la Arusha | Muda mfupi na Mrefu | 280 | Haikuonyeshwa |
| 8.3 Mradi wa Bulongwe na Lufumbi (Masoko Gravity Main) | Ujenzi wa mabomba ya maji | Muda mfupi | 225 | Haikuonyeshwa |
| 8.4 Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Majisafi (KM 55.755) kutoka Kijiji cha Mhangu hadi kijiji Ilogi - Halmashauri ya wilaya ya Msalala | Uhakiki ubora wa mabomba yaliyolazwa *(Hydrostatic Pressure Testing Skills)* | Muda mfupi na mrefu | 87 | Haikuonyeshwa |
| 8.6 Miradi ya Upanuzi wa Mitandao ya Maji kwa vijiji 100 vinavyopitiwa na Bomba Kuu kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama, Shinyanga | Ufungaji wa mabomba, usimamizi wa mikataba | Muda mfupi na mrefu | 1,009 | Haikuonyeshwa |

| Mradi | Aina ya Teknolojia | Muda wa uhaulishaji | Idadi ya Watanzania wanufaika | Gharama ya Uhawilishaji |
|---|---|---|---|---|
| 8.7 Mradi wa Maji wa Same-Mwanga-Korogwe | | Muda mfupi na mrefu | 358 | Haikuonyeshwa |
| 9. Equinor | Mafuta na Gesi | - | 27 | USD 718,684 |
| 10. Shell | Uhawilishaji wa tekinolojia | - | 300 | - |
| 11. PanAfrican Energy | Mafuta na gesi | Muda mfupi na mrefu | 21 | USD 170,265 |
| 12. Songas | Mafuta na gesi | Muda mfupi na mrefu | 51 | USD 263,000 |
| 13. Maurel et Prom | Mafuta na gesi | Muda mfupi na mrefu | 5 | USD 207,751 |
| 14. Migodi ya Madini | Uchimbaji na uchakataji wa uongezaji thamani madini | Muda mfupi na mrefu | - | - |
| 15. Sekta ya Bima | Uongozi madai ya bima na kusimamia vihatarishi | Muda mrefu | 44 | - |

## 11.8. PROGRAMU ZA HUDUMA KWA JAMII

Dhana ya uwajibikaji kwa jamii (CSR) imeendelea kuzingatia na kutekelezwa na makampuni ya uwekezaji, wamiliki wa leseni, wakandarasi wakubwa na watoa huduma mbalimbali ambapo jamii zinazozunguka maeneo ya uwekezaji zimeendelea kunufaika na fursa za huduma za kijamii pamoja na maeneo ambayo Serikali iliona kuna mahitaji muhimu ya kuboresha miradi mbalimbali ya huduma za kijamii. Miradi iliyolengwa pamoja na mambo mengine imewezesha huduma za kijamii kuimarika katika sekta za afya, maji, elimu, utawala bora, n.k.

Aidha, wawekezaji, wakandarasi, watoa huduma na wamiliki wa leseni katika miradi ya kimkakati inayotekelezwa hapa nchini wameendelea kuzingatia dhana ya ushiriki wa watanzania kupitia programu za huduma kwa jamii. Mambo mbalimbali yamefanyika kwa kuzingatia mahitaji ya walengwa na matakwa ya nchi. Aina za huduma zilizotolewa kwa jamii ni pamoja na ujenzi wa viwanja vya michezo, ujenzi wa barabara, zahanati, shule, n.k. Majumuisho ya taarifa ya *Local Content* yanaonyesha uwajibikaji umeendelea kwa jamii (CSR) umeendelea kuzingatiwa na kufuatiliwa ili kubaini faida na changamoto za utekelezaji.

**Jedwali Na. 29: Programu za huduma kwa jamii zilizotekelezwa na Miradi mbalimbali ya kimkakati**

| Mradi | Aina ya Huduma iliyotolewa kwa Jamii | Wilaya, Kata, Mtaa au Kijiji kilichonufaika | Walengwa | Thamani ya Huduma iliyotolewa (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| **1. Mradi wa Kufua Umeme (JNHPP)** | Ujenzi wa Uwanja wa Kituo cha michezo Dodoma, Ujenzi wa barabara ya lami | Dodoma, Fuga na Matambwe | Dodoma, Wanavijiji wa Fuga, Matambwe, TANESCO, na watanzania kwa ujumla | Kifungu cha mkataba kinaelekeza ushiriki wa Jamii |

| Mradi | Aina ya Huduma iliyotolewa kwa Jamii | Wilaya, Kata, Mtaa au Kijiji kilichonufaika | Walengwa | Thamani ya Huduma iliyotolewa (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| | kutoka Fuga hadi eneo la Mradi (35 km), Barabara kwa kiwango cha lami kutoka Matambwe hadi Njia panda ya Fuga (5km) | | | umetengewa 3% ya mkataba (Total Price of the Contact)<br><br>196,750,000,000 |
| **2. Mradi wa Reli ya Kisasa – SGR (Lot 1 & 2)** | Kukarabati kiwanja cha mpira, kununua mashine ya kutolea nakala, kubeba taka hadi dampo, magari 21 ya mchanga, ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu, Magari 90 ya kifusi, mtambo wa kujengea maji kwa ajili ya ukarabatti wa barabara, mifuko 200 ya saruji, Gari la mbao kwa ajili ya kuni, matairi kwa ajili ya usalama, kunyonya lita 30,000 za maji taka, Nguo 65 kwa ajili ya wazee 68 na watu wasiojiweza, chakula, | Shule ya msingi Msuguli, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Kilosa, Halmashauri wilaya ya Kilosa, Shule ya Msingi Kichangani, Kijiji cha Gulwe, Kijiji cha Mkadage, Msikiti wa Mlima Kilosa Lukobe, Kijiji cha Kimambila, Tabora mjini, Shule ya msingi Kondoa, Shule ya msingi Mazinyungu na Kilosa | Wanafunzi, walimu, wananchi, waumini wa kiislam, shule, wafungwa na maofisa magereza wa gereza la Kilosa. | - |
| **3. Mradi wa TIRP** | Ajira za upendeleo kwa wanavijiji | - | - | - |
| **4. Mradi wa Ubungo *Interchange*** | Elimu kuhusu Mradi, Elimu ya Ukimwi (HIV/AIDS) | Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo; NHC; Kibo; UDSM; Kibangu; na Sinza C | Wafanyakazi wa mradi Wananchi, Masoko, Shule, Wafanyabiashara, wajasiriamali wadogo | 54,000,000 |
| **5. Mradi wa *New Salender Bridge*** | Elimu ya kujikinga na maambukuzi ya VVU | Halmashauri za Manispaa na Kinondoni | Wafanyakazi wa Mradi, Wananchi wa watanzania na raia wa kigenii | - |
| **6. Mradi wa JNIA TB III** | - | - | - | - |
| ***7. Miradi ya Ujenzi*** | | | | |

| Mradi | Aina ya Huduma iliyotolewa kwa Jamii | Wilaya, Kata, Mtaa au Kijiji kilichonufaika | Walengwa | Thamani ya Huduma iliyotolewa (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| ***wa Barabara Kiwango cha Lami*** | | | | |
| **7.1 Barabara Urambo-Kaliua** | Uchimbaji wa Mabwawa, Uchongaji barabara, utoaji wa bidhaa (sementi, mabati, kokoto), ajira kwa vijana | Nsenda-Urambo; Ushokola-Kaliua; Michikichini-Urambo motomoto, Vumilia-Urambo na Kaliua Mjini | Mashule; Mahospitali; Misikiti; na Jamii kwa Ujumla | 100,000,000 |
| **7.2 Barabara Nyahua-Chaya** | Vifaa vya Ujenzi (Mchanga; kokoto; mawe; nondo; simenti; misumari; vumbi la kuosha na Mbao), Vifaa vya Elimu (Vitabu, Kalamu, mipira, n.k.) | Wilaya ya Uyui, kata ya Tura, Kata ya Kizengi, Kijiji cha Mpumbuli na Karangasi | Wanakijiji, Ofisi za Serikali, Wanafunzi na Msikiti, wanafunzi, Ofisi za Serikali | TZS 60,000,000 |
| **7.3 Barabara Mbinga-Mbamba Bay** | Ujenzi wa shule za Sekondari, Ujenzi wa zahanati, Vifaa vya shule (Vitabu, kalamu, chaki na mabegi ya shule, Ukarabati wa vyanzo vya maji Ndengu | Halmashauri ya Wilaya za Nyasa, Mbinga (Mitawa, Kijiji cha Mpera) na Mbinga Mji | Shule, Jamii na wakazi wamji wa mbinga | 8,480,000 |
| **8. Miradi ya Nishati Vijijini (REA)** | Elimu Bora ya Matumizi ya Nishati ya Umeme | Mikoa, Wilaya, Kata, vijiji vya Tanzania Bara | Taasisi za elimu (3291), biashara (5,279), Pump za Maji (347), Taasisi za afya (1,315), nyumba za ibada (1,145) na wananchi waishio vijijini | Haiukuonyeshwa |
| ***9. Miradi ya Maji*** | | | | |
| **9.1 Mradi wa maji Ziwa Victoria kwenda Miji ya Tabora, Nzega hadi Igunga** | Ushirikishaji wa wananchi katika hatua ya usanifu wa mradi, fidia kwa wananchi, elimu ya usimamizi wa uendeshaji wa miradi ya maji na elimu ya utunzaji miundombinu, upatikanaji wa maji | Miji ya Tabora, Halmashauri za wilaya za Igunga, Nzega na Uyui | Wakazi milioni 1.2 katika miji ya Tabora, Nzega na Igunga. | Haikuonyeshwa |
| **9.2 Mradi wa** | Elimu ya matumizi | Jiji la Arusha | Wananchi wa Arusha | Haiukuonyeshwa |

| Mradi | Aina ya Huduma iliyotolewa kwa Jamii | Wilaya, Kata, Mtaa au Kijiji kilichonufaika | Walengwa | Thamani ya Huduma iliyotolewa (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| **Ujenzi wa miundombinu ya usambazaji majisafi na uboreshaji huduma ya uondoaji majitaka jiji la Arusha** | bora ya maji, elimu ya fidia, ushirikishwaji wa jamii katika kulinda miundombinu ya maji, | | | |
| **9.3 Mradi wa Bulongwe na Lufumbi** | Kutoa elimu ya utunzaji wa vyanzo vya maji pamoja na miundombinu ya maji, kutoa elimu ya namna ya kujikinga na VVU na namna ya kuishi salama na VVU | Haikuonyesha | Wananchi wa Mbeya | Haikuonyesha |
| **9.4 Mradi wa Ujenzi wa Bomba la Majisafi (Km 55.755)** | - | Kijiji cha Mhangu hadi Kijiji cha Ilogi, Halmashauri ya Wilaya ya Msalala | Wanavijiji wa Msalala | Haikuonyesha |
| **9.5 Miradi ya Upanuzi wa Mitandao ya Maji kwa vijiji 100 vinavyopitiwa na Bomba Kuu kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama, Shinyanga** | Elimu ya kujikinga na VVU | Halmashauri za wilaya za misungwi, Kwimba, Msalala, Shinyanga vijijini, na Kahama Miji | Wananchi zaidi ya 86,117 katika vijiji vilivyopo katika mikoa ya Mwanza na Shinyanga | Haikuonyesha |
| **9.6 Mradi wa Maji wa Same – Mwanga – Korogwe** | - | - | - | Haikuonyesha |
| **Equinor** | Kufadhili maonesho, semina, warsha za sekta za Mafuta na Gesi, Ujenzi wa madarasa, vyoo na ununuzi wa vifaa vya | Lindi, Msimbati, Mnete na Halmashauri (Mtwara, Rufiji, Newala) Ugungo, Mkuranga, | Wizara ya nishati, TPDC, vyuo vya elimu, mashule, Jamii, Vituo vya Afya, Zahanati, Wahandisi, vikundi vya vijana na wanawake | USD (281,000), + GBP 47,499, + SEK 30,000 + TZS 44,700,000 |

| Mradi | Aina ya Huduma iliyotolewa kwa Jamii | Wilaya, Kata, Mtaa au Kijiji kilichonufaika | Walengwa | Thamani ya Huduma iliyotolewa (TZS) |
|---|---|---|---|---|
| | shule, | Dodoma, | | |
| **TPDC** | Uwezeshaji miradi ya afya, maji, elimu na utawala bora | Mikoa, Halmashauri za wilaya, kata na vijiji | Zahanati, shule, visima, n.k. | 1,500,000,000 |
| **Sekta ya Bima** | Michango, shule, kuongeza ujuzi wa mawakala wa Bima, kulipa ada za shule, Afya n.k. | Mikoa, Halmashauri za wilaya, | Mawakala, vituo vya yatima | - |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Ushiriki wa Watanzania, NEEC (2020)*

# 12.0. UWEZESHAJI KWA VIJANA

## 12.1. UTANGULIZI

Katika mwaka wa fedha 2019/20 Serikali kupitia Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (**NEEC**) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa maendeleo limebuni na kuratibu programu mbalimbali nchini za Vijana kwa lengo la kuwajengea uwezo kupata ujuzi ili waweze kujiajiri na kuajirika. Pia, Baraza kupitia mifuko mbalimbali ya uwezeshaji limeweza kuwaunganisha Vijana wengi nchini na fursa za mikopo yenye masharti nafuu ili waweze kukopesheka na kuanzisha miradi mbalimbali ya kimaendeleo na uzalishaji mali.

Serikali imeweka mazingira rafiki kwa Vijana kupitia sera, sheria, miongozo, kanuni na taratibu mbalimbali za Vijana ikiwemo Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana inayotafsiri Vijana kuwa ni wenye umri wa kuanzia miaka **15-35** ambao wanawakilisha kundi kubwa la nguvu kazi nchini.

Kutokana na changamoto mbalimbali zinazowakabili kundi kubwa la Vijana hapa nchini, Serikali imewekeza nguvu kubwa na kujiwekea jitihada za dhati katika kuwapatia vijana elimu na ujuzi kuanzia ngazi ya shule za msingi mpaka vyuo Vikuu ili kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa ajira rasmi katika nyanja za Serikali na Sekta binafsi.

## 12.2. PROGRAMU YA MAFUNZO KWA VIJANA WA JKT

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa kushirikiana na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) walikubaliana katika kutoa mafunzo kwa wakufunzi wa JKT mnamo mwaka 2015. Madhumuni ya mafunzo hayo ni kuwafundisha wakufunzi wa JKT dhana ya ujasiriamali, biashara na Ushirika ili nao waweze kutoa Elimu hiyo kwa vijana wanaojiunga na JKT kwa mujibu wa kujitolea ili waweze kujiajiri mara warudipo majumbani. Programu hii hufikia vijana 10,000 kwa mwaka.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Mhe. Jenista Mhagama akikabidhi vyeti vya mafunzo ya Ujasiriamali yaliyoendeshwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchmi (NEEC).*

Moja ya matokeo muhimu ni uanzishwaji wa viwanda vya nafaka vilivyoanzishwa ambavyo ni pamoja na Mafinga grain mill, Chita Rice Processing, Kanembwa OIl Mill, Kiwandfa cha kumenya Kahawa, Kiwanda cha kukoboa na kusaga Kahawa cha Itende Mbeya, Kiwanda cha kusindika asali cha Msangi Tabora.

Vilevile katika programu hii kilianzishwa kwa kiwanda cha kuchakata nafaka katika kambi ya JKT Mlale Mkoani Ruvuma. Kiwanda hicho kina uwezo wa kuzalisha tani 440 kwa mwezi



*Pichani ni ziara ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayaeshughulikia Sera, Bunge, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu Mhe. Jenista Mhagama alipotembelea kiwanda cha kuchakata sembe chenye uwezo wa kukuzalisha tani 440 kwa mwezi ambacho kipo mkoani Ruvuma katika kambi ya JKT Mlale.*

### 12.3. PROGRAMU YA PROBONO

Programu ya Ujasiriamali ya Probono (Probono Entrepreneurship Programme - PEP) ni programu inayolenga Shule za Sekondari kufanikisha utekelezaji wa dhana ya Ujasiriamali kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi wa kuajirika kwa vijana. Program ya PEP inatekelezwa na kuratibiwa na Serikali kupitia NEEC, Asasi ya Kiraia ya Probono ya Nchini Ujerumani, Asasi ya Kiraia ya - Action for Social Justice (AJISO) - ya Tanzania na Asasi ya Kiraia kutoka Uganda ya Teach A Man To Fish (TAMTF). Programu hii inatekelezwa katika mikoa ya Dar Es Salaam, Kilimanjaro na Arusha.




*Pichani ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Bi. Beng'i Issa akizindua Programu ya Ujasiriamali kwa Shule za Sekondari.*

Programu ya PEP vilevile imezingatia mahitaji na matakwa ya Mwongozo wa Taifa wa Ufundishaji Ujasiriamali (NETF) ili wanafunzi waweze kubuni wazo la biashara/mradi na kuandaa mpango biashara kabla ya kutekeleza biashara zao. Programu hii inalenga kujenga uwezo wa Ujasiriamali kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari za Serikali na binafsi ili kufahamu namna ya kubuni wazo la mradi, kuandaa mpango biashara na kuutekeleza kwa vitendo. Programu hii imeelekezwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Arusha. Jumla ya shule kumi na mbili (12) zinahusishwa kwenye programu hii. Katika Mkoa wa Dar es Salaam shule zifuatazo zinahusika; Shule ya sekondari Mbonea iliyopo Ilala, shule ya sekondari Kiluvya iliyopo Ubungo na shule ya sekondari Fanaka iliyopo Kinondoni. Mkoa wa Arusha unahusisha shule zifuatazo; Iriki Kisongo iliyopo Monduli, EdmundRice iliyopo Arusha City, Ole Sirway iliyopo Arusha City na St. Mary Duluti iliyopo Meru. Shule shiriki katika mkoa wa Kilimanjaro ni; Magnificancy iliyopo Siha, Kisomachi iliyopo Moshi Vijijini, Kiloben iliyopo Mwanga, Shule ya Sekondari Mwanga na Dr. Asha Rose Migiro iliyopo Mwanga. Jumla ya walimu 12 wanahusishwa kwenye programu pamoja na wanafunzi 288. Hadi sasa imefanyika tathmini ya awali ambapo jumla ya shule nne ziliteuliwa ikiwemo; Kiluvya, Mwanga, EdmundRice na Ole Sirway ili kuweza kutambua mahitaji.



*Pichani wanafunzi wakipatiwa mafunzo kupitia Programu ya Ujasiriamali ya Probono.*

### 12.4. AFRICAN-GERMAN YOUTH INITIATIVE ( AGYI )

Programu ya African-German Youth Initiative ( AGYI ) inatekelezwa na Tanzania Youth Coalition ambayo ni Taasisi Isiyo ya Kiserikali iliyoanzishwa mwaka 2002. Dhumuni kubwa la Taasisi hii ni kufanya sauti za vijana zisikike kwenye masuala yote ya kisera. Programu inafanyakazi na vijana wa umri wa miaka 15 mpaka 35. TYC hupeleka taarifa, kudadavua sera na kufanya shughuli za uchechemuzi.

Vilevile hufanya shughuli kujenga uwezo na kuhamasisha mambo yote yanayohusu sera za vijana kama vile kuonesha fursa za uwezeshaji wa kiuchumi kwa vijana. TYC imeshirikiana na Baraza katika kutekeleza programu ya AGYI, ambayo ni programu ya Mabadilishano ya Vijana kutoka nchini Ujerumani na Nchi za Afrika (African-German Youth Initiative - AGYI) ilizinduliwa tarehe 30 Juni, 2017 mjini Bonn, Ujerumani. Programu ya AGYI imefadhiliwa na Serikali ya Ujerumani. Programu hii inaratibiwa na kusimamiwa na Shirika la Kimataifa la GIZ Addis Ababa kwa kushirikiana na Kamisheni ya Umoja wa Afrika (African Union Commission - AUC) kwa kushirikiana na Nchi za Afrika. Programu imetekelezwa katika nchi tatu ambazo ni Tanzania, Benin na Afrika Kusini.

Taasisi ambazo zimefanya utekelezaji wa programu ya AGYI ni Tanzania Youth Coalition - TYC (Tanzania), Youth Beninese Leaders Association (YBLA) na WESSA (Afrika Kusini). AGYI inatekelezwa kwa majaribio katika muda wa miaka 3 ifikapo Septemba, 2020 mradi utakuwa umemalizika.

Serikali inasimamia programu hii kupitia NEEC ambapo Baraza limeshiriki moja kwa moja katika shughuli zote za programu na kupata taarifa za utekelezaji kupitia Taasisi ya TYC ambayo inaratibu utekelezaji kwa upande wa Tanzania. Zaidi ya Vijana wapatao 24 wameweza kupata fursa ya kwenda kujitolea na kujifunza nchini Ujerumani na vilevile takribani Vijana 16 kutoka

Ujerumani wamekuja nchini kupitia programu ya AGYI. Programu hii inahusisha kuunganisha asasi mbalimbali hapa nchini zikiwemo; Tanzania Renewable Energy Association (TAREA), Sustainable Economic and Environmental Conversation Organization (SEECO), Tanzania Gender Empowerment Development Organization (TAGEDO) na MOTO Handcraft Zanzibar.

Mafanikio makubwa ya programu hii yamekuwa ni kutengeneza mwongozo wa shughuli za kubadilishana vijana hapa nchini na nchi zingine na kuwaunganisha vijana kupitia kambi maalum, ambapo katika kipindi hiki jumla ya vijana 300 waliweza kubadilishana uzoefu, kuonesha bidhaa zao na mafanikio ya shughuli zao za kiuchumi kupitia mitandao waliyoitengeneza kwenye kambi hizi.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Mhe. Jenista Mhagama akiwa kwenye picha ya pamoja na waratibu wa Taasisi ya vijana ya Tanzania Youth Coalition (TYC) mara baada ya kufungua kongamano hilo lililofanyika Jijini Dodoma. (Kulia) ni Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Bi. Beng'i Issa, (Kushoto) ni Mkurugenzi wa Tanzania Youth Coalition (TYC) Bw. Lenin Kazoba.*

## 12.5. TANZANIA INNOVATION EXPLORE GALA

Hii ni programu maalumu kwa ajili ya kuwanyanyua vijana wa kati ya miaka 18 hadi 40 kupitia ujuzi walionao na utekelezaji wa ubunifu wao kiuchumi Jamii. Programu inatekelezwa na Taasisi ya Youth for Social Economic Development Organization (Y4SED) ambayo ni Asasi Isiyo ya Kiseriakali ya vijana na inaongozwa na vijana. Lengo kubwa ni kuwahusisha vijana kwenye ubunifu na maadili kwenye maeneo ya afya, Elimu, Ujasiriamali ili kuanzisha na

kuongeza ajira, ujuzi wa ufundi, na uwezeshaji wa kiuchumi kwa vijana. Tangu ianzishwe mwaka 2016, Y4SED imesaidia vijana kwenye zaidi ya mikoa 20 region hapa Tanzania.

Y4SED imetekeleza programu ya TANZANIA INNOVATION EXPLORE GALA ambayo ilianza na mikoa ya mfano ikiwemo; Dodoma, Mbeya, Kigoma, Mwanza, Arusha, Kilimanjaro na Dar es Salaam, ambapo jumla ya vijana 1,248 waliweza kunufaika na programu hii.




*Pichani ni Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia (Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu) Mhe. Anthony P. Mavunde akiwa na watendaji wa asasi ya Y4SED walipokutana kujadili fursa kwa ajili ya vijana hapa nchini.*

**Malengo**

Moja ya malengo ya programu hii ni kutengeneza fursa za Uwekezaji kupitia ubunifu ndani ya nchi yetu, pia kuwaunga mkono Wabunifu vijana kwa kuwasaidia kutekeleza mawazo yao ya ubunifu na kuchochea maendeleo ya vijana kupitia ubunifu na ugunduzi.Vile vile programu imelenga kwenye kuendeleza miradi mbalimbali iliyo kwenye mlengo wa kiuchumi na kijamii.

**Mafanikio**

Programu ilifanikiwa kuifikia mikoa yote sita (6) kama ilivyokua imepangwa.Ingawa mkoa mmoja wa Kilimanjaro uliongezwa baada ya kuona matokeo chanya ambayo vijana wanaweza kuyafikia kupitia programu. Hii ilikuja kutokana na uhitaji na matakwa ya ushiriki wa vijana ndani ya mkoa.

Pia jumla ya wanufaika wa programu hii wapatao 121 waliweza kushindanishwa kwenye mchujo ambapo washindi waliwakilisha mikoa yao kwenye mashindano ya kitaifa yaliyofanyika Dar es Salaam.

Vilevile programu hii iliweza kuwapata Wabunifu/wagunduzi vijana wapatao ishirini na tatu (23) ambao walifanya vizuri zaidi kwenye shughuli zao za ubunifu. Hivyo walikaa kambini kwa

jumla ya siku ishirini na moja (21) ili waweze, kufanyia kazi mawazo yao ya ubunifu na pia kutengeneza fursa za uwekezaji kupitia ubunifu. Pia zaidi ya watu 2040 walishiriki moja kwa moja au kwa namna moja au nyingine kwenye semina mbalimbali na zaidi ya watu 3000 walifikiwa wakati wa utekelezaji wa programu kwa njia mbalimbali.

### 12.6. KIJANA JIANDALIE AJIRA (VIA)

TECC ni Asasi Isiyo ya Kiserikali iliyoanzishwa mwaka 2015 kwa ushirikiano kati ya NEEC, COSTEC na TPSF. Mnamo mwaka 2016 ilisaini makubaliano naInternational Youth Foundation kutekeleza mradi wa Jiandalie Ajira. Programu hii imetekelezwa na Taasisi ya TECC Ikiwa ina malengo ya kuwawezesha vijana wengi kukuza biashara zao pamoja na kutengeneza ajira. Programu hii ikiwa inaelekea mwishoni TECC imedhamiria kuweka jitihada zadi katika kuunga mkono biashara zinazokua na kurasimisha uendeshaji wake ili kuweza kukidhi vigezo vya kisheria pamoja Mamlaka simamizi ili kuweza kufikia huduma mbalimbali ikiwemo mikopo.



*Pichani Naibu Waziri wa Elimu , Sayansi na Teknolojia Mhandisi Stella Manyanya (kulia) akikata utepe wakati uzinduzi wa program ya JIANDALIE AJIRA inayolenga kupunguza tatizo la ajira nchini.*

Programu imetekelezwa katika mikoa minne ya Mtwara, Pwani, Dar es salaam na Dodoma. Katika utekelezaji wa programu taasisi za SIDO, TCCIA, TWCC, NEEC na wataalamu binafsi waendelezaji wa biashara walihusishwa. Jumla ya vijana 2,748 wamefikiwa katika mikoa iliyotajwa ambapo asilimia 72 ni wasichana, katika vijana hao 1,360 walihudhuria mafunzo, 571 walikutanishwa na washauri wabobezi kwenye maeneo ya biashara, viaja 72 walipatiwa mikopo, vijana 331 walianzisha biashara mpya, vijana 176 walirasimisha biashara zao na vijana 70 walitengene  za ajira za wenzao. Katika programu hii vilevile washauri wabobezi 147 walipatiwa mafunzo ya kufanyakazi na vijana na maafisa 102 wa Mamlaka za Serikali za Mitaa walifundishwa mfumo wa ujasiriamali kwa vijana.

### 12.7. TANZANIA YOUTH DIGITAL SUMMIT (TYDS)

Digital Opportunity Trust (DOT) Tanzania ni Asasi Isiyo ya Kiserikali ambayo inaongozwa na vijana wanajishughulisha na ubunifu wa kutatua matatizo ya kijamii ili kuleta fursa, ujuzi, elimu na kubadilisha maisha ya jamii zinazoowazunguka.


Programu ya Tanzania Youth Digital Summit (TYDS) huwa ni shughuli ya kila mwaka ambayo huandaliwa na DOT na wadau wake kusaidia kuongeza ujuzi wa kidijitali kati ya vijana wa kitanzania na kuongoza ubunifu ambao unawezesha kushiriki katika uchumi wa kidijitali kupitia kazi za kidijitali.

Ushirikiano huu uliwezeshwa na *Irish Aid* ikiwa ni mwitikio kwa tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana kwa kuwawezesha katika fursa za kuendeleza ujuzi wa kidigitali ili wajipatie kipato na ajira kwenye uchumi wa kidigitali ili waweze kuwa waasisi/waanzilishi wa biashara na ajira.

Lengo la msingi la programu ya TYDS ni kuunga mkono maendeleo ya ujuzi wa kidigitali kwa vijana wa kitanzania kwa ushiriki bora kwenye uchumi wa kidigitali. TYDS imedhamiria kufanya mabadiliko vyuoni kwa kufanya makongamano ya mwaka kwa kuhusisha mifumo ya kisasa ya kidigitali na kuunga mkono wahudhuriaji vijana ili wapate uzoefu pamoja na kuwapatia mafunzo ya kuongeza ujuzi.

Mafanikio ya programu hii ni pamoja na kufikia jumla ya vijana 513 ambapo wanawake walikua 160 na wanaume 353. Jumla ya vijana 1,111 walituma maombi ya kuwa sehemu ya programu hiyo kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza, ambapo wanawake ni 310 na wanaume ni 801. Waombaji waligawanyika katika makundi ya wanafunzi, wahitimu, waajiriwa na wasio na ajira. ;

**Mchoro Na. 22: Vijana waliofikiwa na programu ya TYDS**



TYDS imewezesha kuongezeka uelewa miongoni mwa vijana na kuweza kutambua ni wapi wanaweza kuwekeza katika karne hii ya 21. Pia kubuni na kuwa na mawazo ya biashara zenye mlengo wa TEKNOHAMA. Zaidi ya vijana 60 walishiriki kwenye kuuza tovuti kwa mara ya kwanza na hivyo kuongeza idadi ya vijana wanaofanya kazi kama washauri waelekezi.

Kuanzishwa kwa vikundi/jamii za ushirikiano miongoni mwa vijana kwa kuchangia taaluma/mawazo na fursa ambapo vilabu viwili viliundwa kwa kutumia makundi ya ‘’Whatsapp’’ kama namna ya kurahisisha mawasiliano ni mojawapo ya mafanikio ya programu hii.

Vilevile kuongezeka kwa mitandao yenye tija miongoni mwa vijana, wataalamu wa TEKNOHAMA na Wabunifu. Hii imeonekaana kupitia mbia anayeitwa Tanzania Developers Communituy (TDC) ambaye ameweza kuanzisha ukurasa unaoitwa TDC Dodoma ambapo jumla ya wanachama 105 walijiunga.

Kuweza kushirikiana na vyuo vinne; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia Chuo cha Habari na Teknolojia ya Mawasiliano, Chuo cha Usimamizi wa Fedha, Chuo cha Mtakatifu Augustine na Chuo Kikuu cha Dodoma. Katika vyuo vyote wakuu wa utawala waliweza kushiriki.

Jitihada za makusudi za kukuza na kujenga ushirikiano kati ya sekta binafsi na sekta za umma ili kuunga mkono matokeo ya programu zilifanyika, ambapo DOT walikutanisha wadau ili kuangalia mtawanyiko wa rasilimali, mitandao na ujuzi.

Kuundwa kwa ‘’Youth Advisory Board’’ ili kuchangia uongozi wa mradi na kutambua vipaumbele vya vijana na maeneo yenye tija, Bodi ilijumuisha vijana watano (wanawake watatu na wanaume wawili).

## 12.8. PROGRAMU YA SERIKALI YA KUKUZA UJUZI

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu (OWM-KVAU) kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kubuni mifumo ya kisheria, mazingira rafiki na wezeshi ya kisera na programu mbalimbali kwa lengo la kuwezesha na kuongeza ajira kwa vijana hapa nchini.

### i. Uwezeshaji Vijana kupitia Programu ya Kitalu Nyumba (Green House)

Programu hii ilianzishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ndio yenye dhamana na masuala ya vijana kwa kuhamasisha kilimo kwa kuwawezesha wakulima kupata mafunzo ya kilimo cha kisasa, pembejeo, zana za kisasa na wataalamu wa ugani pamoja na mbinu za kuyafikia masoko ya uhakika ya mazao yao, ambao ulipelekea kutambua umuhimu wa mchango wa vijana hasa waliopo vijijini.

Programu hii imeweza kufika katika Halmashauri 84, lengo la Serikali likiwa ni kufikisha ujuzi huo kwa Halmashauri zote za Tanzania Bara kwa kuwa asilimia 63 ya fursa za ajira zinapatikana kwenye kilimo na tena maeneo ya vijijini. Programu hii imewawezesha vijana

180,000 kupta mafunzo ya Kilimo kupitia Teknolojoa ya Kitalu nyumba, ambapo wengi wao wamejikita katika kilimo cha mbogamboga, matango, nyanya na hoho.



*Pichani Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Mhe. Jenista Mhagama alipotembelea na kukagua maendeleo ya mafunzo hayo kwa vijana katika Wilaya ya Chemba na Kondoa, Jijini Dodoma*

**ii. Ukuzaji wa Fursa za Ajira**

Serikali pia imeendelea kuratibu juhudi za ukuzaji wa fursa za ajira. Jumla ya ajira 1,577,622 zimezalishwa mwaka huu katika sekta mbalimbali ambapo ajira 579,518 zimezalishwa na sekta rasmi na ajira 998,104 zimezalishwa na sekta isiyo rasmi. Serikali pia, imeendelea na utoaji wa huduma za ajira ili kuwezesha watafuta kazi kumudu ushindani wa soko la ajira. Hadi kufikia tarehe 31 Januari 2020, jumla ya watafuta kazi 6,756 wamesajiliwa na Kitengo cha Huduma za Ajira ili kupatiwa huduma mbalimbali za ajira hususan, ushauri nasihi (*vocational guidance and employment counselling)* na mafunzo ya kumudu ushindani katika soko la ajira. Watafutakazi waliopatiwa huduma ya ushauri nasihi pamoja na mafunzo hayo walikuwa 5,266.

## 12.9. PROGRAMU YA MAFUNZO YA UJASIRIAMALI NA USIMAMIZI WA BIASHARA

Mpango huu umeandaliwa kama mojawapo ya mbinu za kutatua changamoto ya ujuzi kwa vijana wajasiriamali katika kipindi cha muda mfupi na mrefu. Lengo kuu la mafunzo ya ujasirimali na usimamizi wa biashara ni kuwawezesha vijana (wenye umri wa miaka 15 – 35) kupata mbinu stahiki za ujasiriamali na usimamizi wa biashara ili wafanye shughuli zao kwa tija na mafanikio.

Mafunzo ya Ujasiriamali na Usimamizi wa Biashara kwa Vijana Wajasiriamali yalianza kutolewa kuanzia tarehe 30 Julai 2019 Mkoani Dodoma na kuhitimishwa jijini Arusha tarehe 14 Novemba 2019. Jumla ya vijana **1,408** wamefikiwa na mpango huu kati yao vijana wenye ulemavu walikuwa ni **90** sawa na asilimia 6.39 ya idadi ya vijana wote walioshiriki kwenye mafunzo kama jinsi ambavyo jedwali hapo chini linavyoonesha:-

**Jedwali Na. 30: Idadi ya Vijana waliofikiwa na Mafunzo**

| NA. | MKOA | IDADI YA VIJANA | | | JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ME | KE | WENYE ULEMAVU | |
| **1.** | Dodoma | 135 | 78 | 5 | 213 |
| **2.** | Ruvuma | 94 | 67 | 10 | 161 |
| **3.** | Geita | 125 | 36 | 3 | 161 |
| **4.** | Mwanza | 87 | 68 | 14 | 155 |
| **5.** | Mbeya | 123 | 88 | 6 | 211 |
| **6** | Lindi | 61 | 106 | 8 | 167 |
| **7.** | Tanga | 110 | 61 | 22 | 171 |
| **8** | Arusha | 107 | 62 | 22 | 169 |
| **JUMLA** | | **741** | **649** | **90** | **1,408** |

Idadi hii imevuka lengo la mpango kwa asilimia 17.33. Mpango huu wa mafunzo ulikuwa ukiwalenga vijana wajasiriamali wenye umri wa miaka 15 hadi 35 wapatao 1,200 katika Mikoa Nane (8) kwa mgawanyo wa vijana 150 kwa kila Mkoa.

Mada zilizowezeshwa kwenye mafunzo hayo ni pamoja na kujitambua kama mjasiriamali, dhana ya ujasiriamali, bidhaa, huduma na mteja, uchambuzi wa masoko na ushindani kwa wajasiriamali, mkakati wa uendeshaji wa biashara, usimamizi wa fedha katika biashara, vyanzo vya mitaji, mpango wa biashara na jinsi ya kuandaa andiko la biashara, viashiria vya hatari katika biashara na mikakati ya kuvikabili, uimarishaji na ukuzaji wa biashara, taratibu za uanzishaji wa makampuni, fursa za uwezeshaji kwa vijana kiuchumi kupitia mfuko wa maendeleo ya vijana, fursa za uwezeshaji kwa vijana wa kike kupitia mfuko wa maendeleo ya wanawake, fursa za uwezeshaji kwa vijana na watu wenye ulemavu kupitia asilimia 10 za mapato ya ndani ya halmashauri.

### 12.10. KONGAMANO LA MAADHIMISHO YA KITAIFA YA WIKI YA VIJANA

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wetu wenye Ulemavu) waliratibu na kusimamia Maadhimisho ya Kitaifa Wiki ya Vijana lililofanyika mkoani Lindi mwezi Oktoba, 2019. Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni miongoni mwa wadau walioshiriki katika maadhimisho ya wiki ya Vijana ambayo yalihudhuriwa Taasisi na Mashirika zaidi ya 100 kutoka sekta ya Umma na Binafsi katika kuonyesha huduma na bidhaa mbalimbali za Ujasiriamali. Shughuli zilizofanyika huko ni pamoja na kupokea mwenge wa Uhuru pamoja

na kumbukizi ya miaka 20 ya bila ya baba wa Taifa, kulikuwa na mabanda ya maonesho ambapo vijana walionesha kazi mbalimbali za walizobuni.

## 13.0. UWEZESHAJI KIUCHUMI WA WANAWAKE NA WENYE ULEMAVU

### 13.1. UTANGULIZI

Katika kufikia malengo ya nchi ya Serikali yenye Uchumi wa kati, Uchumi wa Viwanda, Ushiriki wa wanawake ni muhimu katika jitihada za kutimiza lengo hili nchini Tanzania. Pamoja na hivyo, wanawake bado wamekuwa nyuma katika kupata fursa za kutosha za kiuchumi hapa nchini na hata duniani kote.

Kwa mujibu wa takwimu za NBS za mwaka 2014, watu 2,225,671 wenye ulemavu nchini Tanzania. Huu ni pamoja na ulemavu wa viungo, wasioona, wasiosikia, ulemavu wa akili, ulemavu mchanganyiko na ulemavu wa aina nyingine. Watu wenye ulemavu nchini Tanzania wanakabiliana na changamoto nyingi katika maisha yao ya kila siku kutokana na uwezo mdogo wa kupata mahitaji ya msingi walionao.

Serikali inaamini watu wenye ulemavu wanayo haki kwa mujibu wa Katiba ya kutambuliwa utu wao, kuendelezwa, kuheshimiwa na kulindwa dhidi ya vitendo vinavyoshusha utu wao ikiwemo ubaguzi, uonevu, ukatili na mila potofu. Vilevile, Uwezeshaji wa wanawake kiuchumi ni muhimu kwani ni silaha tosha katika kuondoa umaskini nchini kwani mchango wa mwanamke katika familia ni mkubwa na muhimu ili kuleta uhakika wa kuishi kwa familia na jamii na nchi kwa ujumla. Kuwezesha wanawake kiuchumi kunawezesha wanawake kumiliki haki za kiuchumi, kumiliki mali na kupata fursa zote za kiuchumi.

Serikali imechukua jitihada za makusudi kuhakikisha kundi hili maalum linalojumuisha wanawake na watu wenye ulemavu kupewa kipaumbele katika fursa mbalimbali za kuwainua kutoka katika kiwango walichopo kwa kuwapa fursa mbalimbali za kiuchumi ili kuweza kujiinua kiuchumi na kuwa na maisha bora na pia kuchangia katika uchumi wa Nchi. Aidha Serikali inaandaa Mpango wa Taifa wa kuimarisha masuala ya utoaji huduma kwa Watu wenye Ulemavu ili kuwezesha kundi hilo maalum kushiriki kwenye sekta mbalimbali

### 13.2. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU MBALIMBALI ZA UWEZESHAJI KWA WANAWAKE NA WENYE ULEMAVU

#### 13.2.1. Program ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi mkoani Kigoma

Mkoa wa Kigoma unatekeleza Programu ya Pamoja ya Kigoma ya Umoja wa Mataifa (Kigoma Joint Program – KJP) ambayo ni jitihada inayohusisha mashirika 16 ya Umoja wa Mataifa (UN) ambayo yamejikita kushughulikia sekta mbalimbali kwa lengo la kuchochea maendeleo katika Mkoa wa Kigoma. Mashirika hayo ni pamoja na FAO, ILO, IOM, ITC, UN WOMEN, UNAIDS, UNCDF, UNDP, UNEP, UNESCO, UNFPA, UNHCR, UNICEF, UNIDO, UNV na WFP. Programu hii inatekelezwa kwa ushirikiano wa mashirika haya na

sekretariati na serikali za wilaya za Mkoa huo. Programu hii ilizinduliwa rasmi mwezi Septemba 2017 na inategemewa kutekelezwa kwa miaka mine (2017 – 2021) kwa kushirikiana na Uongozi wa Mkoa wa Kigoma, Washirika wa maendeleo, jamii za wenyeji, wakimbizi na vyama vya kiraia.

Programu hii ya pamoja inatekeleza maeneo saba ambayo ni Nishati endelevu na mazingira, Uwezeshaji Vijana na Wanawake Kiuchumi, Kutokomeza vitendo vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto, elimu kwa wasichana na wanawake vijana, usafi wa maji na mazingira, kilimo, Afya, VVU na Ukimwi na Lishe.

#### 13.2.2. Manufaa ya Utekelezaji wa Programu ya Pamoja kwa Wanawake Mkoani Kigoma

Program hii ya Pamoja mkoani Kigoma imekuwa mkombozi wa wanawake na vijana kuongeza kipato vyao kwa kuimarisha upatikanaji wa fedha kupitia misaada na mikopo kutoka taasisi za fedha na vikundi vya akiba, pia programu inaimarisha miundombinu muhimu inayosaidia wajasiriamali vijana na wanawake kuimarisha ubora wa bidhaa na kupata masoko makubwa.

Mashirika ua Umoja wa Mataifa ya UNDP na ILO kwa kushirikiana na mkoa wa Kigoma yamefanikisha uwezeshaji wa vikundi vya Wanawake, Vijana, Makampuni na Asasi za Uwezeshaji Wananchi Mkoani Kigoma. Kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020, jumla ya vikundi 17 kutoka Kasuku TC, Kasuku DC, Kibondo DC na Kakonko DC vimefanikiwa kuwezeshwa kifedha jumla ya Shilingi Milioni 277, ujenzi wa majengo ya ofisi na stoo, ujenzi wa maghala ya nafaka na ununuzi wa mashine mbalimbali kama mashine za kutengenezea sabuni, mashine za kukoboa na kusaga nafaka, cherehani 11 zenye thamani ya Shilingi 25,000,000 na ujenzi wa mabanda ya mifugo kwa ajili ya kuendeleza miradi ya kujiinua kiuchumi.

Mashirika ya UNDP na ILO yamewezesha Halmashauri kwa kutoa ajira za muda (mkataba) kwa vijana ambao wamepewa mafunzo kwa ajili ya kufundisha vikundi vya vijana na akina mama katika Wilaya za Kasulu (DC na TC), Kibondo na Kakonko. Vikundi hivi ni vya wajasiriamali. Vijana hawa kupitia Halmashauri zao wamepatiwa vitendea kazi ambavyo ni Pikipiki (12), Kompyuta (12), Printer 12, Projectors 12, Projector screen 12 na posho ya kufanya kazi hizi kila mwezi.



*Pichani: Kikundi cha Wajasriamali cha Blessing Afri Design kilichopo kata ya Kumnyika – Kasulu TC*

### 13.2.3. Mikopo ya Wanawake

Uwezeshaji wanawake kiuchumi ni suala muhimu katika kufikia usawa wa kijinsia na kupunguza umaskini wa kipato katika jamii hivyo Serikali inaendelea kuweka kipaumblele kwa wanawake kama mkakati wa kufikia usawa wa kijinsia katika nyanja zote. Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Benki ya Posta Tanzania imeendelea kuwezesha wanawake kiuchumi kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu. Dirisha la Wanawake la Benki ya Posta Tanzania ambalo limeanzishwa ili kuendeleza huduma zilizokuwa zinatekelezwa na Benki ya Wanawake Tanzania limetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 2,050,100,000.00 kwa wanawake wajasiriamali 3,035 kutoka katika mikoa 26 ya Tanzania Bara.

### 13.2.4. Huduma kwa Watu wenye Ulemavu

Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa miongozo na mipango mbalimbali inayolenga kuongeza upatikanaji wa haki na ustawi wa Watu Wenye Ulemavu na kuhakikisha huduma zinazotolewa katika ngazi zote kwa ajili ya watu wenye ulemavu na wenye mahitaji maalum zinatolewa kwa haki na usawa. Aidha, katika kukabiliana na changamoto zinazowakabili Watu Wenye Ulemavu hususan kiuchumi, Serikali imezielekeza Halmashauri kutenga asilimia 2 ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo kwa watu wenye ulemavu. Kupitia mikopo hiyo jumla ya vikundi 160 vya watu wenye ulemavu vimeundwa na vilipatiwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 3.87.

### 13.2.5. Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu

Serikali imeanzisha Mfuko wa Taifa wa Watu Wenye Ulemavu ambao unasimamiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu**.** Mfuko huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha maisha na huduma za watu wenye ulemavu nchini. Mfuko huu umeanzishwa kwa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na 9 ya mwaka 2010 ambayo inahusu haki na ulinzi kwa Watu Wenye Ulemavu na kuhakikisha wanapatiwa haki hzio ikiwemo masuala ya ajira, elimu, afya na utengamao wa maisha yao ili kuondokana na dhana potofu ya utegemezi kwa kundi hilo.

Mfuko huu wa watu wenye ulemavu unashughulikia masuala mbalimbali ya watu wenye ulemavu ikiwemo kutoa ruzuku kwa vyama vya watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kukua kiuchumi na unawajengea uwezo wa kujaimini na kuanzisha miradi na shughuli mbalimbali zitakazowakwamua kiuchumi. Vilevile Serikali itatumia mfuko huo kuratibu upatikanaji wa rasilimali fedha kutoka kwa wadau ili kuhakikisha Mfuko huo unakidhi malengo ya uanzishwaji wake.



*Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Masuala ya Watu Wenye Ulemavu Mhe. Stella Ikupa (wa pili kutoka kulia) akizungumza na Wadua walioshiriki katika Mkutano kuhusu masuala ya Utoaji wa Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu uliofanyika Disemba 11, 2019 katika Hoteli ya Nashera, Jijini Dodoma.*

### 13.2.6. Baraza la Ushauri la Taifa la Watu Wenye Ulemavu

Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu imezindua rasmi Baraza la Ushauri la Taifa la Watu Wenye Ulemavu ambalo limekuwa likitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Watu wenye Ulemavu Na 9. ya Mwaka 2010 ambayo inaeleza majukumu ya Baraza ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri. Baraza hili linajukumu la kuhakikisha usimamizi wa sekta ya watu wenye ulemavu na kushauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya kundi hili muhimu. Aidha, wajumbe wa Baraza hilo wamepatiwa mafunzo kuhusu Sera, Sheria, miongozo na mipango inayowahusu Watu Wenye Ulemavu ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

### 13.2.7. Programu ya kukuza Ujuzi kwa Wenye Ulemavu

Katika mwaka 2019/2020, wahitimu 167 wa vyuo vikuu wenye ulemavu, walipatiwa mafunzo ya kukuza ujuzi kupitia Programu ya Miaka Mitano ya Kukuza Ujuzi. Serikali itaendelea kuwahamasisha wahitimu wenye ulemavu kujiandikisha kwenye daftari la wanaotafuta ajira ili kupata fursa ya kuajiriwa pale nafasi zinapotangazwa. Aidha, Serikali imefanya jitihada na kufanikiwa kufufua vyuo vitatu vya mafunzo ya ufundi kwa Watu Wenye Ulemavu. Vyuo hivyo ni Mirongo (Mwanza), Ruwanzari (Tabora) na Masiwani (Tanga).

### 13.2.8. Mafunzo ya Ujasiliamali kwa Wanawake na Wenye ulemavu

Serikali imeendelea kutoa fursa za mafunzo ya ujasiamali kwa wanawake,vijana na wenye ulemavu kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kuanzisha na kusimamia na kukuza miradi yao mbalimbali na kujiinua kiuchumi. Mafunzo haya utolewa kupitia ofisi mbalimbali za Serikali zikiwepo Taasisi na Halmashauri mbalimbali nchini.



*Pichani: Afisa Maendeleo ya Jamii Mkuu wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Bi. Margareth Mazwile*

Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imefanikiwa kutoa mafunzo kwa vikundi 117 vya vya wajasiriamali wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika ukumbi wa Karimjee jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 21-22 Novemba, 2019 kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kutumia vema

na kurejesha mikopo ambayo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kila mwaka huitoa kwa vikundi vya aina hiyo.

Mikopo hiyo inatokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani yanayokusanywa na Halmashauri za Jiji la Dar es Salaam hutolewa kila mwaka kwa vikundi hivyo ili kuviwezesha kujikwamua kiuchumi, kujiongeza kipato na kupunguza tatizo la ajira kwa kujihusisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi kwa ajili ya maendeleo ya Jiji la Dar es Salaam.

#### 13.2.9. Programu ya wanawake - Alaska Jamii

Mama Alaska Jamii ni shirika la Kitanzania lililoanzishwa kwa lengo la kuwawezesha wakulima na wasindikaji wadogo na Mama Lishe kuweza kupata mahitaji yao muhimu moja kwa moja kwa bei nafuu na shindani, masoko, huduma za kifedha na vilevile kujijengea uwezo ili kukuza biashara zao na kujikwamua kiuchumi.

Shughuli za uuzaji wa chakula ni moja ya sehemu ya sekta binafsi nchini Tanzania ambayo inajumuisha wajasiriamali wengi ambao asilimia kubwa ni wanawake. Uuzaji wa chakula unahusisha shughuli za kupika na kuuza vyakula mbalimbali kwenye maeneo mbalimbali kama sehemu za masoko, pembezoni mwa barabara, maeneo karibu na sehemu zenye wateja kama maeneo yenye ujenzi au sehemu zenye mkusanyiko kama mikutano na matamasha. Wajasiriamali hawa wamekuwa wakikutana na changamoto nyingi katika kuendesha biashara zao kutokana na kutokuwa na ujuzi wa masuala ya kifedha, utoaji hafifu wa huduma kwa wateja, mazingira mabovu ya kufanyia kazi, kutoweza kudhibiti bei za chakula wanachouza na masuala ya elimu ya biashara.

Mnamo Agosti 2019, Shirika kwa kushirikiana na Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Fedha Tanzania (FSDT) na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) lilianzisha mradi wa kutoa mafunzo wenye lengo la kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa wauzaji wa chakula maarufu kama ***“Mama na Baba Lishe”*** wanaofanya shughuli zao katika jiji la Dar es Salaam ili kuweza kuboresha biashara zao na utoaji huduma katika hali nzuri ambayo italeta kukua kwa biashara zao. Mradi huu unaoitwa **Biashara na Daftari**, umefanikiwa kutoa mafunzo kwa wanaume na wanawake 320 ambao wanajishughulisha na biashara ya chakula katika masoko 10 ambayo ni Makumbusho, Mnazi Mmoja, Kisutu, Ilala, Stereo, Gerezani, Buguruni sokoni na Chama, Mchikichini na Kariakoo yaliyopo jijini Dar es Salaam. Mafunzo yaliyofundishwa ni pamoja na **Biashara na Daftari** kuwezesha elimu ya kuweka kumbukumbu za biashara, Kukuza biashara, huduma kwa wateja pamoja na afya na mazingira.

### 13.3. USHIRIKI WA WANAWAKE NA WENYE ULEMAVU KATIKA MANUNUZI YA UMMA

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi linaendelea kushirikiana na PPRA kusimamia utekelezaji wa marekebisho Sheria ya manunuzi ya Umma ya mwaka 2016 pamoja na utekelezaji wa Mwongozo wa ushirikishwaji wa Makundi Maalum yaani Wanawake, Vijana,

Wazee na Watu wenye Ulemavu katika Manunuzi ya Umma uliopitishwa mwaka 2017 na kutekelezwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) ambao unaelekeza Ofisi za Serikali kutenga asilimia 30 ya manunuzi yao ya umma kwa ajili ya wajasiriamali walio kwenye makundi hayo maalum hapa nchini.

Mpaka sasa Mamlaka ya Ununuzi wa Umma (PPRA) imeandaa kanzidata ambayo imejumuisha taarifa zote za vikundi maalum kama zilivyotumwa na taasisi za serikali zinazokuza na kulea makundi hayo ambapo mpaka sasa idadi ya Vikundi vilivyowasilishwa imefikia 150 ikiwa ni makundi ya walemavu, wazee, vijana na wanawake.

Vilevile inafuatilia idadi ya zabuni zinazotolewa na serikali na kuzitoa kwenye Jarida la Ununuzi wa Umma *(Tanzania Procurement Journal)* na Mamlaka imebaini kuna mwitikio mkubwa wa Watanzania kushiriki katika ushiriki wa zabuni za kazi mbalimbali.

# 14.0. UWEZESHAJI KATIKA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## 14.1. VITUO VYA UWEZESHAJI MIKOANI

### 14.1.1. UTANGULIZI

Uanzishwaji Vituo vya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi 2014 ili kufikisha huduma za uwezeshaji kwa pamoja. Dhumuni la vituo ni kutoa huduma kwa wajasirimali na wananchi kwa ujumla ili waweze kujikwamua kiuchumi kwa kuanzisha ama kuendeleza biashara na miradi mbalimbali ya maendeleo.Vituo vinawakutanisha wadau mbalimbali wa uwezeshaji katika eneo moja ili waweze kutoa huduma kwa walengwa. Aidha, vituo vinategemewa kuwarahisishia wananchi kupata huduma za uwezeshaji katika eneo moja kwa mujibu wa malengo ya uanzishwaji. Pia wasimamizi wa vituo hivi watakuwa na jukumu la kuandaa taarifa ya Uwezeshaji na kuziwasilisha kwenye mamlaka zinazohusika kwa ushauri na maamuzi.

Vituo hivi vinatoa huduma za Urasimishaji wa Biashara, Ushauri wa Kibiashara, Elimu na Mafunzo ya Ujasiriamali, Upatikanaji wa Mitaji na Masoko. Teknolojia na Ufundi Hifadhi za jamii na Afya, na uanzishwaji wa vikundi vya kifedha vya kijamii na vyama vya ushirika vya akiba na mikopo (SACCOS) n.k

### 14.1.2. MUUNDO NA USIMAMIZI WA VITUO VYA UWEZESHAJI


Muundo wa utawala wa vituo una ngazi tatu za usimamizi. Kituo kikianzishwa na mkoa kitasimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa na kikianzishwa na Halmashauri kitasimamiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri. Vilevile kutakuwa na Kamati ya Ushauri ambayo itakuwa ni kamati ya mashauriano ya Mkoa au Wilaya. Kwa ujumla vituo hivi vitasimamiwa na Katibu Tawala wa Mkoa na Mkurugenzi wa Halmashauri ambao watakuwa na majukumu yafauatayo:

i. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa au Ofisi ya Halmashauri husika ndio itakuwa chombo chenye jukumu la kusimamia utekelezaji wa shughuli za Kituo cha Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi.

iii. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa au Ofisi ya Halmashauri husika itatoa taarifa za utekelezaji wa Kituo kwenye kamati ya mashauriano ya Mkoa au Wilaya .

iv. Ofisi ya Mkuu wa Mkoa au Ofisi ya Halmashauri husika, itakuwa na jukumu la kutengeneza mfumo wa usimamizi wa kituo.

**Mchoro Na. 23: Muundo wa usimamizi wa vituo vya uwezeshaji**




## 14.2. VITUO VYA URASIMISHAJI NA UENDELEZAJI WA BIASHARA (ONE STOP BUSINESS DEVELOPMENT CENTRES)

Vituo vya Urasimishaji na Uendelezaji wa Biashara (One Stop Business Development Centres) vinavyotekelezwa na Halmshauri kwa kushirikiana na MKURABITA vilianzishwa kwa lengo la kuwawezesha wamiliki wa rasilimali ardhi na biashara kushiriki katika uchumi rasmi unaosimamiwa na utawala wa sheria. Hii ni pamoja na kuzitumia mali zao zilizokwisha rasimishwa kama dhamana katika kupata mikopo na fursa zinginezo zilizoko katika uchumi wa soko.

Walengwa wa vituo hivi ni wananchi wa mijini na vijijini wanaomiliki rasilimali nje ya mfumo unaotambulika kisheria na wanaoendesha biashara bila kukudhi matakwa ya kisheria. Rasilimali na biashara zinazomilikiwa na kuendeshwa nje ya mfumo rasmi haziwapi fursa wamiliki wake ya kujiongezea mitaji na kuingia katika uchumi wa soko.

### 14.2.1. UTENDAJI WA VITUO VYA URASIMASHAJI NA UENDELEZAJI BIASHARA (ONE STOP BUSINESS DEVELOPMENT CENTRES)

Halmashauri zinasimamia jumla ya vituo 11 vya urasmishaji vilivyopo katika maeneo ya Halmashauri za Majiji ya Tanga na Mwanza (Wilaya ya Nyamagana), Manispaa ya Morogoro, Singida, Mtwara na Tabora; Halmashauri za Miji ya Bariadi, Geita, Babati, Njombe na Kahama pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Urambo. Vituo vinatoa huduma kwa wananchi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama Taasisi za Fedha, TCCIA, SIDO, NSSF, TRA, BRELA,

Baraza la Taifa la Uwezeshaji nk. Vituo hivi kwa pamoja vimefanikisha yafuatayo eneo la urasimishaji Ardhi, biashara na Taifa kwa ujumla:-

**Jedwali Na. 30: Vituo vya urasimashaji na uendelezaji biashara**

| HALMASHAURI | TAASISI ZINAZOTOA HUDUMA |
|---|---|
| Halmashauri ya jiji la Tanga<br>Mwanza (Wilaya ya Nyamagana),<br>Manispaa ya Morogoro<br>Halmashauri ya Mji wa Singida<br>Halmashauri ya Mji wa Mtwara<br>Manispaa ya Tabora<br>Halmashauri ya Mji wa Bariadi<br>Manispaa ya Mji wa Moshi<br>Halmashauri ya Mji wa Geita<br>Halmashauri ya Mji wa Njombe<br>Halmashauri ya Mji wa Kahama<br>Halmashauri ya Mji wa Babati<br>Halmashauri ya Jiji la Dodoma<br>Halmashauri ya Wilaya ya Urambo | Taasisi za Fedha,<br>TCCIA,<br>SIDO,<br>NSSF,<br>TRA,<br>BRELA<br>UHAMIAJI<br>Ofisi za Ardhi |

**a) Urasimishaji wa Ardhi Vijijini na Mijini**

i. Wamiliki 526 wenye Hatimiliki za kimila wametumia hati kama dhamana na kupata mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 4.99. Aidha, vyama vitano (5) vya wakulima vimedhamini wakulima kupata mikopo ya thamani ya shilingi milioni 625.9;

ii. Wakulima 2,367 na viongozi 479 wa vyama vya ushirika na vikundi vya wakulima wamepata mafunzo ya kutumia Hati Miliki zao ili kupata mitaji kutoka katika Taasisi za fedha. Mafunzo haya yamefanyika katika Halmashauri 18 za wilaya ambazo ni Meru, Mwanga, Sumbawanga, Kalambo, Mbinga, Kilombero, Kilosa, Karagwe, Manyoni, Rungwe, Njombe, Ludewa, Misungwi, Mbarali, Tandahimba, Mufindi, Korogwe na Mpwapwa;

iv. Wamiliki 93 waliorasimisha viwanja vyao mjini wametumia hati miliki kupata mikopo ya thamani ya shilingi bilioni 3;

v. Wafanyabiashara 2,300 wamepata mikopo ya thamani ya shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya kuongeza mitaji biashara; na

vi. Kuongeza usalama na uhakika wa miliki za ardhi.

**b) Urasimishaji wa Biashara**

i. Wafanyabiashara 8,736 wamepata mafunzo ya jinsi ya kuendesha biashara zao;

ii. Wafanyabishara 1,173 wamejiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kama sehemu ya kujiwekea hifadhi ya uzeeni; na

iii. Wafanyabiashara 3,465 wamerasimisha na kusajili biashara zao na shilingi 510,995,400/= zimekusanywa na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro kutokana na kulipia leseni za biashara. Aidha, katika Halmashauri ya wilaya ya Urambo wafanyabishara 871 wamepata mafunzo, na wafanya biashara 79 wamesajiri biashara zao na Zaidi shiling 4,500,000/= zimekusanywa kwa njia ya leseni.

**c) Mafanikio kwa Taifa**

i. Kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji, kijiji na kijiji au majirani wanaopakana;

ii. Kuongeza thamani ya ardhi na tija ya uzalishaji wa mazao mbalimbali kutokana na kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi na hasa utekelezaji wa mipango kazi ya jamii;

iii. Kuongezeka kwa walipa kodi ambao wamerasimisha rasilimali ardhi na biashara;

iv. Wananchi kupata uelewa na kukubali kuchangia gharama za urasimishaji ambapo jumla ya Shilingi 151,694,364 zimechangwa na wananchi na kutumika kugharamia urasimishaji katika maeneo mengine kwenye Halmashauri zao;

v. Baadhi ya Halmashauri za Wilaya zilizojengewa uwezo kuanza kutekeleza zenyewe urasimishaji katika maeneo yao na kufanya urasimishaji kuwa endelevu. Halmashauri za wilaya 24 zimetekeleza urasimishaji ambapo jumla ya mashamba 18,394 yamepimwa katika vijiji 224 na kutoa hati za Hakimiliki za Kimila 13,034;

vi. Kuongezeka kwa wananchi wanaomiliki uchumi kwa kumiliki na kuendesha shughuli zinazotambulika kisheria; na

vii. Kuongezeka kwa taasisi zinazofanya urasimishaji ni alama ya watanzania wengi kuelewa umuhimu wa urasimishaji.

## 14.3. VITUO VYA UWEZESHAJI VILIVYOANZISHWA NA HALMASHAURI ZA WILAYA

Mikoa yote Tanzania Bara inapaswa kufungua vituo vya uwezeshaji kama njia moja wapo ya kuwasogezea huduma wananchi.Uwepo wa vituo hivi unaenda sambamba na utekelezaji wa baadhi ya nguzo ndani ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Ili kuhakikisha kuwa vituo vinafungulliwa, Baraza la Uwezeshaji lilitoa ushauri kwa Makatibu Tawala wa Mikoa kuhakikisha kuwa kila Mkoa unafungua angalau Kituo kimoja cha uwezeshaji huku wakiendelea kujipanga kufungua vituo katika kila Halmashauri. Kwasasa kuna jumla ya vituo 8 vilivyofunguliwa na Halmashauri ambavyo viko katika Mkoa wa Kigoma, Singida na Shinyanga. Vituo hivi vipo katika maeneo yafuatayo ya Wilaya:-

i. Mkoa wa Shinyanga: Halmashauri ya Mji wa Kahama
ii. Mkoa wa Singida: Manispaa ya Singida
iii. Mkoa wa Kigoma: KIGOMA MC, KAKONKO DC, KASULU TC, KIBONDO DC, BUHIGWE DC, UVINZA DC

## 14.4. TAARIFA YA KITUO CHA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI KAHAMA

Kituo cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Kahama (KEEC) kilifunguliwa tarehe18 Novemba, 2018. Kituo kipo Kata ya Nyihogo, Halmashauri ya Mji wa Kahama katika Mkoa wa Shinyanga. Kituo hiki kinaratibiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004.

Lengo kuu la kuanzishwa kwa kituo ni kuwezesha upatikanaji wa huduma mbalimbali za kiuchumi kwa wajasiriamali katika eneo moja. Miongoni mwa huduma zinazotolewa ni pamoja na urasimishaji wa biashara, ushauri wa kibiashara, elimu na mafunzo ya ujasiriamali, upatikanaji wa mitaji na masoko, teknolojia na ufundi, hifadhi za jamii na afya, na uanzishwaji wa vikundi vya kifedha vya kijamii na vyama vya ushirika vya akiba na Mikopo (SACCOS) n.k.

Taasisi zinazotoa huduma ndani ya kituo ni Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo(SIDO), SELF Microfinance Fund (SELF MF), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), GSI Tanzania Limited, PASS TRUST, Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (AGITF), Chemba ya Biashara, Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA), Benki ya Taifa ya Biashara (NBC (T) Ltd), na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA). Baraza la Uwezeshaji linaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuongeza wadau ndani ya kituo ili kufanikisha malengo yanayotarajiwa.

### 14.4.1. UTENDAJI WA KITUO

**Mahudhurio ya Wateja**


Kwa kipindi cha kuanzia Mwezi Julai, 2019 hadi Juni, 2020 kituo kimehudhuriwa na wananchi 2,923 ambapo kati ya hao wanawake walikuwa ni 1,286 ambao sawa na asilimia 44 na wanaume walikuwa 1,637 sawa na asilimia 56. Aidha, mahudhurio ya wananchi kwa wateja kwa kila robo mwaka yanaokana katika jedwali hapa chini:

**Jedwali Na. 31: Mahudhurio ya wananchi kwa wateja kwa kila robo mwaka**

| JINSIA | JUL-SEPT,2019 | OKT-DEC,2019 | JAN-MACH,2020 | APL-JUN,2020 | JUMLA | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Wanawake (Ke) | 99 | 407 | 497 | 283 | 1,286 | 44 |
| Wanaume (Me) | 114 | 355 | 725 | 443 | 1,637 | 56 |
| JUMLA | **213** | **762** | **1,222** | **726** | **2,923** | **100** |

Katika mchoro hapa chini inaonekana kituo kimekuwa kikipata watu wengi nyakati za miezi ya Oktoba mpaka mwezi Machi. Inawezekana kwa kuwa kipindi hicho shughuli za kilimo zinakuwa zimeongezeka na hivyo wananchi wanakuwa wanahitaji msaada wa shughuli zao wanazozifanya, aidha mikopo, pembejeo, ushauri, elimu na uchakaji wa mazao yao.

**Mchoro Na. 24: Idadi ya watu waliotembelea kituo cha uwezeshaji Kahama**



**Huduma zilizotolewa na Taasisi ndani ya Kituo**

Taasisi zilizondani ya Kituo zimefanikiwa kutekeleza majukumu yao kama ifuatavyo:-

**Mafunzo**

i. Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) limefanikiwa kutoa mafunzo kwa wajasiriamali 385 (ke-241:me-144) katika maeneo ya Usindikaji vyakula, ujasiriamali na masoko, urasimishaji biashara, stadi za ujasiriamali, menejimenti ya masoko, stadi za usimamizi wa biashara, menejimenti ya mikopo, na huduma kwa wateja;
ii. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kimetoa mafunzo kwa wajasiriamali 91 (Ke-455: M-46) katika eneo la menejimenti ya biashara.
iii. Chuo cha Mafunzo na Elimu ya Ufundi Stadi (VETA) kimetoa mafunzo kwa wananchi 160 (Ke-82: Me -78 ) katika maeneo ya Udereva, Mapambo, Ujasiriamali, Kuendesha Mitambo, Saluni, Kompyuta, Uchomeleaji, Ushonaji, Ufundi Mitambo;
iv. Mfuko wa Pembejeo wa Taifa (AGITF) umetoa mafunzo juu ya utaratibu wa kupata mikopo, vigezo, kuunda vikundi na kuandika maandiko ya miradi kwa wananchi 231 (Ke-91: Me:140); na
v. TCCIA imetoa mafunzo kwa wanawake 30 katika eneo la utafutaji wa masoko.

**Urasimishaji**

i. SIDO imefanikisha urasimashaji kwa Wananchi 12 (Ke- 5 : Me-7) katika eneo la usajili wa biashara na viwango vya ubora;
ii. MKURABITA imefanikisha urasimishaji wa biashara za wajasiriamali 630 (Ke-109: Me-521 )na kupima viwanja vya wananchi 19 (Ke-6: Me-13); na
iii. TCCIA imefanikisha urasimishaji wa leseni, usajili na ubora wa bidhaa kwa wajasiriamali 38(Ke-14:Me-24).

**Kuwaunganishwa na Fursa**

i. SIDO imewaunganisha wajasiriamali 63 na kufanikiwa kununua mashine mbalimbali za uzalishaji kama kama vile: Mashine za kupaki bidhaa, Mashine za kunawa mikono, Mashine za kutengeneza *peanut butter*, Mashine za kutengeneza mkaa, Mashine za usindikaji wa vyakula, Mashine za kufyatulia matofali, Tenki za kutunzia maziwa, Mashine za kutengeneza sabuni na Mashine za kutotoleshea vifaranga.
ii. Mfuko wa Pembejeo wa Taifa umeunganisha wajasiriamali 48 (Ke-35:Me-13) waliokatika kukundi na wanaojishughulisha na kilimo cha bustani katika Benki ya NMB kwa ajili ya kupata mkopo; na
iii. TCCIA imewaunganisha wajasiriamali 38(Ke-17:Me-21) na Taasisi za Brela, TBS, SELF MF na NEMC.

**Huduma ya ushauri wa Biashara**

i. Mfuko wa Pembejeo wa Taifa umetoa ushauri wa biashara kwa wajasiriamali 240 (Ke-160:Me-60) katika kilimo cha mbogamboga na matunda pamoja na usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo
ii. SIDO imetoa ushauri kwa wananchi 498 (Ke-254:Me-244) katika maeneo ya upatikanaji wa malighafi za sabuni, maziwa, viungo, na vifungashio, kuanzisha biashara na viwanda, kurasimisha biashara (TIN, Leseni, Brela & TBS), kutafuta masoko, kupata mashine na vifaa vingine,utunzaji wa kumbukumbu na huduma za Taasisi
iii. TCCIA imetoa ushauri kwa wajasiriamali 145 (Ke-254:Me-244) katika maeneo ya utunzaji wa kumbukumbu za biashara na urasimishaji wa biashara

**Mitaji**

Tangu kituo kianzishwe, kimefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 20.5 kwa wananchi 2,241 ambapo kati ya hao wanawake ni 978 ambao ni sawa na asilimia 44 na wanaume ni 1263 sawa na asilimia 56.

## 14.5. VITUO VYA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI KWENYE MIKOA MINGINE

### 14.5.1. KITUO CHA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI BUHIGWE

Halmashauri ya Buhigwe ina tarafa mbili za Manyovu na Muyama na ina jumla ya kata 20, Vijiji 44 na vitongoji 192. Halmashauri hii ilianza ujenzi wa Kituo cha Uwezeshaji Mwezi Januari 2019 chini ya ufadhili wa shirika la ITC ambao walitoa kiasi cha Tsh. 63,194,010, aidha katika ujenzi huo. Halmashauri ilichangia Shilingi 3,038,000 ambayo ni thamani ya kiwanja kilichotolewa katika Kitalu ‘’A’’ Bwega Na 70. Ukubwa wa eneo la kiwanja hicho ni Mita za Mraba 3,038. Kiwanja hiki kipo Karibu na Ofisi za Halmashauri ya Wilaya.

Lengo la uanzishwaji wa Kituo ni kutoa huduma kwa vijana kutoka katika Kata 44 na Vijiji 44 vya Halmshauri ya Wilaya ya Buhigwe. Kituo kinajumuisha Ukumbi mdogo wa mikutano, Ofisi ya Afisa vijana na Ukumbi kwa ajili ya semina mbalimbali.

**Malengo mahsusi ya Kituo ni:**

i. Kutoa mafunzo ya ujasilimali kwa vitendo kwa vijana kutoka katika maeneo mbambali ya Wilaya ya Buhigwe;
ii. Kutoa mafunzo ya stadi za maisha kwa vijana na elimu ya afya ya uzazi kwa vijana na jinsi ya kukabiliana na changamoto za ujana;
iii. Kutoa mafunzo ya namna ya urasimishaji wa Biashara kwa vijana;
iv. Kuibua fursa mbalimbali za vijana katika Halmashauri ya Wilaya na kutoa ushauri kwa vijana wenzao na namna ya kuchangamkia fursa hizo;

v. Kuhamasisha vijana kushiriki katika michezo mbalimbali ili kukuza vipaji vya michezo na afya kwa vijana katika maeneo ya kutoa elimu mtambuka kama vile Mafunzo ya kijinsia, uhifadhi wa Mazingira, Mapambano dhidiya VVU/ UKIMWI kwa vijana;
vi. Vijana kubadilishana uzoefu Kupata taarifa mbambali zinazohusu vijana na fursa zilizopo kutoka serikalini na Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali; na
vii. Kuainisha mazao yanaweza kuongezewa thamani ili kuongezea mapato kwa vijana na kupendekeza uanzishajiwa viwanda vidogo vya kuchakata mazao yao.

**HUDUMA ZINAZOTOLEWA NDANI YA KITUO**

Kwa sasa kituo hiki hakijaanza kutoa huduma kwa kuwa kipo katika hatua ya umaliziaji wa milango, madirisha na ununuzi wa thamani. Huduma zitakazotolewa pindi kituo kikikamilika ni pamoja na kuhamasisha vijana kujiunga katika vikundi na kuchangamkia fursa mbalimbali za kiuchumi, kutoa mafunzo ya kilimo bora kwa vijana na fursa zilizopo katika kilimo, mafunzo ya ujasiliamali, mafunzo ya stadi za maisha kwa vijana, kutoa mafunzo mtambuka ya kijinsia, uhifadhi wa mazingira, mapambano dhidi ya VVU/Ukimwi kwa vijana.



*Ujenzi wa kituo cha Vijana Halmashauri ya wilaya ya Buhigwe.*

## 14.5.2. KITUO CHA UWEZESHAJI WANANCHI KIBONDO

Kituo cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Kibondo ni kituo kinachoratibiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004.

Madhumuni ya makuu ya kuanzishwa kwa kituo ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa huduma mbalimbali za kiuchumi kwa Wajasiriamali katika eneo moja. Taasisi zinatoa huduma

ndani ya Kituo hiki ni TRA, TMDA, Ardhi na Kitengo cha Biashara. Huduma zinazotolewa ni pamoja na:-

i. Urasimishaji wa Biashara;
ii. Ushauri wa Kibiashara;
iii. Elimu na Mafunzo ya Ujasiriamali;
iv. Upatikanaji wa Mitaji na Masoko;
v. Hifadhi za Jamii na Afya; na
vi. Uanzishwaji wa vikundi vya kifedha vya kijamii na vyama vya ushirika vya akiba na Mikopo (SACCOS) n.k.

**UTENDAJI WA KITUO**

i. Kwa kushirikiana na SIDO, Kituo kimefanikiwa kutoa mafunzo katika maeneo ya Kilimo bora cha matunda na mbogamboga, usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo kwa wananchi 55 ambao kati ya hao wanawake ni 40 na Wanaume walikuwa 15;
ii. Kituo kimetoa ushauri wa biashara kwa wananchi 277 ambao kati ya hao wanawake walikuwa 172 na wanaume 105. Ushauri huo umetolewa katika eneo la Utaratibu wa jinsi ya kupata malighafi za sabuni, maziwa, viungo na vifungashio, utaratibu wa kuanzisha biashara na viwanda, utaratibu wa kurasimisha biashara (TIN, Leseni, Brela & TBS), Masoko, Teknolojia na Ufundi, utunzaji wa kumbukumbu;
iii. Kituo kimetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 35,127,045.22 kwa wajasiriamali 120 miongoni mwa wao wanawake ni 90 na wanaume 30; na
iv. Taasisi zilizo katika kituo zimeendelea kutoa huduma za ushauri wa biashara kwa wananchi wanaokuja kutembelea kituo.

### 14.5.3. KITUO CHA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI KAKONKO

Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko inatumia kituo cha uendelezaji biashara kwa ajili ya kutoa huduma za Uwezeshaji kwa wananchi, aidha Kituo hiki kitaendelea kutoa huduma hiyo hadi Halmashauri itakapofanikiwa kujenga Ofisi maalumu itakayotumika kwa ajili ya kazi hii. Ofisi zinazotoa huduma katika kituo hicho ni Ofisi ya biashara, Ofisi ya TRA, Ofisi ya ardhi na Ofisi ya Uhamiaji.

**HALI YA JENGO LA KITUO**

Kituo hiki kina jumla ya vyumba vitano (5) ambavyo vyote vinatumiwa na wadau mbalimbali kama ofisi kwa ajili ya kutolea huduma. Lengo kuu la kuanzishwa kwa kituo hiki ni kuwezesha upatikanaji wa huduma mbalimbali za uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa Wajasiriamali katika eneo moja. Miongoni mwa huduma zinazotolewa ni pamoja na hizi zifuatazo katika jedwali hapa chini:-

**Jedwali Na. 32: Huduma zinazotolewa na kituo cha Uwezeshaji Kakonko**

| HUDUMA ZA KIBIASHARA | HUDUMA ZA ARDHI | HUDUMA ZA UHAMIAJI |
|---|---|---|
| i. **Urasimishaji wa Biashara**<br>ii. **Ushauri wa Kibiashara**<br>iii. **Elimu na Mafunzo ya Ujasiriamali**<br>iv. **Upatikanaji wa Mitaji na Masoko**<br>v. **Elimu ya kodi**<br>vi. **Malipo ya Kodi**<br>vii. **Teknolojia na ufundi**<br>viii. **Elimu ya afya na Jamii**<br>ix. **Uanzishwaji wa vikundi vya kifedha vya kijamii na vyama vya ushirika vya akiba na Mikopo (SACCOS).** | i. Utoaji wa vibali vya ujenzi<br>ii. Upatikanaji wa Hati miliki za Ardhi<br>iii. Upimaji wa Ardhi | i. Upatikanaji wa vibali vya kusafiri nje ya Nchi<br>ii. Upatikanaji wa huduma zingine muhimu za Uhamiaji |

## MIPANGO YA BAADAYE

Ili kuimarisha utendaji kazi wa kituo, ipo mipango inayotarajiwa kutekelezwa katika siku za usoni kutegemeana na hali ya bajeti, mipango hiyo ni pamoja na:-

a) Kuwakaribisha wawekezaji/wajasiriamali watakaojenga mabanda ya biashara ndani ya kituo ili kuchangamsha kituo pamoja na kukitangaza;
b) Kuwa na maonesho ndani ya kituo yatakayowarahisishia fursa ya masoko wajasiriamali na pia ni fursa ya kukitangaza kituo; na
c) Kukitengenezea taswira nzuri kituo ili kiweze kuwa kituo cha mfano kwa vituo vingine vya uwezeshaji.

### 14.5.4. KITUO CHA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI KASULU

Kituo cha Biashara cha Wilaya "One Stop Bussiness Centre" kimejengwa katika mtaa wa Kimobwa kata ya Kimobwa, Halmashauri ya mji wa Kasulu. Kituo kimejengwa kwa ufadhili wa mradi wa LIC ikishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu pamoja na Halmashauri ya mji wa Kasulu kwa gharama ya kiasi cha Tsh. 49,977,177.61 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004.

Lengo kuu la kuanzishwa kituo ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa huduma mbalimbali za kiuchumi kwa Wajasiriamali katika eneo moja. Kituo cha kibiashra cha Kasulu kilianza kutoa huduma kwa wateja tangu tarehe 1 Desemba, 2018. Miongoni mwa huduma zinazotolewa kwa sasa kupitia kitengo cha biashara ni pamoja na Urasimishaji wa Biashara na Ushauri wa Kibiashara.

**MIPANGO YA KUBORESHA HUDUMA KATIKA KITUO**

Ili kuimarisha utendaji kazi wa kituo, ipo mipango inayotarajiwa kutekelezwa katika siku za usoni kutegemeana na hali ya bajeti, mipango hiyo ni pamoja na:-

i. Kuwakaribisha wawekezaji/wajasiriamali watakaojenga mabanda ya biashara katika maeneo ya kimkakakti ya uendelezaji wa biashara.
ii. Kuwa na Maonesho ya kiwilaya yatakayoratibiwa na kituo ili kutangaza fursa ya masoko kwa wajasiriamali na pia ni fursa ya kukitangaza kituo; na
iii. Kukitengenezea kituo kuwa na taswira ya ushindani katika utoaji wa huduma.

### 14.5.5. KITUO CHA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI UVINZA

Kituo cha uwezeshaji wananchi kiuchumi kilianzishwa mwaka 2017/2018 kama kituo cha biashara ambacho kilijengwa kwa ufadhili wa Mradi wa Local Investment Climate (LIC) kwa kushirikiana na Halmashauri. Kwa sasa kituo kinatumika kuratibu shughuli za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004.

Lengo la kuanzisha kituo hiki ni kuwezesha upatikanaji wa huduma mbalimbali za kiuchumi kwa Wananchi ambao ni wajasiriamali na wafanya biashara katika eneo moja. Taasisi zinazotoa huduma ndani ya kituo ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)**,** Ofisi ya Biashara Wilaya (DTO)**,** Tanzania Chamber of Commerce Investment and Agriculture (TCCIA) na Uhamiaji. Kituo hiki kinafanya kazi zifuatazo:-

Uhamasishaji wa uwezeshaji wa maarifa ya Biashara

i. Ushauri wa Biashara
ii. Upatikanaji wa huduma za biashara na huduma zingine kwa wakati mmoja
iii. Elimu ya ujasiriamali
iv. Elimu na kutoa vibali vya kusafiria nje na kusafirisha bidhaa nje ya nchi
v. Kutoa hati mbalimbali ambazo ni Leseni za biashara, TIN namba za mlipa kodi.
vi. Kusaidia wafanya biashara na wajasiriamali kupata mwenendo wa masoko ya bidhaa zao.
vii. Elimu ya uanzishaji na uendeshaji wa vikundi vya kiuchumi pamoja na mikopo ya aslimia 10 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

**UTENDAJI WA KITUO**

i. Kuanzia mwezi Aprili-Juni, 2020 kituo kimetembelewa na Wananchi 64 ambapo kati ya hao wanawake walikuwa ni 42 na wanaume 29
ii. Kutokana na kuwepo kwa kituo mafunzo mbalimbali yalitolewa katika kipindi hiki nayo ni kama ifuatavyo:

**Jedwali Na. 34: Mafunzo mbalimbali yalitolewa na Kituo cha Uwezeshaji Wananchi Uvinza**

| MAFUNZO YALIYOTOLEWA | MADHUMUNI YA MAFUNZO | TAREHE YA MAFUNZO | TAREHE YA MAFUNZO | | MAHALI |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | ME | KE | |
| ❖ **Ufugaji bora na unenepeshaji wa mifugo, uzito wa mifugo uanaofaa**<br>❖ **Sheria na taratibu za usafirishaji wa mifugo na haki za mifugo.**<br>❖ **Taratibu za kulipia leseni,tozo na ushuru.**<br>❖ **Huduma zinzotolewa na kituo cha Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.** | ❖ Kuwezesha ufugaji bora wa kibiashara , kuwa na mifugo inayohimili ushindani wa soko kwenye minada.<br>❖ Kujenga uelewa juu ya kulipia leseni, tozo na ushuru kwa wafanya biashara wa mifugo hai, bidhaa na wajasiria mali wa bidhaa mbalimbali. | 05/05/2020 | 15 | 2 | Eneo la Mnada - Mwamila |
| | | 30/05/2020 | 32 | 6 | Eneo la Mnada - Mpeta |
| | | 18/06/2020 | 28 | 31 | Eneo la Mnada - Uvinza. |
| **Uvuvi endelevu, uchakataji , ufungashaji na taratibu za usafirishaji wa mazao ya uvuvi/samaki /dagaa ndani na nje ya Wilaya.** | ❖ Kuwa mazao ya uvuvi mengi yenye ubora kwa mlaji na kuhimili ushindani wa soko na kushiriki maonesho ya Nane Nane<br>❖ Kulipia leseni,ushuru na tozo zilizopo kisheria kuepuka usumbufu. | 11/06/2020 | 8 | 7 | Kijiji cha Ndele |
| | | 12/06/2020 | 8 | 7 | Kijiji cha Kaparamsenga |
| | | 14/06/2020 | 8 | 7 | Kijiji cha Sibwesa |
| | | 17/06/2020 | 8 | 8 | Mtegowanoti |
| **Elimu ya uuzaji wa mazao ya kilimo kwa pamoja kwa vikundi vya wakulima .** | ❖ Kuimarisha upangaji wa bei na kumiliki soko ili kupata faida.<br>❖ Kuuza kwa kuzingatia vipimo kuepuka( lumbesa). | 01 /04/2020 | 15 | 35 | Kata ya Kandaga |
| | | 02/04/2020 | 15 | 35 | Kata ya Kazuramimba |
| | | 03/04/2020 | 15 | 35 | Kata ya Basnza |

iii. Kituo kimetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi 53,000,000/= kwa vikundi 9 vya Wanawake, Vijana na Watu wenye ulemavu, kutokana ya 10% ya fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri.

iv. Kujitokeza kwa wananchi kupata uelewa, ushauri na huduma nyingine za kiuchumi.

v. Urahisi wa upatikanaji wa hati za mlipa kodi (TIN) namba na Leseni za Biashara.

vi. Kupungua kwa gharama na muda wa ufuatiliaji wa huduma mbalimbali za ushauri na vibali kwa wateja. Wateja wanatumia muda mfupi kupata huduma kwa pamoja ambazo zilikuwa zinapatikana Mjini Kigoma.

vii. Wajasiriamali, wafanya biashara wamepata uelewa wa kuboresha bidhaa kwa kuzingatia ubora (uchakataji, ufungashaji na utangazaji wa bidhaa kwenye soko), hii imewazesha kupata soko, kushiriki Maonesho ya Nane Nane Kanda ya Tabora ambapo Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza imekuwa ya kwanza kwa Mkoa wa Kigoma.
viii. Wazalishaji wadogo wadogo na wajasiriamali wa chumvi wanauza chumvi yenye ubora iliyochanganywa na madini joto kwa kuzingatia vipimo.
ix. Wananchi wamepata uelewa na kujiunga katika vikundi vya kiuchumi, umoja wa uuzaji mazao ili kujiongezea kipato.
x. Wajasiriamali ambao ni wachakati wa mazao ya uvuvi na misitu kutoka kwenye vikundi na SACCOs walishiriki maonesho ya Nane Nane yaliyofanyika Kanda ya Tabora na kuibuka washindi wa kwanza katika Mkoa wa Kigoma.

**MPANGO WA KUBORESHA HUDUMA ZA KITUO**

i. Kuongeza wadau wengine ambao ni watoa huduma kama:
   a) Wakala wa Vipimo
   b) Maafisa ardhi kurahisisha huduma za urasimishaji wa ardhi zipatikane kwa urahisi.
   c) Afisa masoko watasidia kutangaza kutangaza bidhaa na kutafuta masoko ya mazao na bidhaa zinazopatikana katika Halmashauri ya Wilaya Uvinza
   d) Kuwa na ushirikiano na mawasiliano ya karibu na wadhibiti ubora wa bidhaa kanda ili kuwa na sauti moja .
   e) Kushirikiana na wadau wengine kama SIDO, SACCOs, Vikundi vya wafanyabiashara, wazalishaji wa mazao ya kilimo, wachakataji wa mazao ya misitu, kilimo, mifugo na uvuvi, Dawati la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Mkoa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.
   f) Kuboresha miundombinu na mtandao ya kituo kurahisisha utoaji wa huduma.
   g) Kuongeza samani zinazohitajika ndani ya kituo.

### 14.5.6. KITUO CHA UWEZESHAJI WANANCHI GEITA

Baraza la Uwezeshaji kwa kushirikiana na uongozi wa serikali ya Mkoa wa Geita liko mbioni kufungua Kituo cha Uwezeshaji Kiuchumi katika Halmashauri katika Mkoa wa Geita. Kituo hiki kinachofadhiliwa na Mradi wa Dhahabu Geita (GGML) kitafanya kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama SIDO, TTCIA, GS1, Taasisi za fedha MKURBITA, TRA, BRELA, NSSF, NHIF nk ili kuhakikisha kuwa malengo ya Mwongozo yanatima. Hata hivyo taasisi zinaweza kuongezeka zaidi ya zilizotajwa awali kutokana na mahitaji ya wakati huo.

Lengo ni kutoa elimu ya Uwezeshaji kama utunzaji wa Kikomo, Urasimishaji, Ujuzi na Elimu ya Vikundi na Ushiiriki kwa wafanyabiashara Mkoani Geita ili waweze kuwa na sifa za kushindania katika biashara na shughuli za kiuchumi.

Aidha, Baraza la Uwezeshaji limeingia Mkataba na Taasisi ya GGML tarehe 10 Julai, 2020 kwa ajili ya kuwajengea uwezo wafanyabiashara ili wawe na sifa ya kushinda zabuni zitolewazo na GGML. Makubaliano haya yatatekelezwa kwa kipindi cha mwaka mmoja tu.

**MKAKATI WA BARAZA KUIMARISHA UTENDAJI WA VITUO**

Baraza la Taifa la Uwezeshaji limeweka mkakati wa kuhakikisha kuwa malengo yaliyoanzishwa na vituo yanafikiwa:

i. Kuwajengea uwezo wadau wanatoa huduma ndani ya vituo juu ya dhana ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili waweze kuitekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji 2004;
ii. Kuvijengea uwezo vituo vya urasimishaji Ardhi na Uendelezaji Biashara vifanye kazi za Uwezeshaji wananchi kwa mujibu wa Mwongozo wa Uanzishwaji wa Vituo;
iii. Kupeleka Afisa mmoja katika kila Kituo cha Uwezeshaji kwa ajili ya kusimamia dawati la Uwezeshaji Kiuchumi pamoja na kuandaa taarifa za utendaji kwa kila kipindi, Aidha Afisa huyu atasimamia utekelezaji wa Mwongozo wa Uendeshaji wa Kituo;
iv. Kuhakikisha kuwa kila mdau anaandaa mpango wa mkakati wa utendaji kulingana na madhumuni ya taasisi yake kwa kuoanisha malengo ya uanzishwaji wa Kituo, aidha katika jukumu hili NEEC watasaidiana na Ofisi ya Halmashauri;
v. Kuhakikisha kuwa taarifa ya vipindi ya utendaji wa vituo vyote inaandaliwa kwa kushirikiana na wadau na kuwasilishwa katika mamlaka husika kwa kutolewa ushauri/maoni ama mapendekezo;
vi. Kukutana na Halmashauri zenye vituo vya Uwezeshaji ili kujadiliana kwa pamoja changamoto za vituo vyao na kuzitafutia suluhu;
vii. Kuratibu zoezi la upatikanaji wa watoa huduma ndani ya vituo; na
viii. Kuhakikisha kuwa vituo hivi vinatangazwa ili vifahamike na wananchi.

## 14.6. VITAMBULISHO VYA UJASIRIAMALI

Uanzishwaji wa Mpango wa Taifa wa Vitambulisho vya Wajasiriamali Tanzania, umesaidia sana kuondoa adha ya kutoza kodi nyingi zisizo na tija kwa wafanyabiashara wa hali ya chini. Vilevile umeondoa uonevu na vitendo vya rushwa kwa wafanyabiashara wadogo, ambapo kabla ya mpango huo vitendo hivyo vilikuwepo kwa kiasi kikubwa sana. Mpango huu umeboresha kuondoa tozo, kuwatambua idadi ya wafanyabiashara na wafanyabiashara wadogo kupata maeneo rasmi ya kufanyia biashara bila kubughudhiwa. Vilevile baadhi ya taasisi zimetumia mpango huu kama nyenzo ya kuweza kuwafikia wafanyabiashara hawa. Aidha mashirika na makampuni mbalimbali yameweza kutoa mikopo, mafunzo na kutengeneza programu nyingine za kuwasaidia zaidi. Mnamo Desemba 10 mwaka 2018, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais John Joseph Pombe Magufuli alizindua Mpango wa Vitambulisho 670,000 maalum kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo na kuagiza wakuu wa Mikoa na Wilaya zote Tanzania Bara kuvigawa ili kuboresha mazingira ya kazi ya wajasiriamali nchini.

Kuwatambua na kuwapatia vitambulisho maalum wafanyabiashara wadogo walio kwenye sekta isiyo rasmi kulikuwa na lengo la kumsaidia mjasiriamali anayeingiza fedha chini ya shilingi milioni 4 kwa mwaka na kutangaza gharama ya vitambulisho hivyo kuwa ni Sh. 20,000 tu kila mwaka kwenda Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) na kutosumbuliwa tena na taasisi hiyo hadi mwaka utakapoisha.

### MAFANIKIO

Mpango wa Taifa wa Vitambulisho vya Wajasiriamali Tanzania umeleta mafanikio makubwa sana hasa katika kuwatambulisha wafanyabiashara wadogo kwa serikali, wadau wa maendeleo, taasisi za fedha na jamii ya watanzania kwa ujumla. Vitambulisho hivi kwa sasa vinatumika kufahamu idadi ya wajasiriamali hapa nchini na katika kila mkoa na wilaya.

Vile vile taasisi za fedha zimebuni bidhaa za kifedha kusaidia maendeleo ya wajasiriamali ili waweze kupata au kuongeza mitaji yao kupitia vitambulisho hivi. Bidhaa ambazo zimebuniwa ni rafiki kwa wafanyabiashara hawa maana gharama za mikopo ni nafuu sana na nyingine hazina riba kabisa.





*(Baadhi ya wajasiriamali wa Wilaya ya Kigamboni wakijisajili na akaunti ya JIWEZESHE ya CRDB ili kupata mikopo kwa kutumia vitambulisho vya ujasiriamali)*

Wadau wengi wa maendeleo wametumia fursa hii kubuni miradi mbalimbali ya kuwaendeleza wajasiriamali hawa kwani saa hivi ni rahisi kuwatambua kwa idadi na shughuli wanazozifanya. Hivyo kupitia Mpango huu wa kitaifa sekta hii imewekwa katika mfumo mzuri na hivyo ni rahisi kuendelezwa.

Katika mwaka wa pili wa utekelezaji wa programu hii umekuwa mzuri zaidi na umezingatia uzoefu wa mwaka wa kwanza. Mikoa saba (7) imefikisha lengo la kugawa vitambulisho vyote vilivyopokelewa mkoani, ambapo mwaka uliopita hakuna mkoa hata mmoja ulioweza kufikisha lengo la kugawa vitambulisho vyote.

**Jedwali Na. 35: Mgawanyo wa vitambulisho vya ujasiriamali mpaka Machi 2020**

| MGAWANYO WA VITAMBULISHO | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Na** | **Mkoa** | **Vilivyopokelewa** | **Vilivyogawiwa** | **Mapato (Tsh.)** | **Ufanisi** |
| 1 | Arusha | 125,000 | 96,480 | 1,929,600,000 | 77% |
| 2 | Dar Es Salaam | 175,000 | 175,000 | 3,500,000,000 | 100% |
| 3 | Dodoma | 75,000 | 53,000 | 1,060,000,000 | 71% |
| 4 | Geita | 60,000 | 60,000 | 1,200,000,000 | 100% |
| 5 | Iringa | 12,500 | 12,500 | 250,000,000 | 100% |
| 6 | Kagera | 60,000 | 59,450 | 1,189,000,000 | 99% |
| 7 | Katavi | 60,000 | 29,217 | 584,340,000 | 49% |
| 8 | Kilimanjaro | 65,000 | 65,000 | 1,300,000,000 | 100% |
| 9 | Lindi | 65,000 | 35,324 | 706,480,000 | 54% |
| 10 | Manyara | 60,000 | 43,977 | 879,540,000 | 73% |
| 11 | Mara | 65,000 | 29,565 | 591,300,000 | 45% |
| 12 | Mbeya | 105,000 | 53,597 | 1,071,940,000 | 51% |
| 13 | Morogoro | 65,000 | 53,597 | 1,071,940,000 | 82% |
| 14 | Mtwara | 65,000 | 34,220 | 684,400,000 | 53% |
| 15 | Mwanza | 55,000 | 55,000 | 1,100,000,000 | 100% |
| 16 | Njombe | 60,000 | 44,728 | 894,560,000 | 75% |
| 17 | Pwani | 60,000 | 57,891 | 1,157,820,000 | 96% |
| 18 | Ruvuma | 60,000 | 53,166 | 1,063,320,000 | 89% |
| 19 | Shinyanga | 60,000 | 60,000 | 1,200,000,000 | 100% |
| 20 | Simiyu | 60,000 | 48,470 | 969,400,000 | 81% |
| 21 | Singida | 65,000 | 52,198 | 1,043,960,000 | 80% |
| 22 | Tanga | 35,000 | 27,736 | 554,720,000 | 79% |
| 23 | Kigoma | 60,000 | 45,716 | 914,320,000 | 76% |
| 24 | Rukwa | 60,000 | 22,000 | 440,000,000 | 37% |
| 25 | Songwe | 65,000 | 26,010 | 520,200,000 | 40% |
| 26 | Tabora | 55,000 | 61,000 | 1,220,000,000 | 111% |
| **Jumla** | | **1,752,500** | **1,354,842** | **27,096,840,000** | **77%** |




Katika utekelezaji wa mpango huu mwaka wa pili umekuwa wa mafanikio zaidi, kuanzia idadi ya mikoa iliyofikisha lengo ambayo imekuwa saba (7) kama ilivyoelezwa hapo juu. Vilevile vitambulisho vilivyotolewa mwaka huu vimekuwa pungufu baada ya kupata idadi kamili ya wajasiriamali, vitambulisho vimepungua kwa kiasi cha laki moja (100,000). Pamoja na upungufu wa vitabulisho fedha iliyokusanywa imekuwa zaidi mwaka huu kuliko mwaka jana kwa asilimia 35 (35%). Vilevile ufanisi katika ugawaji wa vitambulisho umekuwa zaidi mwaka huu ambapo vitambulisho vimegawiwa kwa asilimia 77 (77%) na mwaka jana ilikuwa asilimia 55 (55%).

| UCHAMBUZI | 2018/19 | 2019/20 |
|---|---|---|
| Idadi ya vitambulisho vilivyotolewa | 1,850,000 | 1,752,500 |
| Idadi ya vitambulisho vilivyogawiwa | 1,022,721 | 1,354,842 |
| Fedha zilizokusanywa | 20.4bn | 27.1bn |
| Mikoa iliyofikia lengo | 0 | 7 |
| Ufanisi katika ugawaji | 55% | 77% |

### 14.7. MIKOPO YA 10% YA HALMASHAURI

Mamlaka za Serikali za Mitaa zimefanya shughuli mbalimbali za uwezeshaji wananchi kiuchumi kupitia makusanyo ya mapato ya Halmashauri. Serikali kwa kutambua mchango wa makundi maalum ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kama kundi linalokabiliana na changamoto nyingi na linalohitaji kufanyiwa uwezeshaji ilifanyia marekebisho Sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa kupitia Tangazo la serikali Na 286 la 05/04/2019 sura ya 209 ambapo imetungiwa kanuni chini ya kifungu 37A (4) inayozitaka mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga 10% ya mapato yanayokusanywa kwenye vyanzo vya ndani vya mapato kwa ajili ya kutoa

mikopo kwa vikundi vilivyosajiliwa vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Na katika kutekeleza jukumu hili la uwezeshaji kwa mwaka wa fedha 2019/2020 jumla ya vikundi 1,696 vya vijana, vikundi 3,420 vya wanawake na vikundi 301 vya watu wenye ulemavu vilipatiwa mikopo yenye thamani ya Jumla ya Tshs **21,508,390,066.67** mpaka mwezi machi 2020 toka katika mikoa 17 iliyowasilisha taarifa ukilinganisha na kiasi cha shilingi **20,454,420,000** zilizokusanywa toka katika mikoa 26 kwa mwaka wa fedha 2018/19.

**Jedwali Na. 36: Idadi ya vikundi na jumla ya fedha zilizokopeshwa kwa kila Mkoa**

| | IDADI YA VIKUNDI VILIVYONUFAIKA | | | | KIASI CHA FEDHA ZILIZOTOLEWA |
|---|---|---|---|---|---|
| Na. | MKOA | VIJANA | WANAWAKE | WALEMAVU | |
| 1 | Arusha | 205 | 512 | 44 | 1,622,117,041.00 |
| 2 | Dar es Salaam | 433 | 1196 | 90 | 7,753,964,493.53 |
| 3 | Kilimanjaro | 91 | 268 | 12 | 866,932,694.00 |
| 4 | Lindi | 114 | 144 | 12 | 415,818,600.00 |
| 5 | Mtwara | 66 | 67 | 10 | 608,670,000.00 |
| 6 | Njombe | 18 | 30 | 2 | 1,056,994,717.00 |
| 7 | Iringa | 133 | 300 | 17 | 1,336,118,000.00 |
| 8 | Morogoro | 146 | 160 | 12 | 1,227,855,198.00 |
| 9 | Katavi | 26 | 29 | 4 | 364,200,000.00 |
| 10 | Kigoma | 38 | 110 | 11 | 486,777,822.00 |
| 11 | Singida | 9 | 31 | 1 | 122,000,000.00 |
| 12 | Geita | 53 | 105 | 11 | 622,000,000.00 |
| 13 | Shinyanga | 52 | 20 | 5 | 36,200,000.00 |
| 14 | Dodoma | 47 | 90 | 15 | 986,673,650.00 |
| 15 | Mbeya | 118 | 172 | 25 | 2,289,391,032.00 |
| 16 | Tanga | 17 | 29 | 5 | 191,329,915.36 |
| 17 | Pwani | 130 | 157 | 25 | 1,521,346,903.78 |
| | | | | | |
| JUMLA | | 1696 | 3420 | 301 | 21,508,390,066.67 |

*Jedwali hili linaonesha idadi ya vikundi na jumla ya fedha zilizokopeshwa kwa kila Mkoa*

## 14.8. UANZISHWAJI WA MASOKO NA VITUO VYA UNUNUZI WA MADINI UTANGULIZI

Masoko ya madini yameendelea kuanzishwa hususan katika maeneo yote yenye kuchimba madini hapa Tanzania kufuatia maagizo aliyoyatoa Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mhe, John Pombe Joseph Magufuli mnamo tarehe 9 Januari 2019 ili kuweza kuendeleza sekta ya madini na kunufaisha Watanzania pamoja na kuchangia ukuaji wa pato la Taifa. Uanzishwaji wa

masoko hayo pia umelenga kuondoa kero na changamoto mbalimbali zinazowakabili wachimbaji wadogo wa madini ikiwemo ukosefu wa masoko rasmi na ya uhakika ambao unasababisha utoroshaji wa madini na kuuza katika masoko yasiyo rasmi hivyo kusababisha Serikali kukosa mapato.

Serikali kwa kuhakikisha inaweka mazingira mazuri ya kibiashara kwenye sekta ya madini imefuta baadhi ya tozo ambazo zilikuwa ni kero kwa wafanyabiashara wa madini na wachimbaji wadogo zikiwemo kodi ya ongezeko la thamani (VAT) za asilimia 18 na kodi ya zuio ya asilimia 5 kwa wachimbaji wadogo.

## MASOKO YA MADINI NA VITUO VYA UNUNUZI WA MADINI MIKOANI

Kutokana na umuhimu wa masoko ya madini, Mikoa imefanya juhudi kubwa katika uanzishwaji wa masoko hayo ili kuweza kuondoa kero wanazozipata wafanyabiashara na wachimbaji wadogo wa madini na kutekeleza maagizo ya Mheshimiwa Rais. Hadi sasa jumla ya Masoko ya madini 31 yameanzishwa kwenye Mikoa 23, pia kuna jumla ya vituo vya ununuzi wa madini (Mineral Buying Centres) 38 vimeanzishwa ambavyo vinapatikana kwenye Mikoa 9. Majedwali hapo chini yanaonesha taarifa za masoko ya madini pamoja na vituo vya ununuzi wa madini vilivyoanzishwa.

**Jedwali Na. 37: Masoko ya madini yaliyoanzishwa**

| Na. | Jina la Soko | Wilaya | Mkoa |
|---|---|---|---|
| 1 | Soko kuu la Dhahabu Geita | Geita-Mjini | Geita |
| 2 | Soko la Dhahabu Kahama | Kahama | Shinyanga |
| 3 | Soko la Dhahabu Shelui | Iramba | Singida |
| 4 | Soko la Dhahabu Singida | Singida-Mjini | Singida |
| 5 | Soko la Dhahabu Chunya | Chunya | Mbeya |
| 6 | Soko la Dhahabu na Vito Songea | Songea | Ruvuma |
| 7 | Soko la Dhahabu na Almasi Shinyanga | Shinyanga Mjini | Shinyanga |
| 8 | Soko la Dhahabu Katavi | Mpanda | Katavi |
| 9 | Soko la Madini Kakonko | Kakonko | Kigoma |
| 10 | Soko la Dhahabu Tabora | Nzega | Tabora |
| 11 | Soko la Dhahabu Mara | Musoma | Mara |
| 12 | Soko la Dhahabu Madini Mbeya | Mbeya Mjini | Mbeya |
| 13 | Soko la Bati Kyerwa | Kyerwa | Kagera |
| 14 | Soko la Dhahabu na Almasi Mwanza | Nyamagana | Mwanza |
| 15 | Soko la Dhahabu Songwe | Songwe | Songwe |
| 16 | Soko la Dhahabu na Vito Iringa | Iringa | Iringa |
| 17 | Soko la Vito na Dhahabu Tanga | Tanga Mjini | Tanga |
| 18 | Soko la Mdini Njombe | Njombe | Njombe |
| 19 | Soko la Dhahabu Morogoro | Morogoro Mjini | Morogoro |
| 20 | Soko la Dhahabu Dodoma | Dodoma Mjini | Dodoma |
| 21 | Soko la Dhahabu Babati | Babati | Manyara |

| Na. | Jina la Soko | Wilaya | Mkoa |
|---|---|---|---|
| 22 | Soko la Dhahabu Mbulu | Mbulu | Manyara |
| 23 | Soko la Dhahabu Hanan'g | Hanan'g | Manyara |
| 24 | Soko la Vito and Dhahabu Tunduru | Tunduru | Ruvuma |
| 25 | Soko la Dhahabu na Vito Ruangwa | Ruangwa | Lindi |
| 26 | Soko la Vito na Dhahabu Mtwara | Mtwara Mjini | Mtwara |
| 27 | Soko la Vito Mahenge | Mahenge | Morogoro |
| 28 | Soko la Vito Arusha | Arusha Mjini | Arusha |
| 29 | Soko la Madini Same | Same | Kilimanjaro |
| 30 | Soko la Madini Moshi | Moshi | Kilimanjaro |
| 31 | Soko la Madini Dar es salaam | Ilala | Dar es Salaam |

## VITUO VYA UNUNUZI MADINI (MINERALS BUYING CENTRES)

### Jedwali Na. 38: Vituo vya ununuzi wa madini vilivyoanzishwa

| Na. | Jina la Kituo | Mkoa |
|---|---|---|
| 1. | Katoro | Geita |
| 2. | Nyarugusu | Geita |
| 3. | Nyakagwe | Geita |
| 4. | Bukombe | Geita |
| 5. | Chato | Geita |
| 6. | Mbogwe | Geita |
| 7. | Lwamgasa | Geita |
| 8. | Lusaunga | Biharamulo-Kagera |
| 9. | Maganzo | Shinyanga |
| 10. | Mwakitolyo | Shinyanga |
| 11. | Mwanubi | Shinyanga |
| 12. | Tarime | Mara |
| 13. | Nyamongo | Mara |
| 14. | Mwime | Kahama |
| 15. | Mwazimba | Kahama |
| 16. | Mwabomba | Kahama |
| 17. | Kakola | Kahama |
| 18. | Mkwajuni | Songwe |
| 19. | Saza | Songwe |
| 20. | Patamela | Songwe |
| 21. | Makongolosi | Chunya |
| 22. | Itumbi | Chunya |
| 23. | Mbingwa | Chunya |
| 24. | Mapogolo | Chunya |
| 25. | Igundu | Chunya |
| 26. | Shoga | Chunya |

| Na. | Jina la Kituo | Mkoa |
|---|---|---|
| 27. | Chalangwa | Chunya |
| 28. | Ifumbo | Chunya |
| 29. | Sinza | Chunya |
| 30. | Sangambi | Chunya |
| 31. | Matundasi | Chunya |
| 32. | Godima | Chunya |
| 33. | Mkinga | Tanga |
| 34. | Handeni | Tanga |
| 35. | Kilindi | Tanga |
| 36. | Namungo | Lindi |
| 37. | Kiegei | Lindi |
| 38. | Mafinga | Iringa |

## WASTANI WA WATEJA WANAOHUDUMIWA KATIKA MASOKO

Wateja katika masoko ya madini ni wafanyabiashara wenye leseni ndogo na kubwa za biashara ya madini nchini (Dealers and Brokers) ambao ni wastani wa wateja1,200 kila mwezi. Aidha, wachimbaji wadogo kote nchini ambao ni zaidi ya 50,000 wamepata fursa ya kuuza madini yao kila mwezi.

## MANUFAA YA KUANZISHA MASOKO YA MADINI

1. Masoko ya madini yamewezesha wachimbaji wadogo kupata soko la uhakika la madini kwakuwa soko la madini huwakutanisha wafanyabiashara (Wanunuzi wa ndani na nje ya nchi) pamoja na wachimbaji wadogo.

2. Wachimbaji wadogo (Small scale and Artisanal Miners) wanapata fursa ya kuuza madini kwa bei nzuri na elekezi kwakuwa Tume ya Madini inaratibu bei ya madini kwenye masoko na kuhakikisha wachimbaji wadogo wanapata mapato wanayostahiki.

3. Kuondoa tatizo la kupunjwa na kudhulumiwa kwa wachimbaji wadogo na wanunuzi wa madini ambao sio waaminifu kwa kuhakikisha vifaa vya kupimia uzito na ubora vinakuwepo na kutumika ipasavyo kwenye soko.

4. Kuokoa muda na gharama nyingine katika kuendesha biashara ya madini kwa kuhakikisha biashara zote muhimu zinakuwepo kwenye eneo moja zikiwemo TRA, Benki, Halmashauri, Tume ya Madini n.k.

5. Kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali hususan kodi na ushuru wa madini na kupelekea ukuaji wa uchumi wa nchi.

## CHANGAMOTO KWENYE MASOKO YA MADINI

Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana kutokana na uanzishwaji wa masoko ya madini, kumekuwa na changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikikabili uendeshaji wa masoko hayo kama ifuatavyo:-

**Jedwali Na. 39: Changamoto za masoko ya madini na mikakati ya kuzitatua**

| Na | Changamoto | Mikakati ya Kuzitatua |
|---|---|---|
| 1. | Kutokuwepo kwa baadhi ya miundombinu wezeshi kama vile majengo ya kudumu ya kufanyia biashara. | Kushirikiana na Mamlaka za Mikoa na Wilaya kuwezesha upatikanaji wa miundombinu wezeshi. |
| 2. | Elimu na uelewa mdogo wa kufanya biashara katika masoko rasmi ya madini kwa wachimbaji na wafanyabiashara wadogo wa madini. | Kuendelea kwa kampeni ya uelimishaji umma kuhusu umuhimu na faida za kufanya biashara za madini ndani ya masoko.<br><br>Kuendelea kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama kudhibiti uuzaji wa madini nje ya mfumo wa masoko. |

## MIPANGO YA BAADAE

Mikoa kwa kushirikiana na Tume ya madini inaendelea kuboresha masoko ya madini yaliyofunguliwa kwa kuhakikisha masoko yote yanakuwa na vifaa stahiki kwa ajili ya kuendesha shughuli za utoaji wa huduma katika masoko hayo. Ufunguaji wa masoko mapya katika maeneo mbalimbali nchini hutegemea uhitaji wa masoko hayo kulingana na kiwango cha uzalishaji wa madini katika eneo husika. Hadi kufikia sasa Mikoa yote nchini imeshaanzisha masoko ya madini yaliyopo kwenye maeneo mbalimbali; aidha, vituo vya ununuzi wa madini vimekuwa vikiendelea kufunguliwa katika maeneo mbalimbali ya uzalishaji ili kutoa nafasi ya masoko kwa wachimbaji wengi zaidi ambapo hadi sasa jumla ya vituo vya ununuzi 38 vimekwishafunguliwa. Masoko ya madini yataendelea kufunguliwa zaidi pale itakapoonekana kuna uhitaji wa huduma hiyo.

## 14.9. HADITHI ZA MAFANIKIO

### 14.9.1. MPUI SACCOS

Mpui SACCO Ilianza Kama kikundi cha akiba na mikopo kilichosajiliwa mwaka 2004 kikikusanya rasilimali pamoja na kusaidiana baina ya wanachama. Hata hivyo chama ambacho kilianza na wanachama 20 tu kimekuwa mfano wa kuigwa na kila mkulima katika wilaya ya Sumbawanga. Hadithi ya mafanikio ya Mpui SACCO ilianza mwaka 2016/2017 wakati umoja

ulipoanza rasmi kufanya shughuli za kilimo na kukopa kutoka taasisi za fedha kwa kupitia PASS Trust iliyowapatia dhamana za mikopo.




*Viongozi wa Saccos na maafisa kutoka taasisi ya PASS*

Mkopo wa kwanza kuchukuliwa na kikundi ambao ulidhaminiwa na PASS Trust ulikuwa ni TZS 396 Milioni kupitia Benki ya NMB ambao ulitumika miongoni mwa wanachama, kununulia pembejeo za kilimo na kujaribu kutumia teknolojia ya kisasa katika mashamba yao ili kuongeza uzalishaji.

*"Mahindi yetu hayakuwa yakiuzika, yaani, wanunuzi kamwe hawakutufikiria sisi wakati wowote kuja kununua mahindi yetu, na hii ni kwasababu tulikuwa tunafanya kilimo cha jadi kwa kutumia mbegu za kienyeji zilizotokana na mazao ya mwaka uliotangulia na pia sio kwa lengo la kuuza kwa kiasi kikubwa"* anasema Semeni John, Meneja wa chama.

Baada ya kuunganishwa na benki kwa kupitia PASS Trust, wanachama waliamua kubadilisha mtindo wao wa kilimo na kuanza kutumia mbinu bora na za kisasa kwenye kilimo. Hayo yaliwezekana baada ya kupatikana kwa mikopo ya pembejeo za kilimo ikiwa ni pamoja na mbegu bora na mbolea katika mashamba, vilevile kuhudumia mashamba yao kwa wakati hivyo basi uzalishaji wao kuboreshwa na kuanza kulenga wanunuzi wakubwa wa mahindi.

*"Kabla ya kufikiwa na fedha hizi, wanachama wetu walikuwa wakipata magunia 3-4 ya mahindi kwa ekari, sasa tunafurahi kwamba kwa ekari hiyo hiyo sasa inatupatia magunia 15-20" anaongea Semeni".*

Kutokana na sababu ya faida hizi, kundi hilo limeongeza wanachama wake kutoka wanachama wa mwanzo 270 hadi wanachama 1,131 katika kipindi cha miaka miwili.

*"Watu wote hawa wamevutiwa na mikopo ya pembejeo ambazo sisi tumepata kupitia dhamana ya PASS Trust, kwasababu bila ya dhamana ya PASS Trust kusimama na sisi, isingekuwa rahisi kwa sisi kupata mikopo"* anasema James Paulo, Meneja Msaidizi.

James Mwanakato mwenye umri wa miaka 31,ambaye ni afisa mikopo wa kikundi anasema ana furaha kwamba vijana sasa wanafika kwake kwa ajili ya ushauri wa kilimo na matumizi ya mikopo pamoja na malipo.

*"Wanakuja nyumbani kwangu kuona kile ambacho nimekuwa na uwezo wa kukifanya kwa kutumia matunda ya mkopo wangu. Nimeweza kununua mbuzi, nimeongeza ng'ombe, nimejenga nyumba kwa ajili ya familia yangu naishi kwa starehe nimeachana na kupanga. Siku hizi tunakula na kubakiza kuwatupia kuku mabaki wakati kabla ya hapo ilikuwa vigumu kuwa na milo mitatu kwa siku"* anasema Mwanakato.

Ukiacha faida zipatikanazo kwa mwanachama mmoja mmoja, kikundi nacho kimeweza kujenga ofisi iliyokamilika pamoja na samani na kuwa na kitengo cha kompyuta na kompyuta ambazo zinahifadhi taarifa zao. Pia kikundi kimekuwa na uwezo wa kuajiri wafanyakazi 10 kushughulikia kazi zao za kila siku kwa kuwa zinazidi kupanuka kila siku.

*"Infact, tuna wafanyakazi 10 wa kudumu hapa, lakini pia tuna zaidi ya watu 100 ambao wanafanyakazi zetu za shamba. Hii inamaana kwamba tuna familia zaidi ambazo zinafaidika moja kwa moja kutoka kwetu"* anasema Hesroni Mwakajoka, mwenyekiti wa kikundi.

*"Kutokana na maendeleo yetu kupitia shirika la PASS Trust, tumeweza hata kuwavutia mashirika mengine kufanya kazi na sisi na pia kuaminika na taasisi za fedha ambao sasa wanaomba sisi kukopa kwao wakati kabla ya msaada hapakuwa na taasisi ya fedha iliyokuwa tayari kwa ajili ya kutupa mkopo"* anasema Semeni John.

SACCOS imeweza kupata mikopo katika awamu tatu sasa na kuwapatia mikopo wanachama wake na inaendelea kuvutia taasisi za fedha kwa sababu ya uwezo wake wa kulipa mikopo yao ndani ya muda kwa usimamizi imara wa viongozi bora.

### 14.9.2. JACKMA ENTERPRISES CO. LTD (JACKSON MASSAWE)

Bw. Jackson Massawe alianza kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti akiwa na mtaji wa Tshs 2,500,000 akiwa nyumbani kwake Area C. Dodoma. Alipata mafunzo ya usindikaji vyakula mwaka 2008 ambapo mara baada ya kupata mafunzo aliunganishwa kwenye mradi kwa kuwezesha wajasiriamali maarufu kama Business Development Gateway (BDG) na kufanikiwa kupewa mtaji wa Tshs 4,800,000. Mtaji huu ulimsadia kununua mashine nzuri ya kukamua alizeti na kisha kuboresha ubora wa mafuta yake.

SIDO Dodoma, iliendelea kumwezesha kifedha kwa kumkopesha mkopo wa Tshs 2,500,000 kutoka mfuko wa NEDF kwa ajili ya kuwezesha kununua malighafi kama alizeti na hadi sasa anaendelea kukopa.

Mpaka sasa Bw Jackson Massawe amefanikiwa kuendesha kiwanda chake na kukifikisha kwenye thamani ya zaidi ya Shilingi milioni 200 kutokana na uwezeshaji kutoka SIDO Dodoma katika nyanja za mafunzo, ushauri na mikopo.



*Kiwanda kipya alichojenga na gari ya kusambazia mafuta.*



*Bw Jackson Masawe akiwa ndani ya kiwanda kipya cha kukamua alizeti*

### 14.9.3. MJASIRIAMALI TUNGU MABULA MUJENGELA

Tungu Mabula Mujengela ametoka kwenye familia ya Mzee Mabula Mujengele, Kijiji cha CHIBISO Wilaya ya IGUNGA Mkoa wa TABORA, ni mtoto wa kwanza kwenye familia ya Mzee Mabula. Baada ya kumaliza masomo yake ya msingi mnamo mwaka 1989 katika shule ya msingi IMARAIHAYO, hakuweza kuendelea na masomo ya sekondari kutokana hali ya Wazazi wake kushindwa kumudu gharama za masomo ya sekondari, hata hivyo aliona kwamba haikuwa kikwazo kwake kufanikiwa katika maisha, ndipo mnamo mwaka 2014 aliondoka TABORA na kuja Singida kwa ajili ya kutafuta maisha. Alianza biashara ya kununua na kuuza mazao na hasa mpunga ambao alikuwa anaukoboa kwenye viwanda vya wafanya biashara wengine.

Mnamo mwaka 2015 alifanikiwa kupata Mkopo wa Tshs. 2,000,000 kutoka mfuko wa NEDF, mkopo huo ulimsaidia kuanzisha kiwanda kidogo (mashine ya kukoboa mpunga) na kuuza mchele. Ndoto zake za kuwa na kiwanda kikubwa zilianza kuonekana baada ya kukopeshwa na SIDO mkopo mkubwa wa Tshs.5,000,000/=, ambapo kwa kutumia mkopo huo wa SIDO pamoja na akiba aliyokuwa nayo aliweza kununua mashine nyingine kubwa yenye uwezo wa kuweka mchele kwenye daraja zuri. Mkopo huo aliulipa vizuri.

Baada ya kuona maendeleo hayo ya Tungu Mabula Mujengela, SIDO Singida ikaona ni vizuri kumuendeleza zaidi, ndipo SIDO Singida – ikampa mkopo mkubwa zaidi kupitia programme ya SIDO/CRDB CGS ambapo mnamo mwaka 2017 mwezi wa Novemba alipatiwa mkopo wa Tshs. 40,000,000/= Mkopo huo uliweza kutimiza ndoto ya Tungu Mujengela.

Kwa sasa Tungu Mabula Mujengela anauwezo wa kuuza mchele kwa wakazi na Itigi na Manyoni. Pia anatoa huduma ya kuwakoboleshea mpunga kwa wafanya biashara wengi wa mchele ambao hawana mashine ya kukoboa mpunga huduma ambayo anayoitoa kwa wakazi wa Itigi, Mitundu, Sanjaranda, Kitalaka pamoja na wilaya ya Babati.

Kupitia viwanda vyake vitatu vya kukoboa mpunga, Tungu Mabula Mujengela ameweza kununua, nyumba tatu za kisasa mjini Singida, anasomesha watoto shule za sekondari na pia maisha yake yameboreshwa sana. Tungu Mabula Mujengela anaishukuru SIDO Singida kuifikisha ndoto yake ya kuwa milionea.



*Bw. Tungu Mabula akiwa katika kiwandani kwake mjini Singida*

### 14.9.4. BI KIJA MASUNGA

Bi Kija Masunga alipata mkopo kutoka SACCOS ya Magoma iliyoko Wilaya ya Kahama iliyowezeshwa na Mfuko wa SELF. Mkopo huu ulimsaidia kuongeza mauzo ya biashara yake ya dagaa, kupanua biashara kwa kukodisha chumba kikubwa na kuweza kuajiri wafanyakazi wa kudumu.

Kabla ya kupata mkopo kutoka Magoma SACCOS, Bi. Kija Masunga alikuwa anaendesha biashara yake ya kuuza dagaa eneo la nje ya kibaraza. Kuimarika na kupanuka kwa biashara yake kumemsaidia kuongeza mauzo yaliyomwezesha kulipa ada za shule kwa watoto wake hadi ngazi ya chuo kikuu pamoja na kununua ardhi kwa ajili ya kilimo.




### 14.9.5. BWANA AYUBU MULIMU

Bwana Ayubu Mulimu ni mwanachama wa CAGO SACCOS Magoma iliyoko Wilaya ya Kahama iliyowezeshwa na Mfuko wa SELF. Alifanikiwa kupata mkopo uliomsaidia kununua mashine kubwa ya kukata magogo, kupanua biashara kwa kununua magogo yake na kuajiri wafanyakazi sita wa kudumu.

Kabla ya kupata mkopo kutoka CAGO SACCOS, Bwana Mulimu alikuwa akiendesha biashara hiyo kwa faida ndogo kutokana na uwezo mdogo wa mashine wa kukata magogo. Hivyo mkopo ulimuwezesha kupata mashine yenye uwezo mkubwa na mtaji wa kununua magogo yake mwenyewe. Kupitia mradi huu amefanikiwa kuboresha makazi yake na kumudu majukumu ya kifamilia kama kusomesha watoto, chakula, mavazi na matibabu pamoja na kuuza mbao.



## 15.0. UWEZESHAJI WA VODACOM KWA WATANZANIA



## 15.1. Matokeo katika Jamii





**2,884,435**

Jumla ya wanufaika wa moja kwa moja na wengineo



**19**
Mikoa




**2513**

Ushiriki wa washirika kupata taarifa jumuishi za kifedha na pesa



**60,023**
Upatikanaji wa Shule za papo hapo kitaifa



**291**

Upatikanaji wa Kilimo kwa Vianzio vya mitaji na uendelezaji wa ujuzi

**40,055**
Wanufaika waliofikiwa kupitia Michango






**5577**
Wasichana waliowezeshwa Lindi

**11,841,381,072**

Jumla ya Uwekezaji wa Vodacom Tanzania Foundation kwa jamii




**68,809**

Idadi ya wanufaika wa moja kwa moja



**81.2%**
Uwasilishaji chanya wa matokea kwa jamii



## 15.2. Matokeo ya shughuli za Kikanda


Vodacom Tanzania Foundation inashirikiana na asasi husika nchini Tanzania kutatua baadhi ya changamoto zinazoikabiri jamii. Tunafanya kazi katika mikoa yote Tanzania kupitia miradi ya muda mfupi, hatahivyo, kinachooneshwa kwenye ramani hii ni mgawanyo wa kijiografia wa ufadhi li wa miradi ya muda mrefu inayolenga kuleta tunu zakijamii

**Kanda ya Ziwa**

- Afya ya uzazi
- Ushirikishwaji wa kifedha

**Mkoa wa Lindi**

- Mradi wa kuwezesha wasichana



**Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Dodoma & Ruvuma**

- Miradi ya Afya ya Fistula

**Mkoa wa Pwani**

- Shule janja
- Afya ya uzazi
- Mtandao wa wanawake wakulima

### 15.3. Miradi ya Kijamii

Ripoti yetu ya Matokeo kwa Jamii imegusa malengo mahsusi ya tunu za Vodacom Tanzania Foundation katika kuunganisha na kujitathmini uelekeo wa uwekezaji wetu katika jamii kwa mwaka 2014 – 17. Tunapima, tunafuatilia na kuripoti matokeo yetu katika jamii ili kutathmini na kuainisha namna tunavyokidhi ahadi zetu kwa jamii nchini Tanzania.

Mchango wa taasisi yetu katika miradi ni kwa kushirikiana na asasi zisizo za kiserikali; kuimarisha uwezo wa miradi kupata matokeo kupitia matokeo mahsusi na uendelezaji wa riziki katika matokeo yaliyopangwa

Idadi na ubora wa njia za utafiti zilizotumika kupima ufanisi wetu na kupata taarifa za matokeo ya kijamii kwa wanufaika wa program yetu. Taarifa katika ripoti hii inawasilisha kipindi cha kuanzia Januari 2014 hadi 31 Disemba, 2017. Taasisi inatoa msaada wa kiufundi na kifedha katika miradi inayolenga maeneo yafuatayo:-



### 15.4. Uwezeshaji wa Jamii iliyounganishwa

Utafiti wa upimaji wa matokeo ulifanyika kwa kutumia nadharia ya Kielelezo ya Logic. Kielelezo ni mpangilio na njia ya wazi inayowezesha kuelewa mahusiano baina ya rasilimali na kupima matokeo ya kuhusika kwetu katika jamii. Katika taarifa ya utafiti huu na tathmini, matokeo yanakusanywa kupitia njia ya msingi na sekondari za ukusanyaji taarifa.


Mchakato wa ukusanyaji wa taarifa ulijumuisha njia za idadi na ubora pamoja na njia za uchambuzi ambazo zinawezesha tathmini timilifu za tunu za kijamii zilizopatikana. Mahojiano na wadau yalifanyika ilikutengeneza mwongozo wa matokeo na kuhakikisha matokeo yake yanapimwa kwa kutumia njia za ukusanyaji taarifa zilizopo kwa usahihi. Majadiliano ya vikundi lengwa yalifanyika kwa kushirikiana na vikundi vya ushirika katika wanufaika wa miradi maeneo ya vijijini.Mchanganyiko wa mahojiano na tafiti yalifanyika kwa mtu mmoja mmoja kwa wanufaika wa wote wa moja kwa moja na wengineo ikijumuisha wanafunzi, wajumbe wa vijiji, walimu na makundi ya wanawake. Mahojiano yote yalirekodiwa kwa kutumia program za simu za ukusanyaji taarifa kwa ajili ya kuhifadhi usiri.




Iwapo tunahitaji kuwapa wanawake na wasichana nafasi wanazostahiri kustawi katika jamii, ni lazima tuwe na uhakika programu zetu zina uwezo wa kubadilisha kila mnufaika tunayefanya naye kazi.

### 15.5. Kuwasilisha Tunu za Jamii




## 15.6. Matokeo ya Tafiti


Kipengele hiki kinawasilisha matokeo na majadiliano ya ukusanyaji taarifa mahali pa kazi, matokeo ya tafiti na majadiliano ya makundi lengwa. Matokeo ya tafiti yanapatikana kupitia ukusanyaji taarifa wa idadi na ubora. Kipengele hiki kinaonesha makundi maalumu yaliyofanyiwa tafiti kwenye jamii, matokeo yaliyotokana na miradi ya kijamii iliyotekelezwa; matokeo ya miradi ya kijamii yanayopimika/yasiyopimika pamoja na faida zilizopatikana miongoni mwa wadau na jamii kwa ujumla

### Matokeo




81.1% walipokea vizuri huduma zilizotolewa na miradi ya jamii ya VTF, ambapo 39.9% walijibu nzuri sana na 44.2% walijibu nzuri. Wakati huo huo, 15.9% walidhani kwamba ubora wa huduma uliotolewa na mradi wa VTF ulikuwa wa wastani


### Idadi ya Waliofanyiwa Utafiti





### Matokeo ya mradi yanayopimika na yasiyopimika

Matokeo ya tafiti yanaonesha kwamba waliofanyiwa utafiti katika maeneo ya afya, elimu n amiradi ya kilimo waliridhika na utoaji wa mradi wa kijamii na matokeo yake. Kiuhalisia, jumla ya 35.5% katika afya, 34.7% katika elimu na 28.6% katika kilimo walionesha mwitikio chanya katika

### Matokeo chanya ya mradi




### Chati ya ufadhili



## 15.7. Upimaji wa Matokeo

**Kielelezo cha mantiki ya namna ya uendeshaji wa miradi ya jamii**

**Changamoto za Kijamii**

Jamii zilizosahaulika zinakabiliana na changamoto ambazo wengi hupambana kuzitatua hali inayosababisha kuwa na hali duni ya upatikanaji wa huduma muhimu za kijami

**Shughuli**

Tunafanya kazi na wanawake ili kuboresha upatikanaji wa kilimo na masoko

Tunafundisha na kuwezesha wanawake katika afya ya uzazi

Tunafundisha upatikanaji wa TEHAMA katika Elimu

**Zao**

Kuwajengea uwezo, kuwapatia masoko, kuwapatia mitaji

Bidhaa za usafi, ushauri nasaha mafunzo na elimu

Mafunzo ya ualimu, kompyuta, maabara, mafunzo ya vitendo

**Matokeo**

Ujuzi na ujasiriamali

Ushirikishwaji ulioboreshwa na ufaulu wa darasani


Kujiamini, kujitambua, kuboreshwa kwa afya na ustawi

Kuboreshwa kwa ujuzi wa mawasiliano, kuboresha kuingia elimu ya juu

**Athari**

Matokeo chanya ya upatikanaji wa elimu, afya na teknolojia kwa wanawake na wasichana katika jamii


### 15.8. Miradi ya afya ya uzazi







## 15.9. Mradi wa kuwawezesha wasichana

**i. Hakuna Wasichoweza** **MATOKEO**




**ii. Upatikanaji wa kilimo: Mtandao wa wanawake wakulima**



### 15.10. Miradi na michango katika SDGs

Malengo ya Maendeleo Endelevu ni muongozo wa kupata ubora na uendelevu wa baadaye kwa wote. Miradi inatatua changamoto za dunia tunazokabiliana nazo ikiwa ni pamoja na zinazohusiana na umasikini, kutokuwa na usawa, tabianchi, uharibifu wa mazingira, ustawi Amani na haki. Malengo yanaoana na ili kutomuacha mtu nyuma, ni muhimu kama tukifanikiwa kila lengo na shabaha ifikapo mwaka 2030. Malengo ya Maendeleo Endelevu ni mwito kwa sekta binafsi kuchangia kutatua changamoto za maendeleo duniani. Vodacom Tanzania Foundation kupitia ushirikiano wetu na utekelezaji wa miradi unatatua mambo muhimu ndani ya SDGs ili kufanikisha mchango wetu katika malengo ya dunia na kitaifa.




Kilimo ni mwajiri mkuu duniani,kikitoa riziki kwa 40% ya watu wote duniani hivi sasa. Ni chanzo kikubwa cha mapato na kazi kwa kaya masikini za vijijini. Programu yetu imefadhili upatikaji zaidi ya 2513 ya ujumuishi ya huduma za kifedha na zaidi ya wanawake 291 wamenufaika na wanapata kianzio cha mitaji na ukuzaji wa ujuzi...




Uwiano wa vifo vinavyotokana na uzazi, uwiano wa kina mama ambao wanaofariki wakati wa kujifungua kulinganisha na wale wanaopo katika mikoa iliyoendelea bado ni mara 14 zaidi ya mikoa iliyoendelea. Miradi yetu ya jamii imefikia zaidi ya wanafuika wa moja kwa moja na wengine zaidi ya 2,763,897 katika afya na ustawi wa miradi ambayo ni sawa na zaidi ya 69% ya ufadhili wa miradi ya jamii

**4 ELIMU BORA**

Kupata elimu bora ni msingi wa kutengeneza maendeleo endelevu. Pamoja na kuboresha ubora wa maisha, upatikanaji wa elimu maalumu unaweza kusaidia wanajamii kupata nyenzo zinazotakiwa kuendeleza ufumbuzi kupitia ubunifu katika matatizo ya dunia. Vijana milioni 103 duniani kote wanakosa maarifa ya msingi, na zaidi ya 60% kati yao ni wanawake. Programu zetu za elimu zinatoa upatikanaji wa elimu bora kupitia miradi ya shule janja. Wanafunzi 60,023 wanasoma bure kupitia majukwaa ya kiteknolojia za kujifunzia.

**5 USAWA WA KIJINSIA**

Kuboresha matumizi ya teknolojia wezeshi, hususani TEHAMA ili kuhamasisha uwezeshaji wa wanawake. Kuhakikisha upatikaji wa afya ya kijamii na uzazi na haki za uzazi kufuatana na Programu ya Kongamano la kimataifa la watu na maendeleo pamoja na jukwaa la Beijing na nyaraka za matokeo kwa ajili ya kongamano la mapitio yake. Programu zetu zimewezesha zaidi ya vijana wasichana 5777 eneo la Lindi ikiwa na matokeo ya uwezeshaji na kujiamini kupitia program za afya ya uzazi. Miradi yetu ya shule janja imetoa upatikanaji wa teknolojia katika mpango wa maabara zetu za kompyuta

**17 USHIRIKIANO KWA MALENGO**

Zaidi ya watu bilioni 4 hawatumii intaneti, na 90% kati yao wanatoka katika nchi zinazoendelea. Uboreshaji wa upatikanaji wa teknolojia na maarifa ni njia muhimu katika kushirikisha mawazo na kuchochea ubunifu. Kupitia program zetu, zaidi ya wanafunzi 60,023 kitaifa wanatumia shule za papo hapo na teknolojia ya habari kupitia maabara za kompyuta mashuleni


Vodacom tunakuunganisha